JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22



## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MACHI 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255 (026) 2321759, Nukushi: 255(026)2117527, Baruapepe: ocag@nao.go.tz, Anwani: www.nao.go.tz

**Kumb. Na.FA. CGA.319/421/01B** **29 Machi 2023**

Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu, S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
**40400 DODOMA.**

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, ninayo furaha kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa Tawala za Mikoa, na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Ninawasilisha,

Charles E. Kichere
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

## Mamlaka

Majukumu na wajibu wa kikatiba wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi, Sura ya 418.

**Dhima, dira na kaulimbiu**

**01 — Dhima yetu**

Kutoa huduma za ukaguzi zenye kiwango cha juu kwa njia za kisasa zenye kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

**02 — Dira yetu**

Kuwa taasisi yenye Kuaminika na ya kisasa katika ukaguzi wa umma inayotoa huduma za ukaguzi za viwango vya juu zinazoimarisha imani kwa umma.

**03 — Kauli mbiu yetu**

Kuwa taasisi yenye kuaminika na ya kisasa katika ukaguzi wa umma.




**Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo**

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

**Kufanya kazi kwa ushirikiano**

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

**Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo**

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.

**Kufanya kazi kwa utaalam**

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

**Kufanya kazi kwa uadilifu**

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

**Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi**

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

# YALIYOMO


ORODHA YA MAJEDWALI ....................................................................iv
ORODHA YA VIAMBATISHO .................................................................. viii
ORODHA YA VIELELEZO........................................................................ x
VIFUPISHO.........................................................................................xi
TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ................ xiii
MUHTASARI ....................................................................................... xv
SURA YA KWANZA ................................................................................ 1
**MAELEZO YA AWALI** ........................................................................... 1
SURA YA PILI ........................................................................................ 5
**HATI ZA UKAGUZI** ............................................................................... 5
SURA YA TATU ...................................................................................... 9
**UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA** ....... 9
SURA YA NNE ..................................................................................... 16
**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI** ................................................... 16
SURA YA TANO.................................................................................... 27
**USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA** ............................................... 27
SURA YA SITA ..................................................................................... 47
**USIMAMIZI WA MAPATO**........................................................................ 47
SURA YA SABA .................................................................................... 63
**USIMAMIZI WA MATUMIZI** ...................................................................... 63
SURA YA NANE.................................................................................... 74
**USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA**...................................... 74
SURA YA TISA ..................................................................................... 81
**UTATHMINI WA MIFUMO YA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA UTAWALA BORA** .... 81
SURA YA KUMI ..................................................................................... 94
**MFUKO WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU** .................. 94
SURA YA KUMI NA MOJA ........................................................................ 105
**TATHMINI YA MIRADI YA MAENDELEO** ................................................. 105
SURA YA KUMI NA MBILI ....................................................................... 115
**UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA ELIMU** ................................ 115
SURA YA KUMI NA TATU ........................................................................ 122
**UFANISI WA UTENDAJI KATIKA SEKTA YA AFYA**...................................... 122
SURA YA KUMI NA NNE ......................................................................... 137
**UFANISI WA UWEKEZAJI, USIMAMIZI WA MASOKO NA VITUO VYA MABASI** ... 137
SURA YA KUMI NA TANO......................................................................... 148
**SEKRETARIETI ZA MIKOA** ...................................................................... 148
SURA YA KUMI NA SITA ......................................................................... 160
**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** ...................... 160
SURA YA KUMI NA SABA ........................................................................ 191
**MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU**............................................................ 191

SURA YA KUMI NA NANE ................................................................ 194
**MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO** ......................................... 194
**VIAMBATISHO** ........................................................................ 196

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na.2-1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi ...................................... 7
Jedwali Na.3-1: Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita.. 10
Jedwali Na.3-2: Utekelezaji wa Maagizo ya LAAC.................................. 11
Jedwali Na.3-3: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Maagizo ya Muda Mrefu .. 12
Jedwali Na.3-4: Utekelezaji wa Maagizo ya PAC ................................... 13
Jedwali Na.3-5: Utekelezaji wa Maagizo ya PAC ................................... 13
Jedwali Na.3-6: Sekretarieti za Mikoa Zenye Maagizo ya Muda Mrefu ........... 14
Jedwali Na. 4-1: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani Ikilinganishwa na Bajeti ........................................................................ 18
Jedwali Na.4-2: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato Zaidi ya Bajeti ........................................................................ 19
Jedwali Na.4-3: Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato Chini ya Bajeti ........................................................................ 19
Jedwali Na.4-4: Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Iliyopokelewa .................. 20
Jedwali Na.4-5: Fedha za Ruzuku ya Maendeleo Zilizotolewa..................... 21
Jedwali Na.4-6: Fedha ya Mapato ya Ndani Ambazo Hazikupelekwa Katika Miradi ya Maendeleo.......................................................... 22
Jedwali Na.4-7: Fedha Zilizosalia Kwa Miradi ya Ujenzi na Ambazo Hazikutumiwa Ndani ya Muda ........................................................ 23
Jedwali Na.4-8: Matumizi Yasiyokuwepo Kwenye Bajeti na Fedha Zilizobadilishwa Matumizi ........................................................ 24
Jedwali Na.5-1: Halmashauri Zilizofanya ununuzi Bila Kudhinishwa na Bodi za Zabuni ........................................................................ 28
Jedwali Na.5-2: Halmashauri Zilizofanya ununuzi Mdogo Bila Kutolewa Taarifa Kwenye Bodi za Zabuni ........................................................ 28
Jedwali Na.5-3: Ununuzi Uliofanyika Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka . 29
Jedwali Na.5-4: Ununuzi Uliofanyika Bila Ushindanishi wa Bei.................... 30
Jedwali Na. 5-5: Ununuzi uliofanyika Bila Hati ya Kuagiza Vifaa/Bidhaa ........ 31
Jedwali Na.5-6: Mapokezi ya Vifaa/Bidhaa Bila Kufanyiwa Ukaguzi .............. 32
Jedwali Na.5-7: Miradi Iliyotekelezwa Bila Tathimini ya Athari za Mazingira... 33
Jedwali Na.5-8: Mikataba Ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria .............. 33
Jedwali Na.5-9: Manunuzi kwa Wazabuni Wasiokuwa na Mikataba............... 35
Jedwali Na.5-10: Manunuzi ya Bidhaa Kwa Wazabuni............................. 35
Jedwali Na.5-11: Mamlaka za Serikali za Mtaa Zilizofanya Malipo Kabla ya Bidhaa Kupokelewa ........................................................... 36
Jedwali Na.5-12: Ununuzi wa Bidhaa Bila Kuanisha kwa Kina Mahitaji .......... 37
Jedwali Na.5-13: Orodha ya Halmashauri zenye Magari Ambayo Hayajawasilishwa .............................................................. 38
Jedwali Na.5-14: Vifaa vya Ujenzi Ambavyo Havijafanyiwa Vipomo vya Ubora 39
Jedwali Na.5-15: Bidhaa Zilizonunuliwa Zaidi ya Mahitaji Halisi .................. 40
Jedwali Na.5-16: Malipo Bila Vipimo na Kuidhinishwa na Mhandisi............... 41
Jedwali Na.5-17: Malipo kwa Wakandarasi Zaidi ya Kiasi Kilichotakiwa ......... 42
Jedwali Na.5-18: Ununuzi uliyofanyika bila ushindani ........................... 42
Jedwali Na.5-19: Malipo ya awali kwa mkandarasi yenye mapungufu...... 43

Jedwali Na.5-20: Mapungufu katika dhamana za utendaji zilizowasilishwa ........ 45
Jedwali Na.5-21: Malipo ya Wakandarasi Ambayo Hayajalipwa ........ 46
Jedwali Na.6-1: Makusanyo Yasiyowasilishwa Benki ........ 49
Jedwali Na.6-2: Vyanzo vya Mapato Visivyokusanywa ........ 51
Jedwali Na.6-3: Wadaiwa wa Mapato Mbalimbali ........ 53
Jedwali Na.6-4: Taarifa ya Makusanyo ya Mawakala ........ 55
Jedwali Na.6-5: Ankara Zilizorekebishwa Bila Viambatisho ........ 56
Jedwali Na.6-6: Ushuru wa Huduma Usiokusanywa ........ 58
Jedwali Na.6-7: Makusanyo ya Ushuru wa Huduma Bila Uthibitisho ........ 59
Jedwali Na.6-8: Ushuru wa Mazao Usiokusanywa ........ 60
Jedwali Na.7-1: Malipo yasiyo na Risiti za Kielectroniki ........ 64
Jedwali Na.7-2: Malipo yenye viambatisho pungufu ........ 65
Jedwali Na.7-3: Halmashauri zilizotumia fedha za amana kwa matumizi yasiyopangwa ........ 67
Jedwali Na.7-4:Malipo Yaliyofanyika Zaidi ya Amana Iliyopo ........ 68
Jedwali Na.7-5: Malipo katika akaunti ya amana Bila uthibitisho wa amana kupokelewa ........ 68
Jedwali Na. 7-6: Malipo Kwa Fedha Taslimu ........ 69
Jedwali Na.7-7: Halmashauri Zenye Masurufu Yasiyorejeshwa ........ 70
Jedwali Na. 7-8: Halmashauri zenye Kodi ya Zuio Isiyowasilishwa ........ 71
Jedwali Na.7-9: Halmashauri zenye Matumizi Yasiyo na Tija ........ 72
Jedwali Na.8-1: Madai ya Stahiki za Wafanyakazi Ambayo Hayajalipwa ........ 75
Jedwali Na.8-2:Wastaafu Kutolipwa Gharama za Usafirishaji wa Mizigo ........ 76
Jedwali Na.8-3: Michango Ambayo Haikupelekwa Katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi Zingine ........ 77
Jedwali Na.8-4: Makato Kwenye Posho za Madiwani Ambayo Hayakuwasilishwa Benki ya CRDB PLC ........ 78
Jedwali Na.8-5: Halmashauri zenye Wakuu wa Idara Wasio na Sifa ........ 79
Jedwali Na.8-6: Malipo Yaliyofanywa Kwa Wafanyakazi Bila Kuwa na Mikataba Halali ........ 80
Jedwali Na.9-1:Taarifa za Mapato Zilizotagazwa Tofauti na Kiasi Kilichopo Katika Mfumo wa Makusanyo (LGRCIS) ........ 92
Jedwali Na.10-1: Mikopo Iliyogawanywa Miongoni kwa Wanakikundi ........ 96
Jedwali Na.10-2: Halmashauri zenye Vikundi Visivyokuwepo ........ 97
Jedwali Na.10-3: Mikopo Kwa Vikundi Vilivyositisha Biashara ........ 98
Jedwali Na. 10-4: Halmashauri zisizokamilisha Michango Kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ........ 99
Jedwali Na. 10-5: Mwenendo wa michango kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ........ 100
Jedwali Na. 10-6: Halmashauri Zilizotoa Mikopo Kinyume na Uwino Unaotakiwa ........ 101
Jedwali Na.11-1: Miradi Iliyokamilika Lakini Haitumiki ........ 107
Jedwali Na.11-2:Fedha za Miradi ya Maendeleo Zilizobadilishwa Matumizi.. 108
Jedwali Na.11-3: Miradi Iliyochelewa Kukamilika ........ 109
Jedwali Na. 11-4: Kutowasilishwa Kwa Mipango ya Miradi ya CSR ........ 112

Jedwali Na.11-5: Kutotekelezwa Kwa Mipango ya Miradi ya CSR .............. 112
Jedwali Na.12-1: Uhaba Miundombinu ya Shule .................................. 116
Jedwali Na.12-2: Upungufu wa walimu shule za msingi na sekondari ......... 118
Jedwali Na.12-3: Wanafunzi Waliokatisha Masomo Shule za Msingi ........... 119
Jedwali Na.12-4: Wanafunzi waliokatisha masomo shule za sekondari ....... 120
Jedwali Na.13-1: Halmashauri zenye Miradi iliyochelewa kukamilika......... 123
Jedwali Na.13-2: Halmashauri ambazo hazikuwa zimeanza utekelezaji wa miradi ........................................................................... 124
Jedwali Na. 13-3: Miradi iliyokamilika ambayo haitumiki........................ 125
Jedwali Na.13-4: Halmashauri zenye madawa yaliyoisha muda wa matumizi 127
Jedwali Na. 13-5: Dawa na vifaa tiba vilivyolipiwa ambavyo havijapokelewa 129
Jedwali Na.13-6: Bakaa ya Fedha za Dawa na Vifaa Tiba Katika Bohari ya Dawa ........................................................................... 129
Jedwali Na.13-7: Fedha za Dawa Zilizotumika kwa Matumizi Mengineyo..... 131
Jedwali Na.13-8: Vifaa Vilivyonunuliwa Ambavyo Havitumiki .................. 132
Jedwali Na. 13-9: Halmashauri zenye Viwango vya Vifo zaidi ya 100 ......... 133
Jedwali Na.13-10: Halmashauri zenye Ongezeko La Vifo vya Wajawazito ... 134
Jedwali Na.13-11: Halmashauri zenye Viwango Vikubwa vya Vifo vya Watoto Wachanga........................................................................ 135
Jedwali Na.13-12: Idadi ya Vifo vya Watoto Wachanga Katika Halmashauri.. 135
Jedwali Na.14-1: Muda wa Kurejesha Gharama za Uwekezaji Katika Hoteli ya Jiji la Dodoma Kulingana na Makubaliano ya Ukodishaji ........................ 138
Jedwali Na.14-2: Orodha ya Muundo wa Umiliki wa Hisa za Kampuni ......... 139
Jedwali Na.14-3: Vibanda na Fremu za Soko Zilizo Wazi Katika H/M Ubungo 140
Jedwali Na.14-4: Vibanda na Fremu za Soko Zilizo Wazi H/M Morogoro ...... 141
Jedwali Na.14-5: Vibanda na Vyumba Vilivyo Wazi Katika H/Jiji la Dodoma . 141
Jedwali Na.14-6: Vituo vya Mabasi Ambavyo Ujenzi Umechelewa ............ 142
Jedwali Na. 14-7: Viwanda vya Kusindika Mazao ya Nyuki Visivyotumika .... 143
Jedwali Na.14-8: Hisa za Benki ya DCB ............................................ 145
Jedwali Na.15-1: Fedha zilizotolewa kabla ya muda ya utekelezaji wa mradi ........................................................................... 149
Jedwali Na. 15-2: Matumuzi yasiyo na tija ....................................... 150
Jedwali Na.15-3: Malipo yasiyo na nyaraka stahiki.............................. 151
Jedwali Na.15-4: Magari yaliyonunuliwa GPSA ambayo bado hayajapokelewa ........................................................................... 152
Jedwali Na. 15-5: Miradi Iliyotekelezwa Bila Kufanya Athari za Mazingira ... 153
Jedwali Na. 15-6: Nyongeza ya kazi isiyoidhinishwa ............................ 154
Jedwali Na.15-7: Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Uwanja wa Ndege Mwanza ........................................................... 155
Jedwali Na. 15-8: Vifaa vya ujenzi vilivotelekezwa uwanja wa Ndege Mwanza ........................................................................... 155
Jedwali Na.15-9: Kuanzishwa kwa Miradi Bila Kuwa na Hati Miliki............ 156
Jedwali Na.15-10: Madai ya iCHF ambayo hayajlipwa ........................... 158
Jedwali Na.15-11: Fedha za Maendeleo kutumika kwa Lengo lisilokusudiwa 159
Jedwali Na.16-1: Hali ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ............... 161

Jedwali Na.16-2: Kutosimamia dhamana ya mikopo ili kufidia mikopo isiyolipika........................................................................ 171
Jedwali Na.16-3: Kutofanyika kwa marejesho ya mkopo ya mwaka ........... 171
Jedwali Na.16-4: Mtiririko wa fedha pungufu ..................................... 172
Jedwali Na.16-5: Hali ya Utekelezaji wa Shughuli ................................ 174
Jedwali Na. 16-6: Magari Ambayo Hayajawasilishwa ............................. 174
Jedwali Na.16-7: Kutokukusanywa Kwa Mapato ................................... 175
Jedwali Na. 16-8: Mikoa yenye Mradi Iliyo na Kasi Ndogo ya Utekelezaji..... 179
Jedwali Na. 16-9: Kutokatiwa Bima Kwa Mikataba ya Miradi .................... 183

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. 2-1: Mwenendo wa Hati za ukaguzi zilizotolewa................ 196
Kiambatisho Na. 3-1: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita .. 202
Kiambatisho Na. 3-2: Utekelezaji wa maagizo ya LAAC ............................ 208
Kiambatisho Na. 4-1: Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani............ 212
Kiambatisho Na. 4-2: Halmashauri zenye ukusanyaji wa mapato ya ndani zaidi ya bajeti ........................................................................... 216
Kiambatisho Na. 4-3: Halmashauri zenye ukusanyaji wa mapato ya ndani chini ya bajeti ........................................................................... 218
Kiambatisho Na. 4-4: Uchambuzi wa Fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa ............................................................... 220
Kiambatisho Na. 4-5: Uchambuzi wa Fedha za ruzuku ya Maendeleo iliyopokelewa ........................................................................... 222
Kiambatisho Na. 4-6: Tofauti za Ruzuku zilizotolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina dhidi ya kiasi halisi kilichopokelewa ................................................ 224
Kiambatisho Na. 6-1: Makusanyo halisi ya mapato ya ndani........................ 225
Kiambatisho Na. 6-2: Mapato yasiyokusanywa...................................... 228
Kiambatisho Na. 8-1: Malimbikizo ya mishahara na madai ya wafanyakazi ambayo hayakulipwa ....................................................................... 233
Kiambatisho Na. 8-2: Makato ya watumishi ambayo hayakupelekwa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi zingine husika ........................................ 242
Kiambatisho Na. 9-1: Mapungufu katika vitengo vya ukaguzi wa ndani........... 244
Kiambatisho Na. 9-2: Mapungufu katika udhibiti wa mifumo ya ndani na vihatarishi ........................................................................... 246
Kiambatisho Na. 9-3: Mapungufu katika usimamizi wa TEHAMA pamoja na mifumo ya uhasibu ...................................................................... 248
Kiambatisho Na. 9-4: Mapungufu Katika Utendaji wa Kamati za Ukaguzi ........ 249
Kiambatisho Na. 9-5: Udhibiti katika ukusanyi wa mapato (LGRCIS) na mashine za kukusanyia mapato (POS)........................................................... 250
Kiambatisho Na. 10-1: Thamani ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu......................................................................... 251
Kiambatisho Na. 10-2: Michango ya Halmashauri kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu................................................... 253
Kiambatisho Na. 10-3: Kiasi kisichorejeshwa kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ............................................................ 255
Kiambatisho Na. 11-1: Miradi inayotekelezwa bila vibali vya lazima na vyeti vya ujenzi.......................................................................... 257
Kiambatisho Na. 11-2: Miradi ambayo haijakamilika ............................... 259
Kiambatisho Na. 11-3: Kasoro zilizobainishwa katika Utekelezaji wa Miradi..... 272
Kiambatisho Na. 12-1: Fedha pungufu zilizotolewa kwa ajili ya elimu bure ..... 274
Kiambatisho Na. 12-2: Upungufu wa Miundombinu Shule za Msingi ............... 275
Kiambatisho Na. 12-3: Upungufu wa Miundombinu Shule ya Sekondari........... 277
Kiambatisho Na. 12-4: Ufaulu katika shule za sekondari........................... 279
Kiambatisho Na. 13-1: Halmashauri zenye miradi ambayo haijakamilika ........ 281
Kiambatisho Na. 13-2: Halmashauri zenye madai yaliyokataliwa na NHIF........ 287
Kiambatisho Na. 14-1: Vibanda, vyumba na ofisi zilizo wazi kwenye masoko ya H/Jiji Dodoma ........................................................................... 289

Kiambatisho Na. 15-1: Miradi ambayo haijakamilika ................................ 296
Kiambatisho Na. 16-1: Miradi iliyotelekezwa na wakandarasi...................... 297
Kiambatisho Na. 16-2: Kazi za barabara zilizofanyika kwa kiwango cha chini ... 300
Kiambatisho Na. 16-3: Dhamana za utendaji ambazo hazijadaiwa kwenye mikataba iliyositishwa ........................................................................... 303
Kiambatisho Na. 16-4: Mapungufu katika dhamana ya utendaji wa miradi....... 304
Kiambatisho Na. 16-5: Mikataba inayotekelezwa bila ya kukatiwa bima ......... 305
Kiambatisho Na.16-6:Mikataba ambayo bima yake haikuhusisha kipindi cha matazamio ........................................................................... 306

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na 6-1: Mwenendo wa mapato ya ndani .................................... 47
Kielelezo Na 6-2: Mwenendo wa makusanyo yasiyowalishwa benki ................. 50
Kielelezo Na 6-3: Mwenendo wa madai ................................................. 54
Kielelezo Na 7-1: Mwenendo wa Malipo Ambayo Hayakuwa na Viambatisho Vya Kutosha ........................................................................... 66
Kielezo Na 16-1: Mwenendo wa Masurufu ............................................ 187

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AFROSAI-e** | Jumuiya ya Afrika ya Taasisi Kuu za Ukaguzi zinazungumza Kiingereza |
| **ALAT** | Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa Tanzania |
| **AMCOS** | Vyama vya Ushirika |
| **CBMS** | Mfumo Mkuu wa Bajeti |
| **CDCF** | Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo |
| **CHF** | Mfuko wa Afya ya Jamii |
| **CSR** | Uwajibikaji wa Taasisi kwa Jamii |
| **DART** | Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi |
| **EFD** | Kifaa cha Risiti za kieletroniki |
| **EGPAF** | Mfuko wa Elizabeth Glaser wa Kusaidia Afya ya Mtoto |
| **EIA** | Tathmini ya Athari kwa Mazingira |
| **EQUIP-T** | Mpango wa Kuboresha Ubora wa Elimu |
| **ESDP** | Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu |
| **FFARS** | Mfumo wa Taarifa za Kifedha Unaotumiwa katika Ngazi za Chini za Serikali |
| **GACS** | Mfumo wa Kuuunganisha Hesabu za Serikali |
| **GAMIS** | Mfumo wa Mali za Kudumu wa Serikali |
| **GCC** | Masharti ya Jumla ya Mikataba |
| **GePG** | Mfumo wa Malipo wa Serikali |
| **GoT-HoMIS** | Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania |
| **GPE II** | Mradi wa Ushirika wa Kilimwengu kwa ajili ya Elimu - II |
| **GPSA** | Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini |
| **H/Jiji** | Halmashauri ya Jiji |
| **H/M** | Halmashauri ya Manispaa |
| **H/Mji** | Halmashauri ya Mji |
| **H/W** | Halmashauri ya Wilaya |
| **HCMIS** | Mfumo wa Pamoja wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara |
| **iCHF** | Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa |
| **IMEI** | Namba ya Utambulisho wa Kifaa |
| **ISSAI** | Viwango vya Kimataifa kwa Taasisi Kuu za Ukaguzi |
| **LAAC** | Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa |
| **LARAM** | Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato wa Serikali za Mitaa |
| **LGA** | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| **LGDG** | Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa |
| **LGLB** | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa |
| **LGRCIS** | Mfumo wa taarifa za ukusanyaji mapato katika Mamlaka za serikali za Mitaa |
| **LPO** | Hati ya Kuagiza Vifaa |
| **MSD** | Bohari Kuu ya Dawa |
| **MUSE** | Mfumo wa Ulipaji Serikalini |
| **Na.** | Namba |
| **NHIF** | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| **NPL** | Mikopo Isiyofanya Vizuri |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaaa |
| **PAC** | Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali |
| **PPA** | Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2011 |
| **PPRA** | Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma |
| **Sh.** | Shilingi |
| **TAA** | Mamlaka ya Viwanja wa Ndege |
| **TAKUKURU** | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| **TAMISEMI** | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TANePS** | Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi Tanzania |

| | |
|---|---|
| **TANESCO** | Shirika la Umeme Tanzania |
| **TARURA** | Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini |
| **TEA** | Mamlaka ya Elimu Tanzania |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TRA** | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| **UVIKO** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona |



# SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Nina furaha kubwa kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi ya Mwaka wa Fedha 2021/22 iliyolenga kaguzi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ripoti hii ya kina inayojumuisha ripoti 218 inalipatia Bunge na umma uhakika kwamba wanaweza kuziamini taarifa za fedha zilizowasilishwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Toleo la mwaka huu linatofautiana na la miaka ya nyuma kwa kuwa imejumuisha ukaguzi wa Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na taasisi zake, ambazo hapo awali zilikuwa zikitolewa taarifa chini ya Serikali Kuu. Lengo lilikuwa ni kufanya tathmini ya kina ya utendaji wa jumla wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuanzia ngazi ya Wizara, ambapo sera zinatungwa, hadi ngazi za chini ambapo shughuli za maendeleo zinatekelezwa na huduma zinatolewa kwa wananchi. Utaratibu huu wa utoaji taarifa unaongeza kufahamika wa utendaji kazi wa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. na kupitia hili, naamini Serikali inaweza kufikia uwajibikaji na uadilifu unaotakiwa, kuboresha utendaji kazi na kujenga imani kwa wananchi na wadau wengine.

Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mchango wake mkubwa na endelevu kwa Ofisi yangu.

Pia, natoa shukrani zangu kwa Bunge na Kamati zake kwa jukumu lao muhimu la kusimamia na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

Ninapenda pia kuwashukuru wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa juhudi zao kubwa wanazofanya katika ubora wa hali ya juu, jambo

linalodumisha imani na uaminifu ndani ya sekta ya umma. Mbeleni, tutaendelea kujitolea kutanguliza maslahi ya umma kwa kuifanya Ofisi yetu iwe ya kisasa, yenye ustawi kwa wafanyakazi, na inayozidi kuaminiwa na sekta ya umma tunapoendelea kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba. Umuhimu wa kazi tunazofanya uko dhahiri.

Kwa kumalizia, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wadau wote wakiwemo Washirika wa Maendeleo na wale ambao kwa namna moja au nyingine wameunga mkono kazi zetu, na nina ahidi kuwa tutaendelea kujitoa kwa dhati kudumisha dhana ya uwajibikaji na uadilifu katika usimamizi wa rasilimali za Umma.

**Charles E. Kichere**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

# MUHTASARI

## Hati za Ukaguzi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022, nilikagua na kutoa hati kwa taasisi 218. Kati ya hizo, 204(94%) zilikuwa na Hati Inayoridhisha, 13 (6%) zilikuwa na Hati yenye Shaka, na hati mabya moja kama inayvoonekana katika Jedwali hapa chini

| Mwaka wa Fedha | Tasisisi | Hati | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Inayoridhisha | Shaka | Mbaya | Kushindwa kutoa maoni | |
| 2021/22 | Mamlaka za Serikali za Mitaa | 170 | 13 | 1 | 0 | **184** |
| | Sekretarrieti za Miko | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | OR-TAMISEMI | 8 | 0 | 0 | 0 | **8** |
| Jumla | | **204** | **13** | 1 | **0** | **218** |

Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa idadi kubwa ya hati za ukaguzi zinazoridhisha, taasisi zilizokaguliwa bado zilikuwa na hoja zinazotokana na ukiukwaji wa maamuzi ya Bunge, sheria, sera na maagizo ya Serikali, ingawa hayakuwa na athari za moja kwa moja kwenye usahihi wa taarifa za fedha zilizowasilishwa.

## Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita

Kwa ujumla, tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo 11,820 ya ukaguzi wa miaka ya nyuma yaliyotolewa kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa inaonesha kiwango cha chini cha asilimia 42. Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge za Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kilikuwa asilimia 26, ilihali maagizo ya Kamati ya Bunge za Hesabu za Serikali (PAC) yalikuwa na kiwango bora cha utekelezaji cha asilimia 60 kufikia mwaka wa fedha 2021/22.

## Utayarishaji na Utekelezaji wa Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2021/22, jumla ya mapato ya ndani yaliyokusanywa na Halmashauri 184 yalikuwa shilingi bilioni 891.84, ambayo yalivuka makadirio ya bajeti kwa asilimia 102. Kiasi hiki ni ongezeko la shilingi bilioni 122.41 kutoka makusanyo ya mwaka wa fedha uliopita.

Mchanganuo wa fedha zilizotolewa na Halmashauri hizo umebaini kuwa kati ya Halmashauri 184, Halmashauri 76 hazikutenga na kuchangia asilimia inayohitajika ya shilingi bilioni 22.37 katika shughuli za maendeleo.

## Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba

Nilifanya tathmini ya ununuzi na usimamizi wa mikataba na kubaini kasoro mabalimbali katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika Halmashuri, ikiwemo majaribio ya vifaa vya ujenzi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.38 hayakufanyika kwa miradi ya ujenzi, na malipo ya kazi zilizotekelezwa yenye thamani ya shilingi bilioni 7.8 yalichelewa kwa zaidi ya siku 90.

Aidha, kulikuwa na dosari katika kiasi cha awali cha shilingi bilioni 4.13 kilicholipwa kwa wakandarasi, ikiwa ni pamoja na malipo ya ziada, malipo bila dhamana, na wakandarasi kushindwa kuonesha jinsi kiasi cha fedha ya awali ilivyotumika. Halmashauri pia zilishindwa kurejesha malipo ya awali katika baadhi ya miradi.

## Usimamizi wa Mapato

Katika tathmini ya taarifa za mfumo wa mapato (LGRCIS), nilibaini kuwa mapato ya shilingi bilioni 11.07 yalikusanywa kutoka vyanzo vingine kupitia mashine za POS, lakini hayakupelekwa kwenye akaunti za benki za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

Aidha, mapitio ya makusanyo ya mapato kupitia LGRCIS yalibaini mapato ya shilingi bilioni 76.59 hayakukusanywa, hususan yatokanayo na tozo za vizimba vya masoko, uuzaji wa viwanja, mazao ya kilimo, leseni za vileo, ushuru wa uchimbaji wa vifaa vya ujenzi, leseni ya biashara, ushuru wa huduma na ushuru wa kupangisha maduka na nyumba zilizopo katika stendi za mabasi na masoko ya Halmashauri.

Pia nilibaini kulikuwa na shilingi bilioni 13.15 ambazo hazikuwa zimekusanywa kutoka kwa wadaiwa mbalimbali waliopewa hati za madai za mfumo wa mapato (LGRCIS) bila kubainisha sababu. Aidha, shilingi bilioni 4.94 hazikuwasilishwa na mawakala wa ukusanyaji mapato kulingana na makubaliano ya mikataba.

Pamoja na changamoto hizo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefanya maboresho ya kitaasisi katika makusanyo ya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake, ambapo jumla ya shilingi bilioni 891.84 zilikusanywa katika mwaka wa fedha 2021/22, ikiwa ni ongezeko la takribani asilimia 17 kutoka makusanyo ya mwaka uliopita ya shilingi bilioni 760.95.

## Usimamizi wa Matumizi

Nilibaini Halmashauri 111 zilikuwa na matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 11.78 ambayo hayakuwa na nyaraka toshelevu, ambapo, Halmashauri 71 zililipa shilingi bilioni 10.08 bila kudai risiti za EFD, huku Halmashauri 40 zikilipa shilingi bilioni 1.70 bila nyaraka husika. Kutumia pesa za umma bila maelezo na/au viambatisho vya kutosheleza kunatia shaka juu ya uhalali wa malipo hayo.

Pia, Halmashauri 71 zililipa shilingi bilioni 7.7 kutoka kwenye akaunti za amana kinyume na madhumuni ya fedha na bila idhini, na Halmashauri 14 zililipa shilingi bilioni 1.51 kwa fedha taslimu kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma kinyume na Kanuni za ununuzi.

Pia, nilibaini kuwa, Halmashauri Tisa zilitumia shilingi milioni 898.85 katika matumizi yasiyo na manufaa, kati ya kiasi hicho, shilingi milioni 322.29 zilitumika na Halmashauri ya Jiji la Arusha katika ujenzi na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa barabara ambazo hazikuthibitishwa uwepo wake

## Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara

Hata hivyo, Mamlaka za Serikali za Mitaa 113 hazikulipa malimbikizo ya mishaha na stahiki za watumishi yenye thamani ya shilingi bilioni 119.94 kwa zaidi ya mwaka mmoja. Aidha, Halmashauri sita hazikulipa kiasi cha shilingi bilioni 309.67 kwa watumishi 233 waliostaafu ikiwa ni gharama ya kusafirisha mizigo baada ya kustaafu.

Vilevile, nilibaini kuwa Halmashauri 106 zilikuwa na idara na vitengo ambavyo vinaongozwa na watumishi 747 wasio na sifa. Hali hii ilitokana na changamoto zilizojitokeza za mungiliano ya majukumu ya wakuu wa idara na vitengo yaliyoainishwa kwenye muundo wa zamani kwenda kwenye muundo mpya.

### Tathmini ya Mifumo ya Ndani, Usimamizi ya Vihatarishi, na Utawala Bora

Serikali iliidhinisha mfumo wa MUSE kwa ajili ya usimamizi wa malipo hata hivyo, mifumo mingine ya uhasibu kama vile FFARS, GAMIS, na GoTHOMIS ipo kwa ajili ya kusimamia mapato na matumizi ya vituo vya afya pamoja na elimu, usimamizi wa pamoja wa mali na taarifa za vituo vya afya. Hata hivyo, kuwepo kwa mifumo ya kielektroniki ambayo haijawiana na kuunganishwa ipasavyo kuna sababisha kurudiwa kwa kazi na taratibu kunakopelekea kuongezeka kwa gharama za utawala na matengenezo.

Ulinganisho wa taarifa za ukusanyaji wa vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizochapishwa na OR-TAMISEMI na zile zitokanazo na mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) ulikuwa na utofauti wa makusanyo halisi ya mapato kwa Halmashauri sita.

### Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu

Nilibaini kuwa Mamlaka kadhaa za Serikali za Mitaa hazikuweza kukusanya mikopo iliyotolewa kwenye vikundi vya Wanawake, Vijana, na Watu wenye Ulemavu, yenye jumla ya shilingi bilioni 88.42. Hii ilitokana na kutokuwa na ujuzi wa kutosha kwenye Idara za Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wakati wa kufanya upembuzi yakinifu kwa vikundi vilivyoomba mikopo, kuvisimamia vikundi hivyo, kufuatilia urejeshaji wa mikopo, na kutoa mafunzo ya biashara kwa wanufaika.

Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2.25 zinahusiana na vikundi vilivyoacha shughuli za biashara hivyo kuleta mashaka juu ya urejeshwaji wa mikopo hiyo.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Mamlaka tatu za Serikali za Mitaa zilitoa shilingi milioni 895.94 kwa vikundi 48 ambavyo havikuwepo.

Aidha, nilibaini kuwa Mamlaka 53 za Serikali za Mitaa zilishindwa kuchangia jumla ya shilingi bilioni 5.06 kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana, na Watu wenye Ulemavu kutoka katika vyanzo vyao vya mapato kinyume na Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290.

### Tathmini ya Miradi ya Maendeleo

Halmashauri 11 zilitekeleza miradi mikubwa yenye thamani ya shilingi bilioni 36.68 isiyokidhi vigezo. Vilevile Halmashauri 10 zilikamilisha miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 3.31 isiyofanya kazi, na Halmashauri 87 hazikukamilisha miradi mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 112.24.

Kuchelewa kukamilika kwa miradi kunaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama zisizo za lazima.

### Ufanisi wa Uendeshaji katika Sekta ya Elimu

Mwaka wa fedha 2021/22 ulishuhudia upungufu wa shilingi bilioni 5.8 za ruzuku ya elimu bure kwa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri 25. Aidha, Halmashauri 13 zilkuwa na upungufu wa walimu, 7,273 (sawa na 38%) na 2,798 (sawa na 29%) wa shule za msingi na sekondari mtawalia.

Aidha, asilimia 28 ya wanafunzi walioandikishwa kidato cha kwanza mwaka 2018 hawakumaliza na kupata vyeti vya elimu ya sekondari katika Halmashauri 19, wakati asilimia 12 ya wanafunzi walifeli mitihani ya taifa ya kidato cha nne katika Halmashauri 96 kwa mwaka wa masomo 2021.

### Ufanisi wa Uendeshaji Katika Sekta ya Afya

Katika ukaguzi wa sekta ya afya, nilibaini masuala kadhaa yanayohusiana na miradi ya vituo vya afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwanza, kuna miradi ambayo haijakamilika yenye thamani ya shilingi bilioni 82.95 katika Halmashauri 91, na vilevile miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.64 ambayo haijaanza. Pili, miradi iliyokamilika katika Halmashauri 16 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.93 haikuwa imeanza kutumika. Tatu, dawa zenye thamani ya shilingi

bilioni 8.16 zilizoagizwa na Halmashauri 10 kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) hazikufikishwa kwenye vituo vya afya.

Vilevile, nilibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulikataa madai ya ya shilingi bilioni 1.77 kutoka kwa Halmashauri 66 kwa sababu ya kutozingatia miongozo ya NHIF. Aidha, kulikuwa na ongezeko la idadi ya vifo vya wajawazito zaidi ya wastani wa vifo 102 hadi 989 kwa kila vizazi hai 100,000 juu ya shabaha ya vifo 100 kwa kila vizazi hai 100,000 kwa Halmashauri 20 kwa mwaka 2021/22.

Nilibaini kuwa, kwa miaka ya fedha 2020/21 na 2021/22, kulikuwa na vifo vya watoto wachanga 6,335 katika Halmashauri 20; hata hivyo, uwiano wa vizazi hai na vifo kwa watoto wachanga havikuweza kutambuliwa kwa vile takwimu za uzazi hazikupatikana. Pia nilibaini katika Halmashauri mbili kwamba kiwango cha vifo vya watoto wachanga kilikuwa juu sana. Halmashauri ya Jiji ya Mbeya ilikuwa na kiwango cha vifo 135 kwa kila vizazi 1000, huku Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ikiwa na kiwango cha vifo 49 kwa kila vizazi 1000. Viwango hivi ni vya juu kuliko shabaha inayotarajiwa ya vifo 30 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa, ambavyo vinahitaji kufikiwa ndani ya mpango wa miaka mitano.

### Mapitio ya Ufanisi katika Uwekezaji

Kwa lengo la kuongeza wigo wa mapato, Mamlaka za Serikali za Mitaa hufanya uwekezaji katika sekta mbalimbali. Nilichunguza uwiano wa utendaji katika uwekezaji, na ufanisi wa usimamizi wa Serikali za Mitaa katika kutekeleza majukumu hayo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa kubaini changamoto kadhaa kama vile:

Mradi unaopendekezwa wa kuzalisha umeme wa maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje umechelewa kuanza kutokana na uhaba wa fedha. Mradi huo unakadiriwa kuwa wa shilingi bilioni 20.02 ukilenga kuzalisha na kusambaza umeme katika vijiji 43 vya kata 10 za Ileje Mashariki na kuiuzia TANESCO umeme wa ziada chini ya mkataba wa kuuziana umeme.

Aidha, DCB Commercial Bank Plc, iliyoanzishwa kama taasisi ya mikopo midogo midogo mnamo mwezi Aprili 2002, inamilikiwa na taasisi za serikali, huku Halmashauri za Dar es Salaam zikimiliki asilimia 33 ya mtaji wote, huku mamlaka nyingine za serikali zikimiliki

asilimia 31, hivyo kufanya umiliki wa serikali kwa ujumla kuwa asilimia 64. Hata hivyo, benki hiyo haijawahi kuwasilisha taarifa za fedha ofisini kwangu kwa ukaguzi kama inavyotakiwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba na Kifungu cha 9(a) iii & iv cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008.

Pia, nimebaini kuwapo miradi miwili iliyokamilika inayohusiana na usindikaji wa mazao ya nyuki yenye thamani ya shilingi bilioni 1.36 katika Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge na Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo. Hata hivyo, miradi hiyo haijaanza kutumika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa watumishi wenye ujuzi wa kuendesha mitambo hiyo na kutokuwa na mikataba iliyosainiwa kati ya viwanda na vyama vya ushirika vya wafugaji nyuki kwa ajili ya upatikanaji wa asali.

### Sekretarieti za Mikoa

Katika tathmini ya ununuzi na mali katika Sekretarieti za Mikoa nimebaini kwa Sekretarieti za mikoa 15 zililipa shilingi bilioni 4.95 kwa GPSA kwa ajili ya ununuzi wa magari, lakini hadi kufikia mwezi Desemba 2022, magari hayo yalikuwa hayajawasilishwa kwa taasisi zao. Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu iliagiza na kupokea gari aina ya Nissan Patrol GRX 61 yenye thamani ya shilingi milioni 188.67 kutoka GPSA, lakini ilitelekezwa kwenye karakana kutokana na ubovu wa injini.

Aidhanilibaini kuwa Sekretarieti nne zilifanya malipo ya shilingi bilioni 1.02 kwa mabadiliko ya kazi ambayo hayakuidhinishwa.

Pia, nilibaini kuwa sekretarieti nne zilitumia shilingi milioni 71.95 kwa matumizi yasio na tija wakati sekretarieti 10 zililipa shilingi milioni 768.14 kwa wazabuni bila nyaraka toshelevu, hivyo, sikuweza kuthibitisha uhalisia wake.

Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza ilinunua vifaa vya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa shilingi milioni 233.46 lakini vifaa hivyo vilitelekezwa kwenye eneo kutokana na kusitishwa kwa ujenzi wa uwanja huo tangu mwezi Juni 2022. Hii ilitokana na kutokuwepo kwa mipango na michoro iliyoidhinishwa na TAA na kutoshirikishwa kwa washikadau wakuu katika uanzishwaji wake hali iliyosababisha kurekebishwa mara kwa mara kwa miundo ya majengo.

## Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Katika ukaguzi wangu wa OR-TAMISEMI na Taasisi zinazofanya kazi chini ya Wizara, nilibaini mambo kadhaa kama ifuatavyo:-

Katika OR-TAMISEMI, nilibaini kuwa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 20.29 ilitekelezwa na wakandarasi ambao dhamana zao za utendaji kazi zilikuwa zimeisha. Zaidi ya hayo, malipo ya awali ya shilingi bilioni 1.83 yaliyofanywa kwa mkandarasi hayakurejeshwa, wakati dhamana ilikuwa imeisha muda wake hadi kufikia tarehe ya ukaguzi huu.

Aidha, Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi (DART) ilikuwa na ongezeko kubwa la madeni ambayo hayajakusanywa, ambayo yalipanda kutoka shilingi bilioni 4.17 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 8.45 mwaka 2021/22. Pia DART ilifanya malipo ya shilingi milioni 135.82 kwa wauzaji mbalimbali waliotoa risiti feki za EFD.

Katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), nilibaini Bodi hiyo kuwa na ugumu wa kutekeleza makubaliano yake na wakopaji hivyo kushindwa kukusanya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.35.

Aidha, kwa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), nilibaini udhaifu katika usimamizi wa miradi, ikiwa ni pamoja na kutelekezwa kwa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 3.86, kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya barabara yenye thamani ya shilingi bilioni 28.43, na kutozingatiwa kwa athari za tetemeko la ardhi katika usanifu wa muundo wa daraja lenye thamani ya shilingi bilioni 7.9 lililojengwa Berega-Kilosa, Morogoro.

## Matokeo ya Ukaguzi Maalum

Nilifanya kaguzi mbili maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na Halmashauri ya Jiji la Arusha, na kubaini kasoro kadhaa. katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, nilibaini kuwa jumla ya leseni 596 zilitolewa kwa wafanyabiashara lakini kiasi kilichokusanywa cha shilingi milioni 45.99 hakikuwekwa kwenye akaunti ya benki ya Halmashauri.

Aidha katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, kama ilivyoombwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim

Majaliwa (Mb). Nilifanya ukaguzi katika mambo mbalimbali ya uendeshaji wa Halmashauri, ikiwa ni pamoja na usimamizi na utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo, ufuataji wa sheria na kanuni za manunuzi, miamala ya fedha taslimu, maandalizi ya bajeti, ukusanyaji wa kodi na mapato, Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, kuhakiki madeni ya wakandarasi, uhamisho wa wafanyakazi pamoja, na uendeshaji wa kampuni ya Arusha Meat Company.

Matokeo ya ukaguzi huo yamewasilishwa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na mamlaka nyingine zinazohusika kwa hatua zaidi. Hata hivyo, kwa kuwa uchunguzi unaendelea, matokeo na mapendekezo ya ukaguzi huo hayajajumuishwa katika ripoti hii.




# SURA YA KWANZA

## MAELEZO YA AWALI

### 1.0 Utangulizi

Taarifa hii imeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 34(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 na inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa Taarifa za Fedha kwa taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zikiwemo Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022.

Taarifa hii inatoa muhtasari wa matokeo ya kaguzi zilizofanyika kwa mwaka fedha 2021/22, ambazo zilijikita katika kudhihirisha kuwa taratibu za usimamizi wa fedha zinazingatia sheria na kanuni husika; na kwamba taarifa za fedha zilitayarishwa kwa usahihi kwa mujibu wa Mfumo wa Taarifa za fedha unaotumika.

### 1.1 Mamlaka ya Kufanya Ukaguzi

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (pamoja na marekebisho yake) na Kifungu cha 20 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amepewa mamlaka ya kukagua hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge na hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT), angalau mara moja kwa mwaka,.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia anapaswa kuwasilisha taarifa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ataziwasilisha mbele ya Bunge kwa utaratibu uliowekwa chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 34 (2) cha

Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Chini ya Kanuni ya 88 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, ripoti hizi huwasilishwa kwa Rais kabla ya au ifikapo tarehe 31 Machi kila mwaka, ambapo baada ya kupokea taarifa hizo, Rais huagiza taarifa hizo kuwasilishwa Bungeni ndani ya kipindi cha siku saba za kikao cha kwanza cha Bunge.

Baadaye ripoti hiyo hujadiliwa na Kamati za Kudumu za Bunge ambazo ni Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa niaba ya Bunge, na ripoti ya matokeo hayo kuwasilishwa Bungeni.

Aidha, Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma (PPA), 2011 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2016), kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesau za Serikali kujumuisha katika ripoti zake taarifa ya kiwango cha uzingatiaji wa Sheria ya ununuzi wa Umma.

## 1.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ripoti hii inatoa muhtasari wa matokeo na mapendekezo yanayotokana kaguzi zilizofanywa katika taasisi 218 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Taasisi zilizokaguliwa ni pamoja na Fungu 56, ambayo ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, pamoja na taasisi saba zilizo chini yake ambazo ni Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi (DART), Chuo cha Mafunzo ya Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI), Mfuko wa Barabara chini ya TAMISEMI, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB), Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Jumuiya ya Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT), na Fungu namba mbili ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Pia, ukaguzi ulihusisha Sekretarieti 26 za Tawala za Mikoa pamoja na Serikali za Mitaa 184, hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizokaguliwa kuwa 218.

Kama sehemu ya ukaguzi, nilitathmini ufanisi wa mifumo ya uhasibu wa fedha na udhibiti wa ndani, ukaguzi na uhakiki wa taarifa za fedha za mwaka, ripoti za utendaji na taratibu nyingine za kiukaguzi ambazo zilihitajika kufikia hitimisho la ukaguzi. Ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia maeneo hatarishi ili kuhakikisha kuwa mawanda ya ukaguzi yanatosheleza kutoa hati za ukaguzi.

Ni muhimu kutambua kwamba matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yanatokana na nyaraka na taarifa zilizoombwa na kutolewa kwangu kwa ajili ya ukaguzi.

## 1.3 Viwango vya Ukaguzi Vinavyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) na Shirika la Afrika la Taasisi Kuu za Ukaguzi za Nchi zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E).

Kutokana na uanachama wetu, taratibu za ukaguzi zilizotumika zinawiana na Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) iliyotolewa na INTOSAI.

Hii inahakikisha kuwa ukaguzi ulifanywa kwa kuzingatia viwango na miongozo ya ukaguzi inayotambulika duniani, ambayo husaidia kuziamini kazi za ukaguzi.

## 1.4 Mbinu zilizotumika kufanya Ukaguzi

Ukaguzi wangu ulihusisha kufanya majaribio kwenye taarifa za hesabu na kutekeleza taratibu mbalimbali ili kufikia malengo ya ukaguzi. Taratibu za ukaguzi zilizofanyika ni kama ifuatavyo;

- Kupanga ukaguzi ili kutambua na kutathmini hatari za makosa ya kihesabu ya kawaida au yanatokana na udanganyifu, kwa kuzingatia uelewa wa kina wa taasisi zilizokaguliwa na mazingira yao, ikiwa ni pamoja na tathmini ya udhibiti wa mifumo ya ndani.

- Kupata ushahidi wa kutosha na unaofaa wa ukaguzi kuhusu makosa ya kimahesabu, makosa yaliyopo kwa kubuni na kutekeleza njia sahihi za kukabiliana na hatari zilizoainishwa.

- Kuhakikisha utekelezaji wa matokeo ya ukaguzi wa mwaka uliopita, mapendekezo, na maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ili kubainisha iwapo hatua stahiki zimechukuliwa kuhusu masuala yote yaliyojitokeza.

Mchakato wa ukaguzi ulikuwa shirikishi, ambapo taasisi iliyokaguliwa hushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa ukaguzi. Ukaguzi

shirikishi hujumuisha maofisa masuuli, maafisa wakuu wa usimamizi, kamati za ukaguzi na vitengo vya ukaguzi wa ndani, kwa kuwa tunaamini kuwa wako katika nafasi nzuri ya kutoa majibu yanayofaa kuhusu usahihi wa taarifa za fedha na nyaraka nyingine muhimu wakati wa ukaguzi, ikiwa ni pamoja na kufuata sheria na kanuni zinazotumika.

## 1.5 Majukumu ya Taasisi Zinazokaguliwa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 43 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 (Iliyokerekebishwa 2019] na Kifungu cha 30 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Maafisa Masuuli wanapaswa kutengeneza taarifa za hesabu za mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali kwa ajili ya ukaguzi kila ifikapo tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha.

Aidha, Agizo hilo pia linaagiza Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia sheria, kanuni, na miongozo inayotolewa na Wizara husika, Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 na Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa kwa Taasisi za Umma (IPSAS).

## 1.6 Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Madhumuni ya ukaguzi wangu ni mawili. Kwanza, kutoa maoni huru kuhusu taarifa za fedha za taasisi za serikali zinazo wasilishwa kwa kwa mujibu wa viwango vinavyotumika kwenye uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Taasisi za Umma (IPSAS). Pili, kujiridhisha iwapo taarifa za fedha hazikuwa na makosa ya kimahesabu au yatokanyo na ubadhirifu.

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba pamoja na kujiridhisha, ukaguzi hauwezi kuthibitisha uvumbuzi wa dosari zenye madhara yatokanayo na ubadhirifu au makosa. Taarifa zenye dosari zinaweza kuathiri maamuzi ya kiuchumi ya mtumiaji wa taarifa za fedha. Aidha hatari ya kutotambua makosa yatokanayo na ubadhirifu ni kubwa kuliko yale yanayotokana na makosa.

Aidha, nilitathmini pia kama sheria na kanuni zinazotumika zimefuatwa na kama Maafisa Masuuli wametekeleza njia sahihi za udhibiti wa mifumo ya ndani ili kuzuia au kugundua makosa ya kimahesabu.

# SURA YA PILI




# HATI ZA UKAGUZI

## 2.0 Utangulizi

Hati ya ukaguzi hupatikana kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho yatokanayo na ushahidi wa kikaguzi katika kuhakikisha kuwa taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (IPSAS). Hati ya ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Kiwango cha 1200 cha Kimataifa cha Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI 1200).

Hili linafanikiwa na kufikiwa kwa kuandaa na kufanya ukaguzi kwa namna ambayo itamuwezesha Mkaguzi kujiridhisha kuhusu tathmini ya matokeo dhidi ya kiwango cha juu kisichohimilika (Materiality) kilichowekwa.

## 2.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Mkaguzi hutoa hati inayoridhisha au hati zenye kasoro, hati hizi zinaelezewa kama ifuatavyo.

a) **Hati Inayoridhisha** – Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaporidhika kuwa taarifa za fedha alizokagua zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango kubalifu vya kimataifa vinavyohusu uandaaji wa taarifa za fedha.

b) **Hati isiyoridhisha -** Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anapobainisha mapungufu kwa kiwango kisichoridhisha katika taarifa za fedha, au Mkaguzi kushindwa kupata ushahidi wa kutosha kuthibitisha hati husika. Kuna aina tatu za kasoro zitolewazo katika hati za ukaguzi kama zinavyoelezewa hapa chini:

i. **Hati yenye shaka** – Hati hii hutolewa pale taarifa za fedha zinapokuwa zimetayarishwa kwa usahihi isipokuwa kwa athari ya jambo/mambo yafuatayo:

- Pale ambapo Mkaguzi amepata ushahidi wa kutosha wakati wa ukaguzi, akahitimisha kuwa kulikuwa na dosari ama katika eneo moja au kwa ujumla wake, zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika ingawa hazikuathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha kwa ujumla wake kiasi cha kushindwa kutumika katika kufanyia maamuzi.

- Pale ambapo Mkaguzi ameshindwa kupata ushahidi wa kutosha kumwezesha kutoa maoni ya ukaguzi, lakini akahitimisha kwamba dosari zilizotokana na kukosa ushahidi zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika lakini haziathiri taarifa za fedha kwa ujumla wake, kiasi cha kushindwa kutumika katika kufanya maamuzi.

ii. **Hati Mbaya -** Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kulingana na ushahidi wa kutosha wa kikaguzi kuwa, dosari zilizobainika katika eneo moja au kwa ujumla wake, zimeathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha, hivyo kupelekea taarifa hizo kutokuwa sahihi.

iii. **Kushindwa Kutoa Maoni** – Hali hii hutokea pale ambapo nimeshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu zinazoniwezesha kufikia malengo ya ukaguzi, na endapo madhara ya kushindwa kupata ushahidi au nyaraka hizo ni makubwa sana. Hivyo, kuhitimisha kwamba athari zinazoweza kutokea za dosari zisizogundulika za taarifa za fedha, zinaweza kuwa zimezidi kiwango cha juu kisichohimilika na zinaathiri taarifa za fedha kwa ujumla wake kiasi cha kushindwa kutumika katika kufanya maamuzi.

Mkaguzi atashindwa kutoa maoni, katika hali nadra sana inayohusisha kutokuwa na uhakika wa kutosha, atahitimisha kwamba, ingawa amepata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi kuhusu kila hali, haiwezekani kutoa maoni juu ya taarifa za fedha kwa sababu ya kutokuwa na uhakika na uwezekano wa athari zake katika taarifa za fedha.

## 2.2 Aya ya Masuala ya Msisitizo katika Taarifa ya Ukaguzi

Nikiona ni muhimu kutoa angalizo kwa watumiaji kuhusu suala lililowasilishwa au kuelezwa katika taarifa za fedha ambalo, kwa maoni yangu, ni la muhimu na la msingi sana kwa uelewa wa watumiaji wa taarifa za fedha, nitajumuisha aya ya masuala ya msisitizo katika taarifa yangu ya ukaguzi ilimradi nimepata ushahidi wa kutosha kwamba suala hilo halijaripotiwa kimakosa katika taarifa za fedha. Aya hiyo inarejea masuala yaliyooneshwa katika taarifa za fedha.

## 2.3 Masuala Muhimu ya Ukaguzi

Aya hii hutoa taarifa za ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia katika kuelewa masuala ambayo, kwa maoni ya uweledi wangu, yalikuwa na umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha za taasisi husika.

Kubainisha masuala muhimu ya ukaguzi huongeza thamani ya taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa kuonesha uwazi zaidi kuhusu ukaguzi nilioufanya.

## 2.4 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka Unaohusika

Katika mwaka wa fedha 2021/22, hati 218 zimetolewa kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kati ya hizo, 204 ni hati zinazoridhisha, hati 13 zenye shaka, hati mbaya moja na hakuna niliposhindwa kutoa maoni.

Aidha, mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Taasisi nane chini ya OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2018/19 hadi 2021/22 ni kama kwenye **Jedwali Na.2-1 na Kiambatisho Na.1- 1.**

**Jedwali Na.2-1: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi**

| Mwaka | Taasisi | Aina ya Hati | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Hati inayoridhisha | Hati yenye Shaka | Hati Mbaya | Kushindwa Kutoa Maoni | |
| 2021/22 | Mamlaka za Serikali za Mitaa | 170 | 13 | 1 | 0 | 184 |
| | Sekretarieti za Mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | 26 |

| Mwaka | Taasisi | Aina ya Hati | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Hati inayoridhisha | Hati yenye Shaka | Hati Mbaya | Kushindwa Kutoa Maoni | |
| | OR-TAMISEMI | 8 | 0 | 0 | 0 | 8 |
| **Jumla** | | 204 | 13 | 1 | 0 | 218 |
| | | | | | | |
| 2020/21 | Mamlaka za Serikali za Mitaa | 176 | 8 | 1 | 0 | **185** |
| | Sekretarieti za Mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | OR-TAMISEMI | 7 | 1 | 0 | 0 | **8** |
| **Jumla** | | **209** | **209** | **9** | **1** | **0** |
| | | | | | | |
| 2019/20 | Mamlaka za Serikali za Mitaa | 120 | 53 | 12 | 0 | **185** |
| | Sekretarieti za Mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | OR-TAMISEMI | 7 | 1 | 0 | 0 | **8** |
| **Jumla** | | **153** | **153** | **54** | **12** | **0** |
| | | | | | | |
| 2018/19 | Mamlaka za Serikali za Mitaa | 176 | 9 | 0 | 0 | **185** |
| | Sekretarieti za Mikoa | 26 | 0 | 0 | 0 | **26** |
| | **OR-TAMISEMI** | 7 | 0 | 0 | 0 | **7** |
| **Jumla** | | **209** | **9** | **0** | **0** | **218** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa*



# SURA YA TATU

## UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI YA MIAKA ILIYOPITA

### 3.0 Utangulizi

Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 kinanitaka kujumuisha katika Ripoti ya Mwaka ya Ukaguzi, hali ya utekelezaji wa wa mpango mkakati juu ya hoja na mapendekezo iliyoandaliwa na Maafisa Masuuli na kuunganishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG).

Ili kukidhi matakwa haya ya sheria, hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa mapendekezo yangu na maagizo ya Kamati za Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Serikali za Mitaa (LAAC) yanajadiliwa katika sura hii.

Ili kuhakikisha kunakuwepo na mfumo wa udhibiti wa ndani ulio thabiti, OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kutathmini na kuchukua hatua zinazofaa kushughulikia matokeo ya ukaguzi yaliobainishwa katika taarifa yangu pamoja na mapendekezo yake kwa wakati muafaka.

Aidha, kama sehemu ya majukumu yake ya usimamizi, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) hufanya vikao na ufuatiliaji kila mara ili kubaini, pamoja na mambo mengine, kama Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuuli wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanachukua hatua stahiki katika kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya Kamati hizo.

Ninatambua juhudi za Kamati za Bunge za usimamizi katika kuchukua hatua stahiki juu ya mapendekezo ninayoyatoa katika ripoti yangu, hali inayoleta manufaa makubwa kwa umma.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa miaka iliyopita, pamoja na maagizo ya PAC na LAAC imechambuliwa kama ifuatavyo:

## 3.1 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2020/21

Kwa mujibu wa Kanuni ya 93 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009 (GN Na. 47/2009), kila Afisa Masuuli wa taasisi iliyokaguliwa anatakiwa kuandaa majibu ya Ripoti yake ya Ukaguzi na kuiwasilisha ndani ya kipindi cha siku 21 tangu tarehe ambayo ripoti kuu imewasilishwa Bungeni.

Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa awali kwa OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi zilizo chini ya OR-TAMISEMI umefupishwa katika **Jedwali 3-1** na kuelezwa kwa kina katika **Kiambatisho 3-1.**

**Jedwali Na.3-1: Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka Iliyopita**

| Hali ya Mapendekezo | OR-TAMISEMI | | Sekretarieti za Mikoa | | Halmashauri | | Jumla ya mapendekezo | % |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | idadi ya mapendekezo | % | idadi ya mapendekezo | % | idadi ya mapendekezo | % | | |
| Mapendekezo yaliyotekelezwa | 102 | 36 | 415 | 45 | 4,408 | 41 | 4,925 | 42 |
| Utekelezaji unaendelea | 91 | 33 | 248 | 27 | 3,349 | 32 | 3,688 | 31 |
| Mapendekezo hayajatekelezwa | 45 | 16 | 106 | 12 | 960 | 9 | 1,111 | 9 |
| Mapendekezo yamerudiwa | 15 | 5 | 124 | 14 | 1566 | 15 | 1,705 | 15 |
| Mapendekezo yamefutwa kutokana na kupitwa na wakati | 27 | 10 | 22 | 2 | 342 | 3 | 391 | 3 |
| **Jumla** | **280** | **100** | **915** | **100** | **10,625** | **100** | **11,820** | **100** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya ukaguzi kwa mwaka 2021/22*

Kushindwa kutekeleza mapendekezo yangu kunasababisha kujirudia kwa hoja zinazofanana na hizo, na hivyo kuchangia utendaji kazi duni na usio na tija, jambo ambalo lina athiri utoaji wa huduma kwa umma.

**Hivyo, ninasisitiza Maafisa Masuuli wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kurekebisha mapungufu katika kutekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi, ili kuimarisha utendaji kazi na kutoa huduma bora zenye kuzingatia masilahi ya umma.**

## 3.2 Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC)

Kifungu cha 38(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maofisa Masuuli kuzingatia maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusiana na masuala ya usimamizi wa fedha kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa na Bunge.

### 3.2.1 Utekelezaji wa Maagizo ya LAAC

Tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya LAAC hadi mwaka wa fedha 2021/22 ilibaini kuwa, kati ya maagizo 892 yaliyotolewa na Kamati kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, maagizo 228 (26%) yalitekelezwa; maagizo 399 (45%) yapo katika utekelezaji; na maagizo 245 (27%) hayajatekelezwa kabisa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 3-2** na **Kiambatisho 3-2**.

**Jedwali Na. 3-2:** Utekelezaji wa Maagizo ya LAAC

| Hatua ya Utekelezaji | Idadi ya Maagizo | % |
|---|---|---|
| Mapendekezo yaliyotekelezwa | 228 | 26 |
| Mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaendelea | 399 | 45 |
| Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa | 245 | 27 |
| Mapendekezo ambayo yamefutwa kutokana na kupitwa na wakati | 20 | 2 |
| **Jumla** | 892 | **100** |

**Chanzo**: *Taarifa ya ukaguzi kwa Mwaka 2021/22*

Pia nilibaini kulikuwa na maagizo 159 dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 36 ambayo hayajatekelezwa kwa miaka mitano hadi 13 iliyopita kama inavyoonekana katika **Jedwali 3-3.**

**Jedwali Na. 3-3:** Mamlaka za Serikali za Mitaa Zenye Maagizo ya Muda Mrefu

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miaka | Idadi ya Maagizo | Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miaka | Idadi ya Maagizo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Ileje | 13 | 6 | 19. | H/W Iramba | 7 | 6 |
| 2. | H/W Bahi | 12 | 3 | 20. | H/jiji Tanga | 7 | 15 |
| 3. | H/W Muheza | 12 | 8 | 21. | H/W Mbozi | 7 | 1 |
| 4. | H/W Biharamulo | 11 | 2 | 22. | H/W Lushoto | 7 | 5 |
| 5. | H/M Tabora | 10 | 7 | 23. | H/W Bukoba | 7 | 2 |
| 6. | H/W Pangani | 10 | 11 | 24. | H/W Geita | 6 | 1 |
| 7. | H/W Sikonge | 10 | 7 | 25. | H/W Kibondo | 6 | 8 |
| 8. | H/W Bagamoyo | 10 | 2 | 26. | H/W Maswa | 6 | 1 |
| 9. | H/W Handeni | 10 | 5 | 27. | H/jiji Dar Es Salaam | 6 | 1 |
| 10. | H/W Kilindi | 10 | 8 | 28. | H/W Bukombe | 6 | 3 |
| 11. | H/M Iringa | 9 | 6 | 29. | H/W Nanyumbu | 6 | 3 |
| 12. | H/W Iringa | 8 | 3 | 30. | H/W Itigi | 5 | 2 |
| 13. | H/M Temeke | 8 | 7 | 31. | H/W Buchosa | 5 | 7 |
| 14. | H/W Manyoni | 8 | 1 | 32. | H/W Igunga | 5 | 2 |
| 15. | H/W Ukerewe | 8 | 4 | 33. | H/W Nzega | 5 | 3 |
| 16. | H/W Rorya | 8 | 1 | 34. | H/W Rungwe | 5 | 1 |
| 17. | H/W Namtumbo | 7 | 6 | 35. | H/M Ilemela | 5 | 1 |
| 18. | H/W Kaliua | 7 | 8 | 36. | H/W Same | 5 | 2 |
| **Jumla** | | | | | | | **159** |

**Chanzo**: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2021/22*

### 3.2.2 Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC)

Majukumu ya Kamati yameelezwa kwa kina chini ya Agizo la 14 la Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la nyongeza la nane (Juni 2020), na hivyo taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni nyenzo muhimu kwa Kamati kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake kiufanisi.

Katika tathmini ya utekelezaji wa maagizo ya PAC kwa OR-TAMISEMI na Sekretarieti za Mikoa hadi kufikia mwaka wa fedha 2021/22, nimebaini kuwa, kati ya maagizo 102 yaliyotolewa katika ripoti zangu za miaka ya nyuma, maagizo 62 (60%) yalitekelezwa kikamilifu, 23 (23%) yapo katika utekelezaji, maagizo 12 (12%) hayakutekelezwa, wakati maagizo matano (5%) yalipitwa na wakati. Utekelezaji wa maagizo ya PAC umeoneshwa katika **Jedwali 3-4** na kuelezewa kwa kina katika **Kiambatisho 3-3.**

**Jedwali Na.3-4: Utekelezaji wa Maagizo ya PAC**

| Hatua ya Utekelezaji | Idadi ya Maagizo | % |
|---|---|---|
| Mapendekezo yaliyotekelezwa | 62 | 60 |
| Mapendekezo ambayo utekelezaji wake unaendelea | 23 | 23 |
| Mapendekezo ambayo hayajatekelezwa | 12 | 12 |
| Mapendekezo ambayo yamefutwa kutokana na kupitwa na wakati | 5 | 5 |
| **Jumla** | 102 | 100 |

**Chanzo**: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2021/22*

**Jedwali Na.3-5: Utekelezaji wa Maagizo ya PAC**

| Na. | Jina La Halmashauri | Mapendekezo yaliyo tekelezwa | Utekelezaji unaendelea | Mapendekezo haya jatekele zwa | Mapendekezo yamefutwa kutokana na kupitwa na wakati | Mapendekezo yaliyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Sekretarieti za Mikoa** | | | | | | |
| 1 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma | 9 | - | 9 | - | - |
| 2 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 6 | 5 | | | 1 |
| 3 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 6 | 5 | | | 1 |
| 4 | Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga | 6 | 6 | 0 | - | - |
| 5 | Sekretarieti ya Mkoa wa Singida | 6 | 4 | 2 | - | - |
| 6 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar Es Salaam | 5 | 1 | 4 | | |
| 7 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | 5 | 5 | 0 | | - |
| 8 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 5 | 3 | | 1 | 1 |
| 9 | Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara | 5 | 3 | 2 | | |
| 10 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mbeya | 5 | 5 | 0 | - | - |
| 11 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu | 5 | 5 | | | |
| 12 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | 4 | | 1 | 2 | 1 |
| 13 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | 4 | 1 | 2 | 1 | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | 4 | 2 | | 2 | |
| 15 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | 3 | 2 | 1 | - | - |
| 16 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | 3 | | | 3 | |
| 17 | Sekretarieti ya Mkoa wa Songwe | 3 | 2 | 0 | 1 | - |
| 18 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | 2 | 2 | 0 | - | - |
| 19 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | 1 | - | 1 | - | - |
| **Jumla Ndogo(Sekretarieti za Mikoa)** | | **87** | **51** | **22** | **10** | **4** |
| **OR-TAMISEMI** | | | | | | |
| 1 | Wizara-OR-TAMISEMI | 7 | 5 | 1 | - | 1 |
| 2 | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) | 7 | 5 | 0 | 2 | - |
| 3 | Wakala wa mabasi yaendayo kwa kasi Dar (DART) | 1 | 1 | | | |
| Jumla ndogo(OR-TAMISEMI) | | 15 | 11 | 1 | 2 | 1 |
| Jumla kuu | | 102 | 62 | 23 | 12 | 5 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya ukaguzi kwa Mwaka 2021/22*

Pia nilibaini Sekretarieti za mikoa nane zilikuwa na maagizo 22 ya muda mrefu ambayo bado hayajatekelezwa huku yakiwa yamesalia kwa miaka sita hadi 10 bila kutekelezwa kama inavyoonekana katika **Jedwali 3-6.**

**Jedwali Na.3-6: Sekretarieti za Mikoa Zenye Maagizo ya Muda Mrefu**

| Na. | Jina La Halmashauei | Idadi ya Miaka | Idadi ya Maagizo |
|---|---|---|---|
| 1. | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | 6 | 3 |
| 2. | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | 7 | 1 |
| 3. | Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma | 10 | 9 |
| 4. | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 7 | 1 |
| 5. | Sekretarieti ya Mkoa wa Manyara | 7 | 2 |
| 6. | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | 9 | 3 |
| 7. | Sekretarieti ya Mkoa wa Singida | 6 | 2 |
| 8. | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | 7 | 1 |
| **Jumla** | | | **22** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2021/22*

kutotekelezwa kwa maagizo ya PAC na LAAC kwa wakati kunaashiria kuwa, kasoro zilizobainika hazikushughulikiwa ipasavyo.Pia, kuna uwezekano wa taasisi husika kuendelea kuwa na makosa yanayotokana na udanganyifu, ukosefu wa ufanisi na kushindwa kutoa matokeo yanayotarajiwa.

**Kwa hali hiyo, OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zihakikishe kuwa zinatekeleza maagizo ya Kamati ambayo hayakukamilika, huku zikishughulikia chanzo cha mapungufu yaliyobainika na kuzuia mapungufu kama hayo kujirudia mbeleni.**




# SURA YA NNE

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha tathmini ya bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Sekretarieti za Mikoa(OR-TAMISEMI) na taasisi zake, na Mamlaka za Serikali za Mitaa itokanayo na ukusanyaji wa mapato kwa vyanzo vya ndani, ruzuku kutoka Serikali Kuu, dhidi ya makadirio, mwenendo wake na uchunguzi wa jumla wa makadirio na makusanyo kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2022.

Kulingana na kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa 2019) kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kupitisha bajeti ya makadirio ikionesha kiasi cha mapato kinachotarajiwa kupokelewa; kiasi kinachotarajiwa kutolewa na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika;.

Vilevile, Kifungu cha 45 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 (iliyorekebishwa 2020) kinamtaka Afisa Masuuli kusimamia matumizi ya serikali kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina kama ilivyobainishwa katika sheria. Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 ilikuwa awamu ya awali ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambao uliweka kipaumbele katika kukuza uchumi shirikishi na shindani, kuongeza ukuaji wa viwanda na huduma za uongezaji thamani wa kilimo, kuhimiza uwekezaji na biashara, kuweka kipaumbele kwa maendeleo ya watu, na kuhamamsiha maendeleo ya ujuzi.

Janga la UVIKO-19 lilisababisha kupungua kwa utoaji wa huduma, akiba ya fedha ya kigeni na ukuaji wa uchumi hali iliyoilazimu serikali kupata mkopo wa ruzuku wa dola za Marekani 567.25 sawa na shilingi trilioni

1.29 kupitia Mpango wa Mkopo wa Haraka (RCF) kwa lengo la kupunguza athari za UVIKO-19kwa kutenga fedha kwa sekta zilizoathirika zaidi na janga hili.

## 4.1 Mapitio ya Bajeti

Nilifanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 kwa lengo la kutathmini kama OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaendana na Sera ya Bajeti ya Serikali, Taarifa ya Mfumo wa Fedha, na Sheria ya Bajeti ya Fedha. Pia kujiridhisha kama bajeti zilizoidhinishwa zinakidhi matakwa ya kifungu cha 46 (1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, [Sura ya 290 Iliyorekebishwa 2019].

Yafuatayo yamebainishwa katika mapitio ya bajeti ya mapato na matumizi ya OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/22:

## 4.2 Uchambuzi na Tathmini ya Mwenendo wa Bajeti za OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa

### 4.2.1 Mwenendo wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa dhidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Miongoni mwa vipaumbele vya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni ukusanyaji wa mapato ya ndani. Katika kufanikisha hili, Serikali imeboresha mazingira ya biashara kwa walipakodi ikiwa ni pamoja na maelewano, juu ya ufutwaji au punguzo la viwango vya kodi, tozo na ada zenye kero. Pia kuboresha usimamizi wa kodi katika ngazi ya serikali za mitaa kwa kusisitiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA na kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo wa Serikali (GePG) ambapo taasisi zote zitatakiwa kutumia mfumo wa GePG.

Mchanganuo wa taarifa za fedha zilizowasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 ulionyesha makusanyo ya mapato ya yanayotokana na vyanzo vya ndani kwa mwaka wa fedha 2021/22 yalikuwa shilingi bilioni 891.84 ambayo ni asilimia 102 ya makadirio ya bajeti ya shilingi bilioni 873.9.

Ulinganisho kati ya makusanyo ya mwaka wa fedha 2020/21 ya shilingi bilioni 769.42 dhidi ya shilingi bilioni 891.84 kwa mwaka huu nilibaini

ongezeko la shilingi bilioni 122.41 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4-1 na Kiambatisho. 4-1.**

**Jedwali Na.4-1: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani Ikilinganishwa na Bajeti**

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Makusanyo Pungufu (Sh.) | % (Tofauti/Bajeti) |
|---|---|---|---|---|
| 2021/22 | 873,898,493,691 | 891,836,133,308 | 17,937,639,617 | 2 |
| 2020/21 | 822,375,950,562 | 769,422,329,061 | (52,953,621,501) | (6) |
| 2019/20 | 759,907,423,938 | 709,573,567,541 | (50,333,856,397) | (7) |
| 2018/19 | 725,633,451,671 | 639,401,151,405 | (86,232,300,266) | (11) |
| 2017/18 | 677,965,549,714 | 566,729,291,189 | (111,236,258,525) | (16) |

Ingawa kumekuwa na mwelekeo chanya katika ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ni muhimu kuhakikisha kuwa vyanzo vyote vya mapato vilivo ibuliwa vinatumika kikamilifu ili kufikia malengo zaidi.

**Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kubuni mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya mapato vya ndani vilivyopo na kuibua vyanzo vipya ndani ya maeneo yao ya mamlaka. Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuandaa makadirio halisi na yenye tija ili kuziwezesha kufikia viwango vya juu vya ukusanyaji wa mapato.**

### 4.2.2 Tathmini ya Jumla ya Vyanzo vya Ndani vya Mapato

**a) Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa**

Katika tathmini ya bajeti ya shilingi bilioni 413.87 iliyoidhinishwa kwa Mamlaka 102 za Serikali za Mitaa, nilibaini kuwa mamlaka hizo zilikusanya mapato halisi ya shilingi bilioni 479.40 ikiashiria mafanikio ya ukusanyaji kwa asilimia 116 ya mapato yaliyokadiriwa kukusanywa na mamlaka hizo. Aidha, ulinganisho wa ukusanyaji wa mapato halisi yaliyokusanywa mwaka uliopita 2020/21 ni asilimia 109 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4-2 na Kiambatisho Na. 4- 2.**

**Jedwali Na.4-2:** Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato Zaidi ya Bajeti

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Tofauti (Sh.) | % ya utekelezaji halisia | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2021/22 | 413,871,167,926 | 479,401,407,535 | 65,530,239,610 | 116 | 100 |
| 2020/21 | 346,128,129,473 | 376,302,581,046 | 30,174,451,573 | 109 | 64 |
| 2019/20 | 315,579,839,663 | 363,859,170,229 | 48,279,330,566 | 115 | 62 |

**b) Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato chini ya Bajeti Iliyoidhinishwa**

Nilibaini kuwa Mamlaka 82 za Serikali za Mitaa zilipanga kukusanya mapato ya shilingi bilioni 460.03 kutoka vyanzo vya ndani vya mapato. Hata hivyo zilifanikiwa kukusanya mapato halisi ya shilingi bilioni 412.43; sawa na utekelezaji wa asilimia 90 ya makadirio ya mapato yote ikilinganishwa na asilimia 83 ya makusanyo ya mwaka uliopita 2020/21 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4-3 na Kiambatisho Na. 4- 3.**

**Jedwali Na.4-3:** Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato Chini ya Bajeti

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Tofauti (Sh.) | % ya utekelezajil halisi | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2021/22 | 460,027,325,765 | 412,434,725,772 | 47,592,599,993 | 90 | 82 |
| 2020/21 | 476,247,821,089 | 393,119,748,015 | 83,128,073,074 | 83 | 121 |
| 2019/20 | 442,034,532,275 | 343,421,345,312 | 98,613,186,963 | 78 | 123 |

Ni dhahiri kuwa Menejimenti hazikuchunguza kwa kina vyanzo vyote vya mapato ambavyo vingeweza kuchangia mapato ya kutosha kukidhi uendeshaji wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kukusanya mapato kikamilifu na kuibua vyanzo vipya ili kuhakikisha zinafikia malengo yaliyowekwa.**

### 4.2.3 Matumizi ya Kawaida ya Fedha za Ruzuku Kutoka Serikali Kuu

Makadirio yaliyoidhinishwa kwa ajili ya OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa 26, na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 katika mwaka wa fedha 2021/22 yalifikia shilingi trilioni 4.91 ikionyesha upungufu wa shilingi bilioni 436.25 ikilinganishwa na makadirio ya 2020/21 yaliyoidhinishwa ya shilingi trilioni 5.35.

Ukaguzi wa taarifa za fedha za OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa ulibaini kuwa shilingi trilioni 4.81 zilitolewa kama Ruzuku ya Kawaida ya Serikali kwa ajili ya matumizi, ikiwa ni asilimia 98 ya makadirio yaliyoidhinishwa ya shilingi trilioni 4.91 trilioni ikionyesha kuwa, shilingi bilioni 105.71 hazikutolewa.

Aidha, mapato ya ruzuku ya kawaida yaliongezeka kwa shilingi bilioni 46.15 ukilinganisha na shilingi trilioni 4.76 zilizotolewa mwaka wa 2020/21. Mwenendo wa miaka mitatu mfululizo wa makisio pamoja na kiasi halisi kilichopokelewa ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali 4-4** na **Kiambatisho 4-4**.

**Jedwali Na.4-4: Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Iliyopokelewa**

| Mwaka wa fedha | Bajeti Iliyoidhinishwa (Sh.) | Kiasi kilichotolewaa (Sh.) | Kiasi Pungufu (Sh.) | %(Tofauti/ Bajeti |
|---|---|---|---|---|
| 2021/22 | 4,912,836,455,163 | 4,807,125,959,060 | (105,710,496,103) | (2) |
| 2020/21 | 5,349,085,836,370 | 4,760,974,162,598 | (588,111,673,772) | (11) |
| 2019/20 | 5,289,377,847,806 | 4,551,253,607,566 | (738,124,240,240) | (14) |

Kulingana na mwenendo hapo juu, kumekuwa na ongezeko la utoaji wa fedha za matumizi ya ruzuku ya kawaida tangu mwaka wa fedha 2019/20.

### 4.2.4 Fedha za Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Zilizopokelewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ruzuku ya Maendeleo iliyoidhinishwa kwa OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa 26, na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184 kwa mwaka wa fedha 2021/22 Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali ilikuwa shilingi trilioni 3.34 ikiwa ni ongezeko la shilingi trilioni 1.74 (sawa na asilimia 109) ikilinganishwa na makadirio ya 2020/21 ya kiasi cha shilingi trilioni 1.6.

Mapitio ya taarifa za fedha za OR-TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa inaonesha shilingi trilioni 2.71 iliyotolewa kama ruzuku ya maendeleo ya Serikali ikiwa ni asilimia 81 ya makadirio yaliyoidhinishwa. Hivyo, shilingi bilioni 621.85 (sawa na asilimia 19 ya makadirio yaliyoidhinishwa) hazikutolewa.

Pia, ruzuku ya maendeleo kwa mwaka huu iliongezeka kwa shilingi trilioni 1.68 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.03 zilizotolewa mwaka 2020/21. Mwenendo wa bajeti ya ruzuku ya maendeleo na fedha halisi zilizopokelewa kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ilivyochambuliwa

katika **Jedwali 4-5 na Kiambatisho 4-5**.

**Jedwali Na.4-5:** Fedha za Ruzuku ya Maendeleo Zilizotolewa

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Kiasi halisi kilichotolewa (Sh.) | Kiasi Pungufu (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|
| 2021/22 | 3,336,433,680,816 | 2,714,583,117,025 | (621,850,563,791) | (19) |
| 2020/21 | 1,597,103,108,111 | 1,031,777,503,255 | (565,325,604,856) | (35) |
| 2019/20 | 1,516,298,099,316 | 907,147,459,961 | (609,150,639,355) | (40) |

***Chanzo**: Ripoti ya Jumla Iliyopita na taarifa za fedha za mwaka 2021/22*

Kwa mujibu wa **Jedwali 4-5**, makadirio ya matumizi ya ruzuku ya maendeleo ya Serikali yalizidi ya mwaka wa fedha 2020/21. Hata hivyo, ikiwa fedha kwa ajili ya shughuli za maendeleo hazitatolewa kwa wakati, inaweza kuwa na athari hasi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Kwa mfano, baadhi ya Halmashauri zinaweza kushindwa kutimiza wajibu wao wa kimkataba, hivyo kusababisha riba na adhabu ambazo zinaweza kuleta mzigo mkubwa wa madeni kwa Serikali.

## 4.3 Mapato ya Ndani ambayo Hayakutengwa kwa Ajili ya Miradi ya Maendeleo Shilingi Bilioni 22.37

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilitoa barua yenye kumbukumbu Na.CBD.421/422/01/43 ya tarehe 3 Januari, 2018 ambapo Halmashauri ziligawanywa katika makundi mawili “A” na “B na kuzielekeza kutenga asilimia 40 na asilimia 60 ya mapato ya vyanzo vyake vya ndani, mtawalia kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Pia, kipengele cha 143 (ii) cha mwongozo wa bajeti kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya mwaka 2021/22, kinazitaka Halmashauri kuimarisha makusanyo ya mapato ya vyanzo vyake na kuhakikisha kuwa asilimia arobaini (40%) ya vyanzo vya mapato yasivyolindwa zinatengwa na kutumika kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo.

Nilifanya tathmini ya kiasi cha fedha zilizotolewa na Halmashauri 184 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato katika tathimini hiyo nilbaini Halmashauri 76 hazikuchangia fedha za shughuli za maendeleo kulingana na asilimia iliyotakiwa. Kwa ujumla, Halmashauri hizi zilishindwa kutenga na kuchangia shilingi bilioni 22.37 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 4-6.**

**Jedwali Na.4-6: Fedha ya Mapato ya Ndani Ambazo Hazikupelekwa Katika Miradi ya Maendeleo**

| N/A | Jina La Halmashauri | Kiasi(Sh) | N/A | Jina La Halmashauri | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Mbeya | 2,711,670,042 | 39. | H/W Kasulu | 190,356,480 |
| 2. | H/M Ilemela | 1,297,226,325 | 40. | H/W Mkinga | 188,635,435 |
| 3. | H/Jiji Mwanza | 1,204,162,469 | 41. | H/W Nsimbo | 185,857,522 |
| 4. | H/W Nzega | 917,083,604 | 42. | H/W Mkalama | 179,596,487 |
| 5. | H/M Singida | 845,095,980 | 43. | H/W Buchosa | 172,757,104 |
| 6. | H/W Morogoro | 663,634,736 | 44. | H/M Moshi | 169,239,189 |
| 7. | H/W Mpanda | 641,527,445 | 45. | H/W Sumbawanga | 158,339,921 |
| 8. | H/W Kyela | 605,423,050 | 46. | H/W Magu | 157,065,352 |
| 9. | H/W Kaliua | 488,316,353 | 47. | H/W Rombo | 151,969,762 |
| 10. | H/W Makete | 479,551,868 | 48. | H/W Busokelo | 145,144,582 |
| 11. | H/W Shinyanga | 471,349,724 | 49. | H/W Butiama | 136,204,825 |
| 12. | H/W Songea | 463,371,905 | 50. | H/W Msalala | 133,506,277 |
| 13. | H/W Mufindi | 452,827,716 | 51. | H/W Rungwe | 133,115,572 |
| 14. | H/W Lindi | 418,488,506 | 52. | H/Mji Makambako | 130,755,253 |
| 15. | H/W Nkasi | 417,687,571 | 53. | H/W Igunga | 128,651,253 |
| 16. | H/W Serengeti | 381,326,457 | 54. | H/W Ushetu | 125,334,834 |
| 17. | H/M Bukoba | 344,929,742 | 55. | H/W Handeni | 121,438,131 |
| 18. | H/W Mbarali | 341,036,483 | 56. | H/W Iramba | 118,054,434 |
| 19. | H/W Kilindi | 340,101,182 | 57. | H/Mji Handeni | 106,481,052 |
| 20. | H/W Kalambo | 326,127,894 | 58. | H/W Mpimbwe | 104,760,561 |
| 21. | H/Mji Babati | 316,024,990 | 59. | H/W Buhigwe | 93,801,840 |
| 22. | H/W Bunda | 313,495,841 | 60. | H/W Kibiti | 93,465,906 |
| 23. | H/M Kigoma/Ujiji | 292,536,158 | 61. | H/W Lushoto | 89,122,056 |
| 24. | H/W Ngara | 290,614,376 | 62. | H/M Tabora | 88,844,302 |
| 25. | H/W Kilwa | 273,000,887 | 63. | H/W Bumbuli | 84,282,207 |
| 26. | H/W Sikonge | 262,257,240 | 64. | H/M Lindi | 76,177,292 |
| 27. | H/W Itigi | 259,285,872 | 65. | H/W Nachingwea | 68,364,085 |
| 28. | H/M Songea | 253,420,050 | 66. | H/W Bagamoyo | 67,886,636 |
| 29. | H/W Uvinza | 247,397,425 | 67. | H/Mji Kasulu | 65,996,370 |
| 30. | H/W Kilolo | 243,750,907 | 68. | H/Mji Bariadi | 60,868,829 |
| 31. | H/W Korogwe | 242,104,924 | 69. | H/W Njombe | 58,521,551 |
| 32. | H/M Musoma | 238,912,080 | 70. | H/W Simanjiro | 56,421,012 |
| 33. | H/W Muheza | 219,238,021 | 71. | H/M Sumbawanga | 54,261,382 |
| 34. | H/W Rorya | 214,799,378 | 72. | H/W Namtumbo | 49,737,012 |
| 35. | H/W Gairo | 211,826,181 | 73. | H/W Nyasa | 49,189,114 |
| 36. | H/W Arusha | 210,359,302 | 74. | H/Mji Korogwe | 33,885,723 |
| 37. | H/W Uyui | 205,322,943 | 75. | H/W Mwanga | 21,642,913 |
| 38. | H/W Kisarawe | 200,651,159 | 76. | H/W Bukoba | 14,598,753 |
| **Jumla** | | | | | **22,370,267,794** |

Kutozingatia miongozo ya maandalizi ya bajeti na utekelezaji kulisababisha kushindwa kutekeleza shughuli zilizokusudiwa kwa mwaka wa fedha na hivyo kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Narudia pendekezo langu la mwaka uliopita kwamba, Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuzingatia maelekezo na miongozo ya bajeti ya Serikali kwa kuhakikisha zinatenga asilimia sahihi ya mapato ya ndani kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo; aidha kuhakikisha fedha zote za maendeleo zilizotengwa zinatumika katika miradi iliyokusudiwa, badala ya kutumika kukidhi shughuli za kawaida.**

## 4.4 Fedha zilizosalia katika miradi ya ujenzi ambazo hazikutumiwa ndani ya muda Shilingi Bilioni. 11.5

Kanuni ya 21 (1) ya Kanuni ya Bajeti ya mwaka 2015 inawataka Maafisa Masuuli kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali maombi ya matumizi ya bakaa ya fedha zilizotolewa awali siku kumi na tano kabla ya tarehe 30 Juni kila mwaka wa fedha .Aidhaia fedha hizo zitumike ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata.

Nilibaini Halmashauri 12 zilikuwa na fedha jumla ya shilingi bilioni 11.5 ambazo zilivuka mwaka wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu. Hata hivyo, fedha hizi hazikutumika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23, na hapakuwa na uthibitisho ushahidi uliotolewa kuonyesha kwamba zilipata kibali toka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hii ni kinyume na kanuni na taratibu. Fedha za bakaa zimefafanuliwa katika **Jedwali 4-7**

**Jedwali Na.4-7: Fedha Zilizosalia Kwa Miradi ya Ujenzi na Ambazo Hazikutumiwa Ndani ya Muda**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Njombe | 2,147,881,151 | 7. | H/W Chamwino | 747,160,000 |
| 2. | H/Jiji Dar es Salaam | 1,993,362,846 | 8. | H/W Chemba | 612,454,580 |
| 3. | H/W Ileje | 1,737,627,858 | 9. | H/W Ludewa | 427,185,095 |
| 4. | H/W Iringa | 1,280,331,396 | 10. | H/W Kondoa | 114,337,952 |
| 5. | H/Jiji Dodoma | 1,250,000,000 | 11. | H/W Karatu | 85,000,000 |
| 6. | H/W Mufindi | 1,047,326,798 | 12. | H/W Mlele | 60,000,000 |
| **Jumla** | | | | | **11,502,667,675** |

Kutotolewa fedha kwa wakati, kumepelekea kuchelewa kuidhinishwa/kurekebishwa kwa misimbo ya GFS ya fedha za bakaa katika PLANREP, FFARS na MUSE, ni sababu ya kutokamilika kwa miradi na hatimaye kucheleweshwa kwa utoaji wa huduma kwa walengwa. Hali hii inaweza kusababisha gharama za miradi kuongezeka kutokana na athari za mfumuko wa bei.

**Ninashauri Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuingiza miradi husika katika bajeti na kutumia kwa wakati fedha zilizovuka mwaka kwenye miradi iliyoidhinishwa. Aidha , kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango watatue kwa wakati kero zinazohusiana na vifungu hivi vya bajeti ili kuepuka ucheleweshaji wa matumizi ya fedha.**

## 4.5 Matumizi ya Fedha Zisizo Katika Bajeti na zilizobadilishwa Matumizi Shilingi billion 6.49

Agizo Na. 18(5) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa la Mwaka 2009 linakataza matumizi ya fedha kabla ya kupata idhini kutoka baraza la madiwani isipokuwa malipo ya watumishi na fedha zinazofadhiliwa na serikali kuu. Aidha, Agizo Na. 23(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa la Mwaka 2009 linaelekeza kutumia fedha kulingana na bajeti iliyoidhinishwa na kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kinyume na agizo, nilibaini Halmashauri 39 zililipa shilingi bilioni 4.81 ili kutekeleza shughuli ambazo hazikuidhinishwa, na Halmashauri 17 zilitumia shilingi bilioni 1.68 kwa kutumia vifungu visivyo sahihi vya matumizi kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali 4-8**.

**Jedwali Na.4-8: Matumizi Yasiyokuwepo Kwenye Bajeti na Fedha Zilizobadilishwa Matumizi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiashi(Sh) | Na | Jina la Halmashauri | Kiashi(Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi yasiyo Katika Bajeti** | | | | | |
| 1. | H/W Maswa | 575,570,916 | 21. | H/W Mwanga | 61,552,979 |
| 2. | H/M Iringa | 538,112,780 | 22. | H/W Ileje | 57,274,304 |
| 3. | H/Mji Njombe | 449,096,913 | 23. | H/W Ukerewe | 55,484,299 |
| 4. | H/W Shinyanga | 246,099,190 | 24. | H/M Tarime | 55,161,200 |
| 5. | H/Jiji Mwanza | 233,008,646 | 25. | H/W Muheza | 55,036,290 |
| 6. | H/M Tabora | 229,070,446 | 26. | H/W Itigi | 54,400,000 |
| 7. | H/M Musoma | 169,071,556 | 27. | H/M Mafinga | 40,364,790 |
| 8. | H/M Sumbawanga | 161,040,142 | 28. | H/W Manyoni | 39,425,000 |
| 9. | H/W Lushoto | 151,947,341 | 29. | H/W Serengeti | 38,305,000 |
| 10. | H/M Shinyanga | 150,000,000 | 30. | H/W Wang'ing'ombe | 37,472,610 |
| 11. | H/W Nzega | 142,152,985 | 31. | H/W Kilindi | 36,634,400 |
| 12. | H/W Tarime | 140,580,000 | 32. | H/W Buchosa | 31,744,000 |
| 13. | H/Jiji Arusha | 132,412,471 | 33. | H/W Mlele | 31,460,000 |
| 14. | H/W Kaliua | 131,796,500 | 34. | H/W Handeni | 28,749,916 |
| 15. | H/W Songea | 119,000,000 | 35. | H/W Rungwe | 28,544,610 |
| 16. | H/Mji Handeni | 111,182,145 | 36. | H/W Pangani | 21,351,000 |

| Na | Jina la Halmashauri | Kiashi(Sh) | Na | Jina la Halmashauri | Kiashi(Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 17. | H/M Singida | 109,074,248 | 37. | H/W Busega | 19,973,000 |
| 18. | H/W Urambo | 106,802,863 | 38. | H/M Korogwe | 18,111,000 |
| 19. | H/W Kongwa | 103,200,000 | 39. | H/M Makambako | 11,560,000 |
| 20. | H/W Songwe | 90,000,000 | **Jumla Ndogo** | | **4,811,823,540** |
| **Fedha Zilizobadilishwa Matumizi** | | | | | |
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 345,993,000 | 10. | H/W Lushoto | 55,340,324 |
| 2. | H/W Serengeti | 272,210,856 | 11. | H/Mji Bunda | 53,454,608 |
| 3. | H/W Bahi | 214,354,614 | 12. | H/W Handeni | 45,181,308 |
| 4. | H/W Korogwe | 179,005,727 | 13. | H/W Itilima | 38,055,446 |
| 5. | H/W Rorya | 97,769,029 | 14. | H/W Chamwino | 36,143,022 |
| 6. | H/W Musoma | 87,175,952 | 15. | H/W Kigoma | 35,895,301 |
| 7. | H/W Handeni | 72,004,008 | 16. | H/W Mkuranga | 16,889,969 |
| 8. | H/W Busega | 68,208,615 | 17. | H/W Rufiji | 5,164,000 |
| 9. | H/W Bariadi | 58,017,902 | **Jumla Ndogo** | | **1,680,863,681** |
| **Jumla Kuu** | | | | | **6,492,687,221** |

Mapungufu katika udhibiti wa bajeti na kutozingatia maagizo ya randama ya fedha kumesababisha kufanyika matumizi yasiyokuwa kwenye bajeti na yasiyo sahihi, jambo ambalo lilizuia utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

**Ninashauri Katika siku zijazo Menejimenti za Halmashauri husika kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa kuzingatia kanuni za bajeti zilizoidhinishwa. Pia ziombe kibali kutoka Mamlaka husika kwa ajili ya kuhalalisha matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti.**

## 4.6 Tofauti za Ruzuku iliyotolewa kutoka Hazina dhidi ya kiasi halisi kilichopokelewa Katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kifungu cha 45 cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 kinampa Afisa Masuuli kudhibiti matumizi ya serikali yanayotozwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina kama ilivyobainishwa katika sheria. Zaidi ya hayo, fedha zinazotolewa katika mfuko mkuu lazima zilingane na bajeti zilizoidhinishwa na upatikanaji wa fedha.

Katika uthibitisho wangu wa ruzuku iliohamishwa kutoka hazina kwenda kwa Sekretarieti za mikoa, nilibaini tofauti kubwa kwa Sekretarieti za mikoa 12 kupokea kiasi cha shilingi bilioni 22.45 zaidi ya fedha zilizoidhinishwa na Sekretarieti za mikoa nne ikipokea kiasi

cha shilingi bilioni 21.77 pungufu ya kiasi kilichoidhinishwa kinyume na kipengele cha Sheria kilichotajwa hapo awali ambacho kinahitaji udhibiti wa ndani na usimamizi wa bajeti. Maelezo kuhusu Makadirio yaliyoidhinishwa, ruzuku ya hazina halisi kwa akaunti za matumizi ya Sekretarieti za mikoa yameonyeshwa katika **kiambatisho 4-6**

Nina wasiwasi kuwa fedha zinazotolewa kupita kiasi zinakiuka Sheria ya Bajeti na zinaweza kusababisha matumizi katika shughuli zisizopangwa.

**Ninashauri Wizara ya Fedha na Mipango kutoa fedha kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na pale inapotokea mabadiliko, Halmashauri husika ziombe idhini ya bajeti ya ziada kutoka mamlaka husika, kuimarisha udhibiti wa bajeti ya serikali na kuhakikisha Mfumo wa Bajeti Kuu (CBMS) na MUSE imeunganishwa.**




# SURA YA TANO

# USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

## 5.0 Utangulizi

Kama sehemu ya majukumu yangu chini ya Kifungu cha 48(3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura. 418, Nilifanya ukaguzi juu ya uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma katika Halmashauri 184 kwa mwaka wa fedha 2021/22. Madhumuni ya kaguzi hizo ilikuwa ni kutathmini kuwa kila hatua ya ununuzi ulifanywa kwa ufanisi na kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa katika Sheria na kanuni zinazoambatana nazo.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini taasisi zilizokaguliwa hazikuzingatia taratibu zilizowekwa za ununuzi katika baadhi ya maeneo. Udhaifu huu huanzia kwenye uandaaji wa nyaraka hadi usimamizi duni uliopelekea matumizi mabaya ya rasilimali za umma au hata kuchochea fursa za rushwa.

Madhaifu haya yameelezewa kwa undani na kutolewa mapendekezo ya kukabiliana nayo katika aya zifuatazo:

## 5.1 Usimamizi wa Manunuzi

### 5.1.1 Ununuzi uliofanyika bila Kuidhinishwa na Bodi za Zabuni Shilingi Bilioni 4.34

Kanuni ya 55 (2), 163 (4) na 185 (1) za Kanuni za Ununuzi za Mwaka, 2013 Umma, 2013 zinazuia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoa zabuni isipokuwa kama zabuni hiyo imeidhinishwa na bodi husika ya zabuni.

Kinyume na matakwa ya Kanuni, nilibaini kuwa mamlaka 23 za serikali za mitaa zilifanya ununuzi wa bidhaa mbalimbali zenye thamani ya shilingi bilioni 4.34 bila ya kuidhinishwa na bodi za zabuni za

halmashauri husika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5-1.**

**Jedwali Na.5-1: Halmashauri Zilizofanya ununuzi Bila Kudhinishwa na Bodi za Zabuni**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Bariadi | 543,360,068 | 13. | H/W Shinyanga | 123,454,820 |
| 2. | H/W Njombe | 476,279,264 | 14. | H/W Mlele | 118,305,760 |
| 3. | H/Mji Makambako | 440,004,956 | 15. | H/W Bunda | 91,229,800 |
| 4. | H/W Ileje | 348,161,496 | 16. | H/W Mbozi | 85,900,460 |
| 5. | H/W Singida | 319,642,578 | 17. | H/W Nsimbo | 63,155,277 |
| 6. | H/W Chamwino | 301,180,850 | 18. | H/W Kilolo | 56,578,500 |
| 7. | H/W Ruangwa | 284,820,447 | 19. | H/Mji Bunda | 45,893,400 |
| 8. | H/W Kaliua | 277,766,532 | 20. | H/W Manyoni | 45,715,600 |
| 9. | M/W Musoma | 190,639,440 | 21. | H/W Mkinga | 34,240,734 |
| 10. | H/Mji Njombe | 167,077,668 | 22. | H/W Mvomero | 18,210,975 |
| 11. | H/W Nkasi | 153,332,283 | 23. | H/W Handeni | 13,316,600 |
| 12. | H/Mji Tarime | 141,513,000 | **Jumla** | | **4,339,780,508** |

Aidha, Kanuni ya 166 (7) na (8) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 vinataka ununuzi wote mdogo kutolewa taarifa katika bodi za zabuni kila mwezi.

Katika ukaguzi nilioufanya kuhusu nunuzi mdogo katika Mamlaka 16 za Serikali za Mitaa nilibaini kuwa, manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 1.36 yalifanyika bila kutolewa taarifa kwenye bodi za zabuni kila mwezi kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5-2.**

**Jedwali Na.5-2: Halmashauri Zilizofanya ununuzi Mdogo Bila Kutolewa Taarifa Kwenye Bodi za Zabuni**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Momba | 249,394,067 | 10. | H/Mji Nzega | 54,849,637 |
| 2. | H/W Uvinza | 168,778,443 | 11. | H/Jiji Tanga | 39,135,500 |
| 3. | H/W Uyui | 160,130,343 | 12. | H/W Rombo | 36,213,897 |
| 4. | H/W Songwe | 159,833,964 | 13. | H/M Shinyanga | 35,900,000 |
| 5. | H/W Ileje | 124,146,277 | 14. | H/W Siha | 35,057,340 |
| 6. | H/W Tunduru | 110,633,650 | 15. | H/M Singida | 33,747,048 |
| 7. | H/W Bukoba | 87,806,095 | 16. | H/W Mlele | 10,653,532 |
| 8. | H/W Mkalama | 58,266,920 | | **Jumla** | **1,364,546,713** |

Ununuzi uliofanyika bila idhini ya Bodi za Zabuni unainyima bodi kutekeleza majukumu yake ya uangalizi.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuchukua hatua stahiki kwa mamlaka za serikali za mitaa zote zilizobainika kufanya ununuzi**

**bila kupata kibali cha Bodi za Zabuni.**

### 5.1.2 Manunuzi yenye thamani ya Shilingi Bilioni 14.02 yaliofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi wa Halmashauri

Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 inaitaka taasisi nunuzi kufanya makisio ya mahitaji yake ya bidhaa, huduma, na ujenzi kwa usahihi kadiri iwezekanavyo kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo zipo katika mpango kazi na kujumuishwa katika makadirio ya kila mwaka.

Katika ukaguzi nilioufanya kwa mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini kuwa Halmashauri 19 zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi. bilioni 14.02 nje ya mipango yao ya manunuzi ya mwaka kama inavyooneshwa katika. **Jedwali 5-3** hapa chini.

**Jedwali Na.5-3: Ununuzi Uliofanyika Nje ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Nkasi | 7,706,634,454 | 11. | H/W Busega | 99,930,000 |
| 2. | H/W Songea | 1,814,041,864 | 12. | H/W Iringa | 92,812,925 |
| 3. | H/W Chato | 1,440,637,229 | 13. | H/W Missenyi | 85,415,664 |
| 4. | H/W Shinyanga | 890,000,000 | 14. | H/W Mufindi | 73,457,522 |
| 5. | H/W Nsimbo | 500,000,000 | 15. | H/W Iramba | 55,174,000 |
| 6. | H/M Morogoro | 419,357,620 | 16. | H/W Mlele | 45,207,293 |
| 7. | H/W Mkinga | 252,762,578 | 17. | H/M Bukoba | 37,152,200 |
| 8. | H/M Musoma | 172,970,700 | 18. | H/W Urambo | 30,000,000 |
| 9. | H/W Hai | 157,500,140 | 19. | H/W Magu | 8,545,680 |
| 10. | H/M Kahama | 139,620,016 | | **Jumla** | **14,021,219,885** |

Ununuzi unaofanyika nje ya mipango na bajeti ya mwaka, yanaweza kusababisha matumizi yasiyopangwa na kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa.

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhakikisha kuwa Halmashauri zinafanya manunuzi kwa kuzingatia Mipango ya Mwaka. Aidha, inapaswa kuboresha mchakato wa kupanga ununuzi ili kuhakikisha kuwa inaendana na malengo ya kimkakati ya taasisi.**

### 5.1.3 Ununuzi ya Shilingi Bilioni 7.45 yaliyofanyika bila Ushindanishi wa bei

Kanuni ya 164(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaagiza taasisi inayofanya ununuzi kupata nukuu za bei kutoka kwa

wazabuni/wauzaji wasiopungua watatu.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 7.45 yalifanyika katika mamlaka 45 za serikali za mitaa bila kuitisha nukuu za ushindanishi wa bei, hii ni kinyume na matakwa ya kanuni za ununuzi wa umma. Kama inavyoonekana **Jedwali 5-4** hapa chini

**Jedwali Na.5-4: Ununuzi Uliofanyika Bila Ushindanishi wa Bei**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kaliua | 894,815,609 | 24. | H/W Mbarali | 94,708,383 |
| 2. | H/W Missenyi | 648,600,000 | 25. | H/W Mkinga | 91,674,633 |
| 3. | H/W Bunda | 576,039,073 | 26. | H/M Kigoma Ujiji | 91,228,450 |
| 4. | H/W Momba | 445,068,690 | 27. | H/W Nsimbo | 82,068,837 |
| 5. | H/W Arusha | 398,777,989 | 28. | H/W Chato | 79,201,385 |
| 6. | H/W Nyasa | 371,668,850 | 29. | H/Jiji Mwanza | 77,864,756 |
| 7. | H/M Mpanda | 301,887,574 | 30. | H/W Meatu | 72,333,055 |
| 8. | H/W Ileje | 283,356,469 | 31. | H/Mji Babati | 67,185,077 |
| 9. | H/Mji Tunduma | 257,829,333 | 32. | H/W Makete | 54,627,752 |
| 10. | H/W Serengeti | 191,497,139 | 33. | H/W Sengerema | 50,950,550 |
| 11. | H/W Songwe | 181,062,915 | 34. | H/W Longido | 46,420,300 |
| 12. | H/W Uvinza | 173,320,675 | 35. | H/W Mlele | 45,207,293 |
| 13. | H/Mji Bunda | 169,037,056 | 36. | H/W Korogwe | 42,574,500 |
| 14. | H/M Kahama | 165,728,827 | 37. | H/W Mvomero | 40,709,794 |
| 15. | H/Mji Makambako | 165,000,000 | 38. | H/W Msalala | 39,748,000 |
| 16. | H/W Ukerewe | 156,180,277 | 39. | H/W Kilindi | 39,169,500 |
| 17. | H/W Tunduru | 147,730,862 | 40. | H/W Magu | 33,945,972 |
| 18. | H/W Buhigwe | 144,454,134 | 41. | H/Mji Ifakara | 33,046,299 |
| 19. | H/W Malinyi | 136,484,742 | 42. | H/W Ngorongoro | 28,864,567 |
| 20. | H/W Nkasi | 126,507,937 | 43. | H/W Mpwapwa | 28,812,000 |
| 21. | H/M Kigamboni | 117,126,954 | 44. | H/W Kibiti | 15,371,692 |
| 22. | H/W Shinyanga | 112,824,910 | 45. | H/W Pangani | 13,000,001 |
| 23. | H/W Mkalama | 112,140,000 | | **Jumla** | **7,445,852,811** |

Kufanya Ununuzi wa bidhaa unaohusisha kiasi kikubwa cha fedha bila ushindani wa bei kutoka kwa wazabuni, umezuia Halmashauri husika kupata bei shindani zaidi na thamani ya fedha katika ununuzi huo.

**Ninasisitiza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe uzingatiaji wa sheria husika katika mamlaka za serikali za mitaa ili kupata thamani ya fedha na kuwapatia wazabuni fursa ya kushindana.**

### 5.1.4 Ununuzi wa Shilingi Bilioni 1.99 yaliofanyika bila Kutumia Hati ya Kuagiza Vifaa

Kanuni ya 164 (2)(j) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013,

inaeleza kwamba, barua ya mwaliko wa nukuu za bei na kiambatisho chochote kitakuwa na fomu ya mkataba au hati ya kuagiza vifaa (LPO) itakayojumuisha masharti yote ya malipo. Aidha Agizo la 69 la randama ya Fedha za mamlaka za serikali za mitaa ya Mwaka 2009 linataka bidhaa, huduma, na kazi zote zilizofanyika katika mamlaka za serikali za mitaa kuthibitishwa kwa hati ya kuagiza vifaa.

Ukaguzi wangu wa ununuzi ulibaini kuwa, mamlaka 18 za serikali za mitaa zilifanya ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 1.99 bila kutumia hati ya kuagiza vifaa/bidhaa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5-5.**

**Jedwali Na.5-5: Ununuzi uliofanyika Bila Hati ya Kuagiza Vifaa/Bidhaa**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Serengeti | 422,561,827 | 10. | H/W Mbozi | 77,455,800 |
| 2. | H/W Sumbawanga | 243,656,432 | 11. | H/W Maswa | 63,067,616 |
| 3. | H/W Kasulu | 150,724,573 | 12. | H/W Manyoni | 56,492,892 |
| 4. | H/W Momba | 149,627,015 | 13. | H/M Singida | 52,772,400 |
| 5. | H/W Nkasi | 144,915,320 | 14. | H/W Longido | 44,497,800 |
| 6. | H/Jiji Tanga | 138,406,990 | 15. | H/M Kigoma Ujiji | 33,375,920 |
| 7. | H/Mji Tunduma | 123,643,809 | 16. | H/W Pangani | 31,914,750 |
| 8. | H/W Chemba | 122,258,500 | 17. | H/W Busega | 20,790,852 |
| 9. | H/Jiji Dar es Salaam | 100,039,805 | 18. | H/W Korogwe | 15,284,308 |
| Jumla | | | | | **1,991,486,609** |

Mapungufu haya yanaweza kusababisha upotevu mkubwa iwapo wazabuni watashindwa kuwasilisha bidhaa ipasavyo, kwani hakutakuwa na mikataba ya kisheria kati ya wahusika.

**Ninapendekeza kuwa, Uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia matakwa ya kanuni ya ununuzi yailiyotajwa hapo juu na kuchukua hatua stahikidhidi ya wanaokwenda kunyume na sheria.**

### 5.1.5 Mapokezi ya vifaa vilivyonunuliwa vyenye thamani ya shiling bilioni 3.02 bila kukaguliwa.

Kanuni ya 244(1) na 245 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya 2013 inataka taasisi inayofanya ununuzi kukagua bidhaa zinazoletwa na wazabuni na kuzikubali iwapo tu zinakidhi masharti ya mkataba.

Kinyume na Kanuni hiyo, nilibaini mamlaka 27 za serikali za mitaa zilipokea vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.02 kwa wazabuni bila kukaguliwa na kamati zilizoteuliwa, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5-6** hapa chini.

Jedwali Na.5-6: Mapokezi ya Vifaa/Bidhaa Bila Kufanyiwa Ukaguzi

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Songea | 488,379,799 | 15. | H/W Mkinga | 46,963,100 |
| 2. | H/W Mlele | 381,205,253 | 16. | H/W Nsimbo | 38,270,200 |
| 3. | H/W Nyasa | 280,529,445 | 17. | H/W Itigi | 35,440,230 |
| 4. | H/W Uvinza | 271,995,504 | 18. | H/W Mkuranga | 33,575,197 |
| 5. | H/W Maswa | 244,409,466 | 19. | H/W Rufiji | 31,571,920 |
| 6. | H/Mji Tunduma | 186,169,903 | 20. | H/W Mbarali | 29,400,000 |
| 7. | H/Mji Handeni | 162,257,198 | 21. | H/W Gairo | 28,080,000 |
| 8. | H/W Bumbuli | 156,368,200 | 22. | H/W Longido | 25,925,300 |
| 9. | H/W Namtumbo | 145,275,933 | 23. | H/W Korogwe | 21,633,000 |
| 10. | H/W Mkalama | 96,364,011 | 24. | H/W Mvomero | 18,362,260 |
| 11. | H/W Mbozi | 91,909,385 | 25. | H/M Mpanda | 17,500,000 |
| 12. | H/Mji Kibaha | 65,079,275 | 26. | H/W Singida | 8,037,711 |
| 13. | H/M Singida | 57,824,052 | 27. | H/W Handeni | 7,654,000 |
| 14. | H/W Manyoni | 53,272,095 | **Jumla** | | **3,023,452,437** |

Mapokezi ya vifaa vilivyonunuliwa bila kukaguliwa na kamati husika kunaweza kuathiri ubora na utekelezaji wa matakwa ya mkataba na kunaweza kusababisha ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora kwa taasisi nunuzi.

**Ninashauri, Uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa zifuate kanuni husika kwa kukagua ubora na idadi ya bidhaa na huduma zinazonunuliwa kabla ya kufanya malipo kwa wazabuni.**

### 5.1.6 Utekelezaji wa Miradi ya ujenzi yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 23.80 bila kufanya tathmini ya Athari za mazingira

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya ununuzi kufanya tathmini ya athari za kimazingira katika hatua ya maandalizi ya mradi kabla ya kuanza mchakato wa ununuzi. Aidha, Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 kinataka utafiti wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Nimepitia majalada ya miradi na kubaini kuwa mamlaka 12 zilianza utekelezaji wa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 23.80 bila kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza miradi hiyo, kama inavyooneshwa katika **Jedwali 5 - 7**

Aidha, nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo inatekeleza mradi wa ujenzi wenye thamani ya shilingi bilioni 2.80 bila kufanyika

uchunguzi wa kijiolojia.

**Jedwali Na.5-7: Miradi Iliyotekelezwa Bila Tathimini ya Athari za Mazingira**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Bunda | 3,578,773,698 | 7. | H/W Muheza | 1,500,000,000 |
| 2. | H/W Singida | 3,459,892,600 | 8. | H/M Singida | 1,470,000,000 |
| 3. | H/Jiji Dar es Salaam | 2,930,234,090 | 9. | H/W Lushoto | 1,150,000,000 |
| 4. | H/W Rombo | 2,800,000,000 | 10. | H/W Bumbuli | 1,000,000,000 |
| 5. | H/W Monduli | 2,500,000,000 | 11. | H/W Siha | 500,000,000 |
| 6. | H/Mji Geita | 2,407,569,051 | 12. | H/W Songea | 500,000,000 |
| **Jumla** | | | | | **23,796,469,439** |

Utekelezaji wa miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira na uchunguzi wa kijiolojia, unaziweka mamlaka za serikali za mitaa katika hatari za kupata athari za mazingira ambazo zinaweza kuathiri jamii katika maeneo husika, na kusababisha hasara ya upotevu wa rasilimali.

**Ninashauri Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe Mamlaka za Serikali za mtaa zinafanya tathmini ya athari za mazingira na uchunguzi wa kijiolojia kabla ya kuanza kwa mradi wa ujenzi ili kuhakikisha unakuwa salama, na kuepuka zinazotokana na mazingira.**

### 5.1.7 Mikataba ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria yenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.68

Kanuni ya 59 na 60 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 (na marekebisho yake ya mwaka 2016) zinahitaji mwanasheria mkuu au mwanasheria wa taasisi nunuzi kupitia mkataba wa makubaliano husika kabla ya kusainiwa pande zote, mara baada ya kupokea ushauri wa kisheria, Afisa masuuli anatakiwa kujumuisha marekebisho hayo katika rasimu ya mkataba.

Nimekagua usimamizi wa mikataba, na kubaini mamlaka 20 za Serikali za mitaa zilizosaini mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 6.68 kabla mikataba hiyo kupitiwa na mwanasheria kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5-8** hapa chini.

**Jedwali Na.5-8: Mikataba Ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | 3,915,527,364 | 12. | H/W Kigoma | 85,260,000 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | H/W Sengerema | 549,440,000 | 13. | H/W Same | 84,950,000 |
| 3. | H/W Ruangwa | 517,016,360 | 14. | H/W Muleba | 80,420,000 |
| 4. | H/W Kyerwa | 320,265,950 | 15. | H/W Mpimbwe | 78,461,400 |
| 5. | H/W Simanjiro | 240,000,000 | 16. | H/W Nsimbo | 66,170,000 |
| 6. | H/W Singida | 133,076,400 | 17. | H/Jiji Dar es Salaam | 65,257,400 |
| 7. | H/W Ikungi | 98,070,000 | 18. | H/W Mbogwe | 43,935,000 |
| 8. | H/W Kaliua | 97,404,550 | 19. | H/W Ngorongoro | 16,923,300 |
| 9. | H/W Kilwa | 96,500,000 | 20. | H/W Mkuranga | 16,918,800 |
| 10. | H/W Bunda | 91,229,800 | **Jumla** | | **6,687,886,324** |
| 11. | H/W Nachingwea | 91,060,000 | | | |

Aidha, nilibaini Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam haikuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali baada ya uhakiki katika uandaaji wa mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 2.93.

Kusaini mkataba kabla ya kuhakiki na kujumuisha maoni ya Mwanasheria kunaziweka Mamlaka za Serikali za Mitaa husika katika hatari za kisheria.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe mikataba ya mamlaka za Serikali za mitaa inahakikiwa kabla ya kusainiwa ili kuepuka migogoro ya kisheria inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi.**

### 5.1.8 Ununuzi wa bidhaa ya Shilingi Bilioni 7.17 yaliofanyika kwa Wazabuni Ambao hawakuidhinishwa na Wakala wa Ununuzi Serikalini

Katika ukaguzi wangu nilioufanya juu ya usimamizi wa mikataba na ununuzi wa bidhaa, nilibaini kwamba Halmashauri 34 zilifanya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 4.61 kwa wazabuni ambao hawakuwa na mikataba ya makubaliano na Wakala wa Ununuzi Serikalini kinyume na Kanuni ya 131 (4) (b) za Ununuzi za Umma za Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) za 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 la 30/12/2016) Halmashauri zilizonunua bidhaa kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa na wakala wa Ununuzi zimeorodheshwa katika **Jedwali 5-9**

**Jedwali Na.5-9: Manunuzi kwa Wazabuni Wasiokuwa na Mikataba**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Mji Tarime | 1,102,944,090 | 15. | H/W Malinyi | 92,929,022 |
| 2. | H/W Serengeti | 690,931,152 | 16. | H/W Bunda | 80,501,000 |
| 3. | H/M Musoma | 495,037,354 | 17. | H/W Nsimbo | 67,842,540 |
| 4. | H/W Tarime | 442,109,933 | 18. | H/W Mbozi | 66,488,165 |
| 5. | H/Mji Bariadi | 414,034,367 | 19. | H/Jiji Mbeya | 65,195,970 |
| 6. | H/W Busega | 403,121,694 | 20. | H/W Korogwe | 62,108,040 |
| 7. | H/W Chunya | 296,457,500 | 21. | H/W Magu | 56,937,563 |
| 8. | H/W Kyela | 231,505,823 | 22. | H/W Kibondo | 53,220,500 |
| 9. | H/W Mbarali | 187,481,400 | 23. | H/W Mvomero | 48,817,742 |
| 10. | H/Mji Bunda | 169,037,056 | 24. | H/W Meru | 44,429,568 |
| 11. | H/W Butiama | 161,254,740 | 25. | H/W Karatu | 36,872,000 |
| 12. | H/W Singida | 132,388,805 | 26. | H/W Mlele | 35,220,361 |
| 13. | H/W Same | 109,879,282 | 27. | H/W Mpanda | 23,843,517 |
| 14. | H/W Rorya | 106,285,448 | | **Jumla** | **5,676,874,632** |

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Mamlaka 6 za Serikali za mtaa zilinunua bidhaa zinazotumika mara kwa mara (mafuta ya vyombo vya moto na shajala) zenye thamani ya shilingi bilioni 1.49 kutoka kwa wazabuni bila kupata hati ya kutopatikana kwa vifaa hivyo kwa Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 5-10**

**Jedwali Na.5-10: Manunuzi ya Bidhaa Kwa Wazabuni**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Kaliua | 984,151,409 |
| 2. | H/W Nzega | 223,906,788 |
| 3. | H/W Uyui | 154,540,982 |
| 4. | H/W Kilolo | 69,617,415 |
| 5. | H/Jiji Tanga | 42,797,304 |
| 6. | H/W Iringa | 18,257,671 |
| **Jumla** | | **1,493,271,569** |

Kwa maoni yangu, kufanyika kwa ununuzi kutoka kwa wazabuni ambao hawapo kwenye orodha iliyoidhinishwa na Wakala wa Ununuzi Serikalini kunaweza kusababisha kununua bidhaa kwa bei ya juu na kupokea bidhaa zenye ubora wa chini.

**Ninapendekeza Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa, ununuzi wote wa bidhaa na huduma yanafanyika kutoka kwa wazabuni walioidhinishwa na Wakala wa ununuzi serikalini.**

### 5.1.9 Malipo yaliofanyika kwa ununuzi wa bidhaa kabla ya kupokelewa na bidhaa ambazo hazijapokelewa shillingi bilioni 3.29

Kanuni ya 242 (1) na 248 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 zinataka malipo ya bidhaa na huduma kufanyika baada ya bidhaa kupokelewa, kukaguliwa na kukubaliwa na hati ya kukubalika kwa bidhaa iliyoosainiwa itolewe kwa mzabuni na nakala ya hati hiyo zitatumiwa na taasisi nunuzi kusaidia uchakataji wa malipo.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kwamba, mamlaka 12 za serikali za mitaa zilifanya malipo yenye jumla ya shilingi bilioni 1.16 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa kabla ya kupokelewa na mamlaka hizo. Sambamba na hilo, pia malipo ya shillingi bilioni 2.13 yalifanywa na mamlaka nyingine 14 za serikali za mitaa kwa ununuzi wa bidhaa ambazo hazikupokelewa kabisa. **Jedwali 5-11** linaonesha kwa muhtasari juu ya malipo hayo.

**Jedwali Na.5-11: Mamlaka za Serikali za Mtaa Zilizofanya Malipo Kabla ya Bidhaa Kupokelewa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| Malipo yaliyofanyika kabla ya kupokelewa kwa bidhaa nunuliwa | | | | | |
| 1 | H/W Sumbawanga | 256,128,507 | 8 | H/W Ludewa | 43,887,397 |
| 2 | H/M Sumbawanga | 234,576,950 | 9 | H/W Kalambo | 27,502,250 |
| 3 | H/W Chemba | 207,839,094 | 10 | H/M Musoma | 24,620,400 |
| 4 | H/W Butiama | 105,298,734 | 11 | H/W Itigi | 17,997,700 |
| 5 | H/W Kondoa | 104,558,960 | 12 | H/W Njombe | 11,896,500 |
| 6 | H/Mji Bunda | 68,110,000 | | Jumla ndogo | 1,159,358,655 |
| 7 | H/W Tunduru | 56,942,163 | | | |
| Malipo ya bidhaa ambazo hazijawasilishwa | | | | | |
| 1 | H/Jiji Tanga | 454,862,900 | 9 | H/W Kilindi | 67,663,500 |
| 2 | H/W Singida | 410,846,500 | 10 | H/W Mkalama | 32,034,370 |
| 3 | H/M Sumbawanga | 327,646,230 | 11 | H/W Kibaha | 30,687,162.37 |
| 4 | H/W Korogwe | 255,886,455 | 12 | H/W Lushoto | 23,556,000 |
| 5 | H/W Shinyanga | 181,109,950 | 13 | H/Mji Handeni | 9,421,500 |
| 6 | H/W Kyerwa | 150,450,000 | 14 | H/Mji Ifakara | 9,342,000 |
| 7 | H/Mji Kasulu | 91,677,000 | | Jumla ndogo | 2,129,529,767 |
| 8 | H/W Mbinga | 84,346,200 | | | |
| **Jumla kuu** | | | | | **3,288,888,422** |

Malipo kwa wazabuni kabla ya kupokelewa bidhaa kunaiweka Halmashauri kwenye hatari ya upotevu wa fedha endapo wazabuni watashindwa kuwasilisha bidhaa. Pia, ikiwa bidhaa zilizowasilishwa hazikidhi viwango vya ubora unaohitajika au zina kasoro, Taasisi nunuzi inaweza kupata ugumu wa kurejeshewa pesa au kubadilishiwa bidhaa hizo.

**Nashauri Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha malipo ya bidhaa kupokelewa na kukaguliwa ili kujiridhisha juu ya idadi na ubora uliohitajika na mamlaka hizo kutoka kwa wazabuni.**

### 5.1.10 Ununuzi wa bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 1.38 bila kuanisha viwango/vipimo ya kina kuhusu bidhaa hizo

Kanuni ya 164 (2) (b) ya Kanuni za ununuzi wa Umma, 2013 inasema kwamba "Barua ya mwaliko wa nukuu ya bei na viambatisho vyovyote vitakuwa na maelezo kamili ya bidhaa, kazi au huduma zitakazonunuliwa, ikijumuisha sifa za kiufundi au ubora unaohitajika; vipimo, miundo; mipango na michoro inayostahili"

Aidha, Kipengele cha 24.2 cha Mwongozo wa nguvu kazi '*force account*' wa mwaka 2020, kinasema vifaa vya ujenzi vitakavyonunuliwa viendane na mchanganuo wa mahitaji na maelezo yaliyoainishwa na kuidhinishwa na msimamizi wa mradi.

Nilibaini kuwa manunuzi ya vifaa vya ujenzi na bidhaa nyingine zenye thamani ya shilingi bilioni 1.38 katika Halmashauri 20 yalifanyika bila kuanisha viwango/vipimo ya kina kuhusu bidhaa hizo kama inavyooneshwa katika. Kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 5 - 12.**

**Jedwali Na.5-12: Ununuzi wa Bidhaa Bila Kuanisha kwa Kina Mahitaji**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Sumbawanga | 376,552,011 | 11. | H/Mji Handeni | 35,065,000 |
| 2. | H/W Sumbawanga | 183,416,856 | 12. | H/W Tunduru | 29,593,250 |
| 3. | H/W Iramba | 172,215,678 | 13. | H/W Igunga | 27,830,000 |
| 4. | H/W Songea | 124,409,500 | 14. | H/W Mafinga | 26,595,712 |
| 5. | H/W Mkinga | 80,254,819 | 15. | H/W Moshi | 26,000,000 |
| 6. | H/W Nkasi | 68,233,700 | 16. | H/W Lushoto | 20,521,000 |
| 7. | H/W Mlele | 45,207,293 | 17. | H/W Muheza | 17,550,000 |
| 8. | H/W Mbinga | 44,836,200 | 18. | H/M Mpanda | 12,013,990 |
| 9. | H/W Itigi | 39,225,200 | 19. | H/W Mwanga | 6,713,000 |
| 10. | H/W Mbarali | 37,274,300 | 20. | H/W Shinyanga | 6,507,200 |
| | Jumla | | | | **1,380,014,709** |

Ununuzi wa vifaa vya ujenzi na bidhaa nyingine bila kuanisha mahitaji inaweza sababisha kupokelewa kwa bidhaa ambazo haziendani na mahitaji, na kwa upande wa vifaa vya ujenzi, inaweza kusababisha ujenzi wa miradi isiyo bora.

**Ninapendekeza Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa waweke msisitizo katika kutoa viwango na vipimo katika nukuu za bei kulingana na miongozo ya kitaalamu iliyoidhinishwa katika ununuzi wa vifaa vya ujenzi na bidhaa nyingine.**

### 5.1.11 Ununuzi wa Magari yenye thamani ya bilioni 5.68 ambayo hayakuwasilishwa na Wakala wa Ununuzi Serikalini

Kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma (2011) kinasema, pale ambapo kuna upungufu wa uwezo wa kiufundi na, kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa katika kanuni, taasisi inayofanya ununuzi inaweza kushirikisha wakala au huduma za manunuzi kwa watu wengine. Aidha, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ina jukumu la kuhakikisha huduma za ununuzi ni bora kwa taasisi za Serikali kama ilivyobainishwa katika Sheria ya ununuzi wa Umma Sura 410. Pia wakala amepewa dhamana kwa upana juu ya ununuzi wa magari, pikipiki na mitambo kwa taasisi za Serikali. Mamlaka yameainishwa kwenye kanuni ya 130 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (2013) na marekebisho ya Sheria na Kanuni ya 2016. Hii inajumuisha mamlaka ya kununua magari ya umma kwa niaba ya taasisi za serikali.

Nilibaini kuwa, Mamlaka 29 za Serikali za Mitaa zilifanya malipo ya shilingi bilioni 5.68 kwa Wakala wa Ununuzi Serikalini kwa ajili ya ununuzi wa magari. Aidha nilibaini kuwa magari hayo hayakuwa yamewasilishwa katika Halmashauri husika kwa muda usiopungua mwaka mmoja tangu malipo kufanyika. Orodha ya Halmashauri zenye magari ambayo hayajawasilishwa imeoneshwa kwenye **Jedwali 5-13.**

**Jedwali Na.5-13: Orodha ya Halmashauri zenye Magari Ambayo Hayajawasilishwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Nsimbo | 349,505,723 | 16 | H/Mji Geita | 174,036,393 |
| 2 | H/W Karagwe | 320,831,329 | 17 | H/W Kibondo | 167,323,583 |
| 3 | H/W Morogoro | 317,915,805 | 18 | H/W Busokelo | 162,934,584 |
| 4 | H/M Kahama | 287,113,524 | 19 | H/W Meru | 162,934,584 |
| 5 | H/W Mbinga | 252,762,578 | 20 | H/W Songea | 160,415,665 |
| 6 | H/W Ileje | 252,762,578 | 21 | H/Mji Tunduma | 160,415,665 |
| 7 | H/W Mkinga | 252,762,578 | 22 | H/Mji Ifakara | 160,415,664 |
| 8 | H/W Bariadi | 252,762,578 | 23 | H/Mji Babati | 157,500,140 |
| 9 | H/W Shinyanga | 252,762,577 | 24 | H/W Ngorongoro | 150,452,000 |
| 10 | H/W Mlele | 227,441,235 | 25 | H/Mji Kondoa | 92,346,913 |
| 11 | H/W Babati | 215,363,569 | 26 | H/W Simanjiro | 92,346,913 |
| 12 | H/W Mpanda | 210,000,000 | 27 | H/W Malinyi | 92,346,913 |
| 13 | H/W Chalinze | 198,556,088 | 28 | H/Mji Njombe | 92,346,913 |
| 14 | H/W Bumbuli | 184,693,827 | 29 | H/W Ikungi | 92,346,913 |
| 15 | H/W Kwimba | 184,693,826 | **Jumla** | | **5,678,090,658** |

**Nashauri Maafisa Masuuli wa Halmashauri husika kuwasiliana na Wakala wa Ununuzi Serikalini ili kuhakikisha magari yanayonunuliwa yanawasilishwa kwa wakati ili kufanikisha utolewaji wa huduma iliyotarajiwa**

### 5.1.12 Matumizi ya Vifaa vya Ujenzi Vyenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.09 Bila Kufanyiwa Vipimo vya Ubora

Kanuni ya 244(1) ya Kanuni za Ununuzi wa umma (2013) inasema, bidhaa zitakazowasilishwa zinahitajika kukaguliwa, zichukuliwe sampuli na kupimwa na taasisi inayofanya ununuzi, na hazitokubalika kama zitakuwa chini ya viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba. Pia Kanuni ya 246 inasema kuwa, ikiwa bidhaa itahitaji jaribio la kiufundi au la kisayansi, mtaalam au mjuzi wa taaluma husika ataalikwa kwa mashauriano, au bidhaa zaweza tumwa kwa mjuzi huyo kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

Kinyume na matakwa ya kanuni za ununuzi wa umma, nilibaini Malaka 14 za serikali za mitaa zilinunua na kutumia vifaa vya ujenzi vikiwemo nondo na matofali vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.09 katika miradi ya ujenzi bila kufanyiwa vipimo vya ubora kama inavyoonekana katika **Jedwali 5-14** hapa chini.

**Jedwali Na.5-14: Vifaa vya Ujenzi Ambavyo Havijafanyiwa Vipomo vya Ubora**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Muheza | 204,452,500 | 9. | H/W Nkasi | 36,965,962 |
| 2. | H/W Sumbawanga | 160,585,311 | 10. | H/W Kigoma | 29,302,000 |
| 3. | H/Mji Tarime | 141,513,000 | 11. | H/W Mbulu | 29,044,856 |
| 4. | H/W Kaliua | 139,913,500 | 12. | H/W Kibiti | 27,705,225 |
| 5. | H/W Nanyumbu | 97,456,115 | 13. | H/W Kalambo | 18,810,050 |
| 6. | H/W Mkinga | 81,778,800 | 14. | H/W Ikungi | 8,910,240 |
| 7. | H/W Itigi | 65,473,680 | **Jumla** | | **1,090,729,069** |
| 8. | H/M Kahama | 48,817,830 | | | |

Kutofanyika kwa vipimo na majaribio ya vifaa vya ujenzi kumeiweka Halmashauri katika hatari ya kutumia vifaa visivyo na ubora ambavyo vinaweza kuathiri ubora wa miradi.

**Ninashauri Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa husika, katika siku zijazo kufanya vipimo vya vifaa ili kuhakikisha ubora wa kazi za ujenzi.**

### 5.1.13 Vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Shilingi Milioni 435.02 vilinunuliwa zaidi ya Mahitaji

Kipengele cha 11.1 cha Mwongozo wa nguvu kazi 'force account' kwa taasisi nunuzi nchini uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kinaitaka idara inayofanya matumizi au idara ya ufundi kuainisha kazi za ujenzi au matengenezo yanayohitajika kutekelezwa.

Katika tathmini ya vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa na uhakiki wa hatua ziliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi, nilibaini mamlaka 8 za Serikali za mitaa zilinunua vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji halisi. Ununuzi huo uligharimu shilingi milioni 435.02 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5-15.**

**Jedwali Na.5-15: Bidhaa Zilizonunuliwa Zaidi ya Mahitaji Halisi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Shinyanga | 217,141,670 |
| 2. | H/W Korogwe | 64,552,150 |
| 3. | H/Jiji Mwanza | 44,280,000 |
| 4. | H/M Bukoba | 29,325,000 |
| 5. | H/M Moshi | 26,645,714 |
| 6. | H/W Liwale | 23,288,326 |
| 7. | H/W Rorya | 18,333,000 |
| 8. | H/W Muheza | 11,453,930 |
| **Jumla** | | **435,019,790** |

Aidha, katika ziara za miradi, nilibaini kuwa vifaa hivyo vya ujenzi vilikuwa vimeachwa katika vituo vilivyokuwa vikitekeleza miradi hiyo huku ujenzi ukiwa umekamilika.

Kutoandaa mahitaji halisi ya vifaa vya ujenzi kumepelekea ununuzi wa vifaa zaidi ya mahitaji, ambavyo vinaweza kutumika vibaya au kuibiwa.

**Ninapendekeza kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe mahitaji ya vifaa vya ujenzi wa miradi zinaandaliwa kwa usahihi ili kuepuka ununuzi wa vifaa vya ujenzi zaidi ya mahitaji halisi. Pia, uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa unahimizwa kuhakikisha kuwa vifaa vya ujenzi vilivyozidi vinatumika kwa ufanisi ili kuleta tija.**

## 5.2 Mapugufu katika Usimamizi wa Mikataba

Lengo la ukaguzi wa usimamizi wa mikataba ni kutathmini iwapo kuna usimamizi madhubuti katika utekelezaji wa mikataba iliyotekelezwa katika mamlaka za Serikali za mitaa nchini.

Maelezo ya mapungufu yaliyobanika na mapendekezo yameainishwa hapa chini:

### 5.2.1 Malipo yaliyofanyika bila Kupima kazi na Hayakuthibitishwa na Wasimamizi wa Miradi Shilingi Bilioni 2.67

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, inazitaka taasisi inayofanya ununuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na uthibitisho, katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika mikataba na kwamba asilimia kadhaa ya thamani ya kazi zilizotekelezwa kutoka kila cheti cha malipo kinaweza kukatwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matazamio endapo mkataba utaweka takwa hilo.

Ukaguzi wangu ulibaini Mamlaka 16 za Serikali za Mitaa zililipa kiasi cha shilingi bilioni 1.80 kwa kazi za ujenzi zilizotekelezwa na wakandarasi na mafundi bila kuwepo na nyaraka za vipimo vya kazi zilizofanyika, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5-16.**

**Jedwali Na.5-16: Malipo Bila Vipimo na Kuidhinishwa na Mhandisi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Iramba | 396,000,000 | 8. | H/W Songwe | 64,624,180 |
| 2. | H/W Sumbawanga | 366,543,619 | 9. | H/Jiji Dar es Salaam | 57,027,265 |
| 3. | H/Mji Makambako | 200,511,135 | 10. | H/W Chunya | 51,123,975 |
| 4. | H/W Njombe | 158,545,000 | 11. | H/W Rorya | 47,153,400 |
| 5. | H/W Momba | 140,264,731 | 12. | H/W Mbozi | 24,206,000 |
| 6. | H/Mji Tunduma | 80,929,500 | 13. | H/W Nsimbo | 10,543,500 |
| 7. | H/W Namtumbo | 67,290,425 | | **Jumla** | **1,797,314,483** |

Aidha nilibaini kuwa shilingi million 872 zililipwa kwa wakandarasi zaidi ya kiasi kilichopaswa kulipwa katika Halmashauri ya Mji Kondoa na Halmashauri ya Wilaya ya Butiama kama inavyoonekana katika **Jedwali 5-17.**

**Jedwali Na.5-17: Malipo kwa Wakandarasi Zaidi ya Kiasi Kilichotakiwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Butiama | 867,441,350 |
| 2. | H/Mji Kondoa | 4,530,000 |
| | **Jumla** | **871,971,350** |

**Maafisa Masuuli wa Halmashauri husika wanahimizwa kuweka mfumo imara wa udhibiti wa ndani utakaohakikisha kazi zilizokamilika zinapimwa na kuthibitishwa kabla ya malipo kufanyika.**

### 5.2.2 Ununuzi wa Shilingi Bilioni 2.85 yalifanyika Bila Kutumia Njia ya Ushindani wa Bei

Kanuni ya 152 ya Kanuni za ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inahitaji miongoni mwa mambo mengine, taasisi nunuzi kutoa nyaraka za zabuni kwa idadi ndogo ya wazabuni ikiwa: kuna hitaji la dharura kwa bidhaa, kazi au huduma kama taasisi haitakuwa na muda wa kutosha kufanya ushindanishi wa bei, na kama kuna uharaka ambao haukutarajiwa na taasisi na haukusababishwa na matendo ya upande wake au haja ya kufikia lengo la kijamii kwa kuyaita makampuni ya ndani au jamii zishiriki. Pia, Kanuni ya 161 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inahitaji taasisi nunuzi kupata nukuu za bei kutoka kwa mzabuni mmoja, kujadili na kuingia katika mkataba moja kwa moja kama; (a) kuna uhitaji wa dharura wa kazi, au (b) kuna mkandarasi mmoja tu ambaye taasisi inategemea anaweza kufanya kazi inayohitajika; au (c) kuna faida kwa taasisi katika kumtumia mkandarasi ambaye amefanya au anaifanya kazi kama hiyo au (d) kazi ambayo inatekelezwa inahitaji kuongezwa.

Katika ukaguzi nilibaini Mamlaka 10 za Serikali za mtaa zilifanya ununuzi wenye thamani ya shilingi billion 2.85 kwa kutumia mzabuni mmoja, au wachache badala ya njia ya ushindanishi kinyume na matakwa ya sheria .idadi ya taasisi hizo zimeorodheshwa kwenye **Jedwali 5-18.**

**Jedwali Na.*5-18*: Ununuzi uliyofanyika bila ushindani**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Mwanza | 958,924,817 |
| 2 | H/W Karagwe | 800,000,000 |
| 3 | H/W Kibaha | 392,734,592 |
| 4 | H/W Bunda | 157,542,330 |
| 5 | H/W Lindi | 154,262,200 |
| 6 | H/Mji Handeni | 113,576,100 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 7 | H/W Mkinga | 112,772,700 |
| 8 | H/W Maswa | 75,000,000 |
| 9 | H/W Tarime | 49,056,840 |
| 10 | H/M Musoma | 39,000,000 |
| **Jumla** | | **2,852,869,579** |

Kufanya ununuzi kwa mzabuni mmoja au idadi ndogo ya wazabuni kunazuia uwazi na nafasi kwa wazabuni wenye uwezo kuomba kazi na kushindana; hivyo kuzuia matumizi bora ya fedha za umma.

**Ninapendekeza Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa njia za ushindanishi wa bei katika ununuzi wa bidhaa zinatumika ili kuwapo na uwazi, uaminifu na kupata thamani ya fedha.**

### 5.2.3 Mapungufu Katika Malipo ya Awali yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 4.13 Pamoja na Dhamana Zake

Kifungu cha 54.2 cha Masharti ya jumla ya mkataba (GCC) kinasema kuwa, mkandarasi anatakiwa kutumia malipo ya awali katika kulipia gharama za vifaa, mitambo, bidhaa na gharama za kuleta vifaa zinazihitajika katika utekelezaji wa mkataba. Mkandarasi anatakiwa kuainisha matumizi ya malipo hayo kwa kuwasilisha uthibitisho wa nakala za ankara au nyaraka nyingine kwa msimamizi wa mradi kwa ajili ya uhakiki.

Wakati wa mapitio ya utendaji na ufuatiliaji wa mikataba, nilibaini mapungufu mbalimbali katika dhamana za malipo ya awali zilizowasilishwa, malipo yake, matumizi na marejesho ya malipo ya awali ya shilingi bilioni 4.13 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali 5-19.**

**Jedwali Na.5-19: Malipo ya awali kwa mkandarasi yenye mapungufu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 1 | H/Jiji Dar es Salaam | 439,416,615 | Malipo ya awali yaliyofanyika kwa mkandarasi bila kuanishwa kwenye mkataba |
| 2 | H/W Kakonko | 60,340,000 | |
| 3 | H/W Bariadi | 70,000,000 | |
| 4 | H/W Tarime | 15,910,268 | Malipo ya awali kwa kiasi kinachozidi asilimia 15 kama ilivyoainishwa kwenye rasimu ya nyaraka ya zabuni iliyotolewa na Mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma (PPRA) |
| 5 | H/W Iramba | 283,356,469 | |
| 6 | H/W Butiama | 180,994,077 | Malipo ya awali kwa mkandarasi ambayo hayajarejeshwa |
| 7 | H/Mji Tarime | 258,872,579 | |
| 8 | H/ Mji Geita | 314,729,469 | |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 9 | H/W Sumbawanga | 34,320,300 | Malipo ya awali yamefanyika kwa mkandarasi bila kuwasilishwa kwa dhamana |
| 10 | H/M Ubungo | 40,690,667 | Malipo ya awali yalifanyika kwa mjenzi bila mkataba |
| 11 | H/M Kahama | 500,000,000 | |
| 12 | H/Jiji Dar es Salaam | 139,114,942 | Uwasilishaji wa dhamana ya malipo ya awali isiyofaa |
| 13 | H/M Ubungo | 578,530,557 | Wakandarasi hawakuwasilisha vielelezo na nyraraka za uthibitisho wa matumizi ya malipo ya awali |
| 14 | H/Mji Geita | 314,729,469 | |
| 15 | H/W Hanang’ | 894,012,314 | |
| **Jumla** | | **4,125,017,726** | |

Kutokuwepo kwa dhamana na kukubali dhamana ya malipo ya awali isiyofaa kunaziweka halmashauri katika hatari ya kupoteza fedha za umma ikiwa mkandarasi atashindwa kutekeleza mkataba. Zaidi ya hayo, hii inaashiria kuwa wasimamizi wa miradi hawakusimamia na kufuatilia miradi kwa ufanisi wakati wa utekelezaji wa mikataba; kutokana na kushindwa kuthibitisha kama malipo ya awali yalitumiwa kwa ufanisi na mkandarasi.

**Nashauri Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wahakikishe kuwa, dhamana sahihi za malipo ya awali zenye kukidhi kipindi chote cha mkataba zinawasilishwa na wakandarasi, ili kuepuka upotevu wa fedha za umma. Zaidi ya hayo,malipo ya awali kwa mkandarasi yafanyike kwa kuzingatia kiwango kilichoainishwa na Mamlaka ya Udhibiti ya ununuzi wa Umma na kuhakikisha wakandarasi wanarejesha fedha hizo.**

### 5.2.4 Mapungufu yaliyoonekana Katika Dhamana za Utendaji wa Mikataba yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 7.64

Kanuni ya 29 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, inahitaji taasisi nunuzi kutaka dhamana ya utendaji kutoka kwa mzabuni aliyeshinda zabuni ili kuhakikisha utendaji wa mkataba wenye uaminifu na malipo ya wafanyakazi wote, wasambazaji, mafundi na wakandarasi wasaidizi wa mradi, kama wapo.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Mamlaka 10 za Serikali za Mitaa zilitekeleza mkataba wa ujenzi na mapato yenye thamani ya shilingi bilioni 7.64 ambayo dhamana za utendaji wake haikuwasilishwa na nyingine zilikwisha muda wake kabla ya kukamilika kwa mkataba kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 5-20.**

**Jedwali Na.5-20: Mapungufu katika dhamana za utendaji zilizowasilishwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kakonko | 160,963,836 | Kutokuwepo kwa dhamana ya Utendaji kwa mradi wa ujenzi inayotekelezwa |
| 2. | H/Jiji Mwanza | 283,502,000 | |
| 3. | H/W Sengerema | 549,440,000 | |
| 4. | H/W Kishapu | 52,533,980 | |
| 5. | H/W Arusha | 472,800,000 | Dhamana ya utendaji kazi haijawasilishwa na wakala wa kukusanya mapato |
| 6. | H/Jiji Dodoma | 2,831,349,751 | Dhamana ya utendaji kazi imekwisha muda wake kabla ya kukamilika kwa mradi |
| 7. | H/Mji Geita | 2,407,569,051 | |
| 8. | H/W Nsimbo | 388,981,782 | |
| 9. | H/W Sumbawanga | 76,728,040 | |
| 10. | **H/W Arusha** | 414,000,000 | Uwepo wa dhamana ya utendaji iliyoisha muda wake kwa mkataba wa ukusanyaji mapato |
| **Jumla** | | **7,637,868,440** | |

Kutokuwapo kwa dhamana za utendaji na kumalizika kwa muda wa dhamana za utendaji kazi kabla ya kukamilisha utekelezaji wa mikataba, kunaziweka Halmashauri kwenye hatari ya kupoteza fedha za miradi endapo wakandarasi watashindwa kutekeleza mkataba au wakisitisha.

**Ninashauri Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za mitaa husika kuhakikisha wakandarasi wanawasilisha dhamana za utendaji zinazokidhi kipindi chote cha mkataba. Aidha, katika siku zijazo wahakikishe mikataba yote inakuwa na dhamana kwa muda wote wa mkataba ili kuepuka upotevu wa rasilimali za umma.**

### 5.2.5 Ucheleweshwaji wa Malipo kwa Kazi Iliyofanyika yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 7.8

Kanuni ya 44(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inasema kuwa, kwa madhumuni ya kusaidia ukuaji wa makampuni ya ndani na kuwezesha makampuni hayo kutimiza majukumu yao ya kimkataba, taasisi nunuzi zitahakikisha kwamba malipo yanafanyika kwa wakati kwa wazabuni.

Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) yanawataka waajiri kuwalipa wakandarasi kiasi kilichoidhinishwa na Wasimamizi wa Miradi ndani ya siku 28 kuanzia tarehe ya kuwasilishwa cheti cha madai ya malipo kwa mkandarasi.

Mapitio ya uzingatiwaji wa sheria na masharti yaliyoainishwa kwenye mikataba yalibainisha Halmashauri 3 zenye madai ya wakandarasi kiasi cha shiling bilioni 7.8 ambayo hayajalipwa kwa muda wa zaidi ya siku 90 tangu tarehe ya uhakiki. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali 5-21.**

**Jedwali Na.5-21: Malipo ya Wakandarasi Ambayo Hayajalipwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Ubungo | 6,721,159,349 |
| 2. | H/Jiji Dodoma | 768,963,484 |
| 3. | H/M Iringa | 310,830,795 |
| | **Jumla** | **7,800,953,628** |

Kucheleweshwa kwa utoaji wa fedha kunaweza kusababisha athari kwenye muda wa utekelezaji wa miradi, na kusababisha ucheleweshaji wa malipo na hatimaye kuchelewesha kukamilika kwa miradi.

**Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ihakikishe kuwa fedha za miradi ya ujenzi zinatolewa kwa wakati. Hii itarahisisha utekelezaji wa miradi hiyo na kuepusha riba na adhabu zisizo za lazima.**




# SURA YA SITA

# USIMAMIZI WA MAPATO

## 6.0 Utangulizi

Vyanzo vya mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa vinajumuisha kodi, leseni, ada, faini, adhabu, mapato yatokanayo na ubadilishanaji wa bidhaa au huduma, na mapato mengineyo. Ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi ni muhimu katika kuimarisha maendeleo endelevu katika Mamlaka za serikali za Mitaa ili kufanikisha dhana ya uwekezaji katika rasilimali watu, miundombinu na utoaji wa huduma bora kwa Umma.

Kulingana na mwenendo wa hivi karibuni, ukusanyaji wa mapato ya vyanzo vya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeongezeka kufikia shilingi milioni 891.84 katika mwaka wa fedha 2021/22 ikilinganishwa na miaka iliopita kama inavyooneshwa katika **Kilelezo Na 6-1**.

**Kielelezo Na 0-1: Mwenendo wa Mapato ya Ndani**




Ukusanyaji wa mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kimsingi hufanywa kupitia Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS), Mfumo wa Taarifa za Kifedha unaotumiwa

katika ngazi za chini za Halmashauri (FFARS) na Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT–HoMIS).

Mifumo hii inatoa mwanga wa taarifa za kifedha za taasisi, zinazosaidia katika usimamizi bora wa huduma za afya. Utekelezaji wa mifumo hii in wa muhimu katika mamlaka za serikali za mitaa, kurahisisha mchakato wa ukusanyaji wa mapato, kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha, na kuboresha usahihi wa taarifa za kifedha.

kutokana na tathmini yangu ya usimamizi wa makusanyo ya mapato katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mapungufu kadhaa yalibainika, kama yanavyoelezwa kwenye aya zinazofuata hapa chini.

Ili kukabiliana na mapungufu haya, Halmashauri zinapaswa kutekeleza mfumo bora wa udhibiti wa mifumo ya ndani, kutumia kikamilifu mifumo ya kielektroniki ili kupunguza vihatarishi vya ubadhilifu. Pia, uvumbuzi wa vyanzo muhimu vya mapato na utekelezaji wa mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ikiwemo, tathimini ya masoko, elimu kwa walipa kodi na mikakati ya mawasiliano katika ngazi zote za serikali.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kutekeleza mifumo ya usimamizi wa madeni,kutumia mifumo ya kielektroniki kubaini walio katika hatari kubwa ya kutolipa madeni na kuweka kipaumbele katika ufuatiliaji.

## 6.1 Kutowasilishwa Benki Shilingi Bilioni 11.07 za Mapato Yaliyokusanywa Kupitia POS

Kifungu cha 42 (2) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 kinaelekeza kuwa, stakabadhi zote zinazohusiana na mamlaka ya serikali ya mitaa zitalipwa katika akaunti ya benki au akaunti iliyothibitishwa na mamlaka hiyo. Pia, kwa mujibu wa Aya ya 3.4 (v) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuchukua hatua stahiki za udhibiti, ikijumuisha uwekaji wa mapato yanayokusanywa benki kwa haraka ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato.

Nilitathmini taarifa za mapato kutoka mfumo wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vingine vilivyokusanywa kupitia

mashine za POS na kubaini kuwa, wakusanya mapato katika mamlaka 98 za serikali za mitaa hawakuwasilisha jumla ya shilingi bilioni 11.07 katika akaunti husika za benki.

Hii inatokana na kutofanyika kwa usuluhishi wa hesabu mara kwa mara (angalau kwa wiki) na kukosekana kwa ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha makusanyo ya mapato yanawekwa kwenye akaunti ya benki ya Halmashauri pekee na si kwa njia zinginezo kama vile huduma za benki kupitia mitandao ya simu. Pia, kwa kuwa njia pekee inayotumika ni ya wakusanya mapato kuwasilisha wenyewe benki fedha zilizokusanywa, hali hii imesababisha kuongezeka kwa fedha zisizowasilishwa benki hasa kwa wakusanya mapato ambao wapo nje ya miji. Maelezo ya mapato ambayo hayajapelekwa benki yameoneshwa katika **Jedwali Na. 6 -1**

**Jedwali Na.6-1: Makusanyo Yasiyowasilishwa Benki**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 1,097,974,053 | 51. | H/W Chalinze | 39,869,116 |
| 2. | H/W Ushetu | 608,964,726 | 52. | H/W Buchosa | 39,666,921 |
| 3. | H/W Momba | 584,568,405 | 53. | H/Mji Handeni | 37,939,222 |
| 4. | H/W Kilwa | 462,312,040 | 54. | H/W Iringa | 37,011,441 |
| 5. | H/M Kinondoni | 444,758,715 | 55. | H/M Shinyanga | 36,542,500 |
| 6. | H/W Uvinza | 440,485,000 | 56. | H/W Njombe | 32,827,500 |
| 7. | H/W Tabora/UYUI | 381,752,353 | 57. | H/M Temeke | 30,017,500 |
| 8. | H/W Kilindi | 371,482,920 | 58. | H/W Moshi | 29,125,777 |
| 9. | H/W Chemba | 351,513,269 | 59. | H/W Urambo | 28,921,278 |
| 10. | H/W Rufiji | 328,240,356 | 60. | H/W Bumbuli | 24,618,094 |
| 11. | H/W Bunda | 324,565,133 | 61. | H/W Butiama | 22,777,200 |
| 12. | H/W Kisarawe | 310,927,230 | 62. | H/W Igunga | 21,127,420 |
| 13. | H/W Sumbawanga | 309,925,337 | 63. | H/W Busega | 19,829,503 |
| 14. | H/W Kibaha | 238,644,492 | 64. | H/W Manyoni | 18,978,000 |
| 15. | H/W Mafia | 232,619,351 | 65. | H/W Kibiti | 18,349,589 |
| 16. | H/M Iringa | 230,325,110 | 66. | H/W Ileje | 18,335,950 |
| 17. | H/W Kaliua | 209,406,651 | 67. | H/W Maswa | 18,079,600 |
| 18. | H/W Musoma | 194,692,833 | 68. | H/Jiji Mwanza | 16,739,050 |
| 19. | H/W Namtumbo | 194,294,441 | 69. | H/Mji Geita | 14,712,373 |
| 20. | H/W Kalambo | 192,018,700 | 70. | H/W Gairo | 14,666,200 |
| 21. | H/W Itigi | 178,837,075 | 71. | H/W Mpanda | 14,478,200 |
| 22. | H/W Kilolo | 173,775,327 | 72. | H/W Mkuranga | 14,051,300 |
| 23. | H/W Mbarali | 157,199,015 | 73. | H/W Rorya | 14,011,520 |
| 24. | H/W Mbozi | 138,045,037 | 74. | H/W Babati | 13,661,300 |
| 25. | H/W Songwe | 127,029,748 | 75. | H/W Meatu | 13,385,398 |
| 26. | H/W Chunya | 119,681,800 | 76. | H/Mji Babati | 13,119,351 |
| 27. | H/W Msalala | 115,793,599 | 77. | H/W Busokelo | 13,059,395 |
| 28. | H/Jiji Arusha | 113,964,030 | 78. | H/W Nyasa | 12,701,500 |
| 29. | H/W Sikonge | 113,129,836 | 79. | H/W Mbinga | 12,371,950 |
| 30. | H/W Mbeya | 111,374,287 | 80. | H/W Lindi/Mtama | 12,231,557 |
| 31. | H/W Songea | 95,618,775 | 81. | H/W Tarime | 12,198,712 |
| 32. | H/W Serengeti | 93,066,401 | 82. | H/W Kigoma | 9,785,958 |
| 33. | H/W Kyela | 86,115,714 | 83. | H/W Meru | 8,577,500 |

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 34. | H/M Morogoro | 85,231,611 | 84. | H/Mji Mbinga | 8,346,500 |
| 35. | H/W Iramba | 84,142,177 | 85. | H/W Geita | 8,142,900 |
| 36. | H/W Nkasi | 84,041,700 | 86. | H/W Hai | 7,982,550 |
| 37. | H/W Mbogwe | 80,360,474 | 87. | H/M Tabora | 7,631,600 |
| 38. | H/W Kasulu | 79,368,780 | 88. | H/M Songea | 7,148,900 |
| 39. | H/W Nyang'hwale | 77,226,160 | 89. | H/W Nzega | 7,043,700 |
| 40. | H/W Hanang' | 73,460,450 | 90. | H/W Mbulu | 6,858,000 |
| 41. | H/W Kigoma/Ujiji | 72,971,927 | 91. | H/W Mlele | 6,266,757 |
| 42. | H/W Rungwe | 70,393,156 | 92. | H/W Mwanga | 5,629,000 |
| 43. | H/W Nsimbo | 70,013,483 | 93. | H/W Muleba | 5,400,000 |
| 44. | H/Jiji Mbeya | 67,045,837 | 94. | H/W Same | 4,799,700 |
| 45. | H/W Bariadi | 66,830,623 | 95. | H/W Kiteto | 3,916,000 |
| 46. | H/M Lindi | 61,399,151 | 96. | H/W Singida | 3,742,949 |
| 47. | H/W Muheza | 54,908,059 | 97. | H/W Liwale | 3,089,160 |
| 48. | H/W Simanjiro | 53,579,000 | 98. | H/W Arusha | 2,741,700 |
| 49. | H/M Singida | 45,483,582 | | **Jumla** | **11,072,457,731** |
| 50. | H/W Kibondo | 40,392,510 | | | |

Hatahivyo, kiasi cha fedha za mapato kisichowasilishwa benki kwa mwaka 2021/22 kimepungua kufikia shilingi bilioni 11.07 ikilinganishwa na mwaka 2020/21; uwepo wa shilingi bilioni 11.07 kisichowasilishwa benki inaashiria uhitaji wa jitihada za ziada ili kuondosha uvujaji wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa. Mwenendo wa makusanyo ambayo hayajawasilishwa benki ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 6- 2.**

**Kielelezo Na 0-2: Mwenendo wa makusanyo yasiyowalishwa benki**




Kutowasilishwa benki kwa makusanyo ya vyanzo hivyo, hupunguza uwezo wa Halmashauri kufanya shughuli ilizojipangia na kupelekea utegemezi zaidi kwa Serikali Kuu.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI ifanye mapitio ya taratibu za kuwasilisha benki mapato yanayokusanywa kupitia POS na kuweka sera za udhibiti zikiwemo za makubaliano kati ya Halmashauri na watumiaji wa POS juu ya uzingatiaji wa muda wa kuwasilisha makusanyo benki na utozaji wa faini kwa ucheleweshaji ili kuhakikisha fedha zinawasilishwa benki kwa wakati,aidha ninasisitiza Mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kwamba fedha ambazo hazikuwasilishwa benki zinarejeshwa.**

**Zaidi ya hayo, Mamlaka hizo zinashauriwa kuhakikisha zinatumia kiusahihi mifumo ya kielektroniki kupitia makampuni ya simu na mabenki ili kurahisisha uwekaji wa mapato yanayokusanywa kupitia POS.**

## 6.2 Mapato ya Shilingi Bilioni 37.34 Yasiyokusanywa Kutoka katika Vyanzo Muhimu vya Mapato

Nilikagua makusanyo ya mapato kupitia Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kubaini kuwa, jumla ya shilingi bilioni 37.34 hazikukusanywa katika mamlaka 146 za serikali za mitaa. Vyanzo vilivyoathirika ni kodi zitokanazo na upangishaji wa maduka na nyumba vilivyopo katika stendi za mabasi na masoko, kodi za kupangisha vibanda na vizimba vya masoko,kodi ya nyumba, kodi za upangishaji wa maeneo ya wazi, na fukwe uuzaji wa viwanja, ada za uwindaji leseni za biashara, na leseni za vileo.

Hali hii ni kinyume na Agizo la 38 (1) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, linalomtaka mwekahazina kuwajibika kufanya taratibu sahihi za usimamizi wa fedha na uhasibu ili kuhakiki usahihi wa kumbukumbu za madai yote kwa kulinganisha na makusanyo; uhifadhi na uwekaji wa fedha hizo benki. Muhtasari wa vyanzo hivi unaelezewa katika **Jedwali Na. 6-2** na **Kiambatisho Na. 6-2** kinatoa maelezo ya kina kwa mapato ambayo hayajakusanywa.

**Jedwali Na.6-2: Vyanzo vya Mapato Visivyokusanywa**

| Na | Chanzo cha mapato | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Leseni za biashara | 112 | 13,940,477,444 |
| 2 | Mauzo ya viwanja | 17 | 12,292,508,723 |
| 3 | Kodi za pango | 64 | 5,642,483,546 |
| 4 | Ushuru wa Taka | 2 | 3,016,026,871 |
| 5 | Leseni za vileo | 59 | 1,712,215,056 |
| 6 | Fukwe/Maeneo ya wazi | 2 | 292,613,800 |
| 7 | Ushuru wa huduma za uwindaji | 3 | 439,606,284 |
| **Jumla** | | | **37,335,931,724** |

Hatahivyo, uthibitisho wa makusanyo ya fedha kutoka kiwanda cha kufyatua tofali katika Halmashauri ya Jiji la Arusha unaonesha kuwa shilingi milioni 353.41 zilipatikana ambayo ni kati ya makadirio ya mauzo ya shilingi milioni 717.97 kulingana na vifaa vilivyonunuliwa. Ukokotoaji wa ulinganifu wa vifaa viliyonunuliwa na fedha zilizopatikana ulibaini kuwa kuna uwezekano mkubwa wa matumizi mabaya ya shilingi milioni 364.56 kwani hakuna uthibitisho wa kutosha kuhalalisha matumizi hayo ikiwemo vifaa visivyotumika au madeni ya wateja.,

Mapato ambayo hayajakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa yanaweza kusababisha hasara kutokana na juhudi zisizoridhisha za kukusanya fedha hizo.

**Ninanazishauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika kwa kushirikiana na Watendaji wa kata na mitaa/vijiji ziweke mifumo madhubuti ya utambuzi na ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyote vya mapato, mathalani uhuishaji wa kanzidata ya walipaji, ukumbushaji wa wadaiwa/walipa kodi kwa kuwatumia bili husika kupitia jumbe za simu, ufuatiliaji kupitia kikosi kazi cha ukusanyaji wa mapato na utoaji wa taarifa za wadaiwa na mbinu za ufuatiliaji kila mwezi ili kukusanya kikamilifu katika vyanzo vyote vya mapato na kuhakikisha urejeshwaji wa mapato ambayo hayajakusanywa.**

## 6.3 Miamala ya Shilingi bilioni 13.15 ya Madai Mbalimbali ya Mapato Isiyosuluhishwa

Aya ya 6.7 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unataka utengenezaji wa hati za madai na usimamizi wa madai ya mapato ufanyike kupitia Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato. Kisha, walipakodi wenye madeni wafuatiliwe kupitia mfumo huo na kujulishwa kwa wakati ili kuhakikisha malipo yanafanyika kupitia benki au kielekitroniki na kuhuishwa katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato mara tu baada ya malipo kufanyika.

Nilibaini kuwa, kiasi cha shilingi bilioni 13.15 hakikusanywa katika mamlaka 59 za serikali za mitaa kutoka vyanzo mbalimbali ndani ya mfumo wa mapato wa LGRCIS bila kubainisha sababu, kinyume na miongozo iliyotajwa hapo juu.

Bila udhibiti na juhudi za kutosha, kuna uwezekano wa ukusanyaji wa mapato chini ya malengo. **Jedwali Na. 6-3** linaonesha wadaiwa wa mapato mbalimbali.

**Jedwali Na.6-3: Wadaiwa wa Mapato Mbalimbali**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es salaam | 4,273,261,779 | 31. | H/M Mpanda | 58,587,485 |
| 2. | H/W Simanjiro | 1,106,439,925 | 32. | H/W Ngorongoro | 56,697,908 |
| 3. | H/W Kilosa | 712,396,747 | 33. | H/W Missenyi | 49,484,496 |
| 4. | H/M Bukoba | 668,217,232 | 34. | H/W Muleba | 47,679,258 |
| 5. | H/W Morogoro | 533,706,011 | 35. | H/W Njombe | 46,558,653 |
| 6. | H/Jiji Tanga | 450,979,377 | 36. | H/Mji Korogwe | 45,746,895 |
| 7. | H/W Namtumbo | 435,294,332 | 37. | H/W Mkinga | 38,394,612 |
| 8. | H/M Iringa | 416,174,212 | 38. | H/W Kwimba | 35,796,517 |
| 9. | H/W Kilindi | 371,482,920 | 39. | H/Mji Makambako | 33,329,842 |
| 10. | H/W Kilolo | 359,407,937 | 40. | H/M Songea | 32,821,302 |
| 11. | H/Mji Masasi | 285,246,802 | 41. | H/M Moshi | 32,334,300 |
| 12. | H/W Ruangwa | 264,956,830 | 42. | H/W Nsimbo | 27,406,814 |
| 13. | H/W Korogwe | 211,270,206 | 43. | H/W Mbozi | 23,513,931 |
| 14. | H/Jiji Arusha | 203,339,613 | 44. | H/Mji Newala | 22,946,190 |
| 15. | H/W Mpanda | 201,441,963 | 45. | H/W Kalambo | 22,044,995 |
| 16. | H/W Rufiji | 201,366,283 | 46. | H/W Bumbuli | 21,534,507 |
| 17. | H/W Monduli | 178,599,677 | 47. | H/W Longido | 20,732,700 |
| 18. | H/W Songwe | 165,542,500 | 48. | H/W Itigi | 20,520,103 |
| 19. | H/Mji Bariadi | 159,160,416 | 49. | H/W Nanyumbu | 19,644,172 |
| 20. | H/M Shinyanga | 155,595,376 | 50. | H/W Kibaha | 19,164,936 |
| 21. | H/W Nyasa | 149,273,871 | 51. | H/W Maswa | 18,379,930 |
| 22. | H/W Newala | 138,483,991 | 52. | H/W Tarime | 18,154,079 |
| 23. | H/W Meru | 118,980,117 | 53. | H/W Tandahimba | 17,555,290 |
| 24. | H/W Busega | 112,918,293 | 54. | H/W Igunga | 16,887,755 |
| 25. | H/Mji Mbinga | 106,061,402 | 55. | H/M Musoma | 11,290,550 |
| 26. | H/W Muheza | 103,256,463 | 56. | H/W Chalinze | 11,028,224 |
| 27. | H/M Mtwara | 92,393,717 | 57. | H/W Mlele | 7,307,835 |
| 28. | H/W Madaba | 64,092,027 | 58. | H/W Mwanga | 6,279,375 |
| 29. | H/W Uyui | 63,010,942 | 59. | H/Mji Nanyamba | 4,504,570 |
| 30. | H/W Ushetu | 59,532,193 | **Jumla** | | **13,148,210,378** |

Ingawa mamlaka za serikali za mitaa zimefanya jitihada za kupunguza kiasi cha wadaiwa hawa kwa miaka mitatu mfululizo, kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 6-3** hapa chini; hata hivyo, kiasi cha shilingi bilioni 13.15 kinaonesha kuwa bado kuna haja ya kuchukuliwa kwa jitihada zaidi ili kuondoa uwepo wa wadaiwa mbalimbali ambao hawajapatiwa ufumbuzi.

Kielelezo Na 0-3: Mwenendo wa Madai




**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa ziweke udhibiti ili kuhakikisha kwamba wadaiwa wote wanahakikiwa kabla ya kufanya marekebisho na hatimaye kukusanya mapato kwa madai yanayostahili;**

**Aidha, kuwe na utaratibu wa kufanya usuluhishi angalau kila mwezi kuhusiana na wadaiwa husika ili kupunguza vihatarishi vya upotevu na kuhakikisha usimamizi bora katika mapato.**

## 6.4 Kutowasilishwa kwa Shilingi Bilioni 4.94 na Mawakala wa Ukusanyaji Mapato

Kifungu cha 26 (a) na (b) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kinamtaka mtu anayestahili kuteuliwa na mamlaka za serikali za mitaa, kukusanya na kupokea kiasi stahiki kutoka kwa kila mlipakodi katika eneo ambalo amepangiwa; na kuhakikisha kiasi chote kilichokusanywa kinalipwa kwa mamlaka ya serikali ya mtaa inayohusika.

Nilipitia usimamizi wa mapato na kubaini kuwa, menejimenti 1 1 za mamlaka za serikali za mitaa ziliingia mikataba 122 na mawakala wa kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vyenye thamani ya shilingi bilioni 14.46.

Mapitio zaidi ya Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa yalibaini kuwa, ni shilingi bilioni 9.74 pekee ndizo zilizowasilishwa kwa mamlaka za serikali za mitaa, na hivyo kuacha shilingi bilioni 4.72 bila kuwasilishwa kwa mujibu wa mikataba. **Jedwali Na. 6-4** linaonesha orodha ya halmashauri za wilaya ambazo makusanyo hayakuwasilishwa.

**Jedwali Na.6-4: Taarifa ya Makusanyo ya Mawakala**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Mikataba | Kiasi (Sh.) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kimkataba | Kilichowasilishwa | Kinachodaiwa |
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 11 | 2,987,756,000 | 1,877,468,800 | 1,110,287,200 |
| 2. | H/M Morogoro | 2 | 1,789,636,800 | 751,429,629 | 1,038,207,171 |
| 3. | H/M Kinondoni | 11 | 615,055,332 | 0 | 615,055,332 |
| 4. | H/W Buchosa | 19 | 1,025,510,000 | 570,493,481 | 455,016,519 |
| 5. | H/Jiji Mwanza | 13 | 2,171,220,000 | 1,731,269,200 | 439,950,800 |
| 6. | H/W Arusha | 4 | 404,640,000 | 114,973,500 | 289,666,500 |
| 7. | H/W Rufiji | 1 | 99,000,000 | 39,000,000 | 60,000,000 |
| 8. | H/W Iringa | 11 | 2,836,273,409 | 2,799,261,968 | 37,011,441 |
| 9. | H/W Meru | 6 | 67,195,961 | 33,562,656 | 33,633,305 |
| 10. | H/W Bagamoyo | 37 | 69,837,900 | 36,637,200 | 33,200,700 |
| **Jumla** | | **115** | **12,066,125,402** | **7,954,096,434** | **4,112,028,968** |

***Chanzo:*** *Mikataba inayotekelezwa*

Aidha, nilibaini kutowasilishwa benki kwa makusanyo ya shilingi milioni 211.87 yatokanayo na ada ya ukusanyaji taka kutoka kwa mawakala watatu walioingia mkataba na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kinyume na Kifungu cha 4.4 cha mkataba ambacho kinamtaka wakala kuweka makusanyo yote ya mapato benki kila siku.

Hakuna hatua zilizochukuliwa na mamlaka za serikali za mitaa kuhusiana na kiasi ambacho hakijakusanywa kwa mujibu wa mikataba. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa kipengele katika mikataba iliyosainiwa kinachoelezea hatua zitakazochukuliwa dhidi ya wakala atakayeshindwa kufikia malengo ya urejeshaji kwa mujibu wa mkataba.

Kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kupitia mawakala kunazuia utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa katika siku zijazo zifanye upembuzi yakinifu unaoakisi uhalisia wa malengo ya makusanyo katika vyanzo vya mapato, huku zikihakikisha mikataba inaeleza wazi hatua zitakazochukuliwa dhidi ya mawakala watakaoshindwa kuwasilisha kiasi kilichokubaliwa;**

**Kwa mikataba ambayo tayari ina vifungu vinavyoeleza hatua dhidi ya mawakala walioshindwa kuwasilisha makusanyo kulingana na makubaliano, ninashauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuchukua hatua stahiki dhidi ya mawakala hao ili wawasilishe mapato ambayo hayajarejeshwa.**

## 6.5 Marekebisho ya Ankara zenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.79 bila Viambatisho Toshelevu

Agizo la 37 (6) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaeleza kwamba, kama stakabadhi imekosewa, itenguliwe mara moja na itolewe mpya. Stakabadhi halisi iliyotenguliwa ihifadhiwe kwa ukaguzi. Pia, Aya ya 3.4 (vii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha marekebisho na ufutaji wa ankara zisizo sahihi katika Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Usimamizi wa Fedha (IFMIS) au Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) kuidhinishwa na mkurugenzi wa Halmashauri.

Nilipitia marekebisho ya ankara yaliyofanyika katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kubaini kuwa, Mamlaka 14 za Serikali za Mitaa zilirekebisha ankara za kiasi cha shilingi Bilioni 1.79 katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato bila maelezo na/au viambatisho toshelevu ili kuhalalisha mabadiliko ya ankara zinazohusika wakati baadhi ya Halmashauri zilifanya marekebisho bila idhini ya Wakurugenzi.

Kukosekana kwa viambatisho hivyo, sikuweza kuthibitisha juu ya uhalali wa marekebisho yaliyofanywa. Kwa maoni yangu, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika hazikutekeleza kikamilifu hatua za udhibiti kama inavyotakiwa na Agizo la 37(6) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Aya ya

3.4 (vii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019. Maelezo ya marekebisho hayo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 6-5**.

**Jedwali Na.6-5: Ankara Zilizorekebishwa Bila Viambatisho**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Kilindi | 907,543,590 |
| 2. | H/Jiji Tanga | 257,104,456 |
| 3. | H/W Musoma | 101,711,906 |
| 4. | H/W Nyasa | 101,504,544 |
| 5. | H/W Manyoni | 88,419,000 |
| 6. | H/W Kasulu | 75,476,500 |
| 7. | H/Mji Tarime | 67,506,441 |
| 8. | H/M Kahama | 63,100,000 |
| 9. | H/W Uvinza | 30,808,650 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 10. | H/W Iramba | 29,432,771 |
| 11. | H/M Iringa | 24,526,237 |
| 12. | H/M Lindi | 23,816,430 |
| 13. | H/W Wanging'ombe | 12,784,456 |
| 14. | H/W Mwanga | 11,072,487 |
| **Jumla** | | **1,794,807,468** |

*Chanzo:Taarifa ya Mfumo wa kukusanyia mapato*

Kwa maoni yangu, marekebisho bila kuwa na vielelezo vya kutosha na kibali yanaziweka Halmashauri kwenye hatari ya ubadhilifu wa mapato bila kugundulika na uongozi wa Halmashauri.

**Ninatoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka udhibiti sahihi ili kusaidia utunzaji wa viambatisho vya ankara za mapato zinazorekebishwa au kufutwa kwa kuhuisha au kupakia nyaraka husika katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato kabla ya kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri.**

## 6.6 Kutokuwa na Ufanisi Katika Makadirio na Ukusanyaji wa Ushuru wa Huduma Shilingi Bilioni 36.22

Vifungu vya 6(1) (u) na 7(1) (y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kama iliyorekebishwa na Kifungu cha 44 na 45 cha Sheria ya Fedha, 2020 ambavyo vinaeleza kuwa chanzo cha mapato ni pamoja fedha zote zinazotokana na ushuru wa huduma zinazolipwa na taasisi au mtu binafsi anayeendesha biashara, na mwenye leseni halali ya biashara ambayo mauzo ghafi kwa mwaka yanazidi shilingi milioni nne, na utozaji ni kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mauzo ghafi baada ya kupunguza kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa: ili mradi, matawi ya taasisi husika yatalipa ushuru wa huduma katika maeneo ya Halmashauri.

Nimetathmini ufanisi wa ukusanyaji wa ushuru wa huduma na kubaini kuwa, Halmashauri 40 hazikukusanya ushuru wa huduma wa kiasi cha shilingi bilioni 36.22kutoka kwa wafanyabiashara wanaofanya kazi ndani ya mamlaka ya Halmashauri husika.

Hii inatokana na juhudi hafifu za kuwasilisha madai kwa taasisi husika na kukosekana kwa kanzidata yenye taarifa halisi za wafanyabiashara. Orodha ya Halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 6-6.**

**Jedwali Na.6-6: Ushuru wa Huduma Usiokusanywa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 25,961,761,567 | 22. | H/W Chunya | 57,239,267 |
| 2. | H/Jiji Arusha | 6,334,913,229 | 23. | H/M Ilemela | 48,114,055 |
| 3. | H/Jiji Mbeya | 766,747,216 | 24. | H/W Mbarali | 44,840,952 |
| 4. | H/M Iringa | 667,570,073 | 25. | H/W Longido | 40,591,907 |
| 5. | H/M Musoma | 274,060,513 | 26. | H/W Butiama | 37,912,813 |
| 6. | H/W Chalinze | 208,748,489 | 27. | H/W Kwimba | 37,094,759 |
| 7. | H/W Mbinga | 202,041,270 | 28. | H/Mji Korogwe | 29,873,270 |
| 8. | H/W Tunduru | 192,798,754 | 29. | H/W Ileje | 26,633,108 |
| 9. | H/M Kigamboni | 150,250,560 | 30. | H/W Rorya | 24,820,027 |
| 10. | H/W Iringa | 137,959,221 | 31. | H/W Wanging'ombe | 24,748,405 |
| 11. | H/W Muheza | 126,689,895 | 32. | H/W Ukerewe | 24,700,000 |
| 12. | H/W Uyui | 99,284,813 | 33. | H/Jiji Tanga | 23,734,591 |
| 13. | H/W Chato | 82,042,992 | 34. | H/W Mbozi | 14,626,737 |
| 14. | H/Mji Bunda | 77,236,386 | 35. | H/W Muleba | 12,532,350 |
| 15. | H/W Njombe | 76,750,865 | 36. | H/Mji Tunduma | 7,138,235 |
| 16. | H/W Rungwe | 72,847,642 | 37. | H/W Momba | 6,318,153 |
| 17. | H/W Kilindi | 70,574,545 | 38. | H/W Hanang | 2,815,106 |
| 18. | H/W Kilolo | 66,470,081 | 39. | H/W Pangani | 2,780,486 |
| 19. | H/Mji Njombe | 63,812,059 | 40. | H/W Biharamulo | 637,212 |
| 20. | H/W Mufindi | 63,520,184 | **Jumla** | | **36,223,596,056** |
| 21. | H/W Songwe | 60,364,269 | | | |

Kwa maoni yangu, kutozakiwango cha kodi cha kuanzia asilimia sifuri mpaka asilimia 0.3 kinaweza kutoa mwanya wa ukwepaji wa ushuru wa huduma.

Mamlaka za serikali za mitaa husika zimeshindwa kukusanya ushuru wa huduma kama chanzo cha mapato, hali ambayo inaathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

**Ninapendekeza Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa, kanzidata za biashara zinahuishwa na ufuatiliaji wa kutosha unafanyika kupitia ngazi zote ikiwa ni pamoja na Kata na Vijiji ili kukusanya ushuru wa huduma kwa ukamilifu.**

## 6.7 Kutowasiliana kwa Mifumo kumepelekea kutokusanya Ushuru wa Huduma wa Shilingi Bilioni 8.02

Aya ya 6.6.1(iii & iv) ya Mwongozo wa usimamizi wa Mapato ya mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 inafafanua mkakati na taratibu za ukusanyaji wa ushuru wa huduma ukijumuisha utoaji wa fomu ya kukiri jumla ya mauzo ghafi ambayo hujazwa na mlipakodi na inaweza kutumika katika utozaji wa ushuru wa huduma.

Nilibaini kuwa Mamlaka 38 za Serikali za Mitaa zilikusanya ushuru wa huduma wenye jumla ya shilingi bilioni 8.02 bila kupata ushahidi wa taarifa za mauzo ghafi kutoka mamlaka husika au taasisi husika ili kuthibitisha kiasi kilichokusanywa. Maelezo zaidi ya ushuru wa huduma uliokusanywa bila vithibitisho vya mauzo ghafi yametolewa katika **Jedwali Na. 6-7.**

**Jedwali Na.6-7: Makusanyo ya Ushuru wa Huduma Bila Uthibitisho**

| Na. | Jina La Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | 2,098,190,919 | 21. | H/W Mvomero | 63,905,430 |
| 2. | H/W Tarime | 743,351,267 | 22. | H/M Mpanda | 62,663,027 |
| 3. | H/M Bukoba | 606,161,904 | 23. | H/W Mpimbwe | 61,615,558 |
| 4. | H/W Mbeya | 591,712,785 | 24. | H/W Kondoa | 59,040,515 |
| 5. | H/W Misungwi | 548,849,690 | 25. | H/M Shinyanga | 56,370,776 |
| 6. | H/M Kigoma/Ujiji | 424,287,200 | 26. | H/W Babati | 42,917,621 |
| 7. | H/M Songea | 383,015,120 | 27. | H/W Mafia | 42,834,853 |
| 8. | H/W Ngorongoro | 291,061,812 | 28. | H/W Same | 40,617,681 |
| 9. | H/Mji Ifakara | 258,412,781 | 29. | H/W Iramba | 37,890,568 |
| 10. | H/M Kahama | 215,091,868 | 30. | H/W Namtumbo | 31,658,347 |
| 11. | H/W Msalala | 182,304,990 | 31. | H/Mji Kondoa | 28,851,741 |
| 12. | H/M Musoma | 178,409,118 | 32. | H/W Korogwe | 26,654,980 |
| 13. | H/W Shinyanga | 150,006,037 | 33. | H/W Nyasa | 26,262,634 |
| 14. | H/W Biharamulo | 137,148,493 | 34. | H/W Rufiji | 25,680,034 |
| 15. | H/W Chato | 117,385,693 | 35. | H/Jiji Mwanza | 20,524,814 |
| 16. | H/W Kwimba | 101,052,139 | 36. | H/W Busokelo | 20,214,665 |
| 17. | H/W Lushoto | 89,405,677 | 37. | H/Mji Newala | 17,482,194 |
| 18. | H/W Malinyi | 86,573,247 | 38. | H/W Itigi | 11,652,266 |
| 19. | H/W Pangani | 76,918,953 | | **Jumla** | **8,023,104,102** |
| 20. | H/W Handeni | 66,926,705 | | | |

Ushuru wa huduma unaweza kukusanywa pungufu kutokana na kukosekana kwa taarifa za mauzo ghafi ambazo zingeweza kutumika katika kukokotoa kiasi stahiki cha ushuru wa huduma ambacho kinatakiwa kulipwa na mlipa kodi.

**Ninapendekeza kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI katika siku zijazo zihuishe mfumo wa kielektroniki utakaowezesha kupeana taarifa za mauzo ghafi au taarifa nyingine zitakazorahisisha ukokotoaji wa kiasi kinachostahili kulipwa kama ushuru wa huduma. Pia, nawasihi menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kwa kutumia fomu za kukiri mauzo ghafi inayojazwa na mlipakodi kabla ya kumtoza.**

## 6.8 Ushuru wa Mazao Usiokusanywa Shilingi Bilioni 3.03

Kifungu cha 7(1) (g) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 kinaeleza kuwa fedha zote zitokanazo na malipo yoyote yanayolipwa katika chanzo cha mazao ya kilimo au mazao mengine yanayozalishwa katika eneo la Halmashauri ya Wilaya, zilizowekwa chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote isipokuwa kwa mazao muhimu yanayosafirishwa kwaajili ya mauzo ya nje ya nchi ambayo ushuru husika utaanzia kati ya sifuri. na asilimia tano ya bei ya lango la shamba na italipiwa kwenye chanzo cha mauzo.

Pia, sehemu ya 1 ya Jedwali la Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 inataka malipo ya ushuru wa mazao kwa mnunuzi kutozwa asilimia tatu ya bei ya lango la shamba katika mazao ya biashara.

Mapitio yangu ya taarifa za Minada ya Mazao, Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato katika mamlaka za serikali za mitaa, taarifa za mauzo ya makampuni binafsi, taarifa za Vyama vya Ushirika vya Masoko ya Kilimo (AMCOS) na taarifa za Bodi za mazao husika, nilibaini kuwa, Mamlaka 17 za serikali za Mitaa hazijakusanya shilingi bilioni 3.03 kama malipo ya mazao kinyume cha kifungu cha sheria kilichotajwa hapo juu. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali 6-8.**

**Jedwali Na.6-8: Ushuru wa Mazao Usiokusanywa**

| Na | Jina la Halmashauri | Zao husika | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mbinga | Kahawa | 1,467,596,146 |
| 2. | H/W Songea | Kahawa | 294,093,184 |
| | | Ufuta na Maharage ya Soya | 14,157,096 |
| 3. | H/W Mbozi | Kahawa | 180,186,123 |
| 4. | H/W Sikonge | Tumbaku | 153,859,706 |
| 5. | H/W Busokelo | Chai | 132,130,098 |
| 6. | H/W Liwale | Korosho | 122,227,512 |
| 7. | H/W Moshi | Kahawa | 110,683,417 |
| 8. | H/W Kaliua | Tumbaku | 108,659,716 |
| 9. | H/W Tunduru | Korosho | 81,612,735 |
| 10. | H/Mji Korogwe | Mkonge | 81,036,666 |
| 11. | H/W Mpanda | Tumbaku | 78,668,212 |
| 12. | H/W Urambo | Tumbaku | 72,769,281 |
| 13. | H/W Korogwe | Chai | 50,000,000 |
| 14. | H/Mji Njombe | Chai | 24,147,346 |
| 15. | H/W Shinyanga | Pamba | 21,921,483 |
| 16. | H/W Hai | Kahawa | 16,732,116 |
| 17. | H/W Bariadi | | 16,579,620 |
| **Jumla** | | | **3,027,060,457** |

***Chanzo: Taarifa za mazao***

Ushuru wa Mazao ambao haujakusanywa unazinyima Mamlaka za serikali Mitaa husika uwezo wa kuboresha huduma zitolewazo kwa jamii iliyokusudiwa.

**Natoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha ushirikiano kati ya Idara za Fedha na Kilimo ili kufanya ufuatiliaji wa karibu wa ushuru wa mazao kutoka Taasisi na kampuni husika ili kurejesha ushuru ya mazao ambayo hayajatumwa.**

## 6.9 Matumizi Hafifu ya Mfumo wa Usimamizi wa Ukusanyaji Mapato

Aya ya 3.4 (vii) ya Mwongozo wa usimamizi wa Mapato wa Serikali za Mitaa wa 2019 inasema "marekebisho yote ya taarifa zisizo sahihi kwenye mifumo ya IFMIS au LGRCIS au vifaa lazima yawasilishwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kwa ajili ya kuidhinishwa".

**(i) Kutofanyika kwa usuluhishi kati ya POS, LGRCIS na Akaunti ya Benki**

Aya ya 3.4 (ix) cha LARAM, 2019 inahitaji usuluhishi wa mapato ufanywe mara kwa mara, ikiwezekana kila wiki dhidi ya miamala inayokusanywa na POS, inayoonekana katika mfumo wa LGRCIS, na ile iliyowekwa benki.

Nilibaini Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam haikufanya usuluhishi wa mapato yatokanayo na ukusanyaji wa taka, kati ya POS, LGRCIS na kilichowasilishwa Benki ili kuhakikisha kuwa miamala yote inahifadhiwa katika kanzidata ya mfumo, na. pia kiasi kilichokusanywa kinalingana na kiasi kilichopo kwenye taarifa ya benki.

Kutofanya usuluhishi kati ya POS, LGRCIS na Benki kunaweza kusababisha kupotoshwa kwa taarifa kutokana na makosa au ubadhirifu.

(ii) **Mapato Yanayokusanywa nje ya Mfumo wa Ukusanyaji Mapato (LGRCIS)**

Waraka Na.EB.151/257/01/109 uliotolewa na Ofisi ya Raisi-TAMISEMI wa tarehe 28 Januari 2015 unataka mapato yote yakusanywe kupitia Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Serikali za Mitaa (LGRCIS).

Mapitio ya taarifa ya leseni za biashara na vileo zilizotolewa katika mfumo wa LGRCIS, nilibaini kuwa, Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga ilitoa leseni 1,046 zenye ada ya jumla ya shilingi milioni 55.13 zilitolewa nje ya LGRCIS

Aidha Halmashauri ya mji wa Handeni ilikusanya jumla ya Shilinngi milioni 68 nje ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato (LGRCIS).

Katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam mapato yenye jumla ya shilingi milioni 592.95 yalikusanywa kupitia benki za biashara lakini hayakuonekana kwenye LGRCIS.

Ukusanyaji wa mapato bila kutumia mfumo wa LGRCIS huongeza hatari za udanganyifu na vitendo vya rushwa.

**Ninashauri Uongozi wa Halmashauri husika kufanya usuluhishi wa mara kwa mara kati ya POS na LGRCS ili kuepuka upotoshaji wowote wa taarifa kutokana na makosa au udanganyifu**.



# SURA YA SABA

# USIMAMIZI WA MATUMIZI

## 7.0 Utangulizi

Sura hii inajadili kuhusu mgawanyo na usimamizi wa rasilimali za umma unaofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kufuata taratibu za fedha za umma, kuweka vipaumbele vya kimkakati na thamani ya fedha. Usimamizi wa matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa unaohusisha taratibu zote zinazohitajika ili kuhakikisha kwamba malipo yanafanyika kwa uhalali,wakati na kwa utimilifu. Zaidi ya hayo, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unahakikisha kuwa rasilimali za umma zinazotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatumika kikamilifu kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, maagizo na kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Kutokana na ukiukwaji mkubwa wa sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa fedha, Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilifanya matumizi mabaya ya fedha. Sura hii inaeleza kwa muhtasari masuala muhimu ambayo yasiporekebishwa yanaweza kusababisha athari mbaya katika usimamizi wa fedha zinazopelekwa kwenye Mamlaka za serikali za mitaa.

## 7.1 Malipo ya Shilingi Bilioni 11.78 Yasiyo na Viambatisho

Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438 kinamtaka mtu, ambaye anasambaza bidhaa, anatoa huduma au anayepokea malipo kuhusiana na usambazaji wa bidhaa au huduma aliyotoa, kutoa risiti au ankara kwa kutumia mashine za kielektroniki. Aidha Agizo la 34(1) na 104(2) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linamtaka mwekahazina kuweka mfumo mzuri wa uhasibu na utunzaji wa nyaraka zote muhimu, kwa muda usiopungua miaka mitano.

Kinyume na matakwa yaliyotajwa hapo juu, nilibaini malipo ya jumla ya shilingi bilioni 11.78 hayakuwa na viambatisho vya kutosha. Kati ya hizo, Halmashauri 71 zililipa shilingi bilioni 10.08 kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kielektroniki kama inayooneshwa kwenye **Jedwali Na.7-1**, na Halmashauri 40 zililipa shilingi bilioni 1.70 bila viambatisho timilifu kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7-2**

**Jedwali Na.7-1: Malipo yasiyo na Risiti za Kielectroniki**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kaliua | 831,272,284 | 37. | H/W Kasulu | 70,746,600 |
| 2. | H/W Bunda | 801,102,943 | 38. | H/W Songea | 68,735,930 |
| 3. | H/W Musoma | 614,075,760 | 39. | H/W Itigi | 67,989,358 |
| 4. | H/W Chemba | 592,600,415 | 40. | H/W Malinyi | 64,293,724 |
| 5. | H/W Uvinza | 490,733,979 | 41. | H/W Mvomero | 59,905,888 |
| 6. | H/W Longido | 446,223,525 | 42. | H/MJI Babati | 52,873,399 |
| 7. | H/W Mkinga | 346,553,104 | 43. | H/MJI Handeni | **52,393,000** |
| 8. | H/W Mbinga | 303,061,547 | 44. | H/W Bukombe | 49,857,544 |
| 9. | H/W Namtumbo | 297,285,131 | 45. | H/W Pangani | 44,656,130 |
| 10. | H/W Kishapu | 293,934,493 | 46. | H/W Nyasa | 43,020,443 |
| 11. | H/W Arusha | 258,553,091 | 47. | H/W Simanjiro | 40,603,193 |
| 12. | H/W Madaba | 238,186,433 | 48. | H/Mji Kondoa | 38,220,384 |
| 13. | H/W Kigoma | 235,638,175 | 49. | H/Mji Ifakara | 37,022,217 |
| 14. | H/W Busega | 222,345,532 | 50. | H/W Ruangwa | 34,583,500 |
| 15. | H/W Maswa | 216,723,762 | 51. | H/W Chalinze | 34,420,520 |
| 16. | H/W Nsimbo | 216,697,078 | 52. | H/W Singida | 33,921,440 |
| 17. | H/MJI Tunduma | 181,219,687 | 53. | H/W Mbogwe | 32,673,444 |
| 18. | H/W Rorya | 155,797,879 | 54. | H/W Mkalama | 32,034,370 |
| 19. | H/Mji Bunda | 152,832,030 | 55. | H/W Kalambo | 31,407,100 |
| 20. | H/W Chato | 151,237,900 | 56. | H/Mji Nanyamba | 30,670,100 |
| 21. | H/W Lushoto | 149,064,375 | 57. | H/W Itilima | 30,634,047 |
| 22. | H/W Nkasi | 147,631,860 | 58. | H/W Korogwe | 30,174,194 |
| 23. | H/W Iramba | 140,731,303 | 59. | H/W Tandahimba | 29,241,590 |
| 24. | H/W Meru | 127,536,474 | 60. | H/W Kiteto | 28,816,677 |
| 25. | H/W Bahi | 124,071,715 | 61. | H/W Buhigwe | 26,039,054 |
| 26. | H/W Mlele | 122,264,093 | 62. | H/W Rufiji | 25,736,435 |
| 27. | H/W Kongwa | 112,481,855 | 63. | H/W Mpwapwa | 24,724,892 |
| 28. | H/W Butiama | 108,034,087 | 64. | H/W Mwanga | 21,201,501 |
| 29. | H/M Musoma | 107,695,853 | 65. | H/M Mpanda | 20,285,000 |
| 30. | H/W Mbozi | 101,814,620 | 66. | H/W Mafia | 20,017,716 |
| 31. | H/W Liwale | 99,560,574 | 67. | H/W Kisarawe | 17,885,000 |
| 32. | H/W Kondoa | 98,226,380 | 68. | H/W Kibaha | 13,687,170 |
| 33. | H/W Mbarali | 97,751,920 | 69. | H/W Mkuranga | 10,958,797 |
| 34. | H/W Shinyanga | 96,903,930 | 70. | H/W Rungwe | 9,357,610 |
| 35. | H/W Mpanda | 88,947,658 | 71. | H/W Kilolo | 8,762,748 |
| 36. | H/W Ngara | 77,381,780 | **Jumla** | | **10,083,723,940** |

**Jedwali Na.7-2: Malipo yenye viambatisho pungufu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Bahi | 346,852,709 | 21. | H/Mji Bariadi | 21,743,213 |
| 2. | H/Jiji Tanga | 139,645,930 | 22. | H/W Chunya | 21,366,000 |
| 3. | H/W Nyasa | 132,960,678 | 23. | H/Mji Nnyamba | 21,272,607 |
| 4. | H/Jiji Dar-es-salaam | 106,813,285 | 24. | H/W Korogwe | 20,872,388 |
| 5. | H/W Chamwino | 76,700,680 | 25. | H/W Maswa | 20,800,000 |
| 6. | H/M Musoma | 63,470,730 | 26. | H/M Mpanda | 20,700,000 |
| 7. | H/W Chemba | 61,042,640 | 27. | H/W Busega | 20,512,000 |
| 8. | H/W Simanjiro | 52,015,067 | 28. | H/W Igunga | 19,565,700 |
| 9. | H/Jiji Mbeya | 42,440,850 | 29. | H/W Handeni | 19,278,401 |
| 10. | H/W Itigi | 40,702,920 | 30. | H/Mji Ifakara | 18,990,000 |
| 11. | H/W Kishapu | 37,874,200 | 31. | H/W Lushoto | 18,870,960 |
| 12. | H/Mji Kasulu | 35,465,394 | 32. | H/W Rufiji | 15,802,560 |
| 13. | H/M Tabora | 34,665,000 | 33. | H/W Mlele | 15,745,840 |
| 14. | H/W Nkasi | 34,643,533 | 34. | H/W Mvomero | 14,381,840 |
| 15. | H/W Mkuranga | 34,021,653 | 35. | H/W Mafia | 14,105,116 |
| 16. | H/W Nachingwea | 29,290,000 | 36. | H/W Mpimbwe | 11,436,063 |
| 17. | H/M Kigamboni | 27,651,315 | 37. | H/Mji Handeni | 11,557,756 |
| 18. | H/W Kibondo | 26,805,076 | 38. | H/W Ruangwa | 9,924,000 |
| 19. | H/W Mafia | 24,270,000 | 39. | H/W Bagamoyo | 8,650,245 |
| 20. | H/W Ukerewe | 23,158,000 | 40. | H/W Pangani | 6,028,000 |
| **Jumla** | | | | | **1,702,092,349** |

Mchanganuo wa mwenendo wa kiasi cha malipo ambayo hayakuwa na viambatisho timilifu kuanzia mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2021/22 unaonesha kuwa mapungufu yanaendelea kuongezeka kwa kiasi kikubwa, hii inamaanisha kwamba, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuchukua hatua madhubuti za kurekebisha mapungufu hayo na kushughulikia mapendekezo yangu ipasavyo kwa miaka iliyopita kama inavyoonyeshwa kwenye **kielelezo Na 7-1** hapa chini.

**Kielelezo Na 7-1: Mwenendo wa Malipo Ambayo Hayakuwa na Viambatisho vya Kutosha**




Kutokuwa na viambatisho timilifu vinavyothibitisha uhalali wa matumizi, kunaficha uhalali na uhalisia wa matumizi yaliyofanywa,aidha kunatengeneza mianya ya ukwepaji wa kodi kwa wazabuni, hivyo kusababisha ukusanyaji mdogo wa mapato ya Serikali.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania iongeze ufuatiliaji wa kubaini wauzaji wasio waaminifu ambao hawatoi risiti za kielektroniki, na kuchukua hatua stahiki dhidi yao kwa mujibu wa sheria za kodi. Aidha, menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kudai risiti za kielekroniki kwa lengo la kukuza ukusanyaji wa kodi, pamoja na kuhakikisha kuwa matumizi yasiyo na viambatisho husika ikiwa ni pamoja na hati ya madai, hati ya mapokezi,orodha ya walipwaji na mahudhurio yanachunguzwa na vyombo husika vya kiuchunguzi ili kubaini uhalali wa malipo hayo.**

## 7.2 Kutokuwa na Usimamizi Bora Juu ya Fedha Kutoka Akaunti ya Amana Shilingi Bilioni 7.7

Kazi ya msingi ya akaunti ya amana, ni kutunza fedha kutoka kwa waweka amana mbalimbali kwa madhumuni yaliyopangwa.Hivyo dhamana ya kutoa fedha hizo kwenye akaunti, kunategemea hasa uthibitisho wa matumizi sawa na lengo kuu la amana hizo.

Nilibaini kuwa, Mamlaka 31 za Serikali za Mitaa hazikusimamia vizuri fedha za amana, kwa kutoa fedha kwa ajili ya shughuli kinyume na

malengo yaliyokusudiwa. Zaidi ya hayo, Halmashauri zilizokopa jumla ya shilingi bilioni 3.15 kutoka kwenye akaunti za amana bila kurejesha kwa wakati ili kutekeleza shughuli zilizokusudiwa.

Ufinyu wa bajeti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na udhibiti mdogo juu ya usimamizi wa fedha katika akaunti ya amana, ni miongoni mwa mambo yanayochangia matumizi mabaya na ukopaji usiodhibitiwa.

Fedha zlizotolewa kutoka kwenye akaunti za amana ambazo hazijarejeshwa husababisha madeni makubwa kwa Halmashauri na, mwishowe, huiweka serikali katika hatari ya sifa mbaya mbele ya wenye amana Halmashauri zilizoshindwa kusimamia fedha katika akaunti ya amana zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 7-3.**

**Jedwali Na.7-3: Halmashauri zilizotumia fedha za amana kwa matumizi yasiyopangwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Morogoro | 443,990,761 |
| 2. | H/Mji Korogwe | 351,243,908 |
| 3. | H/W Shinyanga | 194,689,640 |
| 4. | H/W Tarime | 186,474,143 |
| 5. | H/M Moshi | 170,037,459 |
| 6. | H/W Morogoro | 150,612,183 |
| 7. | H/Mji Kahama | 119,589,550 |
| 8. | H/M Tabora | 114,555,442 |
| 9. | H/W Newala | 104,240,807 |
| 10. | H/W Songwe | 102,475,400 |
| 11. | H/W Njombe | 102,329,713 |
| 12. | H/Jiji Dar-es-salaam | 102,312,945 |
| 13. | H/W Ngorongoro | 100,305,550 |
| 14. | H/W Butiama | 97,984,000 |
| 15. | H/W Bariadi | 94,471,475 |
| 16. | H/M Musoma | 83,755,127 |
| 17. | H/W Mbeya | 82,717,102 |
| 18. | H/W Ludewa | 71,160,000 |
| 19. | H/M Shinyanga | 60,000,000 |
| 20. | H/W Iramba | 51,409,950 |
| 21. | H/W Gairo | 47,842,000 |
| 22. | H/W Kilwa | 46,323,570 |
| 23. | H/W Rungwe | 39,699,297 |
| 24. | H/W Ushetu | 38,400,590 |
| 25. | H/W Kibiti | 37,000,000 |
| 26. | H/W Liwale | 29,610,780 |
| 27. | H/W Mwanga | 23,656,093 |
| 28. | H/W Kilosa | 21,981,000 |
| 29. | H/W Meatu | 20,118,704 |
| 30. | H/Mji Handeni | 11,896,251 |
| 31. | H/W Lushoto | 52,430,841 |
| **Jumla** | | **3,153,314,281** |

Aidha, nilibaini Halmashauri 13 hazikusimamia ipasavyo fedha za amana kwa kulipa zaidi ya kiasi kilichopokelewa katika akaunti kwa shilingi bilioni 1.28 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.7-4**. Na malipo ya shilingi bilioni 3.27 yaliyolipwa na Halmashauri 27 hayakuthibitishwa kupokelewa katika akaunti ya amana, na kukosa idhini ya kufanya malipo hayo kama inavyooneshwa kwenye Jedwali **7-5.**

**Jedwali Na.7-4:Malipo Yaliyofanyika Zaidi ya Amana Iliyopo**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | 464,776,946 |
| 2. | H/W Mufindi | 210,954,075 |
| 3. | H/W Babati | 144,615,543 |
| 4. | H/W Mpwapwa | 118,662,589 |
| 5. | H/W Monduli | 65,411,053 |
| 6. | H/W Meru | 59,337,342 |
| 7. | H/W Arusha | 56,874,043 |
| 8. | H/W Bariadi | 38,756,806 |
| 9. | H/W Bukoba | 33,368,227 |
| 10. | H/Mji Handeni | 32,435,598 |
| 11. | H/W Kiteto | 24,116,425 |
| 12. | H/W Nyang'hwale | 17,287,772 |
| 13. | H/W Pangani | 12,775,000 |
| **Jumla** | | **1,279,371,419** |

**Jedwali Na.7-5: Malipo katika akaunti ya amana Bila uthibitisho wa amana kupokelewa**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Korogwe | 523,804,544 | 1. | H/Mji Ifakara | 70,432,891 |
| 2. | H/W Namtumbo | 355,392,256 | 2. | H/Mji Bariadi | 64,752,419 |
| 3. | H/W Songea | 291,289,583 | 3. | H/W Kibiti | 64,522,973 |
| 4. | H/W Nyasa | 252,882,153 | 4. | H/W Kwimba | 61,778,450 |
| 5. | H/M Kahama | 195,254,515 | 5. | H/W Mbogwe | 57,443,000 |
| 6. | H/M Songea | 163,525,104 | 6. | H/W Bahi | 53,623,715 |
| 7. | H/W Chato | 157,263,307 | 7. | H/W Simanjiro | 53,283,931 |
| 8. | H/W Msalala | 144,013,739 | 8. | H/W Magu | 51,791,212 |
| 9. | H/W Malinyi | 141,491,404 | 9. | H/W Kilindi | 22,509,000 |
| 10. | H/W Mbinga | 138,161,558 | 10. | H/W Busega | 19,906,197 |
| 11. | H/W Shinyanga | 108,751,766 | 11. | H/W Muleba | 19,026,000 |
| 12. | H/W Uyui | 86,757,593 | 12. | H/W Biharamulo | 11,542,120 |
| 13. | H/W Maswa | 81,348,000 | 13. | H/W Mwanga | 7,583,376 |
| 14. | H/W Arusha | 70,741,479 | **Jumla** | | **3,268,872,285** |

**Ninapendekeza Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI, iagize Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka udhibiti bora wa usimamizi wa fedha katika akaunti ya amana. Aidha, fedha zilizokopwa kutoka kwenye akaunti ya amana, zinarejeshwa haraka ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.**

## 7.3 Malipo ya Shilingi Bilioni 1.51 Yaliyofanywa kwa Fedha Taslimu

Aya ya 6.8.3 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2021 kinazitaka mamlaka ya serikali za mitaa kufanya malipo yote kwa njia ya kielekitroniki katika akaunti ya benki ya mlipwaji, na kwa hali yoyote ile mamlaka isilipe kwa hundi au fedha taslimu.

Nilibaini mamlaka 14 za serikali za mitaa zzilifanya malipo yenye jumla ya shilingi bilioni 1.51 kwa wazabuni mbalimbali kinyume na matakwa ya kifungu tajwa hapo juu kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7-6.**

**Jedwali Na. 7-6: Malipo Kwa Fedha Taslimu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | 383,440,200 |
| 2. | H/Jiji Arusha | 309,160,000 |
| 3. | H/M Iringa | 264,433,521 |
| 4. | H/W Longido | 152,315,818 |
| 5. | H/W Kaliua | 100,268,637 |
| 6. | H/M Singida | 70,180,000 |
| 7. | H/W Urambo | 55,216,500 |
| 8. | H/W Kakonko | 38,963,040 |
| 9. | H/Mji Bariadi | 32,501,768 |
| 10. | H/W Manyoni | 27,060,573 |
| 11. | H/W Busega | 24,593,354 |
| 12. | H/W Mkinga | 21,082,067 |
| 13. | H/W Mkalama | 20,032,993 |
| 14. | H/W Pangani | 7,078,500 |
| **Jumla** | | **1,506,326,971** |

Shinikizo na ukomo wa muda unaotolewa na Serikali katika kukamilisha miradi inayotekelezwa inaweza kuwa sababu ya kutumia fedha taslimu. Kufanya malipo ya fedha taslimu kwa wazabuni kunaweza kuvutia matumizi mabaya ya fedha za umma na kutolipa kodi stahiki kwa serikali.

**Ninapendekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe zinazingatia sheria, na kuzuia matumizi ya fedha taslimu, hasa wakati wa kufanya malipo kwa wazabuni.**

## 7.4 Masurufu Yasiyorejeshwa Shilingi Milioni 809.1

Agizo Na. 40 la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na aya Na. 6.8 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unatoa maelekezo ya jinsi ya uombaji wa masurufu, utoaji na urejeshaji wake, zuio la utoaji wa masurufu zaidi ya mara moja kwa Afisa wa serikal; uandaaji wa rejesta ya masurufu; na adhabu kwa kuchelewa kurejesha masurufu.

Nilibaini kuwa, Halmashauri 17 zina masurufu ya jumla ya shilingi milioni 809.1 ambayo yalilipwa kwa watumishi kwa ajili ya shughuli mbalimbali, bila kurejeshwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 7-7.**

**Jedwali Na.7-7: Halmashauri Zenye Masurufu Yasiyorejeshwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/M Morogoro | 177,019,300 |
| 2. | H/Jiji Arusha | 169,840,000 |
| 3. | H/Jiji Dar Es Salaam | 161,533,554 |
| 4. | H/W Songwe | 42,030,000 |
| 5. | H/W Mbozi | 34,187,463 |
| 6. | H/W Simanjiro | 29,932,852 |
| 7. | H/W Ushetu | 29,504,900 |
| 8. | H/W Nachingwea | 27,227,720 |
| 9. | H/Mji Kondoa | 22,172,696 |
| 10. | H/W Mufindi | 22,026,700 |
| 11. | H/W Rungwe | 16,557,900 |
| 12. | H/W Mkuranga | 16,405,000 |
| 13. | H/W Maswa | 14,312,000 |
| 14. | H/W Kibiti | 12,853,000 |
| 15. | H/W Nyasa | 12,393,250 |
| 16. | H/Mji Mbinga | 11,486,485 |
| 17. | H/W Itigi | 9,618,057 |
| **Jumla** | | **809,100,877** |

Usimamizi usio bora wa masurufu unaonesha mapungufu katika ufuatiliaji wa marejesho ya masurufu kwa wakati, hivyo, kutoa mianya kwa watumishi wasio waaminifu kufanya ubadhirifu wa fedha za umma.

**Ninapendekeza, Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa masurufu, kurejesha kwa**

**wakati pamoja na adhabu ya ucheleweshaji kama inavyotakiwa na sheria na kanuni za usimamizi wa fedha za umma, ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha.**

## 7.5 Kodi ya Zuio Kutowasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania Shilingi Milioni 510.19

Kifungu cha 83 (A) na Aya ya 4(c) (v) cha Jedwali la 1 la Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332, kinataka kila taasisi kukatwa 2% kwa bidhaa na 5% kwa huduma zinazotolewa kwa taasisi za Serikali, na kiasi kilichozuiliwa kutumwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato.

Kinyume na matakwa ya sheria tajwa, nilibaini Halmashauri 15 kukatwa kodi ya zuio ya shilingi milioni 510.19, na kutowasilisha katika Mamlaka Ya Mapato Tanzania kwenye **Jedwali Na. 7-8.**

**Jedwali Na.7-8: Halmashauri zenye Kodi ya Zuio Isiyowasilishwa**

| Na. | Jina La Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Bumbuli | 227,781,363 |
| 2. | H/Mji Tunduma | 71,498,460 |
| 3. | H/W Mbarali | 37,253,652 |
| 4. | H/W Muheza | 28,390,069 |
| 5. | H/W Kibaha | 26,098,081 |
| 6. | H/W Songea | 19,712,660 |
| 7. | H/W Kilindi | 17,167,091 |
| 8. | H/W Longido | 15,278,686 |
| 9. | H/W Mtwara | 15,037,645 |
| 10. | H/W Nanyumbu | 13,319,405 |
| 11. | H/W Itigi | 11,504,545 |
| 12. | H/Mji Kondoa | 10,548,001 |
| 13. | H/W Magu | 5,841,140 |
| 14. | H/W Chalinze | 5,395,801 |
| 15. | H/W Madaba | 5,373,057 |
| **Jumla** | | **510,199,656** |

Kutokuwa na usimamizi bora kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika juu ya uwasilishwaji wa kodi za zuio kwa wakati katika Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuzitumia fedha hizo kwa shughuli nyingine za Halmashauri ndiyo sababu ya kutowasilishwa kwa kodi hiyo.

**Ninapendekeza uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa uweke utaratibu madhubuti juu ya ufuatiliaji wa uwasilishwaji wa kodi kwa Mamlaka ya mapato Tanzania utakaohakikisha, kodi**

**inayokatwa inawasilishwa kwa wakati ili kuepuka adhabu kutokana na kuchelewa au kutopeleka kodi iliyozuiwa.**

## 7.6 Matumizi yasiyo na Tija Shilingi Milioni 898.85

Kwa mujibu wa Kanuni ya 21(2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001, matumizi yasiyo na tija, ni matumizi ambayo yanaweza kuepukika na hayatakuwa na faida. Matumizi yasiyo na tija ni matumizi yanayofanywa bila faida za kiuchumi kwa taasisi.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa, Halmashauri nane zilitumia jumla ya shilingi milioni 576.55 kwa matumizi yasiyo na faida kiuchumi kwa serikali, jambo ambalo liliathiri bajeti ya utekelezaji wa shughuli nyingine.

Matumizi hayo yalijumuisha shilingi milioni 254.84 za Halmashauri ya Jiji la Arusha ambazo zilitumika katika ujenzi wa Soko la Machinga lililotelekezwa eneo la Njiro kutokana na eneo hilo kukosa mvuto kwa machinga na wateja.

Miongoni mwa sababu ni pamoja na uongozi wa Halmashauri kushindwa kudhibiti matumizi na kusababisha malipo kujirudia, adhabu kwa kuchelewesha kulipa marejesho, na malipo ya shughuli ambazo hazijatekelezwa . **Jedwali Na. 7-9** linaonesha Halmashauri zenye matumizi yasiyo na tija.

**Jedwali Na.7-9: Halmashauri zenye Matumizi Yasiyo na Tija**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | 577,138,502 |
| 2. | H/M Temeke | 111,815,294 |
| 3. | H/W Rorya | 80,000,000 |
| 4. | H/W Msalala | 35,000,000 |
| 5. | H/W Hanang' | 34,420,000 |
| 6. | H/Mji Bunda | 26,709,540 |
| 7. | H/M Singida | 16,000,000 |
| 8. | H/W Karagwe | 10,500,000 |
| 9. | H/W Bariadi | 7,265,000 |
| **Jumla** | | **898,848,336** |

Aidha, mapitio ya masurufu ya shilingi milioni 322.29 yaliyolipwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya matengenezo ya barabara yalibaini kuwa hakukuwa na ushahidi wowote wa ukarabati wa barabara ulifanywa.

**Ninapendekeza kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha Halmashauri zinazuia matumizi mabaya ya fedha kwa siku zijazo, kwa kuhakikisha madai yote dhidi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanalipwa kwa wakati, maamuzi yanafuata sheria na kanuni na malipo yanafanyika kwa ajili ya shughuli halali, Pia, hatua stahiki zichukuliwe kwa watumishi waliosababisha matumizi yasiyo na tija, ikiwa ni pamoja na kufikisha suala hilo katika vyombo vya kiuchunguzi, pale itakapofaa.**

.



# SURA YA NANE

# USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

## 8.0 Utangulizi

Usimamizi wa rasilimaliwatu unalenga ajira, utawala, mafunzo na maendeleo ya watumishi ili kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa mahiri katika utumishi wa umma. Hivyo, mifumo ya usimamizi wa rasilimali-watu ndani Halmashauri huwezesha mazingira bora na yenye ufanisi katika utendaji kazi, usimamizi wa rasilimali watu pia, huongeza utendaji wa wafanyakazi wenye tija na utoaji huduma kwa mitazamo sahihi, uzoefu na ujuzi wa kutumikia maslahi ya umma.

Miongoni mwa mambo muhimu ya usimamizi wa rasilimaliwatu unaohusisha usimamizi wa mishahara ya wafanyakazi umejikita katika kutoa mafao, motisha na fidia kupitia tathmini ya utendaji kazi na ya mahitaji yanayoendana na sera na mifumo wezeshi ya taasasi ili kufikia malengo yaliopangwa. Katika ukaguzi nilioufanya, nimebaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa rasilimaliwatu katika mamlaka za serikali za mitaa.

Usimamizi wa rasilimaliwatu ni sababu kuu inayopelekea halmashauri kutoa huduma zenye ufanisi na ufasaha Hata hivyo, inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

## 8.1 Malimbikizo ya Mishahara ambayo Hayakulipwa na Madai ya Wafanyakazi Shilingi Bilioni 119.94

Nilibaini kuwa, Mamlaka za Serikali za Mitaa 113 hazikulipa malimbikizo ya stahiki za watumishi yenye thamani ya shilingi bilioni 119.94 kwa zaidi ya mwaka mmoja kinyume na Kanuni ya E.23 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009.

Madai ya stahiki hizo ni pamoja na; malimbikizo ya mishahara, posho za likizo/safari, gharama za uhamisho,posho ya kuitwa kazini, posho za usumbufu/kujikimu, posho za nyumba, umeme, simu na posho za samani na stahiki nyingine kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na 8-2** na **Kiambatisho Na 8-1.**

**Jedwali Na.8-1: Madai ya Stahiki za Wafanyakazi Ambayo Hayajalipwa**

| Kundi | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Malimbikizo ya mishahara | 90 | 42,257,173,197 |
| Posho za likizo | 101 | 12,122,259,653 |
| Gharama za uhamisho | 98 | 22,961,738,620 |
| Posho ya kujikimu | 69 | 4,871,678,948 |
| Posho ya Samani | 59 | 4,444,427,298 |
| Posho ya Makazi | 46 | 2,008,781,240 |
| Posho ya Matibabu | 75 | 2,089,341,915 |
| Mafunzo | 68 | 1,276,597,652 |
| Malimbikizo mengine | 98 | 27,912,232,383 |
| **Jumla** | | **119,944,230,906** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Hesabu za Mwisho na Majalada ya Kiutumishi, 2022*

Mamlaka za Serikali za Mitaa kutolipa malimbikizo ya mishahara na madai ya wafanyakazi kwa wakati huwakatisha tamaa watumishi na matokeo yake ina athari kwa serikali kufikia malengo yake ya kutoa huduma bora kwa umma.

**Ninashauri Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa na OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa madai ya stahiki za wafanyakazi yanalipwa kwa wakati. Aidha, yajumuishwe kwenye bajeti ya mwaka unaofuata na pale inapobidi kwa siku zijazo kuepuka kuzalisha madeni ya watumishi.**

## 8.2 Wastaafu Kutolipwa Gharama za Usafirishaji Mizigo Zenye Thamani ya Shilingi Millioni 309.67

Kanuni ya J.8 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inazitaka Taasisi za umma kuwalipa wafanyakazi stahiki zao wanapostaafu.

Nilifanya mapitio ya taarifa mbalimbali za wastaafu na kubaini kuwa Halmashauri sita hazikulipa kiasi cha shilingi milioni 309.67 kwa watumishi 233 waliostaafu ikiwa ni gharama ya kusafirisha mizigo yao baada ya kustaafu utumishi wa umma. Aidha kati hao wastaafu 12

wamefariki dunia bila kulipwa madai yao yenye thamani ya shilingi milioni 42.10. Rejea **Jedwali Na 8-2.**

**Jedwali Na.8-2: Wastaafu Kutolipwa Gharama za Usafirishaji wa Mizigo**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya watumishi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kibaha | 49 | 108,432,521 |
| 2. | H/W Nzega | 70 | 84,319,250 |
| 3. | H/W Uyui | 66 | 65,080,121 |
| 4. | H/W Maswa | 25 | 37,950,000 |
| 5. | H/W Gairo | 7 | 10,222,000 |
| 6. | H/W Longido | 6 | 3,663,000 |
| **Jumla** | | **223** | **309,666,892** |

***Chanzo**: Taarifa za Wastaafu wa Halmashauri, 2022*

Ucheleweshaji wa kulipa stahiki za wastaafu una athari mbaya kwa ustawi wao katika jamii.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kujumuisha gharama za usafirishaji mizigo ya watumishi wanaotarajiwa kustaafu katika bajeti ili kuwalipa wastaafu fedha zao bila usumbufu pale wanapokuwa wamefikisha umri wa kustaafu.**

## 8.3 Makato ya Watumishi ambayo Hayakupelekwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi Zingine Husika ya Shilingi Bilioni 260.07

Kifungu cha 18 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma, 2018 kinawataka mwajiri kuchangia Mifuko hiyo asilimia ishirini ya mshahara wa mfanyakazi.

Pia, Kifungu cha 19 (1) na (2) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 2018 kimebainisha kuwa mwajiri ambaye atashindwa kuchangia jumla ya michango ndani ya muda uliopangwa atapewa adhabu ya kulipa faini zilizoainishwa kwa ongezeko la asilimia kulingana na muda wa uchelewasheji.

Nilibaini kuwa, Halmashauri 37 zilizochelewa kuchangia makato/michango ya kisheria na kuzalisha deni la shilingi bilioni 260.07; lililojumuisha michango ya lazima ya mwajiri shilingi bilioni 1.36 na shilingi bilioni 258.41 ni fedha zilizotokana na adhabu ya faini ya kutopeleka michango husika.Pia, makato mengine ya shilingi milioni 296.35 hayakuwasilishwa kwa taasisi za fedha, Mamlaka ya mapato, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, vyama vya wafanyakazi

,Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na makampuni ya bima. Rejea **Jedwali Na 8-3** na **Kiambatisho 8-2.**

**Jedwali Na.8-3: Michango Ambayo Haikupelekwa Katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi Zingine**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Michango kwa Mfuko ya Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma | 35 | 1,364,964,378 |
| 2 | Adhabu Kutokana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma | 22 | 258,405,089,812 |
| 3 | Bima ya Afya ya Taifa | 11 | 129,085,657 |
| 4 | Mamlaka ya Mapao | 7 | 88,955,895 |
| 5 | Taasisi zingine | 5 | **78,307,990** |
| **Jumla** | | **37** | **260,066,403,732** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Malipo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma na Majalada ya Kiutumishi, 2022*

Halmashauri nne zilitozwa faini na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma kiasi cha shilingi bilioni 257.87 kwa kutopeleka michango ya watumishi, Halmashauri hizo ni; H/W Ushetu shilingi bilioni 149.79 , H/W Sikonge shilingi bilioni 62.04, H/W Shinyanga shilingi 45.52 na H/W Mpanda shilingi milioni 514.50 .

Halmashauri nyingine zililipa adhabu ya faini jumla ya shilingi millioni 100.46 ambazo ni H/Jiji Dar es salaam shilingi milioni 65.84,H/W Muheza shilingi milioni 12.80, H/W Biharamulo shilingi milioni 6.00, H/W Kaliua shilingi milioni 5.54 , H/W Mlele shilingi 5.25 na H/W Handeni shilingi milioni 5.03. Kwa maoni yangu haya ni matumizi yasiyo na tija kwa serikali.

**Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa katika siku kwa zijazo kuzingatia Kifungu cha 18 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma, 2018 kwa kuchangia makato/michango ya mishahara kwa wakati kwenye taasisi za fedha. Mamlaka husika zihakikishe makato ambayo hayajawasilishwa yanawasilishwa ili kuepuka adhabu zaidi.**

## 8.4 Makato ya Mikopo Kwenye Posho za Madiwani ya Thamani ya Shilingi Milioni 327.98 ambayo hayajawasilishwa Benki ya CRDB PLC

Halmashauri tatu zilisaini hati za makubaliano ya Mikopo na Benki ya CRDB PLC kwa mikopo iliyotolewa kwa madiwani. Halmashauri hizo zilikubali kufanya marejesho kwa kuwakata Madiwani kwenye posho

zao na kuziwasilisha Benki ya CRDB PLC kwa mujibu wa hati za makubaliano ya urejeshaji.

Ingawa mamlaka hizo zilikubali kutimiza wajibu huo, hawakuwa thabiti katika kutekeleza masharti yaliyokuwa kwenye hati za makubaliano. Nilibaini kuwa shilingi milioni 327.98 zilizokatwa kwenye posho za madiwani hazikuwasilishwa Benki ya CRDB PLC .Pia sehemu ya fedha hizo zilitumika kwa shughuli zisizokusudiwa. Rejea **Jedwali Na 8-4.**

**Jedwali Na.8-4: Makato Kwenye Posho za Madiwani Ambayo Hayakuwasilishwa Benki ya CRDB PLC**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | H/W Busega | 151,223,822.00 |
| 2 | H/W Maswa | 148,198,689.85 |
| 3 | H/W Uvinza | 28,555,469.18 |
| **Jumla** | | **327,977,981.03** |

***Chanzo***: *Taarifa za marejesho ya mikopo*

Hali hii inaweza kuziweka Halmashauri husika katika hatari ya kukabiliwa na madai ya kisheria au kesi mahakamani.

**Ninazishauri Halmashauri husika kuwasilisha marejesho ya mikopo kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba ili kuepuka adhabu na riba zisizo za lazima.**

## 8.5 Idara na Vitengo vya Halmashauri Vinavyoongozwa na Watumishi Wasio na sifa

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitoa maagizo yenye Kumb. Na. CJB.262/317/01/108 ya tarehe 16 Juni 2022 kuzitaka mamlaka zote za serikali za mitaa kufuata na kutekeleza muundo mpya ulioidhinishwa.

Nilibaini kuwa Halmashauri 106 zilikuwa na idara na vitengo ambavyo vinaongozwa na watumishi 747 wasio na sifa. Hali hii ilitokana na changamoto zilizojitokeza za miingiliano ya majukumu ya wakuu wa idara na vitengo yaliyoainishwa kwenye muundo wa zamani kwenda kwenye muundo mpya.

Hata hivyo, Idara na vitengo vinavyoongozwa na wafanyakazi wasio na sifa vinaweza kukabiliwa na athari za utoaji wa huduma usioridhisha. Rejea **Jedwali Na.8-5.**

**Jedwali Na.8-5: Halmashauri zenye Wakuu wa Idara Wasio na Sifa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Wakuu wa idara/viengo | Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Wakuu wa idara/viengo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Babati | 14 | 55. | H/Mji Mbinga | 10 |
| 2. | H/Mji Babati | 11 | 56. | H/W Mbogwe | 8 |
| 3. | H/W Biharamulo | 11 | 57. | H/W Mbozi | 10 |
| 4. | H/W Buchosa | 14 | 58. | H/W Mbulu | 12 |
| 5. | H/W Buhigwe | 11 | 59. | H/Mji Mbulu | 7 |
| 6. | H/W Bukoba | 6 | 60. | H/W Missenyi | 7 |
| 7. | H/M Bukoba | 6 | 61. | H/W Misungwi | 7 |
| 8. | H/W Bukombe | 2 | 62. | H/W Mkinga | 4 |
| 9. | H/W Busokelo | 7 | 63. | H/W Mlele | 5 |
| 10. | H/W Chato | 6 | 64. | H/W Momba | 9 |
| 11. | H/W Chemba | 4 | 65. | H/W Monduli | 2 |
| 12. | H/W Chunya | 8 | 66. | H/W Moshi | 7 |
| 13. | H/W Geita | 2 | 67. | H/M Moshi | 3 |
| 14. | H/W Geita | 1 | 68. | H/W Mpanda | 3 |
| 15. | H/W Hai | 14 | 69. | H/M Mpanda | 1 |
| 16. | H/W Hanang | 10 | 70. | H/W Mpimbwe | 2 |
| 17. | H/W Ileje | 14 | 71. | H/W Msalala | 5 |
| 18. | H/M Ilemela | 7 | 72. | H/W Mtama | 3 |
| 19. | H/W Iramba | 6 | 73. | H/W Mtwara | 7 |
| 20. | H/W Iringa | 13 | 74. | H/W Mufindi | 14 |
| 21. | H/M Iringa | 12 | 75. | H/W Muleba | 10 |
| 22. | H/M Kahama | 7 | 76. | H/W Mwanga | 4 |
| 23. | H/W Kakonko | 9 | 77. | H/W Nachingwea | 6 |
| 24. | H/W Kaliua | 5 | 78. | H/W Namtumbo | 14 |
| 25. | H/W Karagwe | 4 | 79. | H/Mji Newala | 9 |
| 26. | H/W Kasulu | 6 | 80. | H/W Ngara | 5 |
| 27. | H/Mji Kasulu | 4 | 81. | H/W Njombe | 7 |
| 28. | H/W Kibondo | 3 | 82. | H/Mji Njombe | 2 |
| 29. | H/M Kigamboni | 2 | 83. | H/W Nsimbo | 7 |
| 30. | H/W Kigoma | 13 | 84. | H/W Nyanghwale | 10 |
| 31. | H/M Kigoma/Ujiji | 5 | 85. | H/W Nyasa | 13 |
| 32. | H/W Kilolo | 13 | 86. | H/W Rombo | 10 |
| 33. | H/W Kilwa | 6 | 87. | H/W Ruangwa | 5 |
| 34. | H/W Kishapu | 4 | 88. | H/W Rungwe | 1 |
| 35. | H/W Kiteto | 3 | 89. | H/W Same | 8 |
| 36. | H/W Kondoa | 4 | 90. | H/W Sengerema | 10 |
| 37. | H/Mji Kondoa | 1 | 91. | H/W Shinyanga | 8 |
| 38. | H/W Kwimba | 8 | 92. | H/M Shinyanga | 11 |
| 39. | H/W Kyela | 1 | 93. | H/W Siha | 8 |
| 40. | H/W Kyerwa | 6 | 94. | H/W Simanjiro | 14 |
| 41. | H/M Lindi | 5 | 95. | H/W Songea | 6 |
| 42. | H/W Liwale | 7 | 96. | H/M Songea | 5 |
| 43. | H/W Ludewa | 10 | 97. | H/W Songwe | 10 |
| 44. | H/W Madaba | 2 | 98. | H/M Tabora | 3 |
| 45. | H/Mji Mafinga | 14 | 99. | H/W Tandahimba | 8 |
| 46. | H/W Magu | 12 | 100. | H/Jiji Tanga | 4 |
| 47. | H/Mji Makambako | 8 | 101. | H/M Temeke | 3 |
| 48. | H/W Makete | 8 | 102. | H/Mji Tunduma | 6 |
| 49. | H/W Masasi | 4 | 103. | H/W Tunduru | 8 |
| 50. | H/MJi Masasi | 8 | 104. | H/W Ukerewe | 7 |
| 51. | H/W Mbarali | 8 | 105. | H/W Ushetu | 4 |
| 52. | H/Jiji Mbeya | 8 | 106. | H/W Uvinza | 5 |
| 53. | H/W Mbeya | 2 | **Jumla** | | **747** |
| 54. | H/W Mbinga | 11 | | | |

**Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa idara na vitengo vyote vinaongozwa na watumishi wenye sifa na uwezo.**

## 8.6 Malipo Yaliyofanywa kwa Wafanyakazi na vibarua Bila Kuwa na Mikataba halali Shilingi Milioni 239.55

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 inawataka waajiri kusaini mikataba rasmi ya kimaandishi na wafanyakazi wa muda usiojulikana kwa kada zisizo za kitaalamu na zisizo za usimamizi rasmi na wa muda maalumu kwa wataalamu wenye taaluma , kada ya usimamizi na zenye kazi maalumu.

Nilifanya tathmini ya mikataba ya waajiriwa wa wasio wa kudumu ili kufahamu taratibu za ajira na vigezo vilivyotumika katika kufanya malipo yao na kubaini kuwa Halmashauri nne hazikuwa na mikataba ya ajira na vibarua wake . Halmashauri hizi zilifanya malipo ya jumla ya shilingi milioni 239.55 bila kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Rejea **Jedwali Na 8-6**.

**Jedwali Na.8-6: Malipo Yaliyofanywa Kwa Wafanyakazi Bila Kuwa na Mikataba Halali**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya wafanyakazi waliohusihwa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/T Nzega | 63 | 63,520,000 |
| 2 | H/M Musoma | 73 | 68,515,932.24 |
| 3 | H/Mji Makambako | Idadi rasmi haikupatikana | 94,463,800 |
| 4 | H/W Kisarawe | 10 | 13,050,000 |
| **Jumla** | | | **239,549,732.24** |

Kutokuwepo kwa mikataba halali iliyosainiwa ni kikwazo cha kufahamu kiwango halisi ambacho vibarua hawa walipaswa kulipwa kutokana na ajira. Aidha, inaweza kusababisha upotevu fedha endapo kutaibuka migogoro.

**Ninazishauri Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kuimarisha udhibiti wa ndani wa ajira kwa kuwataka watumishi wote walioajiriwa kimkataba kusaini mikataba inayoainisha ujira mahususi kwa vibarua.**




# SURA YA TISA

## UTATHMINI WA MIFUMO YA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA UTAWALA BORA

### 9.0 Utangulizi

Agizo la 11 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na mifumo ya udhibiti wa ndani iliyotimilifu itakayozuia ubadhilifu, rushwa, na upotevu wa rasilimali.

Kuwapo kwa mfumo madhubuti wa ndani kunasaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kudhibiti thamani ya fedha kwa kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa jamii kupitia dhana ya uwajibikaji kwa wale wenye dhamana ya madaraka,

Pia uwapo wa mifumo madhubuti unasaidia katika usimamizi wa vihatarishi na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, taratibu na kanuni. Ikiwa mifumo ya udhibiti wa ndani itasimamiwa imara itazisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kufikia malengo katika utendaji, utoaji wa ripoti na utekelezaji wa sheria.

Usimamizi wa vihatarishi ni pamoja na kutambua, Kusimamia na kudhibiti vihatarishi ili kupunguza madhara yanayoweza kuathiri utekelezaji wa malengo ya mamlaka husika.

Utawala bora unazisaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuhimiza maendeleo ya jamii, utoaji wa huduma bora, uzingatiaji wa sheria na maagizo kupitia utoaji wa taarifa, uongozi, na usimamizi wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nimefanya tathmini juu ya mifumo ya udhibiti wa ndani, usiamamizi wa vihatarishi na utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa,nimebaini maeneo mengi yanayohitaji kuboreshwa ili

kuwezesha utendaji wa kiutawala yafuatayo ni mambo yanayohitaji ufumbuzi:

## 9.1 Mapungufu katika Kitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa kifungu cha 48 cha sheria ya fedha za serikali za mitaa, halmashauri itaajiri wakaguzi wake wa ndani ambao watafanya kazi kwa karibu na wakuu wa idara na watatoa taarifa moja kwa moja kwa afisa masuuli.

Agizo la 13 la randama ya fedha za mamlaka za serikali za mitaa ya mwaka,2009 linafafanua ukaguzi wa ndani kuwa ni tathmini ya udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, inayofanyika kwa kuchunguza na kutathmini ufanisi na uttimilifu wa udhibiti wa ndani.

Nimefanya tathmini ya utendaji katika vitengo vya ukaguzi wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kubaini mapungufu yafuatayo:

**(i)** Taarifa za wakaguzi wa ndani kwa Mwaka 2021/22 ziliangazia zaidi katika maeneo ya miamala na matukio yaliofanyika katika ofisi za makao makuu za Mamlaka za Serikali za Mitaa bila ya kuzifikia shughuli zilizofanyika katika ngazi za chini. Ni maoni yangu kuwa, pamoja na kazi nzuri zilizofanyika katika maeneo hayo, wakaguzi wa ndani wanapaswa kuweka msisitizo katika ukaguzi wa maeneo yanayohusiana na usimamizi wa vihatarishi pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani katika eneo la TEHAMA ili kuongeza thamani katika juhudi za menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutambua, kutathmini na kuzuia vihatarishi mbalimbali ikiwamo vya ubadhirifu;

**(ii)** Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikutoa mafunzo kwa wakaguzi wa ndani ili kuwajengea uwezo katika maeneo mbalimbali ya muhimu kama vile Mfumo wa Kuandaa Hesabu Jumuifu za Serikali (GACS), Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HoMIS), Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi Tanzania (TANePS) na Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE). Hii inawaondolea wakaguzi wa ndani uwezo wa kuhakiki utendaji na kutoa maoni yenye kuleta ufanisi mkubwa katika maeneo tajwa;

(iii) Kuna upungufu wa wakaguzi wa ndani 87 katika Halmashauri 35, hii inaonyesha kuelemewa na uzito wa kazi kunakoweza kupelekea wakaguzi waliopo katika Mamlaka husika za Serikali za Mitaa kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, na kupelekea kukosekana uhakika wa matumizi ya fedha yaliyofanyika;

(iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa 26 hazikuweza kukipatia kitengo cha ukaguzi wa ndani kiasi cha fedha zilizotengwa kulingana na bajeti ya mwaka husika. Kulikuwa na upungufu wa fedha zilizoelekezwa kitengo cha ukaguzi kwa wastani wa asilimia 20 mpaka 90, Hali hii imesababisha kutofanyika kwa kaguzi za matumizi ya fedha katika ngazi za chini;

(v) Kulikuwa na upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, kompyuta mpakato, na samani kwenye Mamlaka 21 za Serikali za Mitaa, jambo ambalo liliongeza changamoto katika utendaji na kupunguza ufanisi katika kazi za ukaguzi;

(vi) Vitengo vya ukaguzi wa ndani katika Mamlaka 29 za Serikali za Mitaa hazikufanikiwa kumaliza kaguzi kuendana na mpango kazi uliokuwepo katika Halmashauri husika, Kutofanyika kaguzi katika maeneo yaliyokusudiwa kunaashiria kuwa menejimenti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika, hazikupata ushauri juu ya tathimini ya udhibiti wa ndani katika maeneo ambayo hayakukaguliwa; na

(vii) Katika Mamlaka sita za Serikali za Mitaa hapakuwa na utayarishaji wa mipango kazi ya ukaguzi kinyume na matakwa ya sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa ambayo inaagiza kuonesha aina ya kazi, madhumuni ya kazi husika na utaratibu wa utekelezaji wa mpango kazi.

Maelezo zaidi ya ufanisi wa vitengo vya ukaguzi wa ndani pamoja na uwepo wa vitendea kazi umeoneshwa zaidi katika **Kiambatisho 9-1.**

**Ninazishauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka uwiano sawa wa rasilimali kulingana na mapungufu yaliyobainishwa, ili kuwezesha ufanisi katika ukaguzi wa ndani.**

## 9.2 Mapungufu katika udhibiti mfumo wa udhibiti wa ndani na vihatarishi.

Serikali ya Tanzania ilitoa mwongozo wa kuandaa na kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa vihatarishi katika sekta za umma mwaka 2022. Mwongozo huo uliambatana na Waraka wa Hazina namba 12 wa mwaka 2012/13 unaowataka maofisa masuuli wote kuanzisha na kuwa na mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi, ikiwa ni pamoja na michakato ya kutathmini, kupunguza na kufuatilia viashiria vya hatari. Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaweza kuweka mifumo imara ya udhibiti wa ndani kama sehemu ya miundo yake ya kiutawala na utoaji taarifa kwa mamlaka husika.

Nilifanya tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani pamoja na usimamizi wa vihatarishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/22 na kubaini kasoro zifuatazo:

(i) Kukosekana kwa sera mahususi na mifumo ya kitaasisi ya kushughulikia tatizo la moto kumeathiri ufanisi katika kuzuia matukio ya moto katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa mfano, matukio ya moto yasiyodhibitiwa yamesababisha hasara ya ekari 181 sawa na shilingi bilioni 2.01 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Pia Halmashauri tano hazina hatua za tahadhari dhidi ya milipuko ya moto katika maeneo yao, kwani hakukuwa na vifaa vya kuzima moto hivyo mali zilizopo katika halmashauri hizo zipo hatarini kutokana na kutokuwepo kwa mipango ya udhibiti wa milipuko ya moto isiyotarajiwa;

(ii) Halmashauri 17 hazikuwa na rejesta ya vihatarishi,ama kuhuisha rejesta za vihatarishi zilizokuwepo. Hii inapunguza ufanisi wa juhudi za usimamizi wa kutambua na kudhibiti viashiria vya hatari vilivyopo kutokana na ukosefu wa kumbukumbu za vihatarishi na utaratibu wa kufuatilia vihatarishi vilivyoonekana;

Rejesta za vihatarishi hazijaonyesha udhibiti wa mifumo ya ndani katika maeneo ya utekelezaji pia hakuna ripoti za tathmini na ufuatiliaji wa viashiria vya hatari vilivyotambuliwa na Halmashauri.

Hii inaweza kusababisha tathmini duni ya viashiria vya hatari, itakayopelekea kutokugundulika na kuzuiwa kwa ubadhirifu wa rasilimali;

(iii) Halmashauri 15 hazikufanya tathmini ya viashiria vya hatari kwenye maeneo hatarishi kama vile katika uaandaaji wa taarifa za fedha, Mfumo wa kukusanyia mapato(LGRCIS) na usimamizi wa mali. Hii ilisababisha kutoandaliwa kwa mifumo bora ya udhibiti kulingana na mazingira husika;

(iv) Halmashauri 5 hazikuwa na waratibu wa masuala ya vihatarishi vya ubadhirifu na wasimamizi wake katika idara/vitengo husika hivyo kuathiri ufanisi katika usimamizi wa vihatarishi katika mamlaka husika za serikali za mitaa; na

(v) Halmashauri 12 hazikuwa na Sera za Usimamizi wa Vihatarishi hivyo hazikuwa na mwongozo juu ya usimamizi huo na namna ya kuwalinda watumishi, mali na namna ya kujenga uimara wa kiuchumi katika mamlaka za serikali za mitaa husika.

(vi) Mamlaka za serikali za mitaa hazikutoa mafunzo kuhusiana na masuala ya usimamizi wa vihatarishi hususani kwa watumishi walioko katika ngazi za chini kama vile shule, vituo vya kutolea huduma za afya na kata. Ni muhimu kwa watumishi wote wa mamlaka za serikali za mitaa kuwa na ufahamu juu ya vihatashiri vya ubadhirifu kama inavyoelezewa katika aya ya 3.3.3.3 ya Mwongozo wa Kuunda na Kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Ubadhirifu katika Sekta za Umma wa Mwaka 2015 ili kuboresha uzingatiaji wa sheria na ushiriki wa watumishi wote katika usimamizi wa vihatarishi;

Maelezo ya Halmashauri husika yameoneshwa katika **kiambatisho 9-2**

**Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuimarisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi ili kuhakikisha kuwa viashiria vya hatari na ubadhilifu vinatambuliwa na kudhibitiwa kabla ya kusubiri matokea pia kuweza kurekebisha udhaifu uliobainika ili kulinda rasilimali za umma.**

## 9.3 Mapungufu katika Usimamizi wa TEHAMA pamoja na Mifumo ya Uhasibu

Agizo la 7(i) la randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa, 2009, linawataka Wakurugenzi wa Halmashauri kuwajibika katika kuhakikisha kuwa mifumo ya kompyuta inafanya kazi,

Ufanisi katika matumizi ya Mfumo wa Habari na Mawasiliano kama chombo cha kukuza utawala bora una mchango mkubwa katika utekelezaji wa sera zitakazopelekea kufikia malengo katika kutoa huduma kwa jamii,hii ni pamoja na kujenga uwajibikaji miongoni mwa watumishi wenye dhamana ya uongozi wanapotekeleza majukumu yao kwa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya TEHAMA pamoja na mifumo ya fedha.

Nimefanya tathmini kuhusu mfumo wa udhibiti wa teknolojia ya habari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/22, na kubaini kasoro zifuatazo:

(i) Kushindwa Kuunganisha Mifumo ya fedha yenye Utendaji Sawa

Serikali imeidhinisha MUSE kuwa mfumo wa usimamizi wa fedha. Hata hivyo, kuna mifumo mingine ya kihasibu kama vile Mfumo wa Uhasibu na utoaji taarifa za kifedha (FFARS) ulioandaliwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ili kusimamia matumizi na mapato kwenye vituo vya afya na elimu. Pia kuna GAMIS, mfumo unaotumika kwa ajili ya usimamizi na utunzaji wa taarifa za mali, pamoja na GoTHOMIS mfumo unaotumika katika vituo vya kutolea huduma za afya, kuwa na mifumo mingi inayofanya kazi sawa hupelekea kuongeza gharama za usimamizi na matengenezo;

(ii) Madeni ya leseni za biashara hayaoneshi uhalisia kutokana na mfumo wa ukusanyaji wa mapato (LGCRIS) kutengenezwa kwa kufuata mwaka wa fedha huku leseni zinazotolewa zikiwa zinadumu kwa muda wa mwaka mmoja tokea kutolewa kwake. Hii inaweza kusababisha utoaji wa taarifa zisizo sahihi;

(iii) Mamlaka 11 za Serikali za Mitaa zilikuwa na upungufu wa watumishi 32 wa TEHAMA na hivyo kusababisha upungufu katika

utoaji wa msaada wa huduma za TEHAMA kwa watumishi na jamii katika Halmashauri husika;

(iv) Halmashauri 16 hazikuwa na kamati ya kimkakati ya technologia ya habari iliyoidhinishwa jambo ambalo lingeweza kusababisha usimamizi hafifu wa masuala ya TEHAMA katika kutimiza malengo ya halmashauri husika. Pia hakukuwa na mpango mkakati wa kuzuia hasara zinazotokana na upotevu wa taarifa unaoweza kusababishwa na majanga kama vile moto, mafuriko na kukatika kwa umeme;

(v) Mamlaka 18 za serikali za mitaa hazikuwa na mipango ya kurejesha taarifa na huduma panapotokea majanga ili kujikinga na upotevu wa taarifa endapo yatatokea majanga kama vile moto, mafuriko au kukatika kwa umeme, Pia mamlaka 10 za serikali za mitaa hazikuwa na muundo sahihi wa kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA inalindwa dhidi ya majanga ya uharibifu kwa kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kutosha kama vile vifaa vya kuzima moto, mifumo ya kutambua uwapo wa moto na viyoyozi.

(vi) Halmashauri 15 hazikuwa na programu za mafunzo ya kujenga uwezo wa TEHAMA kwa wafanyakazi ili kuimarisha matumizi bora ya vifaa vya TEHAMA na usalama wa taarifa za kimifumo;

(vii) Mamlaka 11 za serikali za mitaa hazikuwa na programu iliyohuishwa ya kuzuia virusi katika kompyuta (Anti-virus software) kwa ajili ya kulinda taarifa zake dhidi ya virusi;

Mapungufu katika Usimamizi wa TEHAMA pamoja na Mifumo ya Uhasibu yameelezwa zaidi katika kiambata 9-3

**Ninaishauri Ofisi ya Rais TAMISEMI kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanzisha mfumo mpya,Pia kutumia mfumo mmoja wa uhasibu kwa shughuli zinazofanana kwa kuzingatia ufanisi katika utendaji na kuzingatia matumizi bora ya fedha za umma.**

**Pia, Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa kuboresha mifumo ya TEHAMA kwa kushughulikia mapungufu yaliobainishwa, kwa kuziwezesha idara za TEHAMA vitendea kazi ili kufikia utekelezaji wa sera kupitia matumizi bora ya TEHAMA.**

## 9.4 Mapungufu Katika Utendaji wa Kamati za Ukaguzi

Agizo la 12 la randama ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na aya ya 3.5 ya mwongozo wa kamati ya ukaguzi wa June ,2019 unazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuunda kamati ya ukaguzi ambayo ina wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano ambapo wajumbe wote au wengi wao wapatikani kutokea nje ya halmashauri.

Madhumuni ya msingi ya kamati ya ukaguzi ni kutoa ushauri katika mchakato wa uandaaji wa taarifa za fedha, mchakato wa ukaguzi, kusimamia mifumo ya udhibiti wa ndani, na kusimamia kanuni, taratibu na sheria.

Nilifanya tathmini ya utendaji wa kamati za ukaguzi katika mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/22 na kubaini kasoro zifuatazo:

**(i)** Kamati za ukaguzi katika mamlaka 13 za serikali za mitaa hazikutayarisha na kuwasilisha taarifa za mwaka kwa Waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa, Mkuu wa Mkoa, na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelezwa chini ya agizo la 12(5)(g) la randama ya fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2009. Hii imesababisha mamlaka husika kutokuwa na taarifa za kazi zilizofanyika katika kamati za ukaguzi;

**(ii)** Kamati za ukaguzi katika Mamlaka 11 za serikali za mitaa hazikupitia taarifa za fedha kinyume na agizo la 12(5) la randama ya fedha ya mamlaka za serikali za mitaa,2009 hivyo hakuna ushauri uliotolewa kwa maofisa masuuli katika halmashauri husika kuhusu maboresho ya uandaaji na mapitio ya taarifa za fedha;

**(iii)** Mamlaka tisa za serikali za mitaa hazikuwapatia mafunzo ya awali wajumbe wake wapya wa kamati za ukaguzi ili kuwa na uelewa juu ya majukumu yao. Pia, mamlaka nyingine saba za serikali za mitaa hazikuwafanyia mafunzo wajumbe wake wa kamati za ukaguzi katika maeneo mbalimbali muhimu kama vile usimamizi wa ununuzi, usimamizi wa vihatarishi na mifumo ya

taarifa kama vile FFARS, GoT-HoMIS, HCMIS, TANePS, MUSE na LGRCIS;

**(iv)** Kamati za Ukaguzi katika mamlaka 10 za serikali za mitaa hazikujifanyia tathmini ya kazi zake jambo ambalo ni kinyume na Aya ya 5.1 ya Mwongozo wa Kamati za Ukaguzi wa Mwezi Juni 2019 inayozitaka Kamati za Ukaguzi kila mwaka kujifanyia tathmini ya utendaji na matokeo yaliyopatikana kwa kulinganisha na Mwongozo wa kamati ya Ukaguzi;

**(v)** Katika mamlaka saba za serikali za mitaa hapakufanyika vikao vya kamati za ukaguzi, Kwa mamlaka ambazo vikao vilifanyika kamati zilijadili zaidi taarifa za ukaguzi wa ndani kuliko maeneo mengine kama vile ufanisi katika usimamizi wa vihatarishi, ufuatiliaji wa mazingira ya udhibiti wa ndani na namna mamlaka za serikali za mitaa zinavyozingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Jambo hili linaziondolea kamati nafasi ya kuhusika katika kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani na tathimini ya ufanisi juu ya utawala bora katika mamlaka za serikali za mitaa.

Maelezo kuhusu mapungufu ya utendaji wa kamati za ukaguzi yameoneshwa kwenye **kiambatisho 9-4**

**Ninashauri menejiment za serikali za mitaa kuzihimiza kamati za ukaguzi kujifanyia tathmini ya utendaji wake kila mwaka ambapo kasoro zitakazobainika zinatakiwa kufanyiwa marekebisho ikiwa ni pamoja na kuzipatia kamati mafunzo, vitendea kazi, na kuchukua hatua za kuzuia mapungufu yaliyobainika yasijirudie, hii itaziwezesha kamati hizo katika mamlaka za serikali za mitaa, kutimiza majukumu yao vema kwa maslai ya umma.**

## 9.5 Tathmini katika mfumo wa taarifa za ukusanyaji wa mapato Serikali za Mitaa (LGRCIS) na Mashine za ukusanyia mapato (POS)

### (i) Ukiukwaji wa Kanuni ya Mgawanyo Wa Majukumu

Kifungu cha 6.11.1 (a) cha Mwongozo wa Mapato wa Mamlaka za Mitaa kinafafanua Mgawanyo wa majukumu kama kuwapo kwa uwazi katika mgawanyo wa kazi na kwamba mtumishi mmoja haruhusiwi kushughulikia muamala kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Mfumo wa MUSE una hatua nne za kukamilisha muamala kama namna ya udhibiti

Mapitio ya mchakato wa udhibiti wa ndani juu ya marekebisho ya miamala yaliofanywa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yalibainisha kuwa, marekebisho yanapofanywa katika mfumo na mhasibu kwa kuingiza data za hesabu, huidhinishwa moja kwa moja bila kuangaliwa na kuthibitishwa kabla ya kutolewa kwa idhini na mkurugenzi wa halmashauri husika.

Kutokuwapo kwa mgawanyo wa majukumu ambayo ni nyenzo ya msingi ya usimamizi endelevu wa vihatarishi na udhibiti wa ndani kunaiweka Halmashauri katika hatari kama watumishi wasio waaminifu wataamua kutumia mwanya huo katika kujaribu kufanya vitendo vya ubadhilifu dhidi ya mapato yanayokusanywa.

**(ii) Kuwepo kwa mashine za kukusanyia mapato zilizosajiliwa kwa namba ya utambulisho zaidi ya moja**

Ukaguzi nilioufanya katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS), malipo ya mtandaoni na dashi bodi pamoja na mashine za kukusanyia mapato (POS) nilibaini kuwa, Halmashauri tatu zilisajili mashine 60 za kukusanyia mapato (POS) kwa kutumia namba ya utambulisho (IMEI namba) moja kinyume na matakwa ya sheria.

Kuwa na namba moja ya utambulisho katika usajili wa mashine za kukusanyia mapato kunaweza kusahawishi ubadhirifu wa mapato yanayokusanywa kwani miamala inayofanyika katika mashine hizo zenye namba sawa za utambulisho haitathibitika katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato hivyo itakuwa rahisi kubatilishwa.

**(iii) Kuwepo kwa Mashine za kukusanyia mapato zilizozimwa kwa muda mrefu**

Mapitio ya Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) kwa kuangalia dashibodi ya pamoja ya vyanzo vya mapato, nilibaini kuwa mashine 154 vya POS katika Halmashauri tisa hufanya kazi nje ya mtandao kwa muda mrefu kwa wastani wa siku tisa hadi 391.Hii inaashiria hapakuwa na usimamizi imara katika ukusanyaji wa mapato.

(iv) **Kutokamilika kwa taarifa za usajili wa mashine za kukusanyia mapato(POS)**

Ibara ya 6.11.3 ya randama ya fedha ya serikali ya mitaa,2019 inazitaka Halmashauri kutunza daftari la kupokea na kutoa nyaraka muhimu,na lazima pawepo na kumbukumbu za maelezo yanayojitosheleza juu ya mahali,na taarifa muhimu za afisa anayehusika. Ukaguzi uliofanyika katika daftari la taarifa za mashine za kukusanyia mapato(POS) ilibainika kuwa mashine za 75 katika halmashauri hazikuwa na taarifa za kujitosheleza mahali mashine ilipo,jina na sahihi ya mkusanyaji.Hii inaweza kusababisha ugumu katika kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu anayehusika ikiwa kuna makosa yoyote katika matumizi ya mashine za kukusanyia mapato(POS)

Maelezo kuhusu Usimamizi wa Mashine za kukusanyia mapato (POS) yameonyeshwa kwenye **Kiambatisho 9-5**

**Ninaishauri menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa:**

**(a) Mfumo wa MUSE ufanyiwe muundo ambao hautapitisha muamala unaoingizwa kwenye leja bila ya kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Halamshauri husika.**

**(b) Idhini ya utumiaji wa MUSE ipitiwe na kurekebishwa ili kuonyesha kiwango cha mamlaka kinachohitajika kwa ajili ya majukumu ya mtumiaji ambayo yatazingatia mgawanyo wa majukumu uliopitishwa.**

**(c) Kuimarisha udhibiti katika ukusanyaji wa mapato na kutekeleza kuzingatia taratibu za udhibiti wa ndani zilizowekwa.**

## 9.6 Taarifa za mapato zilizotangazwa kutofautiana na kiasi kilichopo katika mfumo wa makusanyo ya mapato (LGRCIS)

Agizo la 29 (2) la randama ya fedha za mamlaka za serikali za mitaa, 2009 linamtaka Mweka Hazina wa mamlaka ya serikali ya mitaa kuhakikisha anafanya usuluhishi wa kibenki, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa akaunti za benki na kitabu cha fedha na taarifa za benki,

unafanyika kwa muda usiozidi mwezi mmoja; na kufanya ulinganifu wa marekebisho kwa jinsi inavyohitajika

Kwa kulinganisha ripoti ya makusanyo ya vyanzo vya mapato iliyochapishwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI na ripoti ya ukusanyaji wa vyanzo hivyo kupitia mfumo wa makusanyo (LGRCIS) katika sampuli ya Halmashauri nne nilibaini kuwa, ripoti hizo mbili zilikuwa na tofauti hivyo kusababisha makusanyo ya mapato yaliyotangazwa kuwa chini au juu ya makusanyo halisi ukilinganisha na mfumo wa ukusanyaji wa mapato(LGRCIS) kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali namba 9-2

Kutoa taarifa zisizo sahihi kuhusu ukusanyaji wa mapato kunaweza kuwapotosha watumiaji wa taarifa za mapato, aidha kunaweza sababisha uandaaji wa taarifa za fedha zisizo sahihi zitakazoathiri utoaji wa maamuzi kwa wale wenye dhamana ya uongozi na watumiaji wengine wa taarifa hizo muhimu.

**Jedwali Na.9-1: Taarifa za Mapato Zilizotagazwa Tofauti na Kiasi Kilichopo Katika Mfumo wa Makusanyo (LGRCIS)**

| Jina la Halmashauri | Kiasi cha mapato kilichotangazwa na TAMISEMI | Mapato yaliyoonekana katika mfumo wa mapato(LGRCIS) | Tofauti | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| H/W Misenyi | 4,595,291,909 | 4,911,541,984 | 316,250,075 | Kiasi kilichotangazwa ni kidogo kuliko mapato halisi |
| H/M Kigamboni | 10,761,334,792 | 10,301,385,553 | **459,949,239** | Kiasi kilichotangazwa kimezidi mapato halisi |
| H/jiji Tanga | 17,391,716,080 | 15,700,770,224 | 1,690,945,856. | Kiasi kilichotangazwa kimezidi mapato halisi |
| H/M Ubungo | 27,868,406,661 | 24,414,268,232 | 3,454,138,429 | Kiasi kilichotangazwa kimezidi mapato halisi |
| H/W Nyangw'ale | 2,277,947,659 | 2,807,658,963 | 529,711,304 | Maoni Kiliasi kilichotangazwa ni kidogo kuliko mapato halisi |
| H/W Kilindi | 2,300,345,541 | 1,830,258,988 | 470,086,553 | Kiasi kilichotangazwa kimezidi mapato halisi |

**Naishauri OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa taarifa zinazotolewa kwa jamii ziwe sahihi kwa kufanya ulinganifu wa vyanzo vya taarifa hizo kutoka mamlaka za serikali za mitaa husika kabla ya kutoa taarifa hizo kwenye umma.**

# SURA YA KUMI



# MFUKO WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

## 10.0 Utangulizi

Mwaka 1993, Serikali ilianzisha Mfuko wa Fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuwainua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi ambapo wengi wao wamekuwa wakishindwa kukidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kwa kutokuwa na dhamana.Mfuko huu umebainishwa chini ya kifungu cha 17 (1) cha sheria ya maduhuri na ukaguzi [Sura ya 439]. Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia 5 kwa wanawake na asilimia 5 kwa vijana.

Utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu unalenga kukuza uchumi miongoni mwa makundi husika kwa kujishughulisha na katika shughuli za maendeleo na kuboresha hali zao za maisha.

Ili fedha zinazochangwa kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu zizunguke, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha fedha zilizokopeshwa zinarejeshwa kulingana na makubaliano kati ya Halmashauri husika na vikundi vya wanufaika.

Mnamo mwaka 2019, Serikali kupitia Bunge ilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 [Iliyorejewa 2019] kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kifungu cha 37A(1) cha Sheria hii kinazitaka Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu vilivyosajiliwa. Vile vile, kanuni ya 4 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa mikopo kwa

vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5 Aprili 2019) inazitaka Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Mgawanyo wa asilimia za utoaji wa mikopo kwa vikundi ulifanyiwa marekebisho hadi asilimia nne kwa vikundi vya wanawake na vijana, na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290 [Iliyorejewa 2019].

Kwa sasa, Mfuko una thamani ya shilingi bilioni 203.19 kutoka Halmashauri 184. Nilishindwa kuthibitisha kwa uhakika usahihi wa mali zilizoripotiwa kwani haziakisi michango yote ya Halmashauri tangu kuanzishwa kwa mfuko na hii imesababisha Halmashauri nyingi kupata maoni yenye shaka kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na 10-1**

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Mamlaka 184 za Serikali za Mitaa zilichangia shilingi bilioni 59.30 kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.10-2**.

Pamoja na mafanikio kadhaa ya mfuko, nimebaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji kurekebishwa haraka kwa ajili ya uendelevu wa mfuko.

## 10.1 Kutorejeshwa Shilingi Bilioni 88.42 Zilizotolewa kama Mkopo kwenye Vikundi

Kanuni ya 24 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 inafafanua hatua za kinidhamu kwa mtu atakayetumia mkopo kinyume na shughuli zilizoidhinishwa na Kamati ya Fedha na Mipango au kutoa taarifa za uongo kwa lengo la kujipatia mkopo, kuwa atawajibika kulipa faini ya kati ya shilingi 200,000 na shilingi 1,000,000 au kifungo kati ya miezi 12 na 24.

Tathmini yangu juu ya uendeshaji wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu nilibaini kuwa, wanufaika wa mikopo katika Mamlaka 180 za Serikali za Mitaa wameshindwa kurejesha mikopo ya

shilingi bilioni 88.42 kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.10-3**.

Kutorejeshwa kwa mikopo husika pamoja na mambo mengine, kumechangiwa na wahusika kutochukuliwa hatua kali za kisheria zitakazowasukuma walazimike kurejesha mikopo hiyo.

**Ninapendekeza kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI iongeze udhibiti ndani ya mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wanavikundi wanaokiuka mikataba ya mikopo.**

## 10.2 Fedha za Mikopo ya Vikundi kugawanywa Miongoni mwa Wanavikundi Shilingi Milioni 774.66

Kanuni ya 9(1) ya Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 inaeleza kuwa, "mikopo iliyotolewa chini ya kanuni hii itatumika kutekeleza miradi iliyoidhinishwa na Kamati ya Fedha, Mipango na Usimamizi kwa kuzingatia ushauri na mapendekezo ya menejimenti na Kamati ya Huduma za Mikopo".

Nilibaini kuwa vikundi 201 kwenye Mamlaka nane za Serikali za Mitaa vilivyopewa mikopo ya shilingi milioni 774.66 havikutekeleza miradi iliyoidhinishwa, bali fedha hizo ziligawanywa miongoni mwao na hapakuwa na ushahidi wowote kwamba fedha hizo zilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.10-1**.

**Jedwali Na.10.1: Mikopo Iliyogawanywa Miongoni kwa Wanakikundi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/M Ubungo | 23 | 218,800,000 |
| 2. | H/Mji Makambako | 90 | 177,000,000 |
| 3. | H/W Geita | 22 | 112,920,000 |
| 4. | H/W Monduli | 47 | 91,943,500 |
| 5. | H/Jiji Arusha | 10 | 84,000,000 |
| 6. | H/W Makete | 5 | 65,000,000 |
| 7. | H/W Rungwe | 1 | 20,000,000 |
| 8. | H/M Temeke | 3 | 5,000,000 |
| **Jumla** | | **201** | **774,663,500** |

Hakuna uhakika wa urejeshwaji wa fedha zilizokopwa, kwa sababu hapakuwa na miradi ya vikundi vilivyopewa mikopo.

**Ninapendekeza kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI na vyombo vya usimamizi vifanye ufuatiliaji wa karibu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu inatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na hatua stahiki za kisheria zichukuliwe kwa wanakikundi waliotumia fedha hizo vibaya.**

## 10.3 Kutokuwepo kwa Vikundi Vilivyopewa Mikopo ya Shilingi Milioni 895.94

Nilishindwa kujiridhisha juu ya kuwepo kwa vikundi 48 vilivyopewa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 895.94 kwenye Mamlaka tatu za Serikali za Mitaa. Aidha, nilibaini kuwa, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika hawakufahamu lolote kuhusu vikundi hivyo kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.10- 2.**

**Jedwali Na.10.2: Halmashauri zenye Vikundi Visivyokuwepo**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 34 | 698,700,000 |
| 2. | H/M Temeke | 9 | 178,536,140 |
| 3. | H/W Meru | 5 | 18,700,000 |
| **Jumla** | | **48** | **895,936,140** |

Nina shaka juu ya uamuzi wa Mamlaka hizo za Serikali za Mitaa wa kutoa mikopo kwa vikundi ambavyo hata Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika hawana taarifa zao. Hii inaashiria matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Ninashauri Ofisi ya Rais TAMISEMI ichukue hatua stahiki kwa watumishi waliotoa mikopo kwa vikundi ambavyo hapakuwa na taarifa za kuwepo kwao ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwenye vyombo vya uchunguzi.**

## 10.4 Mikopo Inayodaiwa kwenye vikundi Vilivyositisha Shughuli za Biashara Shilingi Bilioni 2.25

Kanuni ya 13 (1) (d)-(f) ya Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2019 inamtaka Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ; kufuatilia uendeshaji na uwepo wa vikundi, urejeshaji wa mikopo

iliyotolewa, ufuatiliaji wa mikopo iliyotolewa ili kuhakikisha kuwa inatumika kama ilivyokusudiwa na kuratibu mafunzo kwenye vikundi.

Tathmini yangu kuhusu mikopo iliyotolewa kwa vikundi nilibaini kuwa, Mamlaka tisa za Serikali za Mitaa zilikuwa zikitoa mikopo ambayo haijakurejeshwa yenye jumla ya shilingi bilioni 2.25 kutoka kwenye vikundi 627 vilivyositisha shughuli zao za biashara kutokana na sababu kama vile; kutokuwepo kwa wateja wa bidhaa au huduma zinazotolewa, kuongezeka kwa bei za malighafi zinazotumika katika uzalishaji, migogoro kati ya wanakikundi, wizi, wanachama kuhamia maeneo mengine na kupata hasara kubwa kwenye biashara. Tazama idadi ya vikundi na maeneo husika katika **Jedwali Na. 10-3**.

**Jedwali Na.10.3: Mikopo Kwa Vikundi Vilivyositisha Biashara**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Vikundi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/Mji Geita | 396 | 1,054,782,100 |
| 2. | H/M Temeke | 19 | 412,630,699 |
| 3. | H/W Maswa | 25 | 179,661,077 |
| 4. | H/W Geita | 57 | 176,529,500 |
| 5. | H/Jiji Arusha | 29 | 141,321,800 |
| 6. | H/W Tandahimba | 31 | 121,541,000 |
| 7. | H/W Monduli | 53 | 105,387,153 |
| 8. | H/W Busega | 3 | 32,920,000 |
| 9. | H/Mji Mbulu | 14 | 27,778,400 |
| **Jumla** | | **627** | **2,252,551,729** |

Nina mashaka kwamba, mikopo ambayo haikurejeshwa kutoka kwenye vikundi vilivyositisha shughuli za biashara inawezekana isirejeshwe, na hivyo kusababisha upotevu wa fedha za Umma.

**Naishauri Ofisi ya Rais TAMISEMI kuziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa siku zijazo; kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa uendeshaji wa vikundi, kuendesha mafunzo na kufuatilia kwa ukaribu vikundi vilivyokopeshwa na kufanya upekuzi wa kina katika ujazaji wa fomu za maombi ya mikopo na mapendekezo ya miradi ya vikundi kabla ya kutoa mikopo. Zaidi za hayo, kutoa taarifa ya vikundi husika kwenye vyombo vya uchunguzi ili virejeshe kiasi kinachodaiwa.**

## 10.5 Mamlaka za Serikali za Mitaa Kutochangia Shilingi Bilioni 5.06 kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa madhumuni ya kufadhili vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu.

Nilibaini kuwa, Mamlaka 53 za Serikali za Mitaa hazikuchangia jumla ya shilingi bilioni 5.06 kwenye Mfuko kutoka kwenye mapato yao ya ndani kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 10-4**. Mwenendo wa uchangiaji kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu kwa miaka mitatu mfululizo umeoneshwa kwenye **Jedwali Na.10-5.**

**Jedwali Na.10.4: Halmashauri zisizokamilisha Michango Kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Kinondoni | 710,646,515 | 28. | H/W Kilolo | 46,232,070 |
| 2. | H/M Ilemela | 555,717,066 | 29. | H/W Namtumbo | 45,490,387 |
| 3. | H/Jiji Mwanza | 351,499,835 | 30. | H/W Arusha | 43,714,538 |
| 4. | H/Jiji Dar es Salaam | 308,937,093 | 31. | H/W Meatu | 38,209,981 |
| 5. | H/M Kigoma/Ujiji | 273,543,946 | 32. | H/Mji Makambako | 37,101,327 |
| 6. | H/W Geita | 272,752,367 | 33. | H/W Chamwino | 36,913,370 |
| 7. | H/M Morogoro | 254,245,993 | 34. | H/W Ruangwa | 33,704,697 |
| 8. | H/W Morogoro | 232,508,166 | 35. | Nanyumbu | 33,657,897 |
| 9. | H/Mji Njombe | 199,505,211 | 36. | H/W Bagamoyo | 31,532,309 |
| 10. | H/W Mufindi | 126,218,663 | 37. | H/W Malinyi | 28,879,613 |
| 11. | H/W Kalambo | 103,949,896 | 38. | H/W Kwimba | 23,776,226 |
| 12. | H/W Chalinze | 97,597,825 | 39. | H/Mji Mbinga | 23,728,495 |
| 13. | H/M Sumbawanga | 96,193,729 | 40. | H/W Bariadi | 23,240,000 |
| 14. | H/W Nkasi | 92,073,386 | 41. | H/W Newala | 21,860,904 |
| 15. | H/W Monduli | 88,886,754 | 42. | H/Mji Kibaha | 18,842,301 |
| 16. | H/W Magu | 74,103,566 | 43. | H/W Kasulu | 17,381,961 |
| 17. | H/W Kibiti | 69,287,768 | 44. | H/W Bukoba | 13,144,188 |
| 18. | H/M Songea | 64,995,892 | 45. | H/W Bahi | 11,635,247 |
| 19. | H/M Iringa | 62,030,785 | 46. | H/Mji Kasulu | 11,572,621 |
| 20. | H/W Ludewa | 59,890,298 | 47. | H/W Mtama | 11,548,901 |
| 21. | H/M Lindi | 58,192,665 | 48. | H/W Nyasa | 8,911,484 |
| 22. | H/W Sumbawanga | 57,565,394 | 49. | H/W Itilima | 7,994,789 |
| 23. | H/W Makete | 55,323,850 | 50. | H/W Kishapu | 7,947,937 |
| 24. | H/W Shinyanga | 53,921,364 | 51. | H/W Iringa | 6,167,464 |
| 25. | H/W Maswa | 51,030,656 | 52. | H/W Kakonko | 5,993,202 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 26. | H/W Longido | 49,436,661 | 53. | H/W Buchosa | 4,897,408 |
| 27. | H/W Njombe | 47,916,014 | **Jumla** | | **5,062,050,675** |

**Jedwali Na.10.5: Mwenendo wa michango kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu**

| Mwaka wa fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2021/22 | 53 | 5,062,050,675 |
| 2020/21 | 83 | 6,857,306,654 |
| 2019/20 | 82 | 5,720,140,159 |

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI na menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapelekwa kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kulingana na matakwa ya sheria.**

## 10.6 Mikopo ya Shilingi Bilioni 20.79 Iliyotolewa Bila Kuzingatia Uwiano wa Utoaji Mikopo

Kifungu cha 37A (1-2) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa madhumuni ya kutoa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Zaidi ya hayo, kinataka fedha zilizotengwa kutolewa kama mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa uwiano wa 40% kwa wanawake, 40% kwa vijana na 20% kwa watu wenye ulemavu.

Tathmini niliyoifanya kuhusu mikopo iliyotolewa kwenye vikundi nimebaini kuwa, Mamlaka 45 za Serikali za Mitaa zilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 20.79 kwenye vikundi bila kuzingatia uwiano wa utoaji mikopo. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizotoa mikopo bila kuzingatia uwiano wa utoaji mikopo imeoneshwa kwenye **Jedwali Na.10-6**.

**Jedwali Na.10-6: Halmashauri Zilizotoa Mikopo Kinyume na Uwino Unaotakiwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Uwiano wa Mikopo (%) | | | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Vijana | Watu wenye Ulemavu | |
| 1. | H/Jiji Arusha | 57 | 38 | 5 | 4,082,537,015 |
| 2. | H/Mji Njombe | 60 | 35 | 5 | 2,578,250,000 |
| 3. | H/W Missenyi | 53 | 44 | 3 | 1,048,941,324 |
| 4. | H/M Moshi | 70 | 27 | 3 | 949,398,700 |
| 5. | H/M Kahama | 59 | 39 | 2 | 754,176,796 |
| 6. | H/M Ilemela | 61 | 36 | 3 | 647,598,000 |
| 7. | H/W Moshi | 52 | 35 | 13 | 646,819,000 |
| 8. | H/W Hanang' | 61 | 35 | 4 | 643,000,000 |
| 9. | H/W Msalala | 46 | 51 | 3 | 606,000,000 |
| 10. | H/W Meru | 77 | 19 | 4 | 483,400,000 |
| 11. | H/M Mtwara | 65 | 29 | 6 | 457,398,000 |
| 12. | H/W Rombo | 35 | 49 | 16 | 435,658,560 |
| 13. | H/W Hai | 32 | 57 | 11 | 432,540,300 |
| 14. | H/W Kongwa | 43 | 49 | 8 | 393,915,580 |
| 15. | H/W Same | 47 | 37 | 16 | 362,600,000 |
| 16. | H/Mji Makambako | 54 | 38 | 8 | 329,000,000 |
| 17. | H/W Ngara | 50 | 48 | 2 | 324,990,000 |
| 18. | H/W Wanging'ombe | 53 | 40 | 7 | 309,920,000 |
| 19. | H/W Ludewa | 35 | 57 | 8 | 298,000,000 |
| 20. | H/W Mkalama | 67 | 31 | 2 | 288,906,230 |
| 21. | H/W Shinyanga | 57 | 41 | 2 | 277,691,097 |
| 22. | H/W Chamwino | 56 | 32 | 12 | 259,900,000 |
| 23. | H/W Ruangwa | 14 | 83 | 3 | 256,158,000 |
| 24. | H/W Siha | 59 | 30 | 11 | 248,793,022 |
| 25. | H/W Misungwi | 53 | 41 | 6 | 246,951,000 |
| 26. | H/W Masasi | 53 | 43 | 4 | 238,000,000 |
| 27. | H/W Kishapu | 51 | 43 | 6 | 214,000,000 |
| 28. | Babati | 11 | 85 | 4 | 190,313,060 |
| 29. | H/W Pangani | 36 | 37 | 27 | 185,455,112 |
| 30. | H/W Magu | 44 | 40 | 16 | 171,668,405 |
| 31. | H/W Nanyumbu | 55 | 33 | 12 | 167,600,000 |
| 32. | Mbulu | 62 | 33 | 5 | 167,535,000 |
| 33. | H/W Makete | 46 | 51 | 4 | 166,400,000 |
| 34. | H/W Mtama | 31 | 56 | 13 | 166,000,000 |
| 35. | H/Mji Nanyamba | 32 | 48 | 20 | 164,420,000 |
| 36. | H/W Mbulu | 53 | 37 | 10 | 156,944,330 |
| 37. | H/W Kondoa | 57 | 25 | 18 | 150,258,000 |
| 38. | H/Mji Kondoa | 60 | 38 | 2 | 140,000,000 |
| 39. | H/Mji Tarime | 64 | 24 | 12 | 127,000,000 |
| 40. | H/W Chemba | 85 | 10 | 5 | 124,000,000 |
| 41. | H/W Kiteto | 47 | 45 | 8 | 123,371,000 |
| 42. | H/W Buhigwe | 34 | 48 | 18 | 123,220,000 |
| 43. | H/W Newala | 42 | 47 | 11 | 116,800,000 |
| 44. | H/W Sengerema | 52 | 31 | 17 | 102,360,000 |
| 45. | H/W Kalambo | 78 | 22 | 0 | 101,247,000 |
| **Jumla** | | | | | **20,790,786,237** |

Kutozingatia uwiano wa utoaji wa mikopo kunavinyima vikundi vingine fursa ya kupata mikopo, pia kunazuia juhudi za Serikali za kukuza uchumi miongoni mwa vikundi husika.

**Ninapendekeza kuwa, Mamlaka husika za Serikali za Mitaa zihakikishe zinazingatia Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kwa kuhakikisha zinatoa mikopo kwa kuzingatia uwiano uliokubalika.**

## 10.7 Kutopelekwa Fedha za Usimamizi na ufuatiliaji wa Vikundi kwenye Ngazi ya Kata

Kanuni ya 23(2) ya Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2019 (zilivyorekebishwa mwaka 2021) inataka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchangia shilingi milioni moja hadi milioni tano kwa mwezi kuzingatia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuwezesha gharama za usimamizi na ufuatiliaji wa vikundi.

Nilibaini kuwa fedha za usimamizi hazikutolewa kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata na Maafisa Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli za Mfuko.

Kutotengwa kwa fedha za usimamizi katika ngazi ya Kata kunaathiri usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za vikundi na kupelekea kuzorota kwa urejeshaji wa mikopo na uendelevu wa miradi ya vikundi.

**Naishauri Ofisi ya Rais TAMISEMI kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapeleka fedha za ufuatiliaji na usimamizi kwenye ngazi za Kata ili kuwezesha ufuatiliaji wa vikundi vilivyopewa mikopo,kutoa mafunzo yanayohitajika kuhusu miradi ya vikundi na kuimarisha urejeshaji wa mikopo iliyotolewa.**

## 10.8 Mikopo ya Shilingi Milioni 147.26 Imetolewa kwa Watu Wenye Ajira Rasmi

Nilibaini kuwa, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilitoa mikopo ya shilingi milioni 147.26 kwa vikundi vitano ambavyo vilikuwa na wanachama wenye ajira rasmi kinyume na Kanuni ya 6(1)(f) ya Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu

Wenye Ulemavu za mwaka 2019 (zilizorekebishwa mwaka 2021) ambayo inazuia utoaji wa mikopo kwa vikundi ambavyo wanachama wake wana ajira rasmi.

Nina shaka kwamba, malengo ya kuanzishwa kwa Mfuko hayawezi kufikiwa kwa vile mikopo ilitolewa kwa watu ambao hawakustahili kupewa mikopo hiyo.

**Napendekeza kuwa, Halmashauri husika kwa siku zijazo izingatie kanuni za utoaji mikopo, ambayo ni kutoa mikopo kwa vikundi ambavyo wanachama wake hawana ajira rasmi.**

## 10.9 Kutoshirikishwa kwa Wataalam wa Usimamizi wa Mikopo katika Mchakato wa Utoaji na Urejeshwaji wa Mikopo

Kanuni ya 8 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019 inataka taratibu zote za utoaji wa mikopo zisimamiwe na mamlaka za serikali za mitaa.

Tathmini niliyoifanya ya taratibu zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa utoaji wa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa, nilibaini changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uwezo mdogo wa watumishi katika Idara za Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri kuweza kufuatilia na kusimamia urejeshwaji wa mikopo hiyo na kutoa elimu juu ya masuala ya maendeleo ya kibiashara kwa wanufaika, jambo ambalo linapunguza uwezo wa Mfuko kufanya kazi ipasavyo.

Pia, nilibaini kuwa uhakiki wa vikundi vilivyoomba mikopo ulikuwa haufanyiki kabla ya mikopo kutolewa. Hii ni kutokana na ukosefu wa utaalamu wa kufanya uhakiki unaostahili katika mikopo. Aidha, kukosekana kwa usaidizi wa kisheria kutoka katika vitengo vya sheria kuhusu masuala ya bima hasa kwa mikopo inayotolewa kwa vijana, ambao mara nyingi walikuwa wakinunua pikipiki na bajaji. Pia, Mfuko hauna sera ya kushughulikia mikopo isiyolipika 'NPL'.

Kutokana na kukosekana kwa watu wenye ujuzi wa kutosha wa kusimamia fedha za Mfuko, kumekuwapo na ongezeko la mikopo ambayo haikurejeshwa kutoka kwenye vikundi hadi kufikia shilingi bilioni 39.72 kwenye Mamlaka 78 za Serikali za Mitaa (kama inavyofafanuliwa katika aya ya 10.1 ya ripoti hii), kutokana na mikopo

isiyolipika na/au ya uwongo, ambayo matokeo yake inaweza kuathiri mzunguko wa fedha za Mfuko na kuathiri uendelevu wa Mfuko.

**Napenda kusisitiza pendekezo langu la mwaka uliopita kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI iangalie uwezekano wa kutumia Benki za Serikali, kama vile Benki ya Biashara Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Mameneja wa Mifuko wenye uzoefu na utaalamu wa kutosha katika kutathmini, kutoa na kusimamia urejeshwaji wa mikopo ili kuhakikisha mikopo inatolewa kwa ufanisi na inafuatiliwa na kulipwa; kwa gharama ndogo za uendeshaji.**

**Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI inashauriwa kuandaa sera ya mikopo isiyolipika 'NPL' ili kusimamia mikopo inayotolewa kwa vikundi kwa lengo la kupunguza upotevu wa fedha zinazotolewa kama mikopo.**



# SURA YA KUMI NA MOJA

# TATHMINI YA MIRADI YA MAENDELEO

## 11.0 Utangulizi

Katika mwaka wa fedha unaoishia Juni 2021/22, mamlaka za serikali za mitaa zilitumia vyanzo mbalimbali kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo ikiwamo, fedha za makusanyo ya mapato ya ndani, ruzuku kutoka serikali kuu, michango ya wananchi, na wafadhili mbalimbali. Baadhi ya vyanzo vya fedha hizo ni Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG), ruzuku ya maendeleo ya sekta ya afya, mfuko wa kuchochea maendeleo ya jimbo na mpango wa kuboresha elimu (EQUIP-T).

Licha ya matumizi ya vyanzo mbalimbali vya fedha,tathmini ya miradi iliyotekelezwa imeonyesha dosari kadhaa zinazohitaji kuangaliwa kwa umakini. Dosari hizo ni pamoja na; kutofautiana katika utekelezaji wa mradi, mifumo hafifu ya ufuatiliaji na tathmini, na ukosefu wa uwazi katika usimamizi wa fedha.

Ili kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa mradi katika siku zijazo, ni muhimu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kushughulikia mapungufu yaliyobainishwa na kutekeleza taratibu sahihi za ufuatiliaji na tathmini.

Nilibaini masuala mbalimbali kuhusiana na matokeo ya utekekelezaji wa miradi na taarifa za fedha kama inavyoainishwa hapa chini.

## 11.1 Miradi zilizotekelezwa bila vibali na vyeti vya awali vyenye thamani ya Shilingi Billioni 36.68

Kifungu cha 29(1) (b) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 Toleo la 334 la mwaka 1999, Kifungu cha 81(2) ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya

mwaka 2004, Kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Upangaji Miji Na.8 ya mwaka 2007, na Kifungu cha 124(1) (C) cha Kanuni za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) za mwaka 2008 vinahitaji nyaraka muhimu, ikiwa ni pamoja na hati ya umiliki, ripoti ya tathmini ya athari za mazingira, na kibali cha ujenzi, kupatikana kabla ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Nilibaini kwamba mamlaka 11 za serikali za mitaa zilitekeleza miradi mikubwa yenye thamani ya shilingi bilioni 36.68 bila kufuata mahitaji muhimu ya awali kinyume na sheria zilizotajwa hapo juu. Hii ilisababishwa na udhibiti duni juu ya upangaji wa Halmashauri katika usimamizi wa miradi na shinikizo la kutekeleza miradi muhimu kwa haraka.

Utekelezaji wa miradi ya ujenzi bila kukidhi mahitaji muhimu kunaweza kuweka mamlaka za serikali za mitaa na watumiaji wake katika hatari isiyo ya lazima, ikiwa ni pamoja na hatari ya afya na migogoro ya umiliki katika kesi ya migogoro ya ardhi. Hii inaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma. Maelezo ya miradi iliyotekelezwa yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 11-I.**

**Ili kuzuia hatari na kuhakikisha fedha za umma zinatumika ipasavyo, Mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe mpangilio sahihi wa usimamizi wa miradi, na kuhakikisha utekelezaji wa matakwa ya kisheria. Mbali na kuchukua hatua, kulinda fedha za umma na kukuza uwazi,uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali.**

## 11.2 Miradi Iliyokamilika lakini Haitumiki yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.31

Nilibaini kuwa, miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 3.31 ilikuwa imekamilika lakini haitumiki ipasavyo kama ilivyopangwa kutokana na uhaba wa rasilimali kama watumishi, stahiki mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa umeme, ukosefu wa wataalam wa kuendesha mifumo mbalimbali na idadi ndogo ya watumishi.

Miradi kutotumika baada ya kukamilika kunamaanisha kutokuwapo kwa mipango thabiti na mahususi wakati wa uanzishwaji ili kuhakikisha miradi hiyo inatumika kikamilifu. Maelezo ya Mamlaka za

serikali za mitaa zenye miradi iliyokamilika lakini haijaanza kutumika zimeoneshwa katika **Jedwali Na 11-1**

**Jedwali Na.11-1: Miradi Iliyokamilika Lakini Haitumiki**

| Na. | Jina la Halmashauri | Jina la mradi | Chanzo cha fedha | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Buchosa | Mgahawa katika halmashauri ya wilaya ya Buchosa | Serikali kuu | 143,111,310 |
| 2 | H/W Buhigwe | Jengo la kuhudumia idara za biashara na uwekezaji (kituo pamoja) | LIC | 50,000,000 |
| 3 | H/W Chamwino | Ujenzi wa ushauri nasaha wa mpango wa vijana | UNFPA | 35,000,000 |
| | | Ujenzi wa maabara shule ya sekondari Mvumi | Serikali kuu | 75,000,000 |
| | | Ujenzi wa madarasa mawili katika shule ya sekondari Dabalo | Serikali kuu | 40,000,000 |
| 4 | H/W Biharamulo | Ujenzi wa sekondari ya Msanzi | Serikali kuu | 12,500,000 |
| | | Ujenzi wa zahanati ya Msipazi | Global Fund | 174,209,079 |
| | | Umaliziaji wa ujenzi wa shule ya sekondari Matai | EP4R, Own source, na TASAF | 571,200,000 |
| 5 | H/W Kaliua | Ujenzi wa kituo cha afya | Serikali kuu | 349,872,600 |
| | | Ujenzi wa kituo cha afya cha Usinge | Serikali kuu | 174,761,109 |
| 6 | H/W Kibondo | Ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika Asali | Serikali kuu | 600,000,000 |
| 7 | H/W Kondoa | Ujenzi wa zahanati ya Potea village | Serikali kuu | 50,000,000 |
| 8 | H/Jiji Mwanza | Ujenzi wa shule ya sekondari Mkolani | SEQUIP | 470,000,000 |
| 9 | H/W karagwe | Ujenzi wa shule ya sekondari Ruhinda | Serikali kuu | 80,000,000 |
| | | Ujenzi wa madarasa shule ya msingi Msumbiji | Serikali kuu | 80,000,000 |
| **10** | H/Mji Kasulu | Ujenzi wa shule ya msingi Nyansha | Serikali kuu | 400,000,000 |
| **Jumla** | | | | **3,305,654,098** |

**Ninazishauri Menejimenti za Halmashauri kuchukua hatua stahiki kuhakikisha miradi iliyokamilika inatumika kulingana dhumuni lililopangwa**

**Hatua stahiki ni pamoja na kutenga rasilimali kutoka katika maeneo mengine au kuomba fedha za nyongeza ili kuhakikisha miradi iliyokamilika inatumika kwa usahihi. Aidha ni vema kuhakikisha fedha za umma zinatumika ipasavyo na kwa ufanisi kwa manufaa ya umma.**

## 11.3 Fedha zilizotolewa kutoka kwenye miradi ya maendeleo kufadhili shughuli zisizokusudiwa Shilingi Billioni 1.60

Kifungu cha 47 (1) (a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 kinasema bajeti ya Serikali na Taasisi za Umma ikiidhinishwa, itatumika tu kwa mujibu wa lengo lililoelezwa na ndani ya kikomo kilichowekwa ndani ya makadirio ya Serikali na Taasisi za Umma.

Nilibaini mamlaka 14 za serikali za mitaa zilielekeza jumla ya shillingi billioni 1.60 kufadhili shughuli ambazo hazikutengewa bajeti.

Matumizi ya fedha kinyume na bajeti kunaathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo zilizopangwa; na kuathiri malengo ya mamlaka za Serikali za mitaa ya kutoa huduma bora kwa jamii. Maelezo zaidi yanaonyeshwa katika **Jedwali 11-2.**

**Jedwali Na.11-2: Fedha za Miradi ya Maendeleo Zilizobadilishwa Matumizi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Chanzo cha fedha | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Longido | Serikali Kuu | 489,150,135 |
| 2 | H/W Ileje | Serikali Kuu | 214,939,843 |
| 3 | H/Jiji Tanga | Mapato ya Ndani | 181,212,578 |
| 4 | H/W Bariadi | Mapato ya Ndani | 110,224,078 |
| 5 | H/W Urambo | Serikali Kuu | 69,630,786 |
| 6 | H/W Rorya | Mapato ya Ndani | 59,802,030 |
| 7 | H/Mji Tarime | Serikali Kuu | 55,161,200 |
| 8 | H/M Singida | Mapato ya Ndani | 43,743,000 |
| 9 | H/W Iramba | Mapato ya Ndani | 43,019,027 |
| 10 | H/W Serengeti | Mapato ya Ndani | 38,305,000 |
| 11 | H/W Monduli | Mapato ya Ndani | 38,211,400 |
| 12 | H/Mji Handeni | Mapato ya Ndani | 41,184,396 |
| 13 | H/W Kilindi | Mapato ya Ndani | 156,747,698 |
| 14 | H/W Muheza | Mapato ya Ndani | 54,392,080 |
| **Jumla** | | | **1,595,723,251** |

**Ninashauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia matakwa ya bajeti na kuimarisha udhibiti na taratibu za kibajeti kwa kubainisha shughuli zote za kipaumbele ili kupunguza uhamishaji fedha baina ya vifungu wakati wa utekelezaji wa bajeti**

## 11.4 Miradi ambayo Haikukamilika pamoja na Iliyochelewa Kukamilika yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 112.24

Nilibaini kuwa miradi mbalimbali yenye thamani ya shillingi billioni 33.28 inayotekelezwa na mamlaka 20 za serikali za mitaa, haikukamilika licha ya muda wa utekelezaji wa mradi kuisha. Maelezo yanaonyeshwa katika **Jedwali Na 11-3.**

**Jedwali Na.11-3: Miradi Iliyochelewa Kukamilika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Jina la Mradi | Gharama ya mradi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | H/W Chunya | Ujenzi wa jengo la Utawala | 292,218,998 |
| 2 | H/Jiji Dodoma | Ujenzi wa soko la Machinga | 9,529,747,200 |
| | | Ujenzi wa majengo shule ya msingi Msalato | 290,000,000 |
| 3 | H/W Geita | Ujenzi wa jengo la utawala | 2,000,000,000 |
| 4 | H/W Kalambo | Ujenzi wa shule ya msingi Kipwa | 400,000,000 |
| 5 | H/W Momba | Ujenzi wa kituo cha afya Msangano | 250,000,000 |
| | | Ujenzi wa shule ya sekondari Ikana | 470,000,000 |
| | | Ujenzi wa jengo la utawala | 1,000,000,000 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi | 150,000,000 |
| 6 | H/Mji Njombe | Ujenzi wa shule ya sekondari Lunyanywi | 317,869,641 |
| 7 | H/M Moshi | Ujenzi wa upanuzi wa jengo la utawala. | 1,000,000,000 |
| 8 | H/W Tarime | Ujenzi wa shule ya sekondari Sirari. | 470,000,000 |
| | | Ujenzi wa sekondari ya Nyasaricho | 1,000,000,000 |
| 9 | H/M Bukoba | Ujenzi wa nguzo za taa kando ya barabara ya mji | 726,400,000 |
| 10 | H/Mji Geita | Ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri | 1,951,612,836 |
| 11 | H/W Kasulu | Ujenzi wa majengo shule ya sekondari Kalela | 470,000,000 |
| 12 | H/W Ngorongoro | Ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri | 1,000,000,000 |
| 13 | H/W Singida | Ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri | 1,000,000,000 |
| | | Ujenzi wa nyumba ya Mkurugenzi | 600,000,000 |
| 14 | H/M Kinondoni | Ujenzi wa madarasa na choo shule ya sekondari Kondo | 311,000,000 |
| | | Ujenzi wa madarasa na choo shule ya sekondari Boko Mtambani | 405,294,000 |
| | | Ujenzi wa shule ya msingi Kunduchi | 240,000,000 |
| | | Ujenzi wa madarasa shule ya sekondari Magomeni | 316,170,242 |
| | | Ujenzi wa madarasa shule ya msingi Tumaini | 90,000,000 |
| 15 | H/M Morogoro | Ujenzi wa madarasa shule ya sekondari Mindu | 37,503,410 |
| | | Ujenzi wa madarasa shule Mji Mpya- | 400,000,000 |
| 16 | H/W Nanyumbu | Ujenzi wa shule ya sekondari Naishelo | 470,000,000 |
| 17 | H/W Gairo | Ujenzi wa majengo mbalimbali shule ya sekondari Leshata | 470,000,000 |
| | | Ujenzi wa jengo la Mkurugenzi | 150,000,000 |
| 18 | H/W Kisarawe | Ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri | 933,889,140 |
| 19 | H/W Mafia | Ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri | 5,539,233,443 |
| 20 | H/W Ulanga | Ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri | 1,000,000,000 |
| **Jumla** | | | **33,280,938,910** |

Aidha, uhakiki wangu wa miradi ya maendeleao ulibaini miradi isiyokamilika yenye thamani ya shillingi billioni 78.96 katika mamlaka 67 za serikali za mitaa kama inavyoonesha katika **Kiambatisho 11-2.** Miongoni mwa miradi ambayo haijakamilika, ni miradi iliyotelekezwa yenye thamani ya shillingi billioni 14.31 katika mamlaka 13 za serikali za mitaa. Miradi hii ilikuwa imeachwa bila kukamilika kwa muda mrefu kuanzia miaka miwili hadi 23.

Kutokamilika kwa miradi kwa wakati, kumechangiwa zaidi na uhaba/kuchelewa kutolewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi, usimamizi na ufuatiliaji wa kutosha wa menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na ushiriki mdogo wa jamii katika utekelezaji wa miradi.

Kucheleweshwa ukamilishaji wa miradi ya maendeleo kunasababisha kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na kuongezeka kwa bei ya bidhaa za ujenzi kunakosababishwa na mfumuko wa bei. Pia, husababisha pia kuchelewa kwa manufaa yaliyokusudiwa kwa jamii.

**Ninashauri OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuanzisha utaratibu madhubuti ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya miradi yote ambayo haijakamilika, kufanya makadirio ya rasilimali zinazohitajika hadi kukamilika, na kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi husika ili kuepusha athari za gharama.**

**Zaidi ya hayo, ninapendekeza kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka kipaumbele katika kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuanza miradi mipya. Pia ninazishauri mamlaka husika kufanya tathmini ya kazi ambazo hazijakamilika za miradi husika na kuandaa mikakati ya kuikamilisha.**

**Aidha, Halmashauri husika zinapaswa kuboresha upangaji, ufuatiliaji na usimamizi wa miradi na kuhamasisha michango ya jamii ili kuhakikisha miradi iliyoanzishwa inakamilika kwa wakati.**

## 11.5 Kasoro zilizobainishwa katika Utekelezaji wa Miradi yenye thamani ya Shillingi Billioni 2.11

Nilibaini kasoro mbalimbali katika mamlaka tano za serikali za mitaa kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye thamani ya

shillingi billioni 2.11. Mapungufu haya yalichangiwa zaidi na kutokuwepo kwa usimamizi wa karibu na usaidizi duni wa kiufundi unaotolewa na Idara ya ujenzi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na usanifu duni wa miradi, kwani miradi mingi iliyobuniwa haikuwa na maelezo na michoro ya kimuundo.

Kutokana na dosari zilizobainika, Halmashauri husika zitatumia gharama ya ziada kurekebisha kasoro zilizoonekana kwenye miradi. Maelezo ya makosa yanaonyeshwa katika **Kiambatisho 11-3.**

**Napendekeza Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zichukue hatua stahiki kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Aidha, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wakati wa utekelezaji wa miradi ni muhimu ili kuhakikisha kuwa miradi inatekelezwa kwa ufanisi na kuzingatia thamani ya fedha.**

## 11.6 Kutowasilishwa na kutotekelezwa kwa Mipango ya Miradi ya CSR Sh 113 Milioni

Kifungu cha 105 (1), (2) na (4) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 inawataka wenye leseni za madini kuandaa mpango wa miradi ya kurudisha kwa jamii (CSR) na kuuwasilisha kwa mamlaka za serikali za mitaa katika eneo linalohusika. zaidi ya hayo, kifungu cha 105(4) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 inahitaji Halmashauri kusimamia utekelezaji wa mpango uliowasilishwa.

Nimepitia majalada ya Halmashauri ya Wilaya Mbinga na kubaini ukiukwaji wa taratibu katika shughuli za uchimbaji madini kama ifuatavyo:

**(i)** Kampuni nane za Madini hazikutayarisha na kuwasilisha mipango ya miradi ya jamii (CSR) kinyume na kifungu kilichotajwa hapo juu. Nina maoni kwamba shughuli za uchimbaji madini zinazofanywa na Makampuni bila kuandaa mipango inayoaminika ya CSR ni uvunjaji wa sheria na masharti yaliyoainishwa katika Sheria ya Madini, Sura ya 123. Orodha ya makampuni ya Uchimbaji madini ambayo hayajawasilisha mpango wa miradi (CSR) yao imeonyeshwa katika **Jedwali 11-4**

**Jedwali Na.11-4: Kutowasilishwa Kwa Mipango ya Miradi ya CSR**

| Na. | Jina la Kampuni | Na. ya Leseni | Aina ya madini | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jitegemee Holding Co.Ltd | PML0983RVM PML0997RVM PML1000RVM PML1087RVM | Makaa ya mawe | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |
| 2 | Umicol Ltd | ML.173/2004 | Dhahabu | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |
| 3 | Johnson K.Nchimbi | PML000004LNZ | Dhahabu | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |
| 4 | Mgaka Gold Mines Limited | ML184/2004 | Dhahabu | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |
| 5 | Market Insight Limited | ML620/2019 | Dhahabu | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |
| 6 | Mbuyula Coal | PML0521RVM PML0529RVM PML0543RVM | Dhahabu | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |
| 7 | Mathayo &Sons Enterprises Ltd | DL10/2019 | Makaa ya mawe | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |
| 8 | Rajesh William & Partners | PML0311RVM | Makaa ya mawe | Mpango wa utekelezaji wa miradi ya jamii haukuwasilishwa |

**(ii)** Pia kampuni mbili za uchimbaji madini zimeandaa mpango kazi wa miradi ya CSR na kuwasilishwa halmashauri, ukiorodhesha miradi itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21 na 2021/22, yenye thamani ya shilingi milioni 163 milioni.

**(iii)** Jukumu la halmashauri lilikuwa ni kuhakikisha miradi iliyopangwa inatekelezwa ipasavyo, hata hivyo miradi yenye thamani ya shilingi milioni 50 pekee ndiyo iliyotekelezwa na kuacha jumla ya miradi yenye thamani ya shilingi milioni 113 milioni ikiwa haijatekelezwa na makampuni hayo ya uchimbaji madini kama ilivyoainishwa kwenye mpango wao wa CSR. Orodha ya makampuni ya Madini ambayo hayajatekeleza miradi yao ya CSR imeonyeshwa katika **Jedwali 11-5.**

**Jedwali Na.11-5: Kutotekelezwa Kwa Mipango ya Miradi ya CSR**

| Na. | Mwaka wa Fedha | Mradi uliopangwa kutekelezwa | Kiasi cha mradi kilichopangwa | Kiasi kilichotekelezwa | Kiasi cha mradi kisichotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ruvuma Coal Limited | | | |
| 1. | 2021/22 | Umaliziaji wa ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Paradiso | 5,000,000 | 0 | 5,000,000 |

| Na. | Mwaka wa Fedha | Mradi uliopangwa kutekelezwa | Kiasi cha mradi kilichopangwa | Kiasi kilichotekelezwa | Kiasi cha mradi kisichotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | 2021/22 | Ukarabati na ujenzi wa madarasa mawili na nyumba mbili za walimu shule ya msingi Paradiso | 20,000,000 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| 3. | 2021/22 | Kuendeleza ujenzi wa zahanati katika kijiji cha sara | 20,000,000 | 0 | 20,000,000 |
| | | Tancoal Energy Ltd | | | |
| 4. | 2020/21 | Kuwezesha ujenzi wa madarasa mawilli na matundu sita ya vyoo shule ya msingi Ntunduwalo | 30,000,000 | 0 | 30,000,000 |
| 5. | 2020/21 | Kuwezesha utoaji wa shajala a ofisi kijijicha ntunduwalo | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 6. | 2020/21 | Kuwezesha utoaji wa huduma nyinginezo kijiji cha ntunduwalo | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 7. | 2020/21 | Kuwezesha utafiti wa upimaji wa viwanja kijiji cha ntunduwalo | 12,000,000 | 0 | 12,000,000 |
| 8. | 2020/21 | Kuwezesha utoaji wa shajala za ofisi kijiji cha Ruanda | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 9. | 2020/21 | Kuwezesha shuhuli nyingine za jamii kama itakavyohitajika kijiji cha ruanda | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 10. | 2020/21 | Ujenzi wa darasa kijiji cha Ruaanda | 20,000,000 | 0 | 20,000,000 |
| 11. | 2020/21 | Kuwezesha utoaji wa huduma za shajala kijiji cha Amani Makoro | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 12. | 2020/21 | Kuwezesha usambazaji na upandaji wa mbegu katika vijij sita vinavyouzunguka mgodi | 6,000,000 | 0 | 6,000,000 |
| **Jumla** | | | **123,000,000** | **10,000,000** | **113,000,000** |

Kutotekelezwa kwa miradi ya CSR kunazuia malengo ya serikali katika kuhakikisha kuwa, jamii inayozunguka eneo la uchimbaji madini inanufaika kutokana na uchimbaji wa madini katika maeneo yanayowazunguka.

Aidha kwa kupuuza miradi ya CSR, kampuni za uchimbaji zinasababisha hatari na madhara kwa jamnii na mazingira,pamoja na kushindwa kutoa msaada wa muhimu kwa jamii iliyoathirika

**Ninasisitiza Menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa;kufuatilia miradi yote ya CSR inayotakiwa kutekelezwa na kampuni husika, ili**

**kuhakikisha jamii inayozizunguka inapata manufaa kutokana na kuwepo kwa shughuli za uchimabji katika mazingira yao.**



# SURA YA KUMI NA MBILI

# UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA ELIMU

## 12.0 Utangulizi

Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kusimamia ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari, watu wazima na elimu isiyo rasmi Tanzania Bara kwa kuhakikisha kuwa elimu bora inatolewa. Ili kufanikisha lengo hili inatakiwa kuwa na rasilimali za kutosha kama walimu wenye uwezo, miundombinu mbalimbali kama madarasa na vifaa vya kufundishia .

Tangu mwaka 1997, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikiandaa Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP) ambayo inatokana na vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025. Dira hii imejikita kufafanua vigezo vya maendeleo ya sekta ya elimu kupitia Mipango ya Maendeleo ya Miaka Mitano, ambapo utekelezaji wa mpango wa sasa ni wa awamu ya III kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26.

Halikadhalika, sura hii imejikita katika matokeo ya ukaguzi wa utendaji na ufanisi wa Serikali za Mitaa katika usimamizi wa sekta ya elimu, ambapo nimeainisha maeneo yanayohitaji maboresho kama hapa chini:-

## 12.1 Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia Kutoa fedha kwa upungufu wa bilioni 5.8 kwa ajili ya elimu bure

Aya ya 1 na 2 za Waraka wa Ruzuku kwa Shule za Serikali kuhusu utoaji wa elimu bila malipo wenye Kumb. Na DC.297/507/01/39 (kwa shule za msingi) na Kumb. Na DC.297/507/01/40 (kwa shule za sekondari) uliotolewa tarehe 28 Desemba 2015, unataka Serikali kutoa fidia ya shilingi 10,000 na shilingi 25,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa shule za msingi na sekondari mtawalia.

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali haikutoa ruzuku ya fedha za kugharamia elimu bure shilingi bilioni 5.8 kati ya shilingi bilioni 33.07 zilizohitajika katika Mamlaka 25 za Serikali za Mitaa. Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizopokea fedha pungufu ni kama ilivyo orodheshwa katika **Kiambatisho 12-1.**

Kutolewa kwa fedha pungufu kunaathiri matokeo ya wanafunzi kitaaluma, kwani shule nyingi hazina mahitaji muhimu kama vile miundombinu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**Napendekeza Hazina na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia utoaji wa elimu bure zinatolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuimarisha utoaji wa elimu bora nchini.**

## 12.2 Upungufu wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/22 hadi 2025/26 umebainisha malengo muhimu katika elimu yanayotakiwa kufikiwa ifikapo mwaka 2026 ambayo ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kama vile ujenzi wa vyumba vya madarasa, ununuzi wa madawati na vitabu, kuboresha uwiano wa vyoo na kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu katika ngazi zote, malipo na makazi kuwa karibu na maeneo ya kazi.

Serikali imeendeleza juhudi za dhati katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari kama madarasa, nyumba za walimu, ofisi, viti na meza; hata hivyo, tathmini yangu juu ya miundombinu nilibaini kuwa shule za msingi na sekondari katika Mamlaka 45 za Serikali za Mitaa zilikuwa na upungufu katika miundombinu mbalimbali kama ilivyoanishwa katika **Jedwali Na. 12-1; Kiambatisho Na. 12-2** na **Kiambatisho 12-3**

**Jedwali Na.12-1: Uhaba Miundombinu ya Shule**

| Idara | Miundombinu/Vifaa | Mahitaji | Yaliyomo | Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| Elimu Msingi | Madawati | 596,872 | 438,806 | 158,066 |
| | Vyoo vya Wanafunzi | 100,630 | 44,100 | 56,530 |
| | Nyumba za walimu | 45,557 | 9,873 | 35,684 |
| | Viti na Meza | 63,764 | 33,935 | 29,829 |
| | Madarasa | 57,866 | 30,550 | 27,316 |
| | Ofisi za Walimu | 4,997 | 2,731 | 2,266 |
| | Vyoo vya Walimu | 1,520 | 898 | 622 |
| | Jumla | **871,206** | **560,893** | **310,313** |

| Idara | Miundombinu/Vifaa | Mahitaji | Yaliyomo | Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| Elimu Sekondari | Viti na meza-Wanafunzi | 193,422 | 161,815 | 31,607 |
| | Nyumba za walimu | 16,722 | 3,156 | 13,566 |
| | Viti na meza-Walimu | 45,190 | 33,215 | 11,975 |
| | Vyoo-Wanafunzi | 19,236 | 10,876 | 8,360 |
| | Maabara | 4,322 | 1,862 | 2,460 |
| | Mabweni | 1,397 | 411 | 986 |
| | Ofisi/Majengo ya Utawala | 1,545 | 579 | 966 |
| | Vyoo-Walimu | 2,276 | 1,384 | 892 |
| | Madarasa | 7,132 | 6,349 | 783 |
| | Maktaba | 464 | 74 | 390 |
| | Vyumba vya Chakula | 292 | 48 | 244 |
| | Vyumba vya kompyuta | 163 | 32 | 131 |
| | Jiko | 172 | 61 | 111 |
| | **Jumla** | **292,333** | **219,862** | **72,471** |

***Chanzo**: Ripoti za Elimu ya Shule za Msingi na Sekondari*

Ufaulu wa kitaaluma unategemea mazingira mazuri ya kujifunzia, hivyo juhudi za muhimu zinahitajika kushughulikia uhaba wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari.

Vilevile, uhaba wa vyumba vya madarasa huwalazimu wanafunzi kusomea katika madarasa yenye msongamano wa wanafunzi, jambo ambalo linadumaza uwezo wao wa kujifunza na walimu wa kufundisha kwa ufanisi, hivyo, kuingilia kati mara moja katika kushughulikia uhaba huu wa miundombinu ya shule ni jambo lisiloepukika.

**Ninashauri Hazina kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kutoa fedha kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na kuendelea kuboresha miundombinu ili kuondoa au kupunguza upungufu huu wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa elimu bora.**

## 12.3 Upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari

Mpango wa III wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/22 hadi 2025/26 unaeleza kuwa, uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi katika shule za msingi unatakiwa kuwa 1:50 (Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 50) na kwa shule za sekondari ni 1:20 (Mwalimu mmoja kwa wanafunzi 20) hadi kufikia mwisho wa mwaka wa 2026.

Tathmini niliofanya katika uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi katika Halmashauri 23 ilibainisha kuwa, kati ya walimu 28,677 wanaohitajika kwa shule za msingi na sekondari, kulikuwa na walimu 18,606 tu, ikimaanisha upungufu wa walimu 10,071 sawa na asilimia 35 kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 12-2.**

Jedwali Na.12-2: Upungufu wa walimu shule za msingi na sekondari

| Na. | Halmashauri | Walimu/Walimu Wa somo | Mahitaji | Waliopo | Pungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| **Shule za Msingi** | | | | | |
| 1. | H/W Bahi | Walimu | 2241 | 768 | 1473 |
| 2. | H/W Singida | Walimu | 1,785 | 872 | 913 |
| 3. | H/W Rombo | Walimu | 1814 | 1085 | 729 |
| 4. | H/Jiji Dodoma | Walimu | 1966 | 1270 | 696 |
| 5. | H/W Babati | Walimu | 2008 | 1318 | 690 |
| 6. | H/W Gairo | Walimu | 1154 | 657 | 497 |
| 7. | H/W Chalinze | Walimu | 1,495 | 1002 | 493 |
| 8. | H/W Longido | Walimu | 910 | 440 | 470 |
| 9. | H/W Kibiti | Walimu | 940 | 606 | 334 |
| 10. | H/W Kibondo | Walimu | 1133 | 842 | 291 |
| 11. | H/W Siha | Walimu | 602 | 384 | 218 |
| 12. | H/W Makete | Walimu | 850 | 654 | 196 |
| 13. | H/W Mafia | Walimu | 383 | 250 | 133 |
| 14. | H/W Meru | Walimu | 1034 | 926 | 108 |
| 15. | H/W Bagamoyo | Walimu | 714 | 682 | 32 |
| Jumla ndogo-Shule za Msingi | | | **19029** | **11756** | **7273** |
| **Shule za Sekondari** | | | | | |
| 1. | H/W Babati | Walimu wa masomo ya sanaa | **570** | **520** | **50** |
| | | Walimu wa sayansi | **292** | **256** | **36** |
| 2. | H/W Bagamoyo | Walimu wa sayansi | **145** | **117** | **28** |
| 3. | H/W Chalinze | Walimu wa masomo ya sanaa | **306** | **313** | **-7** |
| | | Walimu wa sayansi | **280** | **152** | **128** |
| 4. | H/Jiji Dodoma | Walimu | **592** | **411** | **181** |
| 5. | H/W Gairo | Walimu | **262** | **261** | **1** |
| 6. | H/W Hanang | Walimu wa sayansi | **222** | **170** | **52** |
| 7. | H/W Ikungi | Walimu | **1986** | **1046** | **940** |
| 8. | H/W Karatu | Walimu wa maabara | **96** | **62** | **34** |
| | | Walimu wa sayansi | **267** | **177** | **90** |
| 9. | H/Mji Kibaha | Walimu wa masomo ya sanaa | **671** | **661** | **10** |
| | | Walimu wa sayansi | **302** | **218** | **84** |
| 10. | H/W Kibiti | Walimu wa masomo ya sanaa | **200** | **177** | **23** |
| | | Walimu wa sayansi | **150** | **92** | **58** |
| 11. | H/W Kibondo | Walimu | **429** | **284** | **145** |
| 12. | H/W Kiteto | Walimu wa sayansi | **178** | **103** | **75** |
| 13. | H/W Mafia | Walimu wa masomo ya sanaa | **88** | **63** | **25** |
| | | Walimu wa sayansi | **80** | **37** | **43** |
| 14. | H/W Mbogwe | Walimu wa sayansi | **180** | **102** | **78** |
| 15. | H/W Meru | Walimu wa maabara | **137** | **92** | **45** |
| | | Walimu wa sayansi | **508** | **313** | **195** |
| 16. | H/W Monduli | Walimu wa masomo ya sayansi | **211** | **135** | **76** |
| 17. | H/W Morogor | Walimu wa sayansi | **457** | **352** | **105** |
| 18. | H/W Rombo | Walimu wa masomo ya sanaa | **556** | **549** | **7** |
| | | Walimu wa sayansi | **418** | **214** | **204** |
| 19. | H/W Siha | Walimu wa masomo ya sanaa | **198** | **171** | **27** |
| | | Walimu wa sayansi | **173** | **115** | **58** |
| **Jumla Ndogo- Shule za Sekondari** | | | **9,648** | **6,850** | **2,798** |
| **Jumla Kuu** | | | **28,677** | **18,606** | **10,071** |

Upungufu wa walimu katika shule za Msingi na Sekondari unatokana na Serikali kutoajiri idadi ya kutosha ya walimu , na pia kutokuvutia walimu kwa kutoa mazingira bora ya kufundishia na maslahi ya kuvutia.

Kwa maoni yangu, upungufu wa walimu uliobainika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 23 unaathiri kwa kiasi kikubwa ufaulu wa wanafunzi katika shule za umma.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Utumishi kutenga idadi ya kutosha ya walimu kwa shule zilizoathirika zaidi. Aidha, Serikali inashauriwa kuweka juhudi katika kuboresha mazingira ya kufundishia kwa kujenga nyumba za kutosha za watumishi, madarasa na kusambaza vifaa vya kufundishia. Zaidi ya hayo, Serikali inapaswa kuendeleza jitihada zake za kuongeza maslahi ya walimu, kulipa madeni na kutoa motisha kwa walimu.**

## 12.4 Idadi Kubwa ya Wanafunzi Wanaokatisha Masomo Kabla ya Kuhitimu Darasa la VII na Kidato Cha IV

Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/22 hadi 2025/26 unaeleza lengo la uandikishaji kwa ngazi ya elimu ya msingi kuwa asilimia 100 na kwa elimu ya sekondari (Kidato cha I-IV) umepangwa kuwa asilimia 48. Uwekezaji unaoendelea wa Serikali katika sekta ya elimu, umesaidia kuongeza uandikishaji wa wanafunzi kwa ajili ya elimu ya msingi kulichangiwa zaidi na kutolewa kwa elimu bila malipo kutoka msingi hadi kidato cha nne.

Katika Halmashauri 11, nilibaini kuwa; kati ya 2015 na 2021; Wanafunzi 19,945 (25%) kati ya 78,786 waliosajiliwa mwaka 2015 hawakuhitimu darasa la saba.kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 12-3** hapa chini.

**Jedwali Na.12-3: Wanafunzi Waliokatisha Masomo Shule za Msingi**

| Na. | Halmashauri | Walioandikishwa 2015 | Waliomaliza 2021 | Idadi ya walioacha Shule |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Gairo | 5,568 | 4,203 | 1,365 |
| 2. | H/W Kwimba | 18,119 | 9,074 | 9,045 |
| 3. | H/W Uvinza | 8,731 | 6,559 | 2,172 |
| 4. | H/W Kilosa | 13,395 | 11,299 | 2,096 |
| 5. | H/W Nsimbo | 4,770 | 3,225 | 1,545 |
| 6. | H/W Kibondo | 7,910 | 6,494 | 1,416 |
| 7. | H/W Kibaha | 3,015 | 2,209 | 806 |
| 8. | H/W Morogoro | 8,083 | 7,442 | 641 |

| Na. | Halmashauri | Walioandikishwa 2015 | Waliomaliza 2021 | Idadi ya walioacha Shule |
|---|---|---|---|---|
| 9. | H/W Mwanga | 3,521 | 3,061 | 460 |
| 10. | H/W Newala | 3,117 | 2,772 | 345 |
| 11. | H/W Makete | 2,557 | 2,503 | 54 |
| **Jumla** | | **78,786** | **58,841** | **19,945** |

***Chanzo:*** Taarifa za Elimu ya Shule za Msingi

Pia, nilibaini katika Mamlaka 19 za Serikali za Mitaa; Wanafunzi 22,039 sawa na asilimia 28 kati ya 82,236 waliojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2018 hawakufanikiwa kufanya mtihani na kupata cheti cha kuhitimu kidato cha IV kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali 12-4** hapa chini;-

**Jedwali Na.12-4: Wanafunzi waliokatisha masomo shule za sekondari**

| Na. | Halmashauri | Walioandikishwa 2018 | Waliomaliza 2021 | Idadi ya walioacha Shule |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Kinondoni | 10,005 | 5,353 | 4,652 |
| 2. | H/Mji Newala | 6950 | 3167 | 3,783 |
| 3. | H/W Misungwi | 5690 | 3120 | 2,570 |
| 4. | H/W Morogoro | 4171 | 2223 | 1,948 |
| 5. | H/W Moshi | 8698 | 7428 | 1,270 |
| 6. | H/W Kilosa | 5002 | 3756 | 1,246 |
| 7. | H/M Temeke | 12,774 | 11,589 | 1,185 |
| 8. | H/W Buhigwe | 2964 | 2056 | 908 |
| 9. | H/W Gairo | 2159 | 1459 | 700 |
| 10. | H/M Mpanda | 2,188 | 1,497 | 691 |
| 11. | H/W Tandahimba | 2507 | 1822 | 685 |
| 12. | H/W Kalambo | 1917 | 1248 | 669 |
| 13. | H/W Mwanga | 3884 | 3348 | 536 |
| 14. | H/W Busokelo | 1713 | 1245 | 468 |
| 15. | H/W Newala | 3816 | 3363 | 453 |
| 16. | H/M Kigamboni | 2829 | 2403 | 426 |
| 17. | H/Mji Masasi | 1210 | 818 | 392 |
| 18. | H/W Makete | 1587 | 1205 | 382 |
| 19. | H/W Monduli | 2172 | 2127 | 45 |
| **Jumla** | | **82,236** | **59,227** | **23,009** |

Sababu za kukatisha masomo zilikuwa ni pamoja na ujauzito kwa wanafunzi wa kike, umbali mrefu kutoka makazi ya wanafunzi hadi shuleni, malezi ya familia na sababu binafsi.

**Napendekeza kwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa iandae programu za kuzifikia jamii husika, kuhimiza wazazi au/na walezi kuwaandikisha wanafunzi katika shule zilizo karibu, kujenga shule mpya karibu na vijiji, kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujumuisha vifaa vinavyofaa vya kufundishia na kujifunza, kuhimiza michezo na pamoja na kutoa elimu ya taaluma na ufundi stadi.**

## 12.5 Ufaulu Mdogo kwa Wanafunzi wa Sekondari Katika Shule Za Umma

Tathmini yangu kuhusu matokeo ya mitihani ya elimu ya sekondari katika shule za umma nilibaini kuwa; Kati ya wanafunzi 238,141 waliofanya mitihani ya taifa ya kidato cha nne mwaka wa masomo 2021 katika Mamlaka 96 za Serikali za Mitaa, wanafunzi 29,091 (12%) walifeli kwa kupata daraja sifuri na wanafunzi 129,094 (54%) walipata daraja la nne, hivyo kufanya wanafunzi 158,185 sawa na asilimia 66 ya waliofanya mtihani walipata daraja la nne na sifuri.

Hali hii inamaanisha kwamba mazingira magumu ya kujifunzia katika shule za umma ambayo ni magumu kumuwezesha mwanafunzi na mwalimu kufikia matokeo mazuri ya kiwango cha juu. Hali hii nikiielezea mara kwa mara katika ripoti zangu za miaka ya iliyopita. Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye idadi kubwa ya wanafunzi waliofeli zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na 12-4**;

Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi waliofeli katika shule za Sekondari kunaathiri lengo la Serikali kupitia elimu bure la kuhakikisha kila mtoto anapata elimu bora.

**Ninapendekeza kwa Serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuboresha mazingira ya kusomea katika shule za sekondari za umma ili kuondoa au kupunguza idadi ya wanafunzi wanaofeli.**

**Pia, ninashauri Serikali kuboresha hali ya kazi kwa walimu kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kuhakikisha madai ya walimu yanalipwa kwa wakati. Aidha, Ofisi ya Rais-Utumishi inashauriwa kuhakikisha shule za umma zina walimu wa kutosha, wenye sifa na uwezo.**



# SURA YA KUMI NA TATU

# UFANISI WA UTENDAJI KATIKA SEKTA YA AFYA

## 13.0 Utangulizi

Sekta ya Afya ni muhimu katika ustawi wa watu, uimarishaji wa nguvu kazi na ukuzaji wa maendeleo ya taifa letu. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuboresha utoaji wa huduma za afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vipya vya afya, ukarabati wa vituo vilivyopo, utoaji wa vifaa tiba na upatikanaji wa dawa muhimu.

Katika tathmini kuhusu mwenendo wa utoaji huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; nilibaini kuwa, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya, sekta ya afya bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo upungufu wa wataalamu, ufinyu wa bajeti, mazingira duni ya kazi, upungufu wa miundombinu na uhaba wa dawa na vifaa tiba.

Sura hii inaelezea juu ya changamoto zilizoonekana katika sekta ya afya, na inabainisha maeneo muhimu ambayo yanahitaji kusimamiwa kwa umakini na kupendekeza hatua zinazopaswa kuchukuliwa na Serikali na wadau wengine ili kutatua changamoto nilizobaini;

## 13.1 Kuchelewa Kukamilika na Kutoanza kwa Ujenzi wa Vituo vya Afya

Mamlaka za Serikali za Mitaa 91 zilipokea jumla ya shilingi bilioni 82.59 kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati.

Hata hivyo, tathmini yangu kwenye utekelezaji wa mikataba, kupitia taarifa za utekelezaji na kutembelea maeneo ya ujenzi, ilionyesha ucheleweshaji katika ukamilishaji wa kazi za ujenzi wa vituo husika kwa kipindi kinachoanzia miezi mitatu hadi miaka mitatu. Mamlaka za

Serikali za Mitaa zilizochelewa kukamilisha miradi ni kama zilivyo orodheshwa katika **Jedwali Na. 13-1** na kuelezwa kwa kina zaidi katika **Kiambatisho 13-1.**

**Jedwali Na.13-1: Halmashauri zenye Miradi iliyochelewa kukamilika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | 4,215,527,364 | 47. | H/W Meatu | 1,300,000,000 |
| 2. | H/W Arusha | 109,131,278 | 48. | H/W Meru | 370,000,000 |
| 3. | H/Mji Babati | 1,000,000,000 | 49. | H/W Misenyi | 1,600,000,000 |
| 4. | H/W Babati | 1,350,000,000 | 50. | H/W Misungwi | 550,000,000 |
| 5. | H/W Bariadi | 1,900,000,000 | 51. | H/W Mkalama | 1,184,010,800 |
| 6. | H/W Birahamulo | 800,000,000 | 52. | H/W Mkinga | 2,405,000,000 |
| 7. | H/M Bukoba | 560,000,000 | 53. | H/W Mlele | 550,000,000 |
| 8. | H/W Bukoba | 1,200,000,000 | 54. | H/W Mlimba | 150,000,000 |
| 9. | H/W Bukombe | 300,000,000 | 55. | H/W Momba | 1,150,000,000 |
| 10. | H/Mji Bunda | 500,000,000 | 56. | H/M Morogoro | 500,000,000 |
| 11. | H/Jiji Dodoma | 707,996,246 | 57. | H/W Moshi | 1,290,000,000 |
| 12. | H/Mji Geita | 500,000,000 | 58. | H/M Mpanda | 1,305,000,000 |
| 13. | H/W Geita | 1,100,000,000 | 59. | H/W Mpanda | 1,200,000,000 |
| 14. | H/W Handeni | 300,000,000 | 60. | H/W Mpimbwe | 2,020,000,000 |
| 15. | H/Mji Ifakara | 565,000,000 | 61. | H/W Msalala | 590,000,000 |
| 16. | H/W Ikungi | 200,000,000 | 62. | H/W Mtwara | 1,450,000,000 |
| 17. | H/W Ileje | 1,000,000,000 | 63. | H/W Muleba | 1,500,000,000 |
| 18. | H/W Iramba | 2,400,000,000 | 64. | H/M Musoma | 500,000,000 |
| 19. | H/W Itigi | 750,000,000 | 65. | H/W Mwanga | 145,000,000 |
| 20. | H/W Itilima | 1,200,000,000 | 66. | H/Jiji Mwanza | 600,000,000 |
| 21. | H/W Kalambo | 1,190,000,000 | 67. | H/W Nachingwea | 650,000,000 |
| 22. | H/W Karagwe | 950,000,000 | 68. | H/Mji Nanyamba | 1,050,000,000 |
| 23. | H/W Karatu | 500,000,000 | 69. | H/W Ngara | 566,500,000 |
| 24. | H/Mji Kasulu | 700,000,000 | 70. | H/W Ngorongoro | 1,300,000,000 |
| 25. | H/W Kasulu | 2,300,000,000 | 71. | H/W Nkasi | 500,000,000 |
| 26. | H/Mji Kibaha | 1,850,000,000 | 72. | H/W Nsimbo | 500,000,000 |
| 27. | H/W Kibaha | 850,000,000 | 73. | H/W Nyang'hwale | 100,000,000 |
| 28. | H/W Kigoma | 750,000,000 | 74. | H/Mji Nzega | 257,816,318 |
| 29. | H/M Kigoma Ujiji | 550,000,000 | 75. | H/W nzega | 660,000,000 |
| 30. | H/W Kilolo | 750,000,000 | 76. | H/W Pangani | 150,000,000 |
| 31. | H/W Kiteto | 1,200,000,000 | 77. | H/W Rorya | 481,749,000 |
| 32. | H/Mji Kondoa | 200,000,000 | 78. | H/W Rufiji | 390,000,000 |
| 33. | H/W Korogwe | 600,000,000 | 79. | H/W Rungwe | 1,756,913,000 |
| 34. | H/W Lushoto | 1,987,848,342 | 80. | H/W Sengerema | 350,000,000 |
| 35. | H/W Mafia | 1,450,000,000 | 81. | H/M Shinyanga | 250,000,000 |
| 36. | H/W Manyoni | 280,000,000 | 82. | H/W Shinyanga | 569,452,927 |
| 37. | H/Mji Masasi | 1,550,000,000 | 83. | H/W Singida | 250,000,000 |
| 38. | H/W Masasi | 500,000,000 | 84. | H/W Songea | 500,000,000 |
| 39. | H/W Maswa | 300,000,000 | 85. | H/W Songwe | 1,200,000,000 |
| 40. | H/W Mbarali | 1,300,000,000 | 86. | H/M Sumbawanga | 500,000,000 |
| 41. | H/Jiji Mbeya | 2,083,967,846 | 87. | H/W Tarime | 1,000,000,000 |
| 42. | H/W Mbeya | 1,150,000,000 | 88. | H/W Ukerewe | 640,000,000 |
| 43. | H/W Mbogwe | 870,757,000 | 89. | H/W Ulanga | 400,000,000 |
| 44. | H/W Mbozi | 1,300,000,000 | 90. | H/W Ushetu | 1,300,000,000 |
| 45. | H/Mji Mbulu | 500,000,000 | 91. | H/W Uvinza | 900,000,000 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 46. | H/W Mbulu | 50,000,000 | **Jumla** | | **82,951,670,132** |

Pia nilibaini kuwa, Halmashauri saba zilipokea shilingi bilioni 2.64 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya. Hata hivyo, ikiwa ni zaidi ya miezi sita kupita tangu Mamlaka hizo kupokea fedha, bali ujenzi wa vituo husika haukuwa umeanza. Orodha ya Mamlaka za Serikali za mitaa zenye miradi iliyochelewa kukamilika na ambayo haikuwa imeanza ujenzi imeoneshwa katika **Jedwali 13-2**

**Jedwali Na.13-2: Halmashauri ambazo hazikuwa zimeanza utekelezaji wa miradi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es salaam | 860,000,000 |
| 2. | H/W Geita | 200,000,000 |
| 3. | H/W Ileje | 905,005,895 |
| 4. | H/W Magu | 271,096,565 |
| 5. | H/W Malinyi | 150,000,000 |
| 6. | H/W Msalala | 100,000,000 |
| 7. | H/W Mtwara | 150,000,000 |
| **Jumla** | | **2,636,102,460** |

Sababu zilizopelekea kutokamilika kwa miradi hiyo ni ucheleweshaji wa fedha za miradi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, mchakato wa ununuzi kutumia muda mrefu kabla ya kuanza ujenzi, ucheleweshaji katika usambazaji wa vifaa vya ujenzi kutoka kwa wazabuni, ukosefu wa wataalamu, upungufu wa fedha zinazotengwa, athari za hali mbaya ya hewa na kuchelewa kuhamishwa kwa fedha kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda ngazi za chini ambapo miradi inatekelezwa.

Pia, katika baadhi ya miradi nilibaini muda uliotengwa kwa ajili ya ujenzi haukuzingatia ukubwa wa kazi kwani hapakutofautishwamuda mahususi kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi na muda wa matazamio ya uimara wa zege kabla ya kuendelea na hatua zingine za ujenzi.

Kwa maoni yangu, kuna hatari kubwa kwa Serikali kutofikia lengo la kuanzisha na kuboresha vituo vya afya wilayani kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025.

**Ninashauri Serikali kushughulikia kasoro zilizojitokeza ili kuhakikisha kuwa miradi husika inakamilika ndani mwafaka ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Pia, Wizara ya Fedha na**

**Mipango inapaswa kutoa fedha zilizopangwa kwa wakati. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae mipango kazi na orodha ya vifaa vya ujenzi kwa kuzingatia uhalisia wakati wa utekelezaji wa ujenzi. Mpango wa kazi ulioandaliwa unapaswa kuzingatia muda unaohitajika katika kuandaa michoro, maandalizi ya awali, ununuzi wa vifaa vya ujenzi, ujenzi na muda wa matazamio juu ya uimara wa zege.**

## 13.2 Miradi ya Afya Iliyokamilika ambayo Haitumiki yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 4.93

Wakati wa ukaguzi nilibaini miradi ya ujenzi wa vituo vya afya iliyokamilika yenye thamani ya shilingi bilioni 4.93 katika Mamlaka 16 za Serikali za Mitaa lakini haikuanza kutumika. Miradi iliyokamilika lakini haitumiki inajumuisha majengo ya upasuaji, vyumba vya kuhifadhia maiti, wodi, zahanati na vituo vya afya. Miradi hiyo haitumiki kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa tiba vinavyohitajika, ukosefu wa wafanyakazi na miundombinu mingine.

Kutotumika kwa miradi iliyokamilika, kunapunguza thamani ya miradi hiyo kutokana na uchakavu utakao dhihirika. Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye majengo yaliyokamilika lakini hayatumiki ni kama ilivyoorodheshwa katika **Jedwali Na. 13-3**.

**Jedwali Na.13-3: Miradi iliyokamilika ambayo haitumiki**

| Na. | Halmashauri | Mradi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Arusha | Zahanati ya Kivululu | 50,000,000 |
| | | Kituo cha Afya Olorien | 450,000,000 |
| 2. | H/W Buchosa | Kituo cha Afya Irenza | 50,000,000 |
| | | zahanati ya Ilyamchele | 40,000,000 |
| | | Zahanati ya Kamisa | 40,000,000 |
| | | Zahanati ya Katwe | 40,000,000 |
| 3. | H/W Chamwino | Zahanati ya Nhihni | 35,000,000 |
| 4. | H/W Chemba | Jengo la wagonjwa wa nje, maabara na kichomea taka zahanati ya Farkwa | 250,000,000 |
| 5. | H/Mji Handeni | Kituo cha Afya Malezi | 500,000,000 |
| 6. | H/Mji Kasulu | maabara na jengo la wagonjwa wa nje kituo cha Afya Nyansha, ujenzi wa zahanat ya Msambara Zahanati ya KumnyikA, wodi ya wazazi zahanati ya Kigondo | 400,000,000 |
| 7. | H/W Kalambo | Zahanati ya Msipazi | 174,209,079 |
| 8. | H/W Kaliua | Kituo cha Afya Mwongozo | 349,872,600 |

| Na. | Halmashauri | Mradi | Kiasi (Sh.) |
| --- | --- | --- | --- |
| | | Chumba cha Upasuaji na chumba cha maiti Kitup cha Afya Usinge | 174,761,109 |
| 9. | H/W Kondoa | Zahanati ya Kijiji cha Potea | 50,000,000 |
| 10. | H/W Kwimba | Kituo cha Afya Kadashi | 500,000,000 |
| | | Jengo la wagonjwa wa nje Kituo cha Afya Isunga | 250,000,000 |
| 11. | H/Jiji Mwanza | Chumba cha upasuaji Kituo cha Afya Bulale | 124,732,100 |
| | | Jengo la Kufulia Kituo cha Afya Bulale | 26,925,100 |
| | | Jengo la mionzi Kituo cha Afya Bulale | 49,663,400 |
| 12. | H/W Same | Chumba cha upasuaji, wodi ya wazazi na chumba cha maiti Kituo cha Afya Hedaru | 324,652,156 |
| 13. | H/W Songea | Wodi ya Watoto, wanaume na wanawake Hospitali ya Mpitimbi | 500,000,000 |
| 14. | H/M Ubungo | Maabara na jingo la wagonjwa wan je Kituo cha Afya Goba | 250,000,000 |
| 15. | H/W Urambo | Jengo la wagonjwa wan je, maabara na kichomea taka Kituo cha Afya Vumilia | 250,000,000 |
| 16. | H/W Newala | Zahanati ya Chilangala | 50,000,000 |
| **Jumla** | | | **4,929,815,544** |

**Ninapendekeza kwa Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kuchukua hatua stahiki ili kuhakikisha miradi yote iliyokamilika inatumika, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kupata thamani ya fedha iliyotumika katika ujenzi wa miradi hiyo.**

## 13.3 Hasara Iliyotokana na Dawa ambazo Muda wa Matumizi yake ulikwisha Shilingi Milioni 976.58

Aya ya 4.11 na 4.14 za Randama ya Maelewano kati ya Bohari ya Dawa (MSD) na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zinataka Bohari ya Dawa kupanga uteketezaji dawa na bidhaa za afya zilizokwisha muda wa matumizi yake, zilizoharibika au zisizotumika na kuitaarifu Wizara ya Afya juu ya kuwepo kwa dawa na bidhaa za afya ambazo muda wa matumizi yake ulikwisha zaidi ya miezi kumi.

Wakati wa kukagua rejista za dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati katika Mamlaka 16 za Serikali za Mitaa, nilibaini kuwapo kwa dawa na bidhaa za afya zenye thamani ya shilingi milioni 976.58 ambazo muda wake wa matumizi umekwisha kwa kipindi cha kuanzia miezi mitatu hadi miaka 10 ambazo hazikuwa zimeteketezwa. Kuwapo kwa dawa zilizokwisha muda wa matumizi kunasababishwa na kununua au kupokea dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa zenye muda mfupi wa

matumizi na kukosekana kwa mfumo wa upokeaji na utoaji wa dawa unaohakikisha dawa zilizopokelewa kwanza ndizo hutumika kwanza. Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye dawa zilizokwisha muda wa matumizi ni kama zilivyo orodheshwa kwenye **Jedwali 13-4**.

**Jedwali Na.13-4: Halmashauri zenye madawa yaliyoisha muda wa matumizi**

| Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Bahi | 38,445,131 | 9. | H/W Kwimba | 77,567,630 |
| 2. | H/W Bariadi | 25,476,966 | 10. | H/W Lushoto | 95,850,536 |
| 3. | H/W Busega | 31,164,826 | 11. | H/Mj Mafinga | 94,718,208 |
| 4. | H/W Gairo | 111,087,858 | 12. | H/W Maswa | 297,029,713 |
| 5. | H/W Igunga | 2,812,880 | 13. | H/W Meatu | 14,363,828 |
| 6. | H/W Itigi | 23,152,419 | 14. | H/W Morogoro | 17,682,823 |
| 7. | H/W Kilolo | 37,487,678 | 15. | H/W Mpanda | 45,721,964 |
| 8. | H/W Kilosa | 21,878,823 | 16. | H/W Sengerema | 42,138,414 |
| **Jumla** | | | | | **976,579,697** |

Kuendelea kutunza dawa zilizokwisha muda wa matumizi bila kuziteketeza kunaweza sababisha madhara kwa umma, mara zitakapotumiwa na jamii au zikawa mikononi mwa watu wasiokuwa na maadili.

**Ninatoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye dawa zilizokwisha muda wa matumizi yake,zinapaswa kuteketezwa kwa mujibu wa sheria, aidhaa kuhakikisha kiwango cha juu cha uagizaji wa dawa kinazingatiwa.**

## 13.4 Hasara itokanayo kwa kukataliwa kurejeshewa madai kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Shilingi Bilioni 1.77

Tathmini yangu kuhusu madai ya kurejeshewa gharama za matibabu yaliyotolewa kwa wanufaika wa Mfuko wa Bima wa Taifa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nilibaini kuwa, vituo hivyo katika Mamlaka 66 za Serikali za Mitaa viliwasilisha madai yenye thamani ya shilingi bilioni 9.25 kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ikiwa ni gharama za kuhudumia wagonjwa wanaostahiki kupata huduma za afya kwa kutumia bima. Hata hivyo, ni madai ya shilingi bilioni 7.48 pekee yaliyolipwa huku madai ya shilingi bilioni 1.77 yalikataliwa Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo madai yalikataliwa ni kama ilivyoorodheshwa katika **Kiambatisho Na. 13-2**

Kukataliwa kwa madai yaliyowasilishwa kulichangiwa na kutofuata taratibu zinazohitajika katika ujazaji wa fomu za bima na makosa kama vile idhini batili, kutozingatia vifungu vya utambuzi wa magonjwa, kutofuata miongozo ya kawaida ya matibabu, kutoonyesha vipimo vya utambuzi na kujumuishwa kwa huduma ambazo hazikuwa kwenye mwongozo wa matibabu uliotelewa na Mfuko wa Bima wa Taifa.

Madai yaliyokataliwa na Mfuko wa Afya wa Bima yanaathiri ufanisi wa vituo vya kutolea huduma za afya kwa jamii na hivyo kusababisha uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba pamoja na gharama nyingine za uendeshaji wa vituo husika.

**Ninapendekeza kwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI kubuni na kuandaa mafunzo maalumu ya kuwajengea uwezo watumishi wa afya kuhusu ujazaji sahihi wa fomu za madai ya gharama za matibabu kwa njia ya bima ili kuzuia tatizo kujirudia**

## 13.5 Dawa na vifaa tiba vilivyolipiwa ambavyo havijapokelewa kutoka MSD vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.16

Tathmini yangu kuhusu upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na usambazaji wa dawa na vifaa tiba wa Bohari ya Dawa, nilibaini kuwa Bohari ya Dawa haikusambaza dawa na vifaa tiba kama vilivyoagizwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa licha ya Mamlaka hizo kuwa na kiasi kikubwa cha salio la fedha katika akaunti zao zilizopo Bohari ya Dawa.

Sampili katika Mamlaka 10 za Serikali za Mitaa, nilibaini kuwa vituo vya afya viliagiza dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 13.16 kutoka Bohari ya Dawa, lakini ni dawa na vifaa tiba vya thamani ya shilingi bilioni 5.01 (38%) pekee vilipokelewa, na dawa za shilingi bilioni 8.16 haziku pokelewa. Sababu ya kutowasilishwa bidhaa hizo kutoka Bohari ya Dawa ilikuwa ni ukosefu wa bidhaa hizo katika Bohari ya Dawa

Kutopeleka dawa na vifaa tiba vilivyoagizwa katika Halmashauri, kunaathiri uwezo wa vituo vya afya katika utoaji wa huduma bora za afya kwa jamii inayokusudiwa. Mamlaka za Mitaa zilizokosa dawa na vifaa tiba zimeoneshwa kwenye **Jedwali 13-5.**

**Jedwali Na.13-5: Dawa na vifaa tiba vilivyolipiwa ambavyo havijapokelewa**

| Na. | Halmashauri | Bidhaa zilizoagizwa (Sh.) | Bidhaa zilizopokelewa (Sh.) | Bidhaa zisizopokelewa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Buchosa | 500,000,000 | 204,239,600 | 295,760,400 |
| 2. | H/Jiji Dar es Salaam | 6,034,160,979 | 3,082,115,584 | 2,952,045,395 |
| 3. | H/W Ikungi | 300,000,000 | 128,312,694 | 171,687,306. |
| 4. | H/Mji Mbulu | 34,859,152 | 17,429,576 | 17,429,576 |
| 5. | H/W Mlimba | 376,599,999 | 116,550,153 | 260,049,846 |
| 6. | H/W Nyang'hwale | 890,800,266 | 255,539,851 | 635,260,415 |
| 7. | H/W Sengerema | 68,247,861 | 0 | 68,247,861 |
| 8. | H/M Sumbawanga | 421,092,986 | 93,446,756 | 327,646,230 |
| 9. | H/Jiji Tanga | 43,705,174 | 25,686,481 | 18,018,693 |
| 10. | H/M Temeke | 4,491,927,734 | 1,081,911,565 | 3,410,016,169 |
| **Jumla** | | **13,161,394,151** | **5,005,232,260** | **8,156,161,891** |

Aidha, mapitio yangu katika akaunti za Mamlaka 18 za Serikali za Mitaa zilizopo Bohari ya Dawa, nilibaini kuwa vituo hivyo vilikuwa na salio la shilingi bilioni 16.39 kwa ajili ya ununuzi wa dawa; hata hivyo, Bohari ya Dawa ilipeleka dawa za shilingi bilioni 5.84 pekee na shilingi bilioni 10.54 ziliendelea kusalia katika Bohari ya Dawa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye bakaa kubwa katika bohari ya Dawa ni kama zilivyo orodheshwa kwenye **Jedwali 13-6** hapa chini;-

**Jedwali Na.13-6: Bakaa ya Fedha za Dawa na Vifaa Tiba Katika Bohari ya Dawa**

| Na. | Halmashauri | Kiasi Kilichokuwepo (Sh.) | Kiasi Kilichotumika (Sh.) | Kiasi Kilichobaki (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Bariadi | 345,537,819 | - | 345,537,819 |
| 2. | H/W Chemba | 908,264,394 | 328,598,932 | 579,665,462 |
| 3. | H/Jiji Dodoma | 401,296,700 | 189,271,825 | 212,024,875 |
| 4. | H/Mji Geita | 582,944,283 | 264,901,847 | 318,042,436 |
| 5. | H/W Kilosa | 1,323,742,825 | 625,185,197 | 698,557,628 |
| 6. | H/W Kondoa | 594,391,209 | 298,328,327 | 296,062,882 |
| 7. | H/Mji Kondoa | 392,830,036 | 283,767,334 | 109,062,702 |
| 8. | H/W Longido | 480,583,932 | 208,215,322 | 272,368,610 |
| 9. | H/W Madaba | 88,985,946 | 22,237,083 | 66,748,863 |
| 10. | H/W Maswa | 658,652,000 | - | 658,652,000 |
| 11. | H/W Mbogwe | 385,010,304 | - | 385,010,304 |
| 12. | H/W Meatu | 645,807,643 | - | 645,807,643 |
| 13. | H/W Morogoro | 444,784,900 | 203,264,264 | 241,520,636 |
| 14. | H/W Mufindi | 646,670,651 | - | 646,670,651 |
| 15. | H/W Ruangwa | 62,238,217 | - | 62,238,217 |
| 16. | H/W Songea | 175,262,929 | - | 175,262,929 |
| 17. | H/M Temeke | 4,605,207,422 | 2,441,317,908 | 2,163,889,513 |
| 18. | H/M Ubungo | 3,644,760,961 | 978,272,174 | 2,666,488,786 |
| **Jumla** | | **16,386,972,171** | **5,843,360,213** | **10,543,611,956** |

**Ninashauri Serikali kuiongezea uwezo wa usambazaji Bohari ya Dawa (MSD) ili kuhakikisha kuwa dawa na vifaa tiba vilivyoagizwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa vinafikishwa kwa wakati ili kuboresha utoaji wa huduma za afya endelevu.**

**Pia, ninapendekeza Bohari ya Dawa kutoa uthibitisho wa kukosekana kwa dawa kwa wakati ili Mamlaka za Serikali za Mitaa kutafuta njia mbadala za ununuzi wa dawa na vifaa ili kupunguza upungufu wa dawa na vifaa tiba. Pia idadi ya washitiri na wasambazaji iongezwe ili kukidhi mahitaji ya dawa na vifaa tiba kwa muda mwafaka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.**

## 13.6 Fedha Kwa Ajili ya Ununuzi wa Dawa na Vifaa Tiba Zilizobadilishwa Matumizi Shilingi Milioni 455.72

Aya ya 3.2(i) ya Maelekezo ya Usimamizi wa Matumizi ya Fedha zinazotokana na Uchangiaji wa Gharama za Matibabu uliotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa mwaka 2017 inaeleza kuwa 50% ya mapato ya ada zilikusanywa kama gharama za uchangiaji wa matibabu zitatengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba katika vituo husika.

Katika ukaguzi wangu kuhusiana na usimamizi wa fedha zilizokusanywa kutokana na uchangiaji wa gharama za matibabu; nilibaini kuwa, shilingi bilioni 1.46 zilikusanywa na vituo vya afya katika Halmashauri tatu, ambapo shilingi milioni 729.79 ikiwa ni asilimia 50 ya fedha zilizokusanywa zilitakiwa kutengwa na kutumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Hata hivyo, ni shilingi milioni 274.04 pekee zilizotengwa na kutumika kwenye ununuzi wa dawa na vifaa tiba wakati shilingi milioni 455.72 zilitumika kufanya shughuli nyingine kama vile malipo ya posho na matumizi mengine ya kawaida.

Kutenga fedha pungufu kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba kunakwamisha juhudi za Serikali katika kutoa huduma bora za afya kwa jamii inayokusudiwa. Mamlaka za Mitaa ambazo vituo vyake vya afya vilibadili matumizi ya fedha za ununuzi wa dawa ni kama inavyoonekana katika **jedwali 13-7** hapa chini;-

**Jedwali Na.13-7: Fedha za Dawa Zilizotumika kwa Matumizi Mengineyo**

| Na. | Halmashauri | Makusanyo (Sh.) | Asilimia 50 iliyotakiwa kwa ajili ya dawa (Sh.) | Kiasi kilichotumika kununua dawa (Sh.) | Pungufu (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | 1,163,717,462 | 581,858,731 | 195,924,969 | 385,903,792 |
| 2. | H/Jiji Tanga | 231,999,566 | 115,999,783 | 67,580,804 | 48,418,979 |
| 3. | H/W Ushetu | 63,865,200 | 31,932,600 | 10,538,966 | 21,393,634 |
| **Jumla** | | **1,459,582,228** | **729,791,114** | **274,044,739** | **455,716,405** |

**Ninashauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha vituo vya afya vinatenga asilimia 50 inayohitajika kutoka kwenye makusanyo ya fedha za uchangiaji wa gharama za matibabu kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.**

## 13.7 Vifaa Tiba Vilivyonunuliwa Ambavyo Havitumiki

Nilibaini vituo vya afya katika Mamlaka 4 za Serikali za Mitaa zilikuwa na vifaa visivyofanya kazi kwa muda kati ya miezi 3 hadi miaka 3 kutokana na kutokuwepo kwa wataalam wanaohitajika, vitendanishi na kasoro kwenye vifaa husika tangu kupokelewa kutoka Bohari ya Dawa (MSD).

Katika vituo viwili vya afya vilivyopo Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni na Halmashauri ya Wilaya ya Msalala nilibaini mashine za mionzi za CT scan, x-ray na mashine ya kupiga picha (ultra sound) zilizotolewa kwenye vituo hivyo hazifanyi kazi kutokana na kutokuwepo kwa mtaalam wa mionzi. Aidha, nilibaini kuwa, Kituo cha Afya cha Kimbiji katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kiliajiri mfanyakazi wa muda kufanya kazi ya kupiga picha za mionzi kwa kutumia mashine ya X-Ray mara moja kwa kila wiki huku mashine ya mionzi ya CT scan ikiendelea kutofanya kazi.

Licha ya Halmashauri hizo kuomba watumishi wanaohitajika, mamlaka ya ajira haijatoa kibali au kupeleka watumishi wataalam wanaohitajika kuendesha vifaa hivyo. Vifaa katika Mamlaka zingine havitumiki kutokana na ubovu, ukosefu wa vitendanishi na kinga za kuzuia mionzi. Vifaa tiba ambavyo havitumiki katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama ilivyooneshwa katika **jedwali Na 13-8** hapa chini;-

**Jedwali Na.13-8: Vifaa Vilivyonunuliwa Ambavyo Havitumiki**

| Na. | Halmashauri | Kituo | Kifaa | Thamani | Mwaka wa Ufungaji/ Ununuzi | Sababu za kutotumika |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Kigamboni | Kituo cha Afya Kimbiji | Mashine ya Mionzi (X-Ray) | Ghrama Haikupatikana | Agosti 2021 | Hakuna mtaalam wa mionzi |
| | | | Mashine ya mionzi (CT Scan) | - | | |
| 2. | H/W Msalala | Kituo cha Afya Bugarama | Mashine ya mionzi (X-Ray) na mashine ya picha (ultra sound) | 172,000,000 | Julai 2022 | Hakuna mtaalam wa mionzi |
| 3. | H/W Geita | Hospitali ya Nzera | Kichanganuzi cha Kemia chenye otomatiki nusu | 2,035,500 | Agosti 2019 | Hakuna vitendanishi |
| | | | Mashine ya mionzi (X-ray) ya kijiditali | 122,544,600 | Agosti 2019 | Ukosefu wa kinga ya kuzuia mionzi |
| 4. | H/W Mufindi | Kituo cha Afya Kasanga | Mashine ya kudhibiti hewa ya Oksijeni | 7,040,340 | Juni 2022 | Kifaa kilichopokelewa sio kilichoagizwa |
| | | | Mashine ya mapigo ya moyo | 9,796,300 | Mei 2021 | Ubovu |
| Jumla | | | | 313,416,740 | | |

Matarajio ya serikali ya kutoa huduma bora za afya kwa jamii huenda yasifikiwe kutokana na kutofanya kazi kwa vifaa tiba vinavyohitajika katika utoaji wa huduma za afya

**Ninapendekeza OR-TAMISEMI kuongeza jitihada za ziada ili kuhakikisha wataalam wa vifaa tiba wanaajiriwa kwa ajili ya uendeshaji wa vifaa vya matibabu vinavyotolewa. Pia, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitenge fedha katika bajeti zao kwa ajili ya ununuzi wa vitendanishi vinavyohitajika, ukarabati wa vifaa tiba vyenye kasoro mbalimbali, kufanya ununuzi wa vifaa vya tahadhari ili kuhakikisha manufaa yaliyokusudiwa yanapatikana.**

## 13.8 Hatua Hafifu za Kupunguza Viwango vya Vifo vya Wajawazito na Watoto wachanga.

Mwongozo wa mapitio ya vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga uliotolewa Oktoba 2019 unaeleza kuwa Kifo cha Mama mjamzito ni kifo cha mwanamke kinachotokea wakati akiwa mjamzito au ndani ya siku 42 baada ya mimba kutoka, bila kujali miezi ya ujauzito na eneo la ujauzito kutokana na sababu zinazohusiana au kuchochewa na ujauzito au usimamizi wake, lakini sio kwa sababu za ajali au sababu zisizozuilika. Vifo vya watoto wachanga ni kifo cha mtoto mchanga ndani ya siku 28 za kwanza tangu kuzaliwa.

Aya ya 4.4 wa Mpango wa Taifa wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga wa 2021 'one plan III' uliotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeonyesha shabaha ya vifo vya wajawazito kupunguzwa kutoka 250 hadi 100 kwa vizazi hai 100,000. Hata hivyo viwango hivyo vinatofautiana na shabaha ya vifo 180 kwa vizazi hai 100,000 iliyoelezwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/22-2025/26. Kulingana na takwimu zilizochapishwa kwenye tovuti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), hadi kufikia mwaka 2020, Tanzania ilikuwa na makadirio ya vifo vya wajawazito 238 kati vizazi hai 100,000.

Mpango wa Taifa wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga wa 2021 'one plan III' unaeleza shabaha ya kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka 20 kwa vizazi 1,000 hadi vifo 15 kwa vizazi 1,000 ifikapo 2025. Hata hivyo, viwango hivyo vinatofautiana na viwango tarajiwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2021/22-2025/26 ambao unaonyesha kuwa Tanzania imepanga kupunguza vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 36 hadi 30 katika vizazi 1000 ifikapo mwaka 2025/26.

Katika mwaka 2021/22, nilibaini kuwa; kulikuwa na ongezeko la viwango vya vifo vya wajawazito zaidi ya lengo la vifo 100 kwa kila vizazi hai 100,000 katika Mamlaka 20 za Serikali za Mitaa kama inavyoonyeshwa kwenye **jedwali Na 13-9** hapa chini; -

**Jedwali Na.13-9: Halmashauri zenye Viwango vya Vifo zaidi ya 100**

| Na. | Jina la Halmashauri | 2020/21 | | | | 2021/22 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Vifo vya Waja wazito | Vizazi Hai | % za vifo kwa vizazi hai | Vifo kwenye vizazi hai 100,000 | Vifo vya Wajawazito | Vizazi Hai | % za vifo kwa vizazi hai | Vifo kwenye vizazi hai 100,000 |
| 1. | H/Mji Geita | 27 | 12931 | 0.21 | 209 | 28 | 2830 | 0.99 | 989 |
| 2. | H/W Bukombe | 6 | 15100 | 0.04 | 40 | 6 | 1223 | 0.49 | 491 |
| 3. | H/W Chunya | 58 | 8636 | 0.67 | 672 | 40 | 9945 | 0.40 | 402 |
| 4. | H/Mji Njombe | 4 | 4362 | 0.09 | 92 | 14 | 3714 | 0.38 | 377 |
| 5. | H/M Moshi | 55 | 12238 | 0.45 | 449 | 33 | 12024 | 0.27 | 274 |
| 6. | H/M Lindi | 11 | 4036 | 0.27 | 273 | 11 | 4077 | 0.27 | 270 |
| 7. | H/Jiji Mwanza | 75 | 28529 | 0.26 | 263 | 71 | 27209 | 0.26 | 261 |
| 8. | H/Mji Mpanda | 36 | 9219 | 0.39 | 390 | 23 | 9755 | 0.24 | 236 |
| 9. | H/W Mbulu | 15 | 8068 | 0.19 | 186 | 18 | 8201 | 0.22 | 219 |
| 10. | H/Mji Babati | 3 | 10185 | 0.03 | 29 | 12 | 5737 | 0.21 | 209 |
| 11. | H/W Mbeya | 44 | 18526 | 0.24 | 238 | 36 | 20160 | 0.18 | 179 |
| 12. | H/W Kyela | 51 | 7837 | 0.65 | 651 | 14 | 7882 | 0.18 | 178 |
| 13. | H/M Shinyanga | 11 | 8066 | 0.14 | 136 | 16 | 9912 | 0.16 | 161 |
| 14. | H/Jiji Dodoma | 40 | 23906 | 0.17 | 167 | 33 | 24268 | 0.14 | 136 |
| 15. | H/W Liwale | 5 | 3892 | 0.13 | 128 | 5 | 3999 | 0.13 | 125 |
| 16. | H/W Ileje | 1 | 4582 | 0.02 | 22 | 4 | 3319 | 0.12 | 121 |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2020/21 | | | | 2021/22 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Vifo vya Wajawazito | Vizazi Hai | % za vifo kwa vizazi hai | **Vifo kwenye vizazi hai 100,000** | Vifo vya Wajawazito | Vizazi Hai | % za vifo kwa vizazi hai | **Vifo kwenye vizazi hai 100,000** |
| 17. | H/W Sengerema | 26 | 18313 | 0.14 | 142 | 20 | 16895 | 0.12 | 118 |
| 18. | H/W Mbozi | 10 | 23270 | 0.04 | 43 | 20 | 17043 | 0.12 | 117 |
| 19. | H/W Mtama | 9 | 4328 | 0.21 | 208 | 5 | 4738 | 0.11 | 106 |
| 20. | H/W Wanging'ombe | 2 | 3759 | 0.05 | 53 | 4 | 3914 | 0.10 | 102 |

Muhimu: Kiwango cha vifo vya wajawazito katika vizazi 100,000 kinakadiriwa kwa idadi halisi ya vifo vya wajawazito vilivyotekea katika vizazi hai halisi katika Halmashauri husika. Kiwango hicho kinapatikana kwa kuchukua idadi ya vifo halisi kugawanywa na vizazi hai halisi na kuzidishwa na vizazi hai 100,000. Mfano H/Mji Geita mwaka 2021, kiwango ni (27/12,931*100,000=209)

Licha ya kwamba viwango vya vifo vya wajawazito katika Mamlaka 13 za Serikali za Mitaa kuwa chini ya vifo 100 kati ya vizazi hai 100,000, kwa miaka miwili takwimu zilizopatikana zinaonyesha kuwa idadi ya vifo vya wajawazito ilikuwa inaongezeka na kuashiria kuwa katika miaka ijayo viwango hivyo vitakuwa juu ya shabaha inayokusudiwa. Mamlaka za Serikali za Mitaa zenye viwango vya vifo vya wajawazito vinavyoongezeka zimeonyeshwa kwenye **jedwali Na 13-10** hapa chini;

**Jedwali Na.13-10: Halmashauri zenye Ongezeko La Vifo vya Wajawazito**

| **Na.** | **Halmashauri** | **2021** | | | **2022** | | | **Ongezeko** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Vifo vya Wajawazito | Vizazi Hai | **kwenye vizazi hai 100,000** | Vifo vya Wajawazito | Vizazi Hai | **kwenye vizazi hai 100,000** | |
| 1. | H/W Songwe | 3 | 9582 | 31 | 6 | 7561 | 79 | 48 |
| 2. | H/W Hanang' | 2 | 9937 | 20 | 8 | 12160 | 66 | 46 |
| 3. | H/W Mbinga | 0 | 7853 | 0 | 3 | 7582 | 40 | 40 |
| 4. | H/W Momba | 2 | 15599 | 13 | 5 | 10324 | 48 | 36 |
| 5. | H/W Mbeya | 6 | 9551 | 63 | 10 | 10337 | 97 | 34 |
| 6. | H/M Kahama | 9 | 16472 | 55 | 15 | 17864 | 84 | 29 |
| 7. | H/W Kondoa | 2 | 5619 | 36 | 4 | 6224 | 64 | 29 |
| 8. | H/Mji Mbinga | 2 | 7907 | 25 | 4 | 7875 | 51 | 25 |
| 9. | H/W Chato | 3 | 21700 | 14 | 7 | 19297 | 36 | 22 |
| 10. | H/Mji Tunduma | 5 | 11215 | 45 | 5 | 7656 | 65 | 21 |
| 11. | H/W Kiteto | 1 | 4775 | 21 | 3 | 7597 | 39 | 19 |
| 12. | H/Mji Mafinga | 4 | 5117 | 78 | 5 | 5442 | 92 | 14 |
| 13. | H/W Magu | 3 | 18996 | 16 | 5 | 17736 | 28 | 12 |

Pia, katika mwaka 2021/22 niligundua viwango vya vifo vya watoto wachanga katika Mamlaka 2 za Serikali za Mitaa vilikuwa ni vifo 135 na vifo 49 kwa watoto 1000 waliozaliwa ambavyo viwango vikubwa zaidi kuliko lengo la vifo 30 kwa watoto 1000 wanaozaliwa kama ilivyoelezwa katika Mpango wa 'One Plan III'. Maelezo yanaonyeshwa kwenye **jedwali Na 13-11** hapa chini -

**Jedwali Na.13-11: Halmashauri zenye Viwango Vikubwa vya Vifo vya Watoto Wachanga**

| Na. | Jina la Halmashauri | Viwango vya vifo 2020/21 | | Viwango vya vifo 2021/22 | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Early Neonatal 0-7 Days | Late Neonatal 8-28 Days | Early Neonatal 0-7 Days | Late Neonatal 8-28 Days |
| 1. | H/Jiji Mbeya | 147/1,000 | 51/1,000 | 135/1,000 | 23/1,000 |
| 2. | H/W Mbeya | 39/1,000 | 5/1,000 | 49/1,000 | 6/1,000 |

Pia, niligundua kuwa kulikuwa na vifo vya watoto wachanga 6335 katika Mamlaka 20 za Serikali za Mitaa kwa miaka miwili; hata hivyo, kiwango cha vifo kwa watoto 1000 wanaozaliwa hakikuweza kupatikana baada ya kukosekana taarifa za idadi ya watoto waliozaliwa. Idadi ya vifo vilivyotokea ni kubwa inayolazimu kuchukuliwa hatua ili kuondoa vifo vya watoto wachanga na kufikia shabaha ya vifo 30 kwa watoto 1000 wanaozaliwa. Orodha ya Halmashauri yenye vifo vya watoto wachanga nikama inavyoonekana **jedwali Na 13-12** hapa chini; -

**Jedwali Na.13-12: Idadi ya Vifo vya Watoto Wachanga Katika Halmashauri**

| Na. | Jina la Halmashauri | Vifo vya Watoto 2021 | Vifo vya Watoto 2022 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Mwanza | 761 | 402 | 1163 |
| 2. | H/M Moshi | 564 | 353 | 917 |
| 3. | H/Jiji Dodoma | 220 | 324 | 544 |
| 4. | H/W Songea | 256 | 185 | 441 |
| 5. | H/Jiji Mbeya | 198 | 158 | 356 |
| 6. | H/M Kigoma | 222 | 122 | 344 |
| 7. | H/W Mbulu | 89 | 166 | 255 |
| 8. | H/W Sengerema | 112 | 130 | 242 |
| 9. | H/M Bukoba | 103 | 126 | 229 |
| 10. | H/Mji Geita | 132 | 95 | 227 |
| 11. | H/W Kibondo | 100 | 127 | 227 |
| 12. | H/W Igunga | 108 | 96 | 204 |
| 13. | H/M Shinyanga | 65 | 128 | 193 |
| 14. | H/Mji Mafinga | 81 | 70 | 151 |
| 15. | H/M Mpanda | 97 | 45 | 142 |
| 16. | H/M Kahama | 67 | 64 | 131 |
| 17. | H/Mji Masasi | 68 | 60 | 128 |
| 18. | H/W Iringa | 49 | 74 | 123 |
| 19. | H/W Mbozi | 33 | 75 | 108 |
| 20. | H/W Kilolo | 59 | 46 | 105 |
| **Jumla** | | **3440** | **2895** | **6335** |

Sababu kuu za vifo vya uzazi ni kuvuja damu wakati wa kujifungua ambayo husababisha zaidi ya robo moja ya vifo, matatizo ya shinikizo la damu wakati wa ujauzito, upungufu wa damu wakati wa ujauzito,

kifafa cha mimba na magonjwa yanayohusiana na ujauzito. Sababu nyingine ni kuchelewa kwa wajawazito katika vituo vya afya ili kupata huduma ya matibabu kwa wakati wa uchungu, watoa huduma za afya ya msingi na wakunga kutokuwa na ujuzi wa kutosha wakati wa kutoa huduma za kujifungua na uhaba wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga wa 2021 'one plan III' kukosa hewa kwa watoto wanaozaliwa ni chanzo kikuu cha vifo vya watoto wachanga, ikifuatiwa na kuzaliwa kabla ya wakati na maambuzi ya bakteria. Vifo hivi vinaweza kuzuilika kwa kuboresha; upatikanaji wa watoa huduma wenye ujuzi, ubora wa huduma kwa wajawazio kabla na baada ya kujifungua na matunzo ya watoto wachanga wanaozaliwa na wanaoumwa.

Kwa maoni yangu, hatua thabiti zenye ubunifu na ubora zinahitajika kuchukuliwa ili kuzuia viwango vya vifo vya wajawazito na watoto wachanga kufikia shabaha inayolengwa ifikapo mwaka 2025/26.

**Ninapendekeza kuwa, Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe kuwa huduma bora za afya zinatolewa katika vituo vya afya, kuwapatia wahudumu wa afya ya msingi maarifa na ujuzi wa kutosha ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga. Kuongeza ufahamu juu ya umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki mapema na kujifungua katika vituo vya afya.**

**Pia, ninashauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa fedha zinazohusu shughuli za kupunguza vifo vya wajawazito na watoto zinatolewa kama ilivyopangwa ili kuondoa/kupunguza vifo vya uzazi na watoto wachanga kama ilivyolengwa.**




# SURA YA KUMI NA NNE

# UFANISI WA UWEKEZAJI, USIMAMIZI WA MASOKO NA VITUO VYA MABASI

## 14.0 Utangulizi

Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimewekeza katika miradi mbalimbali ili kupata faida, kuongeza mapato, na kudumisha mtiririko wa fedha taslimu ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka katika utoaji wa huduma bora kwa jamii. Uwekezaji huo ni pamoja na kununua hisa, kujenga hoteli, kuwekeza katika majengo, stendi za mabasi na miradi mingine ya kibiashara. Ili kuhakikisha ufanisi katika usimamizi wa uwekezaji, baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeanzisha kampuni tanzu na ubia ili kutekeleza shughuli za taasisi mpya zilizoanzishwa.

Hata hivyo, pamoja na nia njema ya kuongeza vyanzo vya mapato katika Halmashauri husika, kama hautasimamiwa vema, uwekezaji unaofanywa unaweza kuishia kuwa biashara zisizo na faida au zenye kuleta hasara.

Nilifanya uchambuzi wa utendaji katika uwekezaji na ufanisi wa usimamizi katika utekelezaji wa miradi iliyowekezwa ili kubaini kama malengo yaliyotarajiwa yanafikiwa. Pia, nilitathmini uzingatiaji wa sheria zilizopo, kanuni, sera, miongozo na mifumo mingine inayoongoza maamuzi ya uwekezaji ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha fedha za umma zinatumika katika uwekezaji wenye faida. Mambo yafuatayo yalibainika wakati wa ukaguzi:

## 14.1 Maoteo ya Faida ya Uwekezaji Katika Hoteli ya Jiji la Dodoma Yasiyo na Uhalisia

Katika jitihada za kuongeza mapato yake, mwaka 2020 Halmashauri ya Jiji la Dodoma iliwekeza katika ujenzi wa hoteli, kwa gharama ya Sh. bilioni 10.22. Kutokana na upembuzi yakinifu uliofanywa kabla ya

uwekezaji, ilionesha kuwa itachukua miaka 11 kwa mradi husika kurudisha gharama zote za uwekezaji. Katika upembuzi huo, mapato ya kukodisha hoteli hiyo yalikadiriwa kuwa ni shilingi milioni 145.25 kwa mwezi katika mwaka wa kwanza wa uendeshaji wa mradi.

Hata hivyo, nilibaini kuwa, baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, Halmashauri ya Jiji ilisaini mkataba Na. LGA/20/2021-2022/NCS/09 ya Juni 30, 2022, na mzabuni Eclipse Hotel Limited wa kukodisha hoteli hiyo kwa makubaliano ya kuilipa H/Jiji Dodoma shilingi milioni 50 kila mwezi (sawa na shilingi milioni 600 kwa mwaka) kwa muda wa miaka kumi, kiasi ambacho ni asilimia 34 ya mapato yaliyokadiriwa awali ya shilingi milioni 145.25 kwa mwezi. Makadirio ya muda wa malipo na mkataba halisi yameoneshwa kwenye **Jedwali 14-1**

**Jedwali Na.14-1: Muda wa Kurejesha Gharama za Uwekezaji Katika Hoteli ya Jiji la Dodoma Kulingana na Makubaliano ya Ukodishaji**

| Maelezo | Kiasi na muda wa urejeshaji wa gharama |
|---|---|
| Uwekezaji uliofanyika (Gharama za mradi hadi kufikia Juni 30 2022) – (Sh.) | 10,219,671,890 |
| Mapato yote kwa mwaka (Kwa mujibu wa mkataba kati ya H/Jiji Dodoma na mzabuni MS Eclipse Hotels) – (Sh.) | 600,000,000 |
| Muda uliokadiriwa awali wa mradi kurudisha gharama | 11 |
| Muda halisi wa mradi kurudisha gharama baada ya kusaini mkataba wa upangishaji | 17 |

***Chanzo***: Ripoti ya upembuzi yakinifu na mkataba Na. LGA/20/2021-2022/NCS/09

Nina shaka juu ya upembuzi yakinifu wa makadirio hayo kwani Halmashauri haitaweza kufikia lengo lake ndani ya miaka 11 kama ilivyotarajiwa, bali itachukua miaka 17 kulingana na mkataba wa ukodishaji ulioingiwa kati ya H/Jiji na mzabuni MS Eclipse Hotels wa kulipa kiasi cha shilingi milioni 50 kwa mwezi.

Pamoja na hayo, pia nilibaini gharama nyingine za ujenzi wa bwawa la kuogelea, uzio, njia za waenda kwa miguu na maegesho ya magari, ambazo zililipwa na mpangaji, lakini bado hazijawasilishwa kwa mwajiri hivyo hazikuingizwa kwenye gharama ya mradi.

**Napendekeza Halmashauri isimamie mradi kwa ukaribu ili kuhakikisha kuwa muda wa malengo uliokusudiwa unafikiwa,sambamba na hilo, mpangaji kutimiza ipasavyo**

**majukumu yake ya kimkataba.Aidha, nashauri Halmashauri ihakikishe kuwa, kabla ya utekelezaji wa miradi, inafanya makadirio halisi kwa kuzingatia mazingira ili kupata thamani ya fedha kutokana na uwekezaji uliofanyika.**

## 14.2 Mradi Mdogo wa Umeme wa Maji Luswisi uliotarajiwa kugharimu Shilingi Bilioni 20.02 bado Haujatekelezwa

Halmashauri ya Wilaya ya Ileje na wadau wengine walioorodheshwa kwenye **Jedwali Na 14-2,** walikuja na mapendekezo ya kuanzisha mradi wa kufua umeme chini ya kampuni ya BWELUI, ukiwa na lengo la msingi la kuzalisha na kusambaza umeme katika vijiji 43 vya kata 10 za Ileje Mashariki na pia kuliuzia shirika la umeme (TANESCO) umeme utakaobaki chini ya Mkataba wa Kununua Umeme Sanifu (SPPA).

Gharama za uwekezaji wa mradi zilikadiriwa kuwa Dola za Kimarekani 8,554,574, sawa na shilingi bilioni 20.02 katika kiwango cha ubadilishaji cha sasa cha Dola 1 = 2,340. Kulingana na Mkataba wa Makubaliano (MoU), kampuni ilipaswa kumilikiwa na pande tatu, kama ilivyoorodheshwa katika **jedwali 14-2** hapa chini:

**Jedwali Na.14-2: Orodha ya Muundo wa Umiliki wa Hisa za Kampuni**

| Na. | Mwenye hisa | Anuani | Asilimia za umiliki | Wajumbe wa bodi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ileje East Environment conservation group | Box 543 Tukuyu | 30% (kuchangia kipande cha ardhi kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo) | 2 |
| 2. | H/W Ileje | Box 2 Ileje | 30% | 2 |
| 3. | Ensol (T) Limited | Box 42227 DSM | 40% | 3 |

**Chanzo:** Ripoti ya kina ya mradi

Kwa mujibu wa aya ya 10 ya taarifa ya kitaalamu ya mradi, muda uliotengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi ni kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2020. Hata hivyo, hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2021/22, utekelezaji wa mradi haukuwa umeanza kwa kuwa hakuna mchango wowote uliotolewa na pande zote isipokuwa eneo la mradi.

Kuchelewa kutekeleza mradi kunachangiwa na Halmashauri pamoja na Ensol (T) Limited kushindwa kuchangia mtaji unaohitajika kama ilivyokubaliwa katika Mkataba wa Makubaliano (MoU). Ucheleweshaji

zaidi utasababisha kuongezeka kwa gharama za mradi, thamani ya pesa kwenye uwekezaji unaopendekezwa inaweza isifikiwe, na Halmashauri inaweza kushindwa kufikia malengo yake.

**Ninaishauri Halmashauri itenge fedha kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato ili kugharamia mradi. Pia katika siku zijazo, Halmashauri zihakikishe kuwa zinaandaa rasilimali zote kabla ya utekelezaji wa mradi wowote.**

## 14.3 Mapato ya Shilingi Bilioni 1.15 Hayakukusanywa Kutokana na Uendeshaji wa Masoko Usio na Tija Katika Halmashauri Tatu

Katika ukaguzi wangu katika H/M Ubungo, H/M Morogoro na H/Jiji Dodoma, nilibaini maeneo mbalimbali ya masoko ambayo hayakuwa yanatumika hivyo kupunguza tija katika uwekezaji uliofanyika. Kutokana na mapungufu katika uendeshaji wa masoko haya, nilibaini kuna idadi kubwa ya vibanda, fremu, vizimba na meza hazikupata wapangaji kwa mwaka mzima, hivyo kupoteza mapato ambayo yangekusanywa.

Ikiwa vibanda na fremu za maduka katika masoko hayo zingekodishwa na wapangaji mbalimbali, jumla ya shilingi bilioni 1.15 zingepatikana. Kwa kutokodisha vibanda na maduka ya soko husika, Halmashauri husika hazitaweza kufikia malengo ya makusanyo kutokana na uwekezaji uliofanyika, pia lengo lililokusudiwa la utoaji huduma kwa jamii halitafikiwa. Maelezo ya vibanda vya masoko na fremu za Halmashauri hizo yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 14-3**, **Jedwali Na. 14-4** na **Kiambatisho 14-1** mtawalia.

**Jedwali Na.14-3: Vibanda na Fremu za Soko Zilizo Wazi Katika H/M Ubungo**

| Soko | Maelezo | Idadi | Kodi kwa siku (Sh) | Idadi ya siku | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| Soko la Mawasiliano | Vizimba | 159 | 500 | 365 | 29,017,500 |
| | Vibanda | 909 | 500 | 365 | 165,892,500 |
| Soko la Beda | Vizimba | 276 | 500 | 365 | 50,370,000 |
| | Vibanda | 68 | 500 | 365 | 12,410,000 |
| Soko la Shekilango | Meza | 59 | 200 | 365 | 4,307,000 |
| | Vizimba | 6 | 200 | 365 | 438,000 |
| | Vibanda | 142 | 200 | 365 | 10,366,000 |
| Soko la Manzese | Vizimba na Meza | 60 | 500 | 365 | 10,950,000 |
| Soko la Mburahati | Vizimba | 60 | 500 | 365 | 10,950,000 |
| | Kibanda | 1 | 500 | 365 | 182,500 |
| **Jumla** | | | | | **294,883,500** |

***Chanzo:*** Mahojiano na ripoti za soko

**Jedwali Na.14-4: Vibanda na Fremu za Soko Zilizo Wazi H/M Morogoro**

| Na. | Maelezo | Idadi | Bei (Sh) | Miezi | Jumla ya thamani (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Vyumba vya soko | 111 | 100,000/Mwezi | 7 | 77,700,000 |
| 2. | Vibanda | 222 | 10,000/Mwezi | 12 | 26,640,000 |
| 3. | Eneo la kupanga (Mita za eneo) | $M^2$ 4184 | 8,000/Mwezi | 12 | 401,664,000 |
| **Jumla** | | | | | **506,004,000** |

*Chanzo:* Ripoti ya Uendeshaji wa Soko kuanzia Julai-Juni, 2022

**Jedwali Na.14-5: Vibanda na Vyumba Vilivyo Wazi Katika H/Jiji la Dodoma**

| Na. | Jina la Soko | Idadi ya vizimba/duka/vyumba | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Bucha-Ndugai | 8 | 28,800,000 |
| 2 | Maduka-Ndugai | 65 | 70,200,000 |
| 3 | Vizimba 7.8sq-Ndugai | 265 | 66,840,000 |
| 4 | Chang'ombe Block B | 24 | 5,520,000 |
| 5 | Vyumba vya kukatia tiketi-Nanenane | 10 | 10,800,000 |
| 6 | Maduka ya sakafu ya chini-Nanenane | 9 | 37,800,000 |
| 7 | Maduka-Sakafu ya kwanza-Nanenane | 18 | 86,400,000 |
| 8 | Vizimba-Nanenane | 38 | 41,040,000 |
| **Jumla** | | **437** | **347,400,000** |

*Chanzo: Taarifa za Afisa Masoko*

Utendaji duni wa masoko haya unachangiwa na mazingira ya kibiashara yasiyoridhisha, kutokuwepo kwa maeneo ya kutosha ya kuegesha magari na kuwepo kwa maeneo yasiyo rasmi ya biashara.

**Ninazishauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kuhakikisha kuwa maeneo ya biashara yasiyo rasmi yanafungwa ili kuvutia wapangaji kwenye masoko rasmi.**

**Menejimenti hizo pia zinapaswa kujitahidi kuweka mazingira mazuri ya soko kuanzia usafi wa mazingira, maeneo ya kutosha ya maegesho, usalama wa kutosha na ugawaji wa vibanda, fremu na vizimba bila upendeleo.**

## 14.4 Kuchelewa Kukamilika Kwa Stendi Mbili za Mabasi zenye Thamani ya Shilingi Bilioni 7.65

Ujenzi wa stendi za mabasi umekuwa ni uwekezaji muhimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kukuza mapato ya ndani kwa kukusanya ada za viingilio kwa mabasi ya abiria yanayopitia njia ya Halmashauri husika.

Nilibaini Halmashauri mbili zinazoendelea na ujenzi wa stendi za kisasa za mabasi zenye thamani ya shilingi bilioni 7.65 ambazo ziko katika hatua tofauti za ukamilishaji; lakini ujenzi upo nje ya muda uliotakiwa. Pamoja ya kuongezewa muda wa utekelezaji, wakandarasi husika bado hawajakamilisha ujenzi wa miradi hiyo. Maelezo yanaonyeshwa kwenye **Jedwali 14-6.**

**Jedwali Na.14-6: Vituo vya Mabasi Ambavyo Ujenzi Umechelewa**

| Na. | Halmashauri | Mkandarasi | Muda wa Kuanza ujenzi | Tarehe ya kumaliza ujenzi | Bei ya Mkataba | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Mwanzo (Sh.) | Mwisho (Sh.) |
| 1. | H/W Kakonko | M/S Sugwa Contractors Enterprises and JV Chiganda Construction Company Ltd | 14 Juni 2019 | 14 Juni 2020 | 2,146,996,675 | 2,146,996,675 |
| 2. | H/W Hanang' | Elerai Construction Company Ltd | 9 Julai, 2019 | 22 Julai, 2020 | 5,298,789,469 | 5,498,789,469 |
| **Jumla** | | | | | **7,445,786,144** | **7,645,786,144** |

**Chanzo: Majalada ya Mikataba**

Kuchelewa kukamilika kwa mradi kunachangiwa na wakandarasi kutokuwa na mtaji wa kutosha, uhaba wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kulipa madai ya wakandarasi kwa wakati, kukosekana kwa mipango thabiti pamoja na usimamizi duni wa mradi katika kuhakikisha kuwa mkandarasi anatimiza wajibu wake.

Ucheleweshaji zaidi wa ukamilishaji wa miradi hii utapelekea kukosekana kwa thamani ya fedha za mIradi kwa sababu ya gharama za vifaa kuongezeka.

**Ninazishauri Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa husika kufanya usimamizi wa karibu wa miradi na kuhakikisha kuwa wakandarasi wanatimiza wajibu wao, aidha kuhakikisha malipo ya wakandarasi yanafanyika kwa wakati.**

## 14.5 Viwanda vya Kusindika Mazao ya Nyuki vyenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.36 Vilivyokamilika Lakini Havikuanza Kutumika

Ufugaji nyuki na usindikaji wa mazao ya nyuki ni eneo lingine ambalo Halmashauri zinawekeza rasilimali ili kupata faida. Katika ukaguzi wangu nilibaini miradi miwili ya viwanda vya usindikaji wa mazao ya nyuki/asali katika H/W ya Sikonge na H/W ya Kibondo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.36, ambayo ilikuwa imekamilika lakini haijaanza kufanya uzalishaji. Maelezo ya miradi hiyo yameorodheshwa katika **jedwali Na 14-7** hapa chini:

**Jedwali Na.14-7: Viwanda vya Kusindika Mazao ya Nyuki Visivyotumika**

| Na | Halmashauri | Gharama za Mradi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kibondo | 600,000,000 | Mradi umekamilika tangu mwaka 2021/22 lakini haufanyi kazi. |
| 2. | H/W Sikonge | 757,585,290 | Mradi umekamilika tangu tarehe 07 Mei, 2022 lakini bado haujanza kutumika |
| **Jumla** | | **1,357,585,290** | |

*Chanzo*: Faili za mradi na eneo halisi la mradi

Aidha nilibaini kuwa, viwanda hivyo havifanyi kazi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa wataalam wenye ujuzi wa kuendesha mitambo mipya iliyonunuliwa pamoja na kukosekana kwa mikataba kati ya viwanda hivyo na vyama vya ushirika vya wafugaji nyuki kwa ajili ya usambazaji wa asali na mazao mengine ya nyuki.

Ucheleweshaji wa uendeshaji wa miradi hiyo utaharibu malengo ya kuanzishwa kwa miradi hiyo, pia thamani ya fedha za miradi hiyo haitapatikana. Inaweza pia kusababisha kuchakaa na kupungua kwa ubora wa mitambo iliyonunuliwa na kuongeza gharama za matengenezo katika siku za usoni.

**Naishauri Menejimenti ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha inatatua mambo yote yanayokwamisha uzalishaji katika viwanda hivi, ikiwa ni pamoja na ajira za wafanyakazi wenye ujuzi wa kuendesha mitambo, kuhakikisha upatikanaji wa malighafi ya kutosha, na kubuni mikakati mingine muafaka ya kuendesha viwanda hivyo.**

## 14.6 Matukio ya Moto yasiyodhibitiwa na Kusababisha Hasara ya Shilingi Bilioni 2.09

Halmashauri za mkoa wa Njombe zimekuwa zikifanya uwekezaji katika shughuli za upandaji miti kwa lengo la kukuza mapato yake ya ndani. Hata hivyo, uwekezaji huo umekuwa ukikabiliwa na tatizo la milipuko ya moto ya mara kwa mara na kusababisha hasara kubwa kwa Halmashauri husika.

Katika nia ya kukabiliana na changamoto hii, mikakati ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu (PFM) na programu za kilimo endelevu ziliasisiwa ili kuimarisha udhibiti wa moto na kuboresha maisha ya jamii za vijijini (Yanda et al, 2008; URT, 2012). Sambamba na programu hizo, Sera ya Taifa ya Misitu Tanzania ilibainisha uchomaji moto kuwa matishio makubwa ambayo yamekuwa yakisababisha uharibifu wa misitu na mapori (URT, 1998). Hata hivyo, kukosekana kwa sera mahususi na mifumo ya kitaasisi ya kushughulikia tatizo la moto kumeathiri ufanisi wa usimamizi wa zimamoto mkoani Njombe na Tanzania kwa ujumla.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa, H/W Ludewa na H/W Makete zimepata hasara kubwa kutokana na milipuko ya moto. Kwa mujibu wa mapitio ya taarifa za fedha za Halmashauri na taarifa nyinginezo, hasara ya jumla ya Halmashauri zote mbili katika kipindi cha miaka mitatu ilikuwa shilingi bilioni 2.09 (H/W Ludewa shilingi bilioni 2.01 na H/W Makete shilingi milioni 79.45).

Takwimu kuhusiana na taarifa ya idadi ya matukio ya moto ndani ya H/W Ludewa zilionesha kuwa, kuna wastani wa matukio mawili ya moto kwa mwaka ambayo yalisababisha hasara ya ekari 181 za misonobari na mikorosho. H/W Makete haikutoa taarifa zozote kuhusu idadi ya matukio au ekari zilizoharibiwa.

Matukio ya moto yalisababishwa na shughuli za binadamu, ama kwa bahati mbaya au kwa kukusudia na wachomaji moto waliotaka kulipiza kisasi kwa Halmashauri kutokana na kukataliwa kupewa vibali vya kuvuna, leseni, au maeneo ya kilimo. Zaidi ya hayo, Halmashauri hazina vifaa vya kuzimia moto ili kusaidia kupunguza athari za moto pindi matukio hayo yanapotokea.

**Ninazishauri Halmashauri husika kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI kuandaa mikakati madhubuti ya kusaidia kukabiliana na majanga ya moto katika maeneo yao kama vile Mafunzo kwa wafanyakazi juu ya uzimaji moto na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kuzimia moto, vifaa vya redio kama "walkie-talkies" na kuwepo kwa mitandao ya barabara ya kufikia mashambani ili kuongeza ufikaji wa haraka na hivyo kukabiliana na matukio ya moto.**

**Aidha, Halmashauri zinapaswa kukutana na vijiji vinavyozunguka na kuweka mahusiano mazuri ili kuleta amani kati ya jamii na Halmashauri.**

## 14.7 Taarifa za Fedha za Benki ya DCB hazijawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi

Benki ya Biashara ya DCB ilipata usajili tarehe 6 Septemba 2001. Mnamo Aprili 2002, DCB ilianza biashara kama taasisi ya kifedha ya kanda ya kifedha na kufikia tarehe 12 Juni, 2003, benki ilipewa leseni ya kufanya biashara ya benki ikijulikana kama Dar es Salaam Community Bank (DCB). Kulingana na taarifa za fedha zilizochapishwa za mwaka uliomalizika 2021, jumla ya wanahisa wa benki hiyo walikuwa 7,343 kama inavyooneshwa kwenye **jedwali Na. 14-8** hapa chini:

**Jedwali Na.14-8: Hisa za Benki ya DCB**

| Halmashauri | Idadi ya Hisa | Thamani ya Hisa (Sh.) | % Umiliki |
|---|---|---|---|
| H/M Kigamboni | 2,281,502 | 570,375,500 | 2.34 |
| H/M Ubungo | 2,877,367 | 725,002,250 | 2.96 |
| H/M Temeke | 3,422,252 | 855,563,000 | 3.49 |
| H/M Kinondoni | 5,625,019 | 1,406,254,750 | 5.74 |
| NHIF | 6,000,000 | 1,500,000,000 | 6.12 |
| H/Jiji Ilala | 7,866,859 | 1,989,356,500 | 8.12 |
| H/Jiji Dar es Salaam | 10,228,320 | 2,608,023,500 | 10.65 |
| UTT | 23,211,479 | 5,802,869,750 | 23.69 |
| Wanahisa wengine 7335 | 36,134,115 | 9,033,528,750 | 36.89 |
| **Jumla** | **97,646,913** | **24,490,974,000** | **100.00** |

***Chanzo**: Hesabu za mwisho za mwezi desemba 2021*

Kulingana na Jedwali hapo juu, Halmashauri za Dar es Salaam kwa pamoja zinamiliki asilimia 33 ya mtaji wote wa Benki hiyo, ambapo pamoja na mashirika ya Serikali kwa ujumla wanamiliki asilimia 63 ya

mtaji wote. Hii ina maana kwamba Serikali kupitia vyombo na mamlaka zake, ina udhibiti wa maslahi katika uendeshaji wa benki hiyo, kwa kuwa vyombo hivyo vinamilikiwa na Serikali kupitia Msajili wa Hazina. Kwa muktadha huu, DCB inamilikiwa na Serikali kupitia Halmashauri za Serikali za mitaa, UTT, na NHIF. Hata hivyo, benki hii hapo awali ilianzishwa kama benki ya binafsi iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, na kwa hivyo hakuna Sheria ya Bunge ya kuanzishwa kwake.

Kwa sababu hiyo, benki hii haimo kwenye orodha ya mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina na hivyo haijawahi kuwasilisha taarifa za fedha ofisini kwangu kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba na Kifungu cha 9(a) iii & iv cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya mwaka 2008.

**Ninaishauri Serikali, kupitia Hazina, kuhusu hesabu za DCB, kutekeleza uzingatiaji wa Kifungu cha 30(b) na (e) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ambacho kinazitaka taasisi zote ambazo Serikali imewekeza fedha zake na zile ambazo Serikali ndio mwanahisa mkubwa kuwasilisha hesabu zao kwa ajili ya ukaguzi.**

## 14.8 Mapungufu yaliyobainika kwenye uwekezaji unaofanywa na Halmashauri za Serikali za Mitaa

Katika miaka ya hivi karibuni, Halmashauri zimekuwa zikijitahidi kutafuta vyanzo vipya vya mapato kwa kuibua na kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji. Miradi hiyo ni pamoja na viwanda vya kutengeneza matofali, viwanda vya kusindika mazao ya nyuki na asali, maduka ya dawa, ujenzi wa hoteli na mengine mengi. Nilitathmini utendaji wa uwekezaji huu na kubaini mapungufu yafuatayo:

i. **Hakuna sera ya Uwekezaji**

Katika tathmini yangu, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina sera za uwekezaji zinazotoa mwongozo katika kuanzishwa hadi uundaji na uendeshaji wa miradi. Hili husababisha kukosekana kwa ufanisi kwenye uendeshaji wa miradi hiyo kutokana na kukosekana kwa dira ya kuendesha miradi hiyo kwa sababu ya mipango isiyoridhisha, ambapo niliona viwanda viwili vya kusindika mazao ya nyuki vilivyokamilika lakini havikuanza kutumika kutokana na ukosefu wa wafanyakazi wenye ujuzi wa kuendesha mashine hizo.

ii. **Hakuna akaunti maalum ya Benki kwa miradi ya uwekezaji**
Nilibaini kuwa halmashauri zote zenye miradi ya viwanda vya matofali zinatumia akaunti ya amana kuhifadhi mapato ya mauzo ya matofali na shughuli nyingine za mradi. Kwa maoni yangu, kutumia akaunti ya amana kuweka fedha zinazohusu mradi wa uwekezaji kunaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo katika shughuli zisizohusiana na mradi.

iii. **Hakuna kumbukumbu za kihasibu na ufungaji wa hesabu**
Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitayarishi kumbukumbu za hesabu, ikiwa ni pamoja na hesabu za mwisho wa mwaka, ili kuziwezesha kufanya uchambuzi wa utendaji wa mradi na kubaini kama unaendeshwa kwa faida au kwa hasara. Kwa sasa, hesabu za miradi hii zinaunganishwa na hesabu za mwisho za Halmashauri, hivyo kufanya ugumu wa kupata ripoti mahususi na kubainisha mali halisi ya miradi hiyo.

Katika kufuatilia, nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hazioneshi nia ya kuomba kibali cha kufungua akaunti za benki kutoka Hazina. Kuendesha miradi ya uwekezaji bila kuwa na kumbukumbu za kutosha za uhasibu na akaunti mahususi za benki kunahatarisha uhai wa miradi hii, ambapo baadaye inaweza kufa bila kufikia malengo yaliyopangwa.

**Ninazishauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka usimamizi mzuri na wa kutosha wa uwekezaji kwa kuhakikisha uwepo wa wafanyakazi wenye ujuzi wa kuendesha mitambo, kufungua akaunti tofauti ili kuweka fedha zinazohusiana na au zinazotokana na uwekezaji,aidha kuweka kumbukumbu za hesabu zilizo fasaha ili kurahisisha ukokotoaji wa faida au hasara ya kiuhasibu na kujua taarifa nzima ya mtiririko wa fedha ili kusaidia katika maamuzi zaidi ya uwekezaji.**

**Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapaswa pia, chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, kuhakikisha uundaji wa sera za uwekezaji ili kuongoza katika uanzishaji, uundaji na uendeshaji wa miradi ya uwekezaji.**



# SURA YA KUMI NA TANO

# SEKRETARIETI ZA MIKOA

## 15.0 Utangulizi

Ibara ya 61 (1) na (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza juu uanzishwaji pamoja na majukumu ya Mkuu wa Mkoa. Pia, Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya mwaka 1997, kinaeleza kuhusu kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Mkoa kama Idara ya Serikali katika kila Mkoa.

Katibu Tawala wa Mkoa ambaye ni Afisa Masuuli wa Sekretarieti ya Mkoa, ana jukumu la kusimamia na kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza sera zao za kimaendeleo. Malengo ya Sekretarieti hizo ni pamoja na kuimarisha utawala bora, huduma za kiutawala, huduma za rasilimali watu, kuboresha upatikanaji wa huduma bora za kijamii, kuhakikisha upatikanaji bora na wa kutosha wa miundombinu ya kiuchumi, kuwezesha kujiandaa na majanga, na usimamizi wa mazingira.

Sura hii inahusika na masuala yote muhimu ya kaguzi zinazohusu taarifa za fedha na ufanisi wa kiutendaji ndani ya Sekretarieti za Mikoa 26 za Tanzania Bara.

Hatahivyo,katika Sura hii nitazungumzia zaidi utekelezaji wa bajeti, usimamizi wa matumizi na ununuzi pamoja na miradi inayotekelezwa kupitia nguvu kazi '*force account*'.

## 15.1 Usimamizi wa matumizi

### 15.1.1 Fedha Taslimu Zilizotolewa kabla ya Utekelezaji wa Shughuli Zinazostahili Shilingi Milioni 211.01

Kanuni ya 93(2) ya Kanuni ya fedha za Umma, GN Na. 132/2001 inaeleza kuwa, pale ambapo malipo yanafanyika kwa fedha taslimu lazima nyaraka za malipo zitiwe saini wakati wa malipo.

Kinyume na Kanuni hiyo, Sekreatrieti mbili za Mikoa zilifanya malipo ya Shilingi milioni 211.01 kupitia Akaunti ya Masurufu kwa ajili ya shughuli mbalimbali, na fedha hizo kuhifadhiwa ofisi ya fedha zikiwa taslimu kwa zaidi ya siku 60 bila kulipwa kwa wahusika, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 15-1.**

**Jedwali Na.15-1: Fedha zilizotolewa kabla ya muda ya utekelezaji wa mradi**

| Na. | Jina la Sekretarieti ya Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Njombe | 177,170,000 |
| 2 | Rukwa | 33,843,680 |
| | **Jumla** | **211,013,680** |

Aidha, nilibaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga ililipa kiasi cha shilingi milioni 170.11 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali kwa fedha taslimu. Kiasi hiko kinazidi kikomo shilingi milioni 5 kwa mujibu wa Jedwali la Saba la Kanuni za ununuzi wa Umma, 2013.

Fedha taslim kutolewa kwenye Akaunti na kuhifadhiwa ofisini kwa muda mrefu, kunaweza kusababisha malipo yasiyo halali na inashawishi matumizi yasiyo sahihi ya fedha za umma.

**Ninapendekeza Menejimenti ya Sekretarieti za Mikoa, ziimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa fedha taslimu ambao utahakikisha malipo yanafanyika kama ilivyoelekezwa na Kanuni Na. 93 (2) ya Kanuni ya Fedha za Umma, GN Na. 132/2001 ili kupata thamani ya fedha katika matumizi ya fedha za umma.**

### 15.1.2 Matumizi yasiyo na Tija yenye Thamani ya Shilingi milioni 71.95

Kulingana na Kanuni ya 21(2) ya Kanuni za Fedha za Umma GN Na. 132/2001, malipo yasiyokuwa na tija ni malipo yanayoweza kuepukika na endapo yakifanyika hayatakuwa na faida kwa taasisi; hii inamaanisha kuwa ni yale yanayofanywa bila kuleta faida za kiuchumi kwa taasisi husika, kama vile malipo yaliyofanywa juu ya kiwango kilichoidhinishwa, riba au adhabu zinazotokana na kushindwa kutimiza

wajibu wa kimkataba, pia na malipo ya posho kwa wafanyakazi kwa shughuli ambazo hazikutekelezwa.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, Sekretarieti za Mikoa minne zilitumia jumla ya shilingi milioni 71.95 kwa matumizi yasiyo na faida za kiuchumi kwa Serikali. Hali hii iliathiri utekelezaji wa shughuli nyingine zilizopangwa katika bajeti. Matumizi hayo ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 15-2.**

**Jedwali Na.15-2: Matumuzi yasiyo na tija**

| Na. | Jina la Sekretarieti ya Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Njombe | 28,694,968 |
| 2 | Mwanza | 25,419,544 |
| 3 | Dar es salaam | 12,205,499 |
| 4 | Kagera | 5,629,749 |
| **Jumla** | | **71,949,760** |

Kati ya vitu vilivosababisha matumizi yasiyo na tija ni pamoja na riba kwa kuchelewa kulipa hati ya madai kutoka kwa mkandarasi, malipo yaliyohusisha kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mtoa huduma ambaye hajasijiliwa kulipa kodi ya ongezeko la thamani, na gharama za kubomoa majengo yaliyojengwa kabla ya kupata kibali.

**Ninapendekeza kwamba, Sekretarieti ya Mikoa husika zihakikishe madai yote yanalipwa kwa wakati na kwa shughuli halali; na pia zizingatie vigezo na masharti yaliyomo ndani ya mikataba wakati wa kufanya maamuzi ili kuepuka kujirudia kwa matumizi hayo yasiyo na tija.**

### 15.1.3 Malipo yasiyo na nyaraka sahihi na zilizokamilika Shilingi Milioni 768.14

Kanuni ya 95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma, GN Na, 132/2001, inafafanua hati ya malipo ambayo haijakamilika kwa sababu ya kutokuwa na nyaraka zote zinazothibitisha uhalali wa malipo hayo, kuwa itambulike kama hati ya malipo iliyokosekana.

Nilibaini kuwa, shilingi milioni 768.14 zililipwa na Sekretarieti za Mikoa 10 kwa wasambazaji mbalimbali wa bidhaa na huduma bila kuambatishwa na nyaraka husika kama vile risiti za kielekitroniki, stakabadhi nyingine za kukiri kupokea fedha na viambatisho vingine. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali 15-3.**

**Jedwali Na.15-3: Malipo yasiyo na nyaraka stahiki**

| Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kagera | 204,275,561 | 6 | Coast | 52,523,161 |
| 2 | Ruvuma | 186,100,956 | 7 | Lindi | 93,276,039 |
| 3 | Kilimanjaro | 68,288,054 | 8 | Dar es salaam | 23,718,500 |
| 4 | Arusha | 65,757,648 | 9 | Shinyanga | 15,577,040 |
| 5 | Katavi | 52,694,638 | 10 | Kigoma | 5,923,800 |
| | | | **Jumla** | | **768,135,397** |

Udhibiti wa ndani usiojitosheleza kwenye matumizi ulisababishwa na Menejimenti za Sekretarieti za Mikoa kufanya malipo bila kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma, GN Na. 132/2001.

Malipo yasiyo na nyaraka sahihi na zilizokamilika yanaashiria upotevu wa fedha za serikali, kwani uhalali wa malipo yaliyofanywa haukuweza kuthibitika.

**Ninapendekeza kwamba, Menejimenti za Sekretarieti za Mikoa husika ziimarishe udhibiti wake wa ndani ili kuhakikisha kwamba nyaraka sahihi zinatunzwa vizuri na kuambatishwa kwenye malipo husika.**

## 15.2 Usimamizi wa Manunuzi

### 15.2.1 Magari yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.95 yaliyonunuliwa kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) Hayajapokelewa

Kanuni ya 242 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 inazitaka taasisi zinazofanya ununuzi, kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika baada ya kupokea bidhaa kwa mujibu wa mkataba. Pia, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ana dhamana ya ununuzi wa jumla wa magari, pikipiki na mitambo kwa ajili ya taasisi za Serikali kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 130 (1) ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 (kama ilivyorekebishwa 2016).

Nilibaini kuwa, Sekretarieti za Mikoa 15 zililipa GPSA kiasi cha shilingi bilioni 4.95 kwa ajili ya ununuzi wa magari, lakini hadi wakati wa ukaguzi Disemba 2022, magari hayo yalikuwa hayakupokelewa na mikoa husika. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali 15-4.**

**Jedwali Na.15-4: Magari yaliyonunuliwa GPSA ambayo bado hayajapokelewa**

| Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tanga | 508,044,076 | 9 | Arusha | 310,681,857 |
| 2 | Pwani | 505,525,156 | 10 | Manyara | 300,000,000 |
| 3 | Dodoma | 494,009,279 | 11 | Geita | 248,823,904 |
| 4 | Katavi | 460,137,161 | 12 | Mwanza | 198,695,106 |
| 5 | Songwe | 431,294,989 | 13 | Lindi | 160,415,665 |
| 6 | Shinyanga | 347,801,857 | 14 | Morogoro | 160,415,665 |
| 7 | Tabora | 345,109,491 | 15 | Dar es salaam | 160,415,665 |
| 8 | Mtwara | 320,831,329 | **Jumla** | | **4,952,201,200** |

Zaidi ya hayo, Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu iliagiza na kupokea gari moja aina ya Nissan Patrol GRX 61 lenye thamani ya shilingi milioni 188.67 kutoka GPSA; hata hivyo, gari hilo limetelekezwa katika karakana ya Nissan kutokana na hitilafu katika injini. Ilibainika kuwa Nissan Tanzania iliandika barua isiyo na kumbukumbu namba ya tarehe 22 Aprili 2022 ikimtaarifu Mkurugenzi Mtendaji wa GPSA kuwa, gari hilo lilipata hitilafu kutokana na mafuta machafu na kuendeshwa umbali mrefu hivyo kusababisha kasoro katika injini ya gari. Hadi Januari 2023, gari hilo lilikuwa bado kwenye karakana ya Nissan bila ya makubaliano kati ya GPSA na Sekretarieti ya Mkoa kuhusu kubadilisha gari au injini.

Kwa maoni yangu, hali hiyo inaashiria kwamba Sekretarieti za Mikoa zinaweza kupokea magari ambayo hayakidhi vigezo na ubora kama walivyoagiza.

**Ninapendekeza kwamba, OR-TAMISEMI ihakikishe GPSA inawasilisha magari kwa Sekretarieti za Mikoa husika kwa kuzingatia Kanuni ya 242 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013.**

### 15.2.2 Kuanza kwa Utekelezaji wa Miradi yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 33.4 Kabla ya Kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 na Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 vinazitaka taasisi zinazofanya ununuzi kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza au kufadhili mradi wowote.

Nimepitia majalada ya miradi na kubaini kuwa, Sekretarieti tatu za Mikoa zilitekeleza miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 33.4 bila

kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 15-5.**

**Jedwali Na.15-5: Miradi Iliyotekelezwa Bila Kufanya Athari za Mazingira**

| Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Dar Es Salaam | 28,030,161,949 |
| 2. | Kigoma | 4,079,498,343 |
| 3. | Songwe | 1,290,000,000 |
| | **Jumla** | **33,399,660,292** |

Miongoni mwa sababu zilizopelekea kutekelezwa kwa miradi bila kufanyika kwa tathmini ya athari za mazingira, ni fedha za utekelezaji wa miradi kutohusisha gharama za kufanya tathmini ya athari za mazingira na kuanza utekelezaji wa mradi bila kufanya hatua muhimu za awali.

Utekelezaji wa miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira unaziweka Sekretarieti za Mikoa katika hatari za kupata athari za mazingira ambazo zinaweza kuathiri jamii katika maeneo husika, na hatimaye kusababisha matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

**Ninashauri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe Sekretarieti za Mikoa zinafanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha eneo linafaa na mradi ni endelevu, ili kuepuka madhara yanayotokana na athari za mazingira.**

### 15.2.3 Nyongeza ya Kazi Isiyoidhinishwa yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.02

Kanuni ya 110(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 (na Marekebisho yake ya Mwaka 2016) na Sehemu ya 24.2 ya Mwongozo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (GL/05/2020/FA) kwa ajili ya kutekeleza kazi chini ya *"force account"*, zinahitaji tofauti zilizopendekezwa zipelekwe kwenye bodi ya zabuni kwa ajili ya kuidhinishwa, maelekezo yatolewe kwa mzabuni, vifaa vya ujenzi vikidhi vigezo na vipimo viidhinishwe na Meneja wa Mradi.

Nilibaini kuwa, malipo ya shilingi bilioni 1.02 yalilipwa na Sekretarieti nne za Mikoa kinyume na Kanuni na Mwongozo tajwa hapo juu. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 225.12 zililipwa kwa ajili ya ununuzi wa

vifaa vya ujenzi zaidi ya idadi iliyoidhinishwa, na shilingi milioni 790.79 zililipwa kwa mkandarasi kwa Cheti cha malipo bila nukuu ya bei husika kuidhinishwa na bodi ya zabuni. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali 15-6**.

**Jedwali Na.15-6: Nyongeza ya kazi isiyoidhinishwa**

| Na. | Jina la Sekretarieti | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Dar es salaam | 790,787,721 |
| 2. | Mbeya | 129,492,660 |
| 3. | Kigoma | 87,705,900 |
| 4. | Morogoro | 7,920,000 |
| | **Jumla** | **1,015,906,281** |

Hii inaweza kuwa imesababishwa na kutofanyika mipango sahihi ya miradi, au imefanywa kwa makusudio ya kukiuka udhibiti wa ndani wa kuidhinisha mabadiliko ya kazi yanayotokea.

Malipo ya vifaa tofauti na ilivyoidhinishwa, yanaweza kusababisha mkandarasi kulipwa zaidi ya kazi alizozifanya.

**Ninaishauri Menejimenti ya Sekretarieti za Mikoa kufanya tathmini ya kifedha ya miradi, ili kubaini kiwango cha mwisho cha mkataba kinachotarajiwa na kupata kibali kwa tofauti zitakazojitokeza kwa mujibu wa Kanuni ya 110(5) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 (Na marekebisho yake ya 2016) na Sehemu ya 24.2 ya Mwongozo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma.**

## 15.3 Tathmini ya Miradi ya Maendeleo Inayotekelezwa Chini ya Sekretarieti za Mikoa

### 15.3.1 Miradi yenye Thamani ya Shilingi Milioni 548.76 Iliyokamilika bila kutumika

Nilibaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi, ilikamilisha ujenzi wa nyumba sita za watumishi zenye thamani ya shilingi milioni 548.76, ambazo hata hivyo hazikutumika kama ilivyokusudiwa.

Sababu kubwa ilikuwa ni Menejimenti kutochukua hatua stahiki ili kuhakikisha maofisa waliostahili, wanahamia kwenye nyumba hizo, na pia kulikuwa na mipango isiyoridhisha katika hatua ya awali ili kuhakikisha miradi hiyo inakamilika na kutumika ipasavyo; jambo ambalo linaweza kuathiri ubora wa nyumba hizo na kusababisha gharama za ziada za kuzikarabati kabla ya kuanza kutumika.

**Ninaishauri Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi ihakikishe mipango ya miradi inafanywa vizuri na miradi iliyokamilika inapaswa kutumika ili kufanikisha makusudio pamoja na kupata thamani ya fedha zilizotumika katika miradi.**

### 15.3.2 Vifaa vya ujenzi vilivyotelekezwa Uwanja wa Ndege Mwanza vyenye thamani ya Shilingi Milioni 233.46

Ujenzi wa Jengo la Uwanja wa Ndege Mwanza ulikadiriwa kugharimu shilingi bilioni 13.25 na ujenzi ulipangwa kuanza tarehe 19 Septemba 2019 na kukamilika tarehe 30 Mei 2020.

Nilibaini kuwa, Sekretarieti ya Mkoa ilipokea jumla ya shilingi bilioni 12.29 kutoka vyanzo mbalimbali kama ilivyoneshwa katika **Jedwali Na. 15-7.**

**Jedwali Na.15-7: Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Uwanja wa Ndege Mwanza**

| Ilipokelewa kutoka | Kiasi (Sh.) |
|---|---|
| Wizara ya Fedha | 9,469,465,477 |
| H/M Ilemela | 1,420,000,000 |
| H/Jiji Mwanza | 1,400,000,000 |
| **Jumla** | **12,289,465,477** |

Zaidi ya hilo, nilibaini kuwa kufikia Disemba 2022, shughuli za ujenzi katika mradi huo zilikuwa zimesimama. Hata hivyo, vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa vyenye thamani ya shilingi milioni 233.46 vilitelekezwa katika eneo hilo kwa kipindi cha kuanzia miezi 6 hadi 24, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 15-8.**

**Jedwali Na.15-8: Vifaa vya ujenzi vilivotelekezwa uwanja wa Ndege Mwanza**

| Vifaa vilivyonunuliwa | Vipimo | Kizio | Idadi | Kiasi (Sh.) | Jumla (Sh.) | Leja |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Vigae vya sakafu | 60*60 | Boxes | 1195 | 52,542 | 62,788,049 | Haijaoneshwa |
| Ubao wa Saruji na Nyuzi | | PC | 777 | 50,000 | 38,850,000 | SA/2/99 |
| Bati MM- Ando | 6mm | PC | 226 | 108,000 | 24,408,000 | SA/2/16 |
| Bati G28 -Ando | 7.2mm | PC | 184 | 129,600 | 23,846,400 | SA/2/1 |
| Vigae vya sakafu | 40*40 | Boxes | 897 | 25,442 | 22,821,806 | Haijaonyeshwa |
| Nondo | 16mm | | 313 | 50,415 | 15,779,973 | SA/2/63 |
| Nondo | 8mm | | 972 | 13,337 | 12,963,846 | SA/2/61 |
| Saruji | 42.5 | bags | 568 | 20,000 | 11,360,000 | SA/2/107 |
| Vigae vya Ukutani | 25*40 | | 457 | 19,500 | 8,911,500 | SA/2/44 |

| Vifaa vilivyonunuliwa | Vipimo | Kizio | Idadi | Kiasi (Sh.) | Jumla (Sh.) | Leja |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Rangi ya Mafuta "silk" | 20Lts | EA | 34 | 150,450 | 5,115,300 | SA/2/70 |
| Vigae vya sakafu | 25*40 | Boxes | 168 | 19,500 | 3,276,000 | Haijaonyeshwa |
| Rangi ya Nje "weather guard" | 20Lts | EA | 13 | 132,700 | 1,725,100 | SA/S/72 |
| Nondo | 12mm | | 56 | 28,795 | 1,612,515 | SA/2/62 |
| **Jumla** | | | | | **233,458,488** | |

Kukosekana kwa mpango na usanifu majengo ulioidhinishwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na kutoshirikishwa kwa wadau muhimu, kulisababisha marekebisho ya mara kwa mara ya miundo mbinu ya ujenzi hivyo kusababisha kusimamishwa kwa ujenzi huo tangu Juni 2022.

**Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na TAA wanapaswa kutatua kero zinazohusu ujenzi wa kituo cha uwanja wa ndege Mwanza ili kuruhusu kukamilika kwa mradi huo na kuepuka hasara inayoweza kutokea kwa vifaa vilivyonunuliwa kupoteza ubora wake.**

### 15.3.3 Kuanzishwa kwa Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 9 bila Kupata Hati Miliki

Kifungu 29(1) (b) cha Sheria ya Ardhi Na. 4 Sura ya 334, 1999 kinaeleza kuwa, kamishna ataamua kutoa haki ya kurasmisha ardhi kwa mtu ambaye anaimiliki au kutoa haki ya kumiliki ardhi kwa kumpa cheti kinachoitwa Cheti cha umiliki wa ardhi.

Nilibaini kuwa, Sekretarieti tatu za Mikoa zilitekeleza miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 9 bila kupata hati miliki kutoka kwa kamishna wa ardhi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 15-9.**

**Jedwali Na.15-9: Kuanzishwa kwa Miradi Bila Kuwa na Hati Miliki**

| Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Kigoma | 4,079,498,343 |
| 2. | Songwe | 2,952,000,000 |
| 3. | Shinyanga | 1,973,000,000 |
| | **Jumla** | **9,004,498,343** |

Nilibaini kuwa, utekelezaji wa mradi kabla ya kupata hati miliki ulitokana na jitihada zisizoridhisha za Sekretarieti za Mikoa za kupima ardhi inazozimiliki. Hali hii inaweza kusababisha upotevu wa mali za

umma endapo kutatokea migogoro ya kisheria na Sekretarieti za Mikoa zikashindwa kesi hizo kutokana na kukosekana kwa umiliki wa kisheria.

**Ninapendekeza kwamba, katika siku zijazo Menejimenti ya Sekretarieti zipate hati miliki za maeneo kabla ya kuanzisha miradi ili kuepusha migogoro ya ardhi na upotevu wa fedha. Pia, zichukue hatua stahiki kuhakikisha kuwa maeneo yote ya ardhi yanayomilikiwa na Sekretarieti yanapimwa na kupata hati miliki kutoka kwa Kamishna wa ardhi.**

### 15.3.4 Miradi iliyochelewa kukamilika yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 8.11

Nilibaini kuwa, miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 8.11 iliyotekelezwa na Sekretarieti nane za Mikoa haikukamilika mpaka kufikia Disemba 2022.

Kuchelewa kukamilika kwa miradi hii kunaweza kuwa kumetokana na mipango isiyoridhisha, usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa Sekretarieti za Mikoa, ucheleweshwaji na kutolewa kwa fedha pungufu na jamii kutokuwa na mwamko kwenye kuchangia miradi ya maendeleo. Hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kutokana na mfumuko wa bei, pia inainyima jamii inayowazunguka kupata faida zilizokusudiwa kutokana na mradi huo.

Maelezo kama yanavyooneshwa kwenye **Kiambatisho 15-1.**

**Menejimenti ya Sekretarieti husika, inapaswa kutathmini kazi zilizosalia za miradi ambayo haijakamilika na kuandaa mikakati ya kukamilika kwake ili kuepuka gharama zisizo za lazima.**

## 15.4 Mfuko wa Afya ya Jamii Uliboreshwa

### 15.4.1 Madai yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 2.94 ya Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa hayajalipwa.

Aya 1.2.5 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Fedha na Uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF) uliotolewa Aprili, 2019 inaeleza kuwa, malipo ya Tele kwa Tele yatazingatia mwongozo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na yatalipwa moja kwa moja katika akaunti ya pamoja iliyopo Benki Kuu. Baada ya maombi ya Mkoa ya

Tele kwa Tele kuidhinishwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Katibu Mkuu OR-TAMISEMI atajulishwa kiasi cha fedha kilichoingizwa katika akaunti ya pamoja na mchanganuo wa kila Mkoa.

Nilibaini kuwa, Sekretarieti nne za Mikoa zilikuwa zinadai jumla ya shilingi bilioni 2.94 kama malipo ya Tele kwa Tele, lakini madai hayo hayakulipwa. Aidha, nilibaini kuwa mwongozo wa Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa hauzungumzii hasa ni chombo gani kati ya Serikali Kuu na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kinahusika na kuuwezesha Mfuko wa Pamoja wa Afya. Maelezo yanaoneshwa kwenye **Jedwali 15-10.**

**Jedwali Na.15-10: Madai ya iCHF ambayo hayajlipwa**

| Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Dodoma | 2,288,959,999 |
| 2. | Kagera | 281,010,000 |
| 3. | Manyara | 208,200,000 |
| 4. | Ruvuma | 162,335,000 |
| **Jumla** | | **2,940,504,999** |

Hii inaashiria kutozingatiwa kwa Mwongozo wa afya ambao unaitaka Serikali kuchangia Mfuko wa Pamoja wa Afya, hivyo kuathiri huduma za afya zinazotolewa na vituo vya afya na kuongeza gharama za matibabu kwa Halmashauri husika.

**Ninapendekeza kwamba, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ihakikishe fedha za Mfuko wa afya ya Jamii zinatolewa ili kusaidia Sekretarieti husika kutekeleza shughuli za afya kama zilivyopangwa.**

## 15.5 Utekelezaji wa Miongozo ya Bajeti

### 15.5.1 Fedha za Maendeleo Zilizotumika kwa Lengo Lisilokusudiwa Shilingi Bilioni 1.10

Kifungu. 27 (4) ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, kinataka vibali vilivyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi vitumike tu kwa mujibu wa lengo lililokusudiwa, na ndani ya kiwango kilichowekwa kwenye makadirio.

Hata hivyo, nilibaini kuwa fedha za Maendeleo zenye thamani ya shilingi bilioni 1.10 zilibadilishiwa matumizi bila kibali kutoka

Mamlaka husika. Maelezo ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali 15-11 .**

**Jedwali Na.15-11: Fedha za Maendeleo kutumika kwa Lengo lisilokusudiwa**

| Na. | Jina la Mkoa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Iringa | 615,827,856 |
| 2 | Rukwa | 260,000,000 |
| 3 | Kagera | 105,418,520 |
| 4 | Njombe | 80,000,000 |
| 5 | Shinyanga | 34,443,700 |
| | **Jumla** | **1,095,690,076** |

Kutumia fedha za maendeleo kutekeleza shughuli zisizokusudiwa kunaathiri shughuli zilizokusudiwa na kufanya shughuli hizo zitekelezwe kwa sehemu au kutotekelezwa kabisa.

**Ninapendekeza kuwa, OR-TAMISEMI ifanye uchunguzi kuhusu fedha za maendeleo zilizobadilishiwa matumizi ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zililipwa kwa shughuli halali, na kuchukua hatua stahiki kwa maofisa wote wanaohusika kubadilisha matumizi ya fedha za maendeleo bila kibali.**



# SURA YA KUMI NA SITA

# OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## 16.0 Utangulizi

Sura hii inazungumzia masuala yaliyojitokeza katika ukaguzi wa TAMISEMI (Fungu 56) na taasisi zilizo chini yake. TAMISEMI ilianzishwa chini ya Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Majukumu ya Wizara ni kusimamia utawala bora wa maendeleo ya mikoa na kuratibu sera, mikakati na shughuli za Sekretarieti za Mikoa, vijijini na mijini.

Wizara pia inalenga kujenga uwezo wa kiutawala wa serikali za mitaa na kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali kuu na serikali za mitaa ili kugatua madaraka katika ngazi za vijii na mitaa na hatimaye kuboresha maisha ya Watanzania.

Taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ni pamoja na Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka (DART), Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI), Mfuko wa Barabara, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa(LGLB), Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Nilifanya ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) na taasisi nyingine zilizo chini yake na kubaini yafuatayo:

## 16.1 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)

Aya hii inaangazia masuala ya ukaguzi wa OR-TAMISEMI. Katika ukaguzi, nilbaini mapungufu yafuatayo:

### 16.1.1 Kutotekelezwa kikamilifu kwa Shughuli zilizopangwa na TAMISEMI kuhusu Ufuatiliaji na Usimamizi wa Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa

Nilipitia mpango wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na TAMISEMI pamoja na taarifa za utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2021/22 na kubaini kuwa, TAMISEMI ilikuwa na jumla ya shughuli 205 zilizopangwa kutekelezwa na menejimenti kupitia idara na vitengo mbalimbali vilivyo chini ya Wizara.

Hata hivyo hadi kufikia mwisho wa mwaka, shughuli 93 za ufuatiliaji na usimamizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa sawa na asilimia 89 ya mpango zilitekelezwa kikamilifu huku shughuli 82 za ufuatiliaji na usimamizi wa Sekretarieti za Mikoa zikitekelezwa kwa sehemu sawa na asilimia 82 ya mpango. Kwa ujumla, Menejimenti ya TAMISEMI imeweza kutekeleza shughuli 175 kati ya shughuli 205 zilizopangwa ikimaanisha kuwa shughuli 30 sawa na asilimia 15 hazikutekelezwa kama ilivyoainishwa katika **Jedwali 16-1** hapa chini.

**Jedwali Na.16-1: Hali ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa**

| Maelezo | Number of activities implemented | Idadi ya shughuli zilizopangwa | % |
|---|---|---|---|
| Shughuli zilizotekelezwa kikamilifu (ufuatiliaji na usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa) | 93 | 105 | 89 |
| Shughuli zilizotekelezwa kwa sehemu (Ufuatiliaji na usimamizi wa Sekretarieti za Mikoa) | 82 | 100 | 82 |
| **Jumla** | **175** | **205** | **85** |

***Chanzo***: *Mpango kazi wa mwaka wa TAMISEMI na taarifa za utekelezaji*

Matukio yasiyotarajiwa ikiwa ni pamoja na ufinyu wa bajeti yalipelekea kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa. Kutokamilika kwa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za ufuatiliaji na usimamizi wa Serikali za Mitaa na Sekretarieti za Mikoa kunaweza kuikosesha jamii iliyokusudiwa kunufaika na malengo yaliyotarajiwa.

**Ninapendekeza kwa Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe inaweka mikakati bora ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutosha na mipango sahihi ili kuhakikisha kuwa shughuli zote zilizopangwa zinatekelezwa kikamilifu.**

### 16.1.2 Fedha za Malipo ya Awali zisizo na Dhamana katika Mradi wa Ujenzi wa Jengo la TAMISEMI Shilingi Bilioni 1.83

Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilifanya malipo ya awali ya shilingi bilioni 3.04 kwa mkandarasi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais TAMISEMI katika Jiji la Serikali-Mtumba, Dodoma baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo ya awali kuanzia tarehe 6 Oktoba 2021 hadi 5 Oktoba 2022.

Nilibaini kuwa malipo ya awali yalirejeshwa kwa asilimia 40 ikimaanisha kuwa asilimia 60 ya fedha za malipo ya awali sawa na shilingi bilioni 1.83 zilikuwa bado hazijarejeshwa wakati dhamana iliyowasilishwa ilikuwa imekwisha muda wake na haikuhuishwa.

Usimamizi dhaifu wa mkataba kutoka kwa meneja wa mradi ulisababisha kiasi cha shilingi bilioni 1.83 kutokuwa na dhamana ambazo zinaweza kupotea endapo mkandarasi atashindwa kutimiza wajibu wake.

**Ninashauri Ofisi ya Rais TAMISEMI ihakikishe kuwa dhamana ya malipo ya awali kwa mradi unaoendelea inawasilishwa ili kufidia asilimia 60 iliyobaki ya kiasi ambacho hakijarejeshwa. Aidha, Menejimenti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI inasisitizwa kuimarisha udhibiti wa ndani katika usimamizi wa mikataba juu ya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa mkandarasi anahuisha dhamana ya utendaji kazi kabla ya muda wake kwisha. Hii inafanywa kwa kuwakumbusha wakandarasi mapema.**

### 16.1.3 Dhamana ya Utendaji Kazi iliyoisha Muda wake Kabla ya Kukamilika kwa Mradi Shilingi Bilioni 20.29

Kanuni ya 29(1) na (2) ya Kanuni za ununuzi wa Umma, 2013 ililazimu uwasilishaji wa dhamana ya utendaji kazi ili kuhakikisha utendakazi wa uaminifu wa mkataba. Kwa hivyo, ni wajibu wa taasisi ya ununuzi kubainisha katika hati ya maombi mahitaji yoyote kuhusiana na mtoaji na asili, fomu, kiasi na sheria na masharti mengine kuu ya usalama wa utendaji unaohitajika

Aidha, kanuni ndogo ya 29(6) inaeleza kuwa, dhamana ya utendaji itatunzwa na taasisi nunuzi hadi kukamilika kwa mkataba na itatolewa baada ya kutolewa kwa cheti cha kukubali ripoti ya mwisho au cheti cha kukamilika kwa kazi. au huduma ikiwa hakuna dai lililowasilishwa dhidi ya mzabuni, mdhamini wa kandarasi au kampuni ya mdhamini.

Nilibaini kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI iliingia mkataba wa shilingi bilioni 20.29 na Mkandarasi wa ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TAMISEMI katika Jiji la Serikali-Mtumba, Dodoma. Mkandarasi aliwasilisha dhamana ya utendaji kazi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.03 ambayo muda wake uliisha tarehe 27 Oktoba 2022.

Hata hivyo, nilibaini kuwa, mradi ulikuwa bado haujakamilika na dhamana ya utendaji kazi ilikuwa haikuhuishwa ikimaanisha mradi ulikuwa ukiendelea kutekelezwa bila ya kuwa na dhamana ya utendaji.

Kasoro niliyobaini ilitokana na udhibiti duni katika usimamizi wa mradi na mikataba unaofanywa na meneja wa mradi. Aidha, kukosekana kwa dhamana hai ya utendaji kazi kwa mradi unaoendelea kunaashiria kushindwa kwa menejimenti ya TAMISEMI kusimamia ipasavyo, jambo ambalo linaiweka Wizara katika hatari ya upotevu wa fedha iwapo mkandarasi atashindwa kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

**Ninapendekeza kwamba, Menejimenti ya OR-TAMISEMI iwasiliane na wakandarasi ili kuwasilisha dhamana halali ya utendaji kazi katika mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya TAMISEMI. Aidha, Menejimenti ya TAMISEMI inapaswa kuhakikisha kuwa inafuatilia dhamana ya utendaji kazi katika kipindi chote cha mradi kuhakikisha kuwa mradi unakuwa na dhamana hai.**

### 16.1.4 Uhamisho wa Watumishi Bila Kulipwa Stahiki zao Kiasi cha Shilingi Milioni 189.24

Nilibaini kuwa Menejimenti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ilishindwa kulipa shilingi milioni 189.24 kwa watumishi 33 kama stahiki za kuhamishwa kutoka ofisi mbalimbali za serikali kwenda TAMISEMI kinyume na Kanuni ya L.5 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2019 inayohitaji Posho ya kujikimu kulipwa kwa Mtumishi wa Umma, mke na mume, watoto au wategemezi kwa usiku ambao lazima itumike katika safari za kwenda kituo kipya .

Ni muhimu kwa OR-TAMISEMI kuhakikisha stahiki zote za wafanyakazi zinalipwa kwa wakati na kwa usahihi ili kudumisha mazingira mazuri ya kazi na kuzingatia matakwa ya kisheria.

Kutolipa stahiki za wafanyakazi baada ya uhamisho kunaweza kumsababishia mtumishi kuwa na mazingira magumu ya utekelezaji

wa majukumu yake,pia, kuleta taswira mbaya ya ongezeko la madeni ya Serikali.

**Ninapendekeza kuwa Menejimenti ya TAMISEMI kuhakikisha kuwa stahiki za uhamisho zinazodaiwa na watumishi hao 33 zinalipwa kwa wakati. Aidha, Ofisi ya Rais TAMISEMI inashauriwa kuweka utaratibu mzuri na udhibiti sahihi ili kuhakikisha kuwa stahili zote za watumishi zinalipwa kwa kadri zinavyotokea kwa mujibu wa sheria na kanuni.**

## 16.2 Mfuko wa Barabara

Mfuko wa Barabara ulianzishwa mwaka 1998 kwa kutunga Sheria ya Ushuru wa Barabara .Wakala wa utekelezaji ni TANROADS kwa upande wa barabara kuu, za mikoa na TARURA kwa upande wa barabara za Wilaya na Mijini ambapo asilimia 70 ya fedha zimetengwa kwa barabara kuu na za Mikoa na asilimia 30 kwa barabara za wilaya, mijini na barabara kuu.

TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi zimekuwa zikitekeleza shughuli za Mfuko wa Barabara kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara tangu mwaka 2000/01. Mpango kazi huo unatokana na Mkataba wa Utendaji kazi uliotiwa saini kati ya Bodi ya Mfuko wa Barabara na Ofisi ya Rais TAMISEMI, unaolenga kuzisaidia Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi nyingine zinazoshirikiana nayo katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mapitio ya Mfuko wa Barabara, uliofanywa na Ofisi ya Rais TAMISEMI, nilibaini mambo yafuatayo:

### 16.2.1 Fedha za Mradi zilizokopeshwa kwa Manispaa ya Kinondoni na TAMISEMI Pasipo Kurejeshwa kwa Muda Mrefu Shilingi Bilioni 2.15

Kifungu cha III (3.3) cha Makubaliano ya Utendaji Kazi kwa mwaka 2021/22 kinamtaka Katibu Mkuu wa TAMISEMI kuwajibika kwa fedha za barabara zinazopokelewa na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa ajili ya shughuli kulingana na bajeti yampango wa uendeshaji.

Nilibaini kuwa tarehe 8 Oktoba 2017, Mfuko wa Barabara ulitoa mkopo wa shilingi bilioni 2.52 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, ambayo marejesho yake yalipaswa kufanywa kikamilifu kabla ya

tarehe 30 Septemba 2018. Hata hivyo shilingi milioni 450 pekee ndicho kilichorejeshwa kufanya kiasi kilicho salia kurejeshwa kuwa ni shilingi bilioni 2.07 .

Aidha, nilibaini kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI ilikopa shilingi milioni 82.99 kwa ajili ya shughuli zisizojulikana zilizotolewa maelezo kuwa ni kwa ajili ya "kazi maalumu". Fedha hizo nazo hazikurejeshwa kwa zaidi ya miezi 10, hivyo kufanya jumla ya fedha za mradi zilizokopwa na Manispaa ya Kinondoni na TAMISEMI kuwa shilingi bilioni 2.15.

Kasi ndogo ya urejeshaji wa madeni yaliyokaa muda mrefu inasababishwa na usimamizi duni katika ukusanyaji wa madeni na wadaiwa kutotimiza masharti ya mikataba ya ulipaji. Hii inatia shaka kwani inaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli za barabara zilizopangwa.

**Ninapendekeza kwamba, Menejimenti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ifuatilie kwa karibu ili kuhakikisha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inarejesha kiasi cha mkopo kilichobaki cha shilingi bilioni 2.07. Aidha, OR-TAMISEMI inashauriwa kurejesha kiasi cha fedha inachodaiwa na Mfuko wa Barabara.**

### 16.2.2 Ununuzi wenye Thamani ya Shilingi 183.8 uliofanyika Nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki

Kanuni ya 342 ya Kanuni ya ununuzi wa Umma ya mwaka 2013, inazitaka taasisi za ununuzi kutekeleza manunuzi ya kielektroniki kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa umma. Pia, Serikali ilitoa agizo kupitia barua yenye Kumb Na. EB/AG/485/01/Vol. XII ya tarehe 23 Oktoba 2019 kwa taasisi zote za ununuzi za serikali kuunganisha na kutumia ipasavyo mfumo ulioanzishwa wa ununuzi unaojulikana kama Mfumo wa Kitaifa wa Ununuzi wa Kielektroniki Tanzania (TANePS) kuanzia tarehe 1 Januari 2020.

Ukaguzi wa miamala ya ununuzi uliofanywa na Mfuko wa Barabara, nilibaini kuwa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi.milioni 183.8 zilinunuliwa bila kutumia mfumo wa TANePS.

**Menejimenti ya OR-TAMISEMI inashauriwa kuhakikisha kwamba, katika siku zijazo, miamala ya ununuzi wa Mfuko wa Barabara inafanyika kupitia TANePS ili kuongeza haki, uwazi na uchumi katika mchakato wa ununuzi.**

## 16.3 Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi (DART)

Wakala wa Mabasi Yaendayo Kasi (DART) ni taasisi yenye mamlaka ya kuanzisha na kuendesha mfumo wa mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam. Taasisi hii ilianzishwa kupitia Tangazo la Serikali (G.N. 120) la tarehe 25 Mei 2007 chini ya Sheria ya Wakala Tendaji namba 30 ya 1997.

Jukumu kubwa la DART ni uanzishaji na kuendesha mfumo wa mabasi yaendayo haraka kwa Dar es Salaam, na unalenga kufikia malengo mbalimbali yakiwemo; uanzishaji na uendeshaji wa mfumo wa mabasi yaendayo haraka kwa Dar es Salaam, kuhakikisha kunakuwepo na mpangilio mzuri wa magari katika mitaa ya mjini na barabarani ukisimamiwa na Wakala chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).Katika ukaguzi nilibaini udhaifu ufuatao unaohusu Wakala:

### 16.3.1 Malipo yenye Risiti za EFD za Kughushi Shilingi Milioni 135.82

Kanuni ya 48 ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi za Mwaka 2016 inasema, "Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anachezea au kusababisha Kifaa cha Kielektroniki kufanya kazi vibaya, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi 100 au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja."

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa Wakala alifanya malipo ya jumla ya shilingi milioni 135.82 kwa wauzaji mbalimbali ambapo walipatiwa risiti za kielektroniki. Hata hivyo, wakati wa uthibitisho wa uhalali wa risiti hizo kupitia mfumo wa TRA, ilibainika kuwa risiti hizo zilikuwa za kughushi.

Kuambatisha risiti za EFD za kughushi kunamaanisha kuwa, taarifa za mauzo kwenye miamala iliyothibitishwa na risiti za kughushi za EFD hazikufika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA),kwa hivyo, kodi stahiki haiwezi kukusanywa na Serikali.

**Ninapendekeza kuwa Menejimenti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kuchukua hatua stahiki dhidi ya wahusika walioghushi risiti za kielektroniki (EFD) katika malipo ya shilingi milioni 135.82.**

### 16.3.2 Utendaji Duni wa Kampuni ya Uendeshaji wa Mabasi yaendayo Kwa Kasi (BRT) uliosababisha Deni la Shilingi Bilioni 8.45

DART iliingia makubaliano na Mtoa Huduma ambae ni UDA Rapid Transit Plc (UDART). Mkataba unamtaka Msimamizi/TSP wa Mabasi Yaendayo Kwa Kasi (BRT) kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa abiria, na kushindwa kufikia viwango vya utendaji kazi inapelekea adhabu.

Nilibaini kuwa kampuni ya uendeshaji ya UDART hakufikia viwango vya utendaji vilivyotakiwa na kusababisha kutozwa faini, ada na riba ya shilingi bilioni 2.23 katika mwaka wa fedha 2021/22 kuongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka shilingi milioni 731.42 kwa mwaka 2019/20 ikimaanisha udhaifu huo haujafanyiwa kazi ipasavyo na menejimenti ya DART.

Usimamizi dhaifu wa wa BRT umesababisha malimbikizo ya madeni kufikia shilingi bilioni 8.45 ambayo hayakurejeshwa na UDART kwa mwaka 2021/22 kutoka bilioni 4.17 mwaka 2019/20..

Kutokamilika kwa uwekaji wa Mfumo wa Usafiri wa ITS kunapelekea utendaji duni wa huduma za kawaida kwa BRT kupunguza utoaji wa huduma zilizokusudiwa za usafiri wa mabasi yaendayo kasi, na kusababisha malalamiko kutoka kwa abiria na hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Ninapendekeza kuwa, Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Menejimenti ya DART kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa karibu wa uendeshaji wa mtoa huduma wa mpito (TSP) kwa kuhakikisha kuwa mfumo wa ITS unatumika ili kuimarisha utoaji wa huduma bora za usafiri wa umma. Aidha, vigezo vyote vya tathmini ya kiwango cha utendaji vilivyotolewa na msimamizi vinapaswa kutekelezwa ili kufikia viwango vya uendeshaji wa mabasi yaendayo haraka. Pamoja na hayo, ada, faini na riba zilizowekwa kutokana na kutofuata vigezo muhimu vya utendaji kazi zikusanywe ili kuepuka upotevu wa madeni.**

### 16.3.3 Magari ya Wakala Ambayo Hayajakatiwa Bima Shilingi Bilioni 1.02

Kanuni ya 9.1 ya Kanuni za Fedha za DART na Aya ya 24 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma [uliorekebishwa mwaka 2019] inamtaka Mtendaji Mkuu wa DART kuhakikisha kuwa magari yanalindwa dhidi ya wizi, hasara, matumizi mabaya na hivyo kuyawekea bima.

Kinyume na sheria hiyo, niliona kuwa Wakala ana pikipiki moja na magari tisa ambayo yalinunuliwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.02, hata hivyo, magari hayo hayakuwa na bima. Pia, nilibaini kuwa gari moja lilipata ajali mnamo tarehe 23 Julai 2022 halikufanyiwa matengezo.

Magari kutokatiwa bima kunayaweka katika hatari ya kushindwa kulipiwa fidia katika matukio ya ajali. Aidha, gari lililopata ajali, lingelikuwa limekatiwa bima, bila shaka lingeshafanyiwa matengenezo kwa kutumia bima hiyo.

**Ninapendekeza kwa Menejimenti ya Wakala ihakikishe inatengwa, bajeti ya kutosha kwa ajili ya bima ya magari ya Wakala ili kuyalinda magari dhidi ya hatari ya kushindwa kufidiwa pindi yanapopata ajali. Aidha, Menejimenti inasisitizwa izingatie matakwa ya Aya ya 24 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma (kama ilivyorekebishwa mwaka 2019).**

## 16.4 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)

Tume ya Utumishi wa Walimu ilianzishwa chini ya Sheria namba 25 ya mwaka 2015 Kifungu cha 5, kama Tume huru ya serikali yenye jukumu la usimamizi wa rasilimali watu katika sekta ya elimu.

Majukumu yake ni pamoja na kutunza daftari la walimu wenye sifa, kuajiri na kuweka walimu waliosajiliwa, kuwezesha maendeleo ya kitaaluma na uhamisho wa walimu, kusimamia hatua za kinidhamu dhidi ya walimu, kutathmini uwiano baina ya mgawanyoi na mahitaji ya walimu, na kutoa mwongozo kwa Serikali kuhusu masuala yanayohusu taaluma ya ualimu.

Wakati wa ukaguzi wa Tume, mapungufu kadhaa yaliyobainika ambayo yanahitaji kuchukuliwa hatua kwa haraka. Mapungufu hayo ni pamoja na uhaba wa usajili wa walimu wenye sifa, upangaji wa kutosha wa

walimu waliosajiliwa, ucheleweshaji wa kushughulikia masuala ya nidhamu, changamoto katika kutathmini uwiano wa ugavi na mahitaji ya walimu, na miongozo ya kutosha kwa Serikali kuhusu masuala yanayohusu taaluma ya ualimu.

Mapungufu hayo yanadhoofisha ufanisi wa Tume katika kutekeleza majukumu yake. Hatua za kurekebisha lazima zichukuliwe ili kuboresha ubora wa utoaji huduma.

### 16.4.1 Ucheleweshaji wa Utoaji Maamuzi ya Rufaa kutoka kwa Walimu

Kifungu cha 5(e) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, 2015 kinasema kuwa TSC ina wajibu wa kuamua rufaa kutokana na maamuzi ya mamlaka za nidhamu, na Kifungu cha 13(2) cha sheria hiyo kinaelekeza kuwa walimu ambao hawajaridhishwa na uamuzi wa Tume. ngazi ya Wilaya, kukata rufaa kwa Tume. Zaidi ya hayo, Kanuni ya 62(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022 inataka rufaa ikamilishwe ndani ya siku 90 baada ya kupokea uwakilishi wa rufaa kutoka kwa mamlaka za nidhamu.

Ukaguzi wangu umebaini kuwa, kati ya rufaa 198 zilizopokelewa katika mwaka wa fedha 2021/22, rufaa 22 zilikuwa bado hazijaamuliwa. uchunguzi zaidi, umeonesha kuwa, rufaa tisa ziliamuliwa nje ya siku 90 baada ya kupokea rufaa kutoka kwa mamlaka za nidhamu, ikimaanisha kukosekana kwa ufanisi kutokana na kuchelewa kukamilika kwa rufaa ambapo rufaa zilitumia siku 120 hadi 166 kukamilishwa.

Kutokamilika kwa wakati kwa maamuzi ya rufaa kwa wakati kutoka kwa walimu waliotuhumiwa, kunachangiwa na idadi ndogo ya vikao vinavyofanywa na Makamishina na mapungufu ya kutosajili kwa wakati rufaa zinazopokelewa kutoka kwa walimu.

**Ninapendekeza kwamba Menejimenti ya Tume ya Utumishi ya Walimu ihakikishe kwamba rufaa ambazo hazijaamuliwa zinakamilishwa na kuamuliwa kwa wakati kama inavyohitajika na pia kuomba fedha zaidi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kuongeza idadi ya vikao vitakavyowawezesha kufanya maamuzi ya rufaa kutoka kwa Walimu kwa wakati.**

## 16.5 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) ilianzishwa chini ya kifungu cha 56 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura. 290.

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ina jukumu la kutoa mikopo kwa serikali za mitaa nchini Tanzania ili kufadhili miradi ya miundombinu kama vile barabara, madaraja, shule na vituo vya afya. Jukumu la Bodi ni kuhakikisha kuwa serikali za mitaa zinapata mikopo nafuu ili kufadhili mipango yao ya maendeleo.

Wakati wa ukaguzi nilibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na menejimenti:

### 16.5.1 Kushindwa Kusimamia Dhamana ya Mikopo Ili Kufidia Kiasi cha Mikopo Isiyolipika Shilingi Bilioni 2.35

Aya ya 9(2) ya Mkataba wa Mkopo kati ya Bodi na Mamlaka za Serikali za Mitaa inataka kwamba katika matukio ya kushindwa kufanya marejesho ya mkopo, Bodi ina mamlaka ya kusimamia dhamana (mali ya kudumu) ambayo mkopo huo unadhaminiwa kwa madhumuni ya kukusanya mapato ili kufidia kiasi chote cha mkopo ambacho bado hakijalipwa na riba yake.

Nilibaini kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa tano zilikuwa na mikopo isiyolipwa ya jumla ya shilingi bilioni 2.35, mikopo hiyo hakuirejeshwa kwa zaidi ya miezi 25, kinyume na mikataba yao ya mikopo. Aidha, Bodi ya Mikopo haikuchukua hatua za kutosha kutekeleza mikataba ya dhamana iliyodhamini mikopo hiyo, ambayo ingeweza kusaidia kurejesha mikopo ambayo haikulipika na riba husika, kama ilivyoainishwa katika mikataba ya mikopo. Maelezo zaidi ya mikopo inayodaiwa kwa muda mrefu yanaonyeshwa kwenye **Jedwali 16-2.**

**Jedwali Na.16-2: Kutosimamia dhamana ya mikopo ili kufidia mikopo isiyolipika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Tarehe mkopo ulipotolewa | Tarehe ya mwisho ya kulipa mkopo | Dhamana ya mkopo | Kiasi cha mkopo na riba (Sh.) | Salio la mkopo (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Kishapu | 17/01/2017 | 19/11/2020 | Kituo cha Mabasi Kishapu | 1,028,799,993 | 1,007,069,503 |
| 2 | H/W Ruangwa | 27/07/2019 | 04/02/2021 | Jengo la Ghala na Uwanja wa Mpira wa Kasim Majaliwa | 800,250,000 | 565,268,500 |
| 3 | H/W Namtumbo | 27/04/2017 | Hakuna malipo yaliyofanyika | Ofisi za Halmashauri ya Namtumbo & Soko la Namtumbo | 465,097,500 | 465,097,500 |
| 4 | H/W Mbinga | 01/04/2020 | 16/02/2021 | Soko la Halmashauri ya Halmashauri ya Mbinga na Kituo cha Mabasi | 410,000,000 | 301,200,000 |
| 5 | H/W Pangani | 01/08/2018 | 30/04/2019 | Jengo la Pangadeco | 74,587,500 | 12,506,752 |
| Jumla | | | | | **2,778,734,993** | **2,351,142,255** |

***Chanzo**: Rejista ya Mikopo*

Aidha, nilibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, Bodi ilitarajiwa kukusanya shilingi bilioni 1.15 kama marejesho ya mikopo kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 zenye mikopo ambayo haijalipwa, kiasi hiki kinajumuisha kiasi cha mkopo (kianzio) na riba.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Bodi ilifanikiwa kurejesha shilingi milioni 298.24 pekee, ambayo ni sawa na asilimia 26 ya fedha zote zilizodaiwa na kusababisha mikopo ambayo haikurejeshwa kufikia shilingi milioni 849.72 kinyume na Kifungu cha 2 cha Mikataba ya Mikopo kati ya Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na Mamlaka za Serikali za Mitaa inayotaka marejesho ya mkopo yafanywe kulingana na ratiba iliyoambatanishwa ya malipo.kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali 16-3.**

**Jedwali Na.16-3: Kutofanyika kwa marejesho ya mkopo ya mwaka**

| Jina la Halmashauri | Kiasi cha Mkopo (Sh.) | Kiasi cha Malipo kinachopaswa kufanyika kwa mwaka (Sh.) | Kiasi kilicholipwa (Sh.) | Kiasi ambacho hakikulipwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| H/W Ruangwa | 565,268,500 | 160,050,000 | 0 | (160,050,000) |
| H/W Morogoro | 687,381,944 | 164,971,667 | 137,476,389 | (27,495,278) |
| H/W Namtumbo | 465,097,500 | 155,284,590 | 0 | (155,284,590) |
| H/W Singida | 28,318,540 | 6,000,000 | | (6,000,000) |
| H/W Pangani | 12,506,752 | 12,506,752 | 0 | (12,506,752) |
| H/W Bukombe | 1,055,700,000 | 117,300,000 | 20,000,000 | (97,300,000) |

| Jina la Halmashauri | Kiasi cha Mkopo (Sh.) | Kiasi cha Malipo kinachopaswa kufanyika kwa mwaka (Sh.) | Kiasi kilicholipwa (Sh.) | Kiasi ambacho hakikulipwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| H/Mji Mbinga | 758,692,343 | 157,738,392 | 131,448,297 | (26,290,095) |
| H/W Kishapu | 1,007,069,503 | 242,070,600 | 0 | (242,070,600) |
| H/W Tunduru | 12,044,547 | 12,044,547 | 9,319,975 | (2,724,572) |
| H/W Mbinga | 301,200,000 | 120,000,000 | 0 | (120,000,000) |
| **Jumla** | | **1,147,966,547** | **298,244,661** | **(849,721,887)** |

***Chanzo:*** *Rejista ya Mikopo*

Kushindwa kusimamia dhamana kunaathiri ufanisi wa Bodi na kuiweka kwenye hatari kubwa za kifedha. Hii inaweza kuhatarisha uwezo wa Bodi wa kutoa mikopo kwa Serikali za Mitaa na kuathiri shughuli zake kwa ujumla.

**Ninapendekeza kwamba Bodi ihakikishe mikopo inayotolewa inasimamiwa ipasavyo kulingana na makubaliano ya mkopo na ichukue hatua za kutekeleza mikataba ya dhamana na kurejesha mikopo ambayo imeshindwa kulipika ndani ya muda uliokubaliwa.**

### 16.5.2 Mtiririko wa Fedha Pungufu Kuwezesha Kukidhi Gharama za Uendeshaji za Bodi

Kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2021/22, Bodi ilipanga kukusanya shilingi milioni 656.96 kutoka vyanzo vyake na ruzuku za serikali kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Bodi.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa, kiasi cha shilingi milioni 306.21kilikusanywa kutokana na shughuli za uendeshaji, wakati matumizi ya uendeshaji ni shilingi milioni 825.55, na kusababisha nakisi ya shilingi milioni 519.34. Hii inaonyesha kushindwa katika usimamizi wa fedha. Maelezo yanaonyeshwa katika **Jedwali 16-4**.

**Jedwali Na.16-4: Mtiririko wa fedha pungufu**

| Na. | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Bodi | 306,210,212 |
| 2 | Fedha zilizotumika katika shughuli za uendeshaji wa Bodi | 825,552,555 |
| **Nakisi/matumizi zaidi ya fedha zilizopokelewa** | | **519,342,343** |

***Chanzo:*** *Bajeti ya Mwaka na Taarifa ya Fedha*

Uwezo wa Bodi kuendelea kutoa huduma na kufanya shughuli zake kama ilivyokusudiwa upo katika hatari ikiwa Bodi itaendelea kutumia

fedha za michango kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama chanzo chake kikuu na kuna uwezekano wa hatari kwamba Bodi inaweza kushindwa kutoa mikopo kwa Halmashauri katika siku zijazo kutokana na matatizo ya kifedha.

**Ninapendekeza kwamba, Bodi ije na mpango madhubuti juu ya usimamizi wa bajeti dhidi ya matumizi yake, ili kuhakikisha kuwa hazina ya Bodi inatumika kulingana na mpango uliokusudiwa. Aidha, Bodi inapaswa kubuni mikakati mipya ya kuongeza rasilimali za mapato ili kurejesha shilingi milioni 519.34 zilizotumika zaidi ya kiasi kilichokusanywa.**

## 16.6 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali namba 245 na kutangazwa rasmi katika Tangazo la Serikali namba 211 la tarehe 12 Mei 2017. Wakala huo ulianza kazi zake rasmi Julai 2017.

TARURA ilianzishwa ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza wakati wa kusimamia Mtandao wa Barabara za Wilaya chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kuboresha ufanisi na huduma katika sekta ya barabara. TARURA ina jukumu la kusimamia matengenezo, ukarabati na ujenzi wa Mtandao wa Barabara za Wilaya unaosimamiwa na Halmashauri, chini ya uratibu wa OR-TAMISEMI.

Kwa kuzingatia hilo, wakati wa ukaguzi wa TARURA kwa mwaka wa fedha unaosihia 2021/22 nilibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji kuboreshwa;

### 16.6.1 Kutotekelezwa Kikamilifu kwa Shughuli za Barabara Zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha

Ibara ya VI (6.1) ya Makubaliano ya Utendaji ya Mwaka 2021/22 kati ya TAMISEMI na TARURA inataka kazi zote za maendeleo zifanyike kulingana na programu ya kazi zilizomo kwenye mpango kazi na malengo ya utendaji kwa asilimia 100.

Nilibaini kuwa TAMISEMI iliidhinisha shughuli saba za utekelezaji wa TARURA kupitia Mfuko wa Barabara chini ya Mpango wa Maendeleo. Hata hivyo, hadi mwisho wa mwaka wa fedha wa 2021/22, utekelezaji wa jumla wa shughuli zilizopangwa ulikuwa kwa asilimia 75 tu,

ikionyesha kuwa asilimia 25 ya shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa. Maelezo yanaonyeshwa katika **Jedwali 16-5**.

**Jedwali Na.16-5: Hali ya Utekelezaji wa Shughuli**

| Shughuli | Idadi ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa | Shughuli zilizotekelezwa | % |
|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara za changarawe kwa kiwango cha Lami | 175.14 | 122.35 | 69.86 |
| Ujenzi wa barabara za udongo kwa kiwango cha changarawe | 8,982.27 | 6,740.54 | 75.04 |
| Ujenzi wa madaraja na makalvati makubwa | 944 | 741 | 78.49 |
| **Utekelezaji wa jumla** | | | **74.46** |

***Chanzo****: Taarifa ya utekelezaji*

Kushindwa kutekeleza shughuli zilizopangwa ndani ya muda uliowekwa kunaweza kuzuia jamii inayokusudiwa kunufaika na huduma za barabara zilizokusudiwa. Ucheleweshaji huu unaweza pia kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi.

**Ninapendekeza kwamba Menejimenti ya TARURA izingatie na kutekeleza taratibu juu ya udhibiti wa bajeti ili kuhakikisha utekelezaji kamili wa shughuli zote zilizopangwa bila kutumia gharama za ziada au kuathiri ubora uliokusudiwa.**

### 16.6.2 Ucheleweshaji wa Uletwaji wa Magari ya Shilingi Bilioni 16.7

TARURA ilinunua magari 124 kutoka GPSA kwa shilingi bilioni 16.7 kwa makubaliano kwamba magari hayo yatawasilishwa ndani ya miezi minne hadi sita kuanzia tarehe ya malipo, kama ilivyoelezwa kwenye barua zenye Kumb. Nambari ya CDA.260/318/06/AG/99 na Kumb. CDA.260/318/06/AG/99 ya tarehe 22/12/2020 na 11/01/2022 mtawalia kutoka GPSA kwenda kwa Mtendaji Mkuu wa TARURA.

Nilibaini kuchelewa kwa zaidi ya miezi tisa katika uwasilishaji wa magari hayo kutoka tarehe ya malipo kwa GPSA. Maelezo zaidi yanapatikana katika **Jedwali 16-6.**

**Jedwali Na.16-6: Magari Ambayo Hayajawasilishwa**

| Maelezo ya Gari | Idadi ya Magari | Bei kwa Gari(Sh.) | Jumla | Tarehe ya malipo kwa GPSA | Muda uliochukuliwa |
|---|---|---|---|---|---|
| Toyota L/C pick up D/cabin | 94 | 148,175,472 | 13,928,494,367 | 16/11/2021 | 11 Months |
| Toyota Hilux D/cabin pick up | 30 | 92,346,918 | 2,770,407,545 | 20/1/2022 | 9 Months |

| Maelezo ya Gari | Idadi ya Magari | Bei kwa Gari(Sh.) | Jumla | Tarehe ya malipo kwa GPSA | Muda uliochukuliwa |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla | 124 | | 16,698,901,912 | | |

Uwezo wa TARURA wa kusimamia kazi za barabara kwa ufanisi unategemea uwepo wa magari. Hata hivyo, ucheleweshaji umetatiza shughuli zao. Ucheleweshaji huo unawezekana kutokana na GPSA kutokuwa na uwezo wa kushughulikia maagizo mengi kutoka kwa mashirika mbalimbali ya serikali.

**TARURA ifuatilie GPSA ili kuhakikisha magari 124 yaliyobaki yanafika kama ilivyotarajiwa**

### 16.6.3 Kutokusanywa kwa Mapato ya Shilingi Milioni 385.22

Kanuni ya 57 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka , (Tangazo. No. 132 of 2001) inawataka Maofisa Masuuli kuhakikisha kwamba watu wote wanaopaswa kulipa mapato wanapewa taarifa za ankara, notisi za madai au notisi nyinginezo za madeni yanayodaiwa, na kukumbushwa mara kwa mara, aidha hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe kuhakikisha kuwa makusanyo yanafanyika ipasavyo.

Nilibaini kuwa Mawakala licha ya kupewa mamlaka ya kukusanya mapato ya shilingi bilioni 1.52. Hata hivyo, uhakiki nilioufanya wa mapokezi ya mapato ulibaini kuwa TARURA ilifanikiwa kukusanya shilingi bilioni 1.13 tu, na kusababisha kiasi cha shilingi milioni 385.22 kutokukusanywa. Maelezo zaidi yametolewa katika **Jedwali 16-7.**

Kutofuatwa kwa mikataba ya ukusanyaji mapato kunaweza kusababisha TARURA kupata hasara ya upotevu wa mapato.

**Jedwali Na.16-7: Kutokukusanywa Kwa Mapato**

| Mwezi | Makadirio ya makusanyo(Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Kiasi ambacho hakijakusanywa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Julai 2021 | 138,000,000 | 108,182,600 | 29,817,400 |
| Agosti 2021 | 138,000,000 | 113,836,100 | 24,163,900 |
| Septemba 2021 | 138,000,000 | 107,991,100 | 30,008,900 |
| Oktoba 2021 | 138,000,000 | 98,498,300 | 39,501,700 |
| Novemba 2021 | 138,000,000 | 107,696,400 | 30,303,600 |
| Disemba 2021 | 138,000,000 | 95,481,400 | 42,518,600 |
| Januari 2022 | 138,000,000 | 96,428,900 | 41,571,100 |
| Februari 2022 | 138,000,000 | 98,973,700 | 39,026,300 |
| Machi 2022 | 138,000,000 | 110,966,800 | 27,033,200 |
| Aprili 2022 | 138,000,000 | 90,464,200 | 47,535,800 |
| Mei 2022 | 138,000,000 | 104,264,000 | 33,736,000 |

| Mwezi | Makadirio ya makusanyo(Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Kiasi ambacho hakijakusanywa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| Jumla | 1,518,000,000 | 1,132,783,500 | 385,216,500 |

**Ninashauri Uongozi wa Wakala wa Barabara (TARURA) kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha wakandarasi wanatekeleza masharti ya mikataba, na kuchukua hatua za kuzuia upotevu wa mapato. Pia iimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanapelekwa benki kwa wakati na yanaingizwa kwenye taarifa za fedha.**

### 16.6.4 Miradi Iliotelekezwa yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.86

Kanuni ya 114(b),(c), na (d) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inaitaka taasisi nunuzi kuwa na usimamizi bora wa ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi yoyote inayofanya na itafuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati, kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba. Kuchukua au kuanzisha hatua za kurekebisha au kuadhibu ukiukwaji wa masharti ya mkataba; na kuhakikisha kwamba majukumu yaliyowekwa juu yake na mkataba yanatekelezwa kikamilifu.

Hata hivyo katika ziara yangu nilithibitisha uwepo wa miradi iliyotelekezwa na wakandarasi yenye thamani ya shilingi bilioni 3.86 katika Mikoa ya Rukwa, Simiyu, Arusha, Shinyanga, Kigoma, Manyara na Tarime. Maelezo ya miradi yanaoneshwa katika **Kiambatisho 16-1**.

Utelekezwaji wa miradi unachangiwa na ufinyu wa bajeti, usimamizi duni wa miradi, na mapungufu ya kitaalamu katika kusimamia miradi. Kutokamilishwa kwa miradi hii kunainyima jamii kusudiwa kunufaika na miradi hiyo kama ilivyolengwa. Aidha, kutelekeza miradi kunaweza kusababisha gharama kubwa ya kuikamilisha, na hivyo kuhatarisha maamuzi ya baadaye ya utoaji wa fedha na mgawo wa rasilimali.

**Ninashauri Uongozi wa Wakala kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ili kufuatilia maendeleo ya miradi na kubaini masuala yoyote yanayoweza kujitokeza ili kuwezesha hatua za marekebisho kuchukuliwa kwa wakati na kushughulikia masuala yoyote kabla hayajatokea.**

**Pia ninapendekeza kwamba Wakala idai dhamana za utendaji kazi kabla ya muda wake kuisha, ili kuepuka kusimamishwa kwa mradi**

**na gharama zinazohusiana. Menejimenti inapaswa kulipa madai ambayo hayajalipwa kutoka kwa wakandarasi.**

**Kwa kuchukua hatua hizi, TARURA inaweza kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati na ndani ya bajeti, na kwamba jamii inaweza kunufaika nayo kama ilivyokusudiwa**

### 16.6.5 Ongezeko la Gharama za Ufungaji Taa za Barabarani kwa Shilingi Bilioni 3.22

Kifungu cha 46.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC) kinazuia msimamizi wa mradi kubadilisha kiasi cha mkataba wa awali kwa zaidi ya 15% isipokuwa kwa idhini ya mwajiri. Pia, Kifungu cha 3.7.1 cha Mwongozo wa Usanifu wa Barabara Tanzania, wa mwaka 2002 kinaitaka Taasisi nunuzi kuandaa michoro ya kazi kufuatia tafiti za kina, usanifu na uchunguzi utakaopelekea upatikanaji wa kiasi na makadirio ya gharama kuhusiana na kazi zilizokadiriwa kutekelezwa.

TARURA iliingia mkataba na mzabuni tarehe 15 Oktoba 2019, wenye jumla ya shilingi bilioni 88.11. Mchanganuo wa makadirio ya gharama (BOQ) ulionesha kuwa taa 738 za barabarani zilipaswa kufungwa lakini hapakuwa na michoro ya kina hivyo kuhitaji mabadiliko ya usanifu.

Hata hivyo, nilibaini kuwa idadi ya taa za barabarani zilizohitajika iliongezeka kutoka 738 hadi 1,453 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 3.22 ukilinganisha na makadirio ya gharama ya awali.

Usanifu uliofanyika bila kufanya utafiti wa uhalisia wa mahitaji na makadirio ya gharama ya mradi wa uwekaji taa za barabarani ulichangia idadi ya taa kuongezeka. Hii inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama, matumizi mabaya ya fedha za umma, na kuathiri uwezo wa Wakala wa kutekeleza mradi ndani ya bajeti.

**Ninapendekeza kwamba Menejimenti ya TARURA ifanye utafiti wa kina katika miradi ili kupata makadirio ya gharama yenye uhalisia wa mahitaji, ili kupunguza ucheleweshaji wa mradi na ongezeko la gharama. Aidha, ninashauri Menejimenti ya TARURA ihakikishe kuwa wasimamizi wa miradi wawe wanafanya marekebisho yoyote ndani ya wigo wa bajeti ya kazi husika na kuidhinishwa kabla ya utekelezaji.**

### 16.6.6 Kutokufanyika kwa Upembuzi Yakinifu Kabla ya Kuanza Utekelezaji wa Miradi yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 20.34

Aya ya 3.2 ya Mwongozo wa Kijiometri wa Barabara kutoka Wizara ya Kazi Toleo la Mwaka 2011 unahitaji upembuzi yakinifu kufanyika kabla ya kutekeleza miradi ya barabara.

Katika ukaguzi wa miradi ya TARURA Mkoa wa Iringa nilibaini kuwa mkoa ulitekeleza miradi miwili, uboreshaji wa barabara ya Kidabaga-Bomalang'ombe (kilomita 18.3) yenye thamani ya shilingi bilioni 8.17 na barabara ya Sawala-Mkonde-Iyegeya (kilomita 30.3) yenye thamani ya shilingi bilioni 12.17 kwa kiwango cha lami miradi hiyo ilitekelezwa bila ya kufanya upembuzi yakinifu.

Kukosekana kwa upembuzi yakinifu kumeifanya TARURA kupata ugumu katika kutathmini kwa usahihi madhara ya muda mrefu ya uboreshaji wa barabara. Hii inaweza kusababisha barabara zilizoboreshwa kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa

**Ninapendekeza kuwa TARURA ihakikishe miradi yote ya uboreshaji wa barabara katika nyakati zijazo inafanyiwa upembuzi yakinifu wa kina ili kuongeza uwezekano wa mafanikio katika kufikia malengo ya mradi.**

### 16.6.7 Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Miradi yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 28.43

Kanuni ya 114 (b), (c), na (d) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inaitaka taasisi nunuzi kuwa na usimamizi bora wa ununuzi wowote ya kazi inazozifanyia na itafuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba; kuchukua au kuanzisha hatua za kurekebisha au za kisheria za ukiukwaji wa masharti ya mkataba; na kuhakikisha kwamba majukumu yaliyowekwa juu ya mkataba yanatekelezwa kikamilifu.

Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa utekelezaji wa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 28.43 umekuwa ukiendelea kwa kasi ndogo ukilinganisha na ratiba ya kazi zilizopangwa.

Mapitio ya majalada ya mawasiliano na ziara ya miradi husika nilibaini Kuchelewa kwa utekelezaji wa miradi hiyo kunaweza kusababisha gharama za ziada na kusababisha miradi kutofikia malengo

yaliyokusudiwa. Orodha ya mikoa yenye miradi ambayo kasi ya utekelezaji wake ilibainika kuwa ndogo ni kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali 16-8** hapa chini.

**Jedwali Na.16-8: Mikoa yenye Mradi Iliyo na Kasi Ndogo ya Utekelezaji**

| Na. | Mkoa | Thamani ya mradi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Mbeya | 8,080,680,409 |
| 2. | Njombe | 3,067,824,716 |
| 3. | Songwe | 1,499,482,000 |
| 4. | Geita | 405,905,500 |
| 5. | Kigoma | 7,524,102,920 |
| 6. | Mwanza | 1,440,796,069 |
| 7. | Morogoro | 5,656,173,300 |
| 8. | Lindi | 759,532,000 |
| **Jumla** | | **28,434,496,914** |

***Chanzo**: Taarifa ya ukaguzi ya TARURA*

Kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi kunatia mashaka kwani kunaweza kusababisha gharama za ziada na miradi isifikie malengo yaliyokusudiwa.

**Ninashauri Menejimenti ya TARURA ichukue hatua za haraka kushughulikia ucheleweshaji huo wa miradi na kuhakikisha kuwa miradi inakamilika ndani ya muda uliokubaliwa. Pia, Menejimenti inatakiwa kuimarisha mifumo yake ya usimamizi wa miradi ili kuboresha ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi na kuhakikisha kuwa miradi inayochelewa inatambuliwa na kushughulikiwa kwa haraka.**

### 16.6.8 Kazi za Barabara zilizofanyika Chini ya Kiwango

Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Ushuru wa Barabara na Mafuta ya mwaka 2016 inamtaka wakala wa utekelezaji kuhakikisha kuwa kazi yoyote iliyopangwa inatekelezwa ndani ya muda, gharama na ubora ulioainishwa kwenye mkataba husika.

Katika uhakiki wa hali ya utekelezaji wa miradi mbalimbali iliyotekelezwa katika mwaka 2021/22, nimebaini kasoro kadhaa zilizosababisha miradi kutojengwa ipasavyo. Kasoro zilizobainika ni pamoja na:

(i) **Uwepo wa nyufa kwenye kalavati zilizojengwa**: Nilibaini kuwa baadhi ya makalavati yaliyojengwa wakati wa mradi yalikuwa na nyufa, hali inayoashiria ujenzi usio na ubora. Hii inahatarisha sana

usalama wa watumiaji wa barabara na inaweza kusababisha mafuriko kipindi cha mvua kubwa.

(ii) **Miundo ya barabara isiyoshindiliwa ipasavyo**: Niligundua kuwa baadhi ya miundo ya barabara haikuunganishwa vya kutosha, jambo ambalo linaweza kusababisha barabara kutokuwa sawa, mashimo na kuongezeka kwa uchakavu wa magari yanayotumia barabara.

(iii) **Kutojengwa kwa mifereji ya maji ili kuruhusu maji kupitia mitaro:** Mapitio yangu pia yalibainisha matukio ambapo mifereji ya maji haikujengwa ili kuruhusu maji kutiririka. Hii inaweza kusababisha mafuriko, ambayo yanaweza kuhatarisha zaidi usalama wa barabara na kusababisha uharibifu wa mifereji ya maji.

(iv) **Ukamilishaji usiofaa wa madaraja yaliyojengwa**: Nilibaini kuwa baadhi ya madaraja hayajakamilika ipasavyo, hivyo kusababisha kuhatarisha watumiaji wa barabara, hasa waendesha pikipiki.

(v) **Kutoweka alama za barabarani kwenye barabara zilizojengwa:** Hatimaye, niligundua kuwa baadhi ya barabara zilizojengwa hazikuwa na alama za kutosha, hivyo kuwaletea ugumu watumiaji wa barabara kupita barabarani na kuongeza hatari ya ajali.

Maelezo ya makosa yanaonyeshwa katika **Kiambatisho 16-2.**

Kujenga barabara zenye kiwango duni kunaonesha kuwa thamani ya fedha zilizotumika haikupatikana ipasavyo hivyo kukwamisha kufikiwa kwa malengo ya mradi, ambayo ni kutoa huduma endelevu za barabara kwa jamii.

**Ninapendekeza kwamba, Menejimenti ya TARURA ichukue hatua za haraka kurekebisha mapungufu yaliyoainishwa ili kuhakikisha kuwa miradi iliyojengwa inakidhi viwango vinavyotakiwa na ni salama kwa matumizi ya wananchi.**

**Pia, menejimenti ya TARURA inatakiwa kuchukua hatua za kuzuia dosari hizo kutokea katika siku zijazo, kama vile kuboresha udhibiti wa ubora na ufuatiliaji wakati wa mchakato wa ujenzi na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa miradi inakidhi viwango vinavyotakiwa.**

### 16.6.9 Gharama Ambazo Hazikukatwa kutokana na Kusitishwa Mikataba yenye Thamani ya Shilingi Milioni 470.75

Kifungu cha 58 (2) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 kinasema kwamba, "mzabuni aliyeshinda zabuni atalazimika kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi, kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa kwenye mkataba". Aidha, Kanuni ya 114 (b) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma, 2013 zinaitaka taasisi nunuzi kufuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba.

Nilibaini kuwa Wakala hakukata gharama zozote kutokana na dhamana za utendaji wa mkataba husika, licha ya kusitisha mikataba iliyokadiriwa kugharimu shilingi milioni 470.75 kama ilivyofafanuliwa katika **Kiambatisho 16-3**.

Usitishwaji wa mikataba bila kuzingatia matakwa ya kukata gharama zilizotumika umesababisha upotevu wa fedha za umma na kuiwekea mzigo Serikali wa kutenga fedha za ziada nje ya bajeti ili kukamilisha kazi zilizobaki kwenye mikataba ambayo haijakamilika.

**Ninapendekeza kuwa, Menejimenti ya TARURA ipitie upya taratibu zake za kusitisha mikataba na kuhakikisha ina utaratibu wa kurejesha gharama kutoka katika dhamana za utendaji kazi mikataba inapokoma.**

**Aidha, Wakala unapaswa kupitia upya mikataba yote ambayo imesitishwa ili kubaini iwapo gharama zozote zilizoingiwa zimefidiwa kwa kukatwa kutoka kwa wakandarasi na kuchukua hatua stahiki kurejesha gharama hizo.**

### 16.6.10 Udhaifu katika Usimamizi wa Dhamana za Utendaji

Kanuni ya 29 (1) ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya 2013 inamtaka mzabuni aliyeshinda zabuni kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi kwa taasisi nunuzi ili kuwa na uthibitisho wa utekelezaji kwa mkataba, na malipo ya wafanyakazi, wazabuni, wahandisi, na wakandarasi wadogo.

Kinyume chake, nilibaini udhaifu katika usimamizi wa dhamana za utendaji kazi katika miradi mingi iliyotekelezwa katika mwaka 2021/22. Udhaifu huu ni pamoja na kuchelewa kuwasilisha dhamana

ya utendaji kazi, dhamana za utendaji kazi ambazo zinachukua muda mfupi, uwasilishaji wa dhamana za utendaji kazi baada ya kazi kukamilika, uhalali usiothibitishwa wa dhamana za utendaji kazi, mikataba kubadilishwa bila kupata dhamana mpya za utendaji kazi na dhamana za utendaji kazi ambazo muda wake umeisha kabla ya kukamilika kwa mradi. Maelezo ya miradi na ukiukwaji husika katika uwasilishaji wa dhamana ya utendaji kazi yanaonyeshwa katika **Kiambatisho 16-4**.

Udhaifu huu huongeza hatari kwamba miradi haitakamilika kama ilivyopangwa, au kunaweza kuwa na gharama za ziada au ucheleweshaji wa kukamilisha miradi. Aidha, kukosekana kwa usimamizi kwa wakati na sahihi wa dhamana za utendaji kunaweza kusababisha hasara ya fedha kwa Wakala na athari mbaya katika ubora na wigo wa miradi.

**Ninaishauri Menejimenti ya TARURA kuandaa na kutekeleza sera na taratibu zinazoeleweka za usimamizi wa dhamana za utendaji kazi, ikijumuisha mahitaji ya uwasilishaji kwa wakati, uthibitisho wa uhalali na ufuatiliaji wa tarehe za mwisho wa matumizi ya dhamana za utendaji kazi.**

**Aidha, Wakala uzingatie na kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa hali ya dhamana za utendaji kazi ili kuhakikisha kuwa zinasimamiwa ipasavyo.**

### 16.6.11 Kutokatiwa Bima kwa Mikataba ya Miradi yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 5.56

Kifungu cha 17.1 cha masharti ya jumla ya mkataba kinasema kuwa mkandarasi atatoa bima kuanzia tarehe ya kuanza hadi mwisho wa kipindi cha matazamio ya mradi kwa ajili ya kufidia matukio yafuatayo ambayo ni: hasara au uharibifu wa kazi, mtambo na vifaa; kupoteza au uharibifu wa vifaa; hasara au uharibifu wa mali (isipokuwa kazi, mitambo, na vifaa) kuhusiana na mkataba; na kuumia binafsi au kifo.

Nimepitia majalada ya mikataba na hati za bima kwa mikataba iliyotekelezwa mkoani Katavi na kubaini kuwa, mikataba yenye thamani ya Silingi bilioni 3.01 ilitekelezwa bila kuwa na bima kwa kuwa wakandarasi walishindwa kuwasilisha uthibitisho unaohitajika kwa ajili ya bima. Maelezo yanaonyeshwa katika **Kiambatisho 16-5.**

Aidha, malipo ya bima yaliyowasilishwa kwa ajili ya utekelezaji wa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 2.53 hayakuhusisha kipindi cha matazamio ya kasoro kama ilivyoelezwa katika masharti ya jumla ya mikataba. Kumaanisha kuwa wakandarasi hawawezi kuwajibika kwa kasoro au uharibifu wowote unaotokea baada ya kukamilika kwa mradi.Kama ilivyoorodheshwa katika **Jedwali Na 16-9** hapa chini.

**Jedwali Na.16-9**: Kutokatiwa Bima Kwa Mikataba ya Miradi

| Na. | Halmashauri | Namba ya mkataba | Kiasi cha mkataba (Sh.) | Kiasi cha bima kilichohitajika (Sh.) | Kipindi kilichohusishwa na bima | Kipindi ambacho hakijajumuishwa katika bima | Kipindi cha matazamio ambacho hakina bima (miezi) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mtwara | Na.AE/092/2021-2022/MT/W/60 | 445,640,500 | 12,000,000 | 10/10/2021 - 09/03/2022 | 10/10/2021 - 09/03/2023 | 12 |
| 2. | M/Mji Nanyamba | Na.AE/092/2021-2022/MT/W/32 | 115,571,500 | 12,000,000 | 07/09/2021 -6/01/2022 | 07/09/2021 - 07/01/2022-06/07/2022 | 6 |
| 3. | H/W Mtwara | Na.AE/092/2021-2022/MT/W/69 | 523,978,604 | 12,000,000 | 31/03/2022 - 29/09/2022 | 31/03/2022 - 29/09/2023 | 1 |
| 4. | H/W Nanyumbu | Na.AE/092/2021-2022/MT/W/74 | 950,000,000 | 12,000,000 | 22/12/2021 - 21/12/2022 | 22/12/2021-20/7/2023 | 7 |
| 5. | H/W Masasi | Na.AE/092/2021-2022/MT/W/83 | 499,818,000 | 12,000,000 | 29/10/2021 - 28/10/2022 | 29/10/2021 - 28/03/2023 | 5 |
| **Jumla** | | | **2,535,008,604** | **60,000,000** | | | |

Upungufu wa kushindwa kuiwekea miradi hiyo bima unatokana na usimamizi dhaifu wa mikataba unaofanywa na Wakala. Kukosekana kwa bima za mikataba ya miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 5.56 kunaiweka Serikali katika hatari ya kupata hasara kwa kushindwa kupata fidia kutokana na ajali au matukio yoyote yanayohusiana na miradi hiyo.

**Naishauri Menejimenti ya TARURA kuhakikisha mikataba yote inatekelezwa kwa kuzingatia bima zinazohitajika, na ziwe bima kubwa 'comprehensive' na zinakidhi kipindi cha dhima ya kasoro. Zaidi ya hayo, malipo ya bima yanayolipwa kwa wakandarasi yanapaswa kuhalalishwa na kuthibitishwa.**

### 16.6.12 Kutozingatiwa kwa Athari za Mitetemo Katika Usanifu wa Daraja la Berega-Kilosa Lililopo Mjini Morogoro Shilingi Bilioni 7.9

Madaraja katika maeneo yenye mitetemeko ya ardhi huguswa na athari za matetemeko ya ardhi, haswa kuhamishwa na mitetemo kwa sababu ya kasi ya ardhi. Kwa hivyo, lazima ziundwe na kujengwa ipasavyo kwa kuzingatia athari za tetemeko la ardhi.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa TARURA ilitekeleza mradi wenye thamani ya shilingi bilioni 7.9 wa ujenzi wa daraja la urefu wa mita 140 kila upande, ikihusisha barabara za kuelekea Berega Kilosa. Hata hivyo, ukaguzi wangu umebaini suala muhimu la kiufundi katika muundo wa awali wa daraja, unaohusiana na kutozingatiwa kwa athari za mitetemo. Kuzingatia athari za mitetemo kwenye muundo ni muhimu haswa katika mikoa kama Morogoro ambayo imeainishwa kama inayokumbwa na tetemeko la ardhi.

Pia mapitio ya viwango vya Kitengo cha Utafiti wa Majengo (BRU) yameonesha kuwa mkoa wa Morogoro uko katika maeneo yenye masafa adimu na yasiyojulikana ya tetemeko la ardhi na unaweza kukumbwa na mawimbi ya tetemeko. Matukio ya tetemeko la ardhi sio tu yamesababisha uharibifu wa kibinadamu na kimwili, pia yameweza kusababisha athari za kiuchumi katika maeneo yaliyo hatarini.

Kushindwa kuzingatia athari za mitetemo kwenye usanifu wa muundo wa daraja ni kasoro kubwa ambayo inaweza kuhatarisha uimara na usalama wa daraja na watumiaji. Kwa kuzingatia hatari zinazoweza kuhusishwa na matetemeko ya ardhi, ni muhimu kwamba miundombinu yoyote iliyojengwa katika eneo hilo izingatie athari zinazoweza kutokea kutokana na matukio ya tetemeko la ardhi.

**Ninapendekeza kwamba, katika siku zijazo, Menejimenti ya TARURA izingatie athari za matukio ya mitetemo katika usanifu wa muundo wa madaraja. Aidha, Menejimenti inashauriwa kufanya tathmini za vihatarishi vya mitetemo katika daraja lililojengwa ili kubaini athari zinazoweza kutokea kutokana na matukio ya tetemeko la ardhi na kuandaa hatua zinazofaa za kupunguza vihatarishi hivyo.**

## 16.7 Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT)

Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa Tanzania (ALAT) ni asasi yenye uanachama iliyoanzishwa mwaka 1984 baada ya kuanzishwa upya kwa mfumo wa Serikali za Mitaa nchini Tanzania.

Wajumbe wa Jumuiya hiyo ni Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Miji, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya na Mijini, Wabunge mmoja kutoka kila Tawi la ALAT Mkoa na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa kutoka kila mkoa.

Majukumu ya kikatiba ya ALAT ni kukuza maendeleo ya serikali za mitaa; kuendesha maslahi, haki na maadili ya mamlaka za mitaa; kushawishi na kutetea sera iliyoboreshwa na sheria kwa serikali za mitaa; kuwakilisha maoni ya Halmashauri, na kutoa huduma za kiufundi na kitaalamu kwa wanachama wake.

### 16.7.1 Kutokusanywa kwa Michango Kiasi cha Shilingi Bilioni 5.16 kutoka kwa Wanachama wa Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa Tanzania

Ibara ya 6(2) ya Katiba ya Jumuiya ya Tawala za Serikali za Mitaa (ALAT) inazitaka Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kushiriki katika kuchangia Jumuiya kila mwaka.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa ALAT ilipanga kukusanya michango yenye jumla ya shilingi blioni 5.56 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2021/22. Hata hivyo, jumla ya shilingi millioni 400.22 pekee ambayo ni sawa na 7% ilikusanywa na kuacha michango isiyokusanywa ya shilingi bilioni 5.16 sawa na 83%.

Kutokusanywa kwa michango kunaashiria wanachama kuwa na imani hafifu ya utoaji huduma na kunaiweka Jumuiya katika hatari ya kushindwa kuendelea kutoa huduma kwa wanachama wake kwa kipindi kijacho.

**Ninapendekeza kwamba, Menejimenti ya ALAT ihakikishe utoaji wa huduma kwa wanachama wake unakuwa wa kiwango cha juu iwezekanavyo ili kuongeza imani kwa wanachama wake katika jitihada za ufuatiliaji wa kuongeza michango.**

### 16.7.2 Kutofanyika kwa Tathmini ya Shughuli za Uendeshaji za Jumuiya Kutokana na Kutokuwepo kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Kanuni ya 28 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 inawataka Maofisa Masuuli kuanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani chenye ufanisi. Kukosekana kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Jumuiya kunaikosesha kipengele muhimu cha utawala bora wa taasisi.

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa, ALAT haikuwa na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa sababu hiyo, kazi ya ukaguzi wa ndani ya miamala na shughuli za Jumuiya haikufanyika kwa miaka mitatu mfululizo. Aidha, nilibaini kuwa, Jumuiya haina mpango wa kuajiri wakaguzi wa ndani kutokana na kutokuingizwa kwa jambo hilo kwenye bajeti.

Kutokufanyika kwa ukaguzi wa ndani katika Jumuiya kunatokana na ufinyu wa bajeti na ukosefu wa muundo wa utawala bora kulikopelekea kutokuajiri Mkaguzi wa Ndani. Hii inasababisha kushindwa kufanya utambuzi wa masuala yenye viashiria vya hatari katika usimamizi wa fedha na shughuli za Jumuiya ikiwemo ubadhirifu, kutokana na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani.

Uwepo wa mhasibu mmoja tu katika Jumuiya kunaashiria kuwa hakuna udhibiti wa kuweza kufanya uhakiki wa kazi aliyofanya mtu mwingine, na kuongeza hatari ya udanganyifu au ubadhirifu.

**Ninashauri Menejimenti ya Jumuiya kuhakikisha kwamba, inaajiri mkaguzi wa ndani ili kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani na utawala bora katika Jumuiya.**

## 16.8 Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI)-Hombolo

Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 396 ya Sheria za Tanzania kama Taasisi inayojitegemea. Madhumuni ya Chuo cha Serikali za Mitaa ni kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine wenye nia kwa kutumia mafunzo, utafiti, ushauri na afua zinazofaa. Hatimaye, jukumu la taasisi ni kuwezesha michakato ya ugatuaji wa madaraka kwa ugatuzi, utawala bora, utoaji wa huduma bora, kupunguza umaskini na kukuza ustawi wa kijamii na kiuchumi wa watu nchini kote. Wakati wa ukaguzi wa LGTI, mapungufu yafuatayo yalibainika:

### 16.8.1 Masurufu Ambayo Hayarejeshwa Shilingi Milioni 203.93

Kanuni ya 103 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 (zilizorekebishwa mwaka 2004) inataka masurufu yafanyiwe marejesho mara tu hitaji la masurufu hayo litakapokoma. Endapo Afisa aliyepewa masurufu atashindwa kufanya marejesho kikamilifu ndani ya siku 30 baada ya kuisha kwa mwaka wa fedha katika kipindi masurufu yalipotolewa, kiasi kilichobaki kinaweza kurejeshwa mara moja kutoka kwenye mshahara wowote au malipo mengine au kutokana kwa kiasi kingine chochote anachostahili afisa huyo.

Ukaguzi wa nyaraka za masurufu kwa mwaka wa fedha 2021/22 nilibaini kuwa, masurufu ya jumla ya shilingi milioni 203.93 yalitolewa kwa watumishi mbalimbali kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2021/22, lakini masurufu hayo yalikuwa hayajarejeshwa na baadhi ya watumishi kinyume na matakwa ya Kanuni za Fedha za Umma.Kiasi cha masurufu ambayo hayarejeshwa yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka ikimaanisha kuwa, hapakuwa na hatua kali zilizochukuliwa dhidi ya waliokiuka taraibu za masurufu ili kuepuka hasara kutokana na kutorejeshwa kwa masurufu. Mwenendo wa masurufu ambayo muda wake umechelewa kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2021/22 ni kama inavyoonyeshwa kwenye **Kielelezo Na.16-1** hapa chini.

**Kielelezo Na 0-1: Mwenendo wa Masurufu**




Udhibiti dhaifu wa ndani wa usimamizi wa masurufu unaweza kusababisha urejeshwaji wa masurufu kuwa mgumu hivyo basi ubadhirifu wa fedha za umma unaweza kutokea kwa kutumia fedha hizo kwa matumizi binafsi.

**Ninapendekeza Menejimenti ya Chuo cha Serikali za Mitaa uhakikishe kuwa masurufu ambayo hayajarejeshwa ya shilingi milioni 203.93 yanarejeshwa na watumishi waliolipwa fedha hizo au kukatwa kutoka katika mishahara yao.**

### 16.8.2 Kazi za Ukarabati wa Majengo ya Chuo zenye Thamani ya Shilingi Milioni 440 zilizofanyika kwa Kiwango cha Chini

Katika mwaka wa fedha 2020/21, uongozi wa Chuo ulitenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya nyumba za watumishi daraja la A-F, hosteli ya Mbagala AB na CD, hosteli ya Kawawa, hosteli ya Karume, hosteli ya Nyerere, choo cha umma, uzio wa umeme na nyumba za madereva ulifanywa kwa njia ya 'Force Account'. Hata hivyo, tarehe 12 Januari 2023 nilifanya uhakiki na kubaini kuwa kazi zenye thamani ya shilingi milioni 440 za ukarabati wa majengo katika Chuo zilifanyika kwa kiwango duni unaoonesha ukarabati usio na viwango.

Baadhi ya kazi nilizobaini kuwa zilifanyika kwa kiwango cha chini ni pamoja na maji machafu kujaa kwenye bafu, sehemu za kufulia nguo za wanafunzi, milango na madirisha ambayo hayajawekwa nakishi, madirisha yenye vioo vilivyoharibika bila kutengenezwa, kutumika kwa mbao laini katika mlango badala ya mbao ngumu, kutokamilika kwa kazi ya mabomba, na kuwekwa kwa marumaru zenye kiwango duni tofauti na maelekezo.

Kazi zisizo na viwango zinatokana na usimamizi dhaifu wa miradi wakati wa utekelezaji. Kuwepo kwa kazi duni kunamaanisha kuwa, malengo yaliyokusudiwa ya matengenezo hayajafikiwa na thamani ya fedha kwa ajili ya shughuli za matengenezo haijafikiwa.

**Nashauri menejimenti ya Chuo cha Serikali za Mitaa kuimarisha usimamizi wa mikataba ya matengenezo katika miradi ijayo ili kuepuka kazi zisizokidhi viwango, na kuhakikisha kuwa, kasoro zote zilizobainika zinarekebishwa.**

### 16.8.3 Kazi za Ujenzi zenye Thamani ya Shilingi Milioni 44.95 Zilizoidhinishwa na Meneja wa Mradi Kabla ya Kutekelezwa

Kanuni ya 114 (a) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 inaeleza kuwa, "taasisi nunuzi itawajibika kusimamia ununuzi wowote wa bidhaa, huduma au kazi inazozifanya na itafuatiliagharama na

utoaji wa bidhaa na huduma kwa wakati kwa viwango sahihi na kwa ubora ulioainishwa katika kila mkataba”.

Nilipitia majalada ya ujenzi wa Hosteli ya Karume & Nyerere, Hosteli ya Mbagala A-D, Daraja C, Nyumba za Madereva, Bweni la Kawawa na majengo ya Daraja E nilibaini kuwa mnamo tarehe 8 Novemba 2022 meneja mradi alipitisha hati ya mwisho ili mkandarasi aweze kulipwa shilingimilioni 44.95, ambayo pia iliidhinishwa na Kaimu Mkuu wa Chuo mnamo tarehe 12 Desemba 2022. Hata hivyo, katika uhakiki wa miradi nilioufanya tarehe 12 Januari 2023 nilibaini kuwa kazi zote zilizoidhinishwa kulipwa kwenye cheti cha mwisho bado hazikufanyika.

Uidhinishaji huu wa kazi kabla ya kuzifanya huashiria kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani wa uidhinishaji wa vyeti vya malipo, na kupelekea kuidhinishwa kwa kazi amabazo bado kufanyika

**Ninapendekeza Menejimenti ya Chuo isitishe malipo ya cheti cha mwisho na kuunda kamati mpya ya kutathmini kazi iliyofanyika na kufanya maamuzi ya malipo kulingana na kazi halisi iliyotekelezwa. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe na Uongozi wa Chuo dhidi ya wanakamati wote kwa kushindwa kutimiza wajibu wao na kupelekea kuidhinisha kazi zilipwe huku wakijua kazi hizo bado hazijafanyika.**

### 16.8.4 Ununuzi wa Bidhaa Bila Kuzingatia Kipengele cha Vipimo katika Mchakato wa Ununuzi wa bidhaa za Shilingi Milioni 236.7

Kanuni ya 164 (2) (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inahitaji barua ya mwaliko wa nukuu iwe na maelezo kamili ya bidhaa, kazi au huduma zitakazonunuliwa ikijumuisha vipimo, miundo, na michoro.

Nilibaini kuwa bidhaa zenye thamani ya shilingi milioni 43.4 zilinunuliwa kinyume na vipimo vilivyotolewa na idara tumizi. Aidha, bidhaa zenye thamani ya shilingi milioni 193.3 ziliagizwa bila kueleza vipimo. Kasoro hii inaweza kusababisha uwasilishaji wa bidhaa zenye ubora duni na zisizokusudiwa na idara tumizi, hivyo kutofikiwa kwa thamani ya fedha.

**Menejimenti ya Chuo inasisitizwa kuhakikisha kuwa, kipengele cha vipimo kinazingatiwa ipasavyo katika mchakato wa ununuzi kama inavyotakiwa na kanuni za ununuzi wa umma.**

### 16.8.5 Ushindani Usio wa Haki katika Zabuni ya Shilingi Milioni 109.82

Kifungu cha 47 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 kinazitaka taasisi kuhakikisha kuwa, katika mchakato wa ununuzi panakuwa na usawa, haki na uwazi kwa wazabuni wote.

Ukaguzi wa nyaraka za zabuni ya ununuzi wa vifaa vya mabomba ulibaini kuwa, Bodi ya Zabuni kupitia kikao chake kilichofanyika tarehe 25 Juni 2021 iliamua kutoa zabuni yenye thamani ya shilingi milioni 109.82 kwa mzabuni ambaye hakushiriki katika mchakato wa zabuni, kwa sababu nukuu yake haikuwa miongoni mwa nukuu zilizowasilishwa kwa taasisi nunuzi kwa ajili ya kushindanishwa.

Kuchagua mzabuni ambaye hakushiriki katika mchakato wa kutoa zabuni kunamaanisha ushindani usio wa haki wa zabuni.

**Ninapendekeza Uongozi wa Chuo uhakikishe kuwa sheria na kanuni za ununuzi zinazingatiwa ili kuweka ushindani wa haki katika mchakato wa ununuzi. Aidha, Uongozi wa Chuo uchukue hatua stahiki kwa maofisa waliotunuku zabuni kwa mzabuni ambaye hakushiriki katika mchakato wa ununuzi.**



# SURA YA KUMI NA SABA

# KAGUZI MAALUM

## 17.0 Utangulizi

Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 pamoja na Kanuni ya 78 na 79 (1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009 zinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu pale anapoona inafaa au kwa ombi maalumu la maandishi kutoka kwa Afisa Masuuli, au mtu yeyote, taasisi, mamlaka ya umma, wizara, idara inayojitegemea, wakala, mamlaka ya serikali za mitaa, au chombo kingine chochote.

Katika kipindi ninachotolea taarifa nilifanya kaguzi maalumu katika Mamlaka mbili za Serikali za Mitaa, ambazo zinajumuisha zile zilizoombwa na wadau mbalimbali. Matokeo ya kaguzi hizi yameelezwa kwa kina katika ripoti zinazojitegemea zilizowasilishwa kwa taasisi zilizoomba kaguzi hizo.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa ni Halmashauri ya Jiji la Arusha na Halmashauri ya wilaya ya Ngara

Masuala muhimu ambayo yalibainika katika ripoti za kaguzi maalumu hizo yameainishwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

## 17.1 Halmashauri ya Wilaya ya Ngara

Nilifanya ukaguzi maalumu wa Fedha za Mapato yanayotokana na ada za leseni za biashara kwa kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2022 na kubaini masuala yafuatayo;

### 17.1.1 Malipo ya Ada ya Leseni kutowasilishwa Benki Shilingi milioni 45.99

Nilibaini kati ya leseni 5,352 nilizohakiki, leseni 596 zenye jumla ya shilingi milioni 45.99 zilitolewa kwa wafanyabiashara bila ya malipo yake kuwasilishwa Halmashauri kupitia benki. Kati ya kiasi hicho, shilingi milioni 33.81 zinatokana na leseni 423 zilizotolewa kwa wafanyabiashara bila kulipa kiasi chochote katika akaunti ya Halmashauri na shilingi milioni 12.18 kinatokana na leseni 173 zenye thamani ya shilingi milioni 21.37 zilizotolewa kwa wafanyabiashara waliolipa jumla ya shilingi milioni 9.19 pekee.

Kutowasilishwa fedha benki kunatokana na kukosekana kwa uaminifu baina ya watumishi wa halmashauri kupokea fedha toka kwa wafanya biashara na kutumia kwa shughuli zao binafsi, na kupelekea Halmashauri kupata hasara ya shilingi milioni 45.99

**Ofisi ya Raisi TAMISEMI ikahikishe hatua stahiki zinachukuliwa kwa watumishi waliohusika na upotevu wa fedha za mapato ya ada za leseni, ikiwa ni Pamoja na kuhakikisha Jumla ya shilingi milioni 45.99 zinarejeshwa kutoka kwa watumishi husika na kuwasilishwa katika akaunti ya Halmashauri.**

## 17.2 Halmashauri ya Jiji la Arusha

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa (MB) aliniomba kufanya Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Miongoni mwa malengo ya ukaguzi huo ni kuangalia utekelezaji wa miradi ya mbalimbali, na namna sheria ya ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na kanuni zake za mwaka 2013 zinavyofuatwa,

Zaidi ya hayo, nilifanya uhakiki wa kina wa taratibu za usimamizi, ugawaji na urejeshaji wa fedha, ikiwa ni pamoja na kuthibitisha uhalali wamalipo mbalimbali yaliyofanywa kwa fedha taslimu, na usahihi wa madeni ya wakandarasi.

Aidha,nilipitia mikataba yote ya ukusanyaji wa kodi na mapato,ili kuhakikisha sheria na kanuni za ununuzi ya umma inafuatwa. Pia nilifanya ukaguzi wa kina wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ili kuhakikisha mikopo inatolewa kwa vikundi

vinavyostahili na marejesho yanafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha

Aidha, nilichunguza taratibu za uhamisho wa watumishi katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, na kuhakiki uhalali wa uhamisho huo. Pia nilichunguza mwenendo, utendaji kazi, na uhusiano kati ya viongozi wa Jiji na Mkoa wa Arusha. Katika ukaguzi huo, nilikagua pia shughuli za kampuni ya Arusha Meat ili kubaini kama kulikuwa na ubadhilifu wa fedha za umma.

Matokeo ya ukaguzi yalifikishwa TAKUKURU na mamlaka nyingine husika kwa hatua zaidi, Kwa kuwa uchunguzi bado unaendelea,matokeo ya ukaguzi huo hayajawekwa wazi katika ripoti hii.



# SURA YA KUMI NA NANE

# MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO

## Mapendekezo ya Jumla

Licha ya juhudi za Serikali za kuboresha uwazi,na ufanisi, Taarifa hii inaibua hitaji muhimu la kuchukua hatua kwa haraka katika taratibu za usimamizi wa fedha za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.Afua hizi lazima ziweke kipaumbele katika uimarishaji wa udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi, na taratibu za utawala ili kupunguza hatari za usimamizi holela wa kifedha na mapungufu kadha wa kadha katika udhibiti wa ndani.

Ili kushughulikia masuala haya, Ofisi ya Raisi-TAMISEMI, Tawala za mikoa, na Serikali za Mitaa lazima ziandae mpango kazi wa kina ambao utawezesha utekelezaji wa haraka wa mapendekezo yanayojirudia, ikijumuisha mikakati ya kiutendaji ya kutekeleza mapendekezo ya muda mrefu.

Mpango kazi unapaswa kujumuisha mkakati wa kina wa kuimarisha udhibiti wa ndani, udhibiti wa vihatarishi, na taratibu za utawala katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuanzia ngazi ya wizara mpaka ngazi za chini.

Aidha, mpango wa utekelezaji unapaswa kujumuisha hatua za kujenga uwezo wa kutosha na mpango wa mafunzo kwa watumishi wanaohusika katika mchakato wa usimamizi wa fedha. Hii itahakikisha kwamba mifumo na taratibu mpya zinaeleweka vyema na kutekelezwa kwa ufanisi.

Vilevile, Matumizi ya mifumo ya kielektroniki yanapaswa kuhimizwa ili kuboresha ufanisi, usahihi na uwazi katika michakato ya usimamizi wa fedha, hivyo kupunguza hatari za makosa, na dosari nyinginezo

hasa katika maeneo ya taarifa zinazohusu mapato na fedha.

Hatimaye, ni lazima hatua kali zichukuliwe kwa watendaji wote wanaohusika na uvunjaji wa sheria, hasa katika masuala yanayohusu manunuzi na ukusanyaji wa mapato.

## Hitimisho

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wadau wetu wote, ikiwa ni pamoja na Serikali, Bunge, na Taasisi zote zilizokaguliwa kwa michango yao ya thamani na msaada thabiti katika kuwezesha utayarishaji wa taarifa hii. Ni matumaini yangu ya dhati kwamba Taarifa hii itafanyika kuwa nyenzo muhimu kwa umma, watunga sera,pamoja na wataalam

Kwa kufanya kazi pamoja kwa ushirikiano wa karibu, nina imani kwamba tunaweza kuimarisha utendaji kazi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kiasi kikubwa. Hivyo, ni Imani yangu kwamba, tutaendeleza ushirikiano wetu katika kufanya kazi pamoja kwa mustakabali wa ujenzi wa Taifa katika miaka ijayo.

Charles E. Kichere
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho Na.2-1: Mwenendo wa Hati za ukaguzi zilizotolewa

| Na. | Jina la Taasisi | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 2. | H/W Arusha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 3. | H/W Babati | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 4. | H/Mji Babati | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 5. | H/W Bagamoyo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 6. | H/W Bahi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 7. | H/W Bariadi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 8. | H/Mji Bariadi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 9. | H/W Biharamulo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 10. | H/W Buchosa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 11. | H/W Buhigwe | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 12. | H/W Bukoba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 13. | H/M Bukoba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 14. | H/W Bukombe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 15. | H/W Bumbuli | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 16. | H/W Bunda | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Mbaya | Inayoridhisha |
| 17. | H/Mji Bunda | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 18. | H/W Busega | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 19. | H/W Busokelo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 20. | H/W Butiama | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 21. | H/W Chalinze | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 22. | H/W Chamwino | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 23. | H/W Chato | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 24. | H/W Chemba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 25. | H/W Chunya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 26. | H/Jiji Dar es salaam(Awali H/W Ilala) | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha |
| 27. | H/Jiji Awali Dar es salaam | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Yenye Shaka | Haipo |
| 28. | H/Jiji Dodoma | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 29. | H/W Gairo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 30. | H/W Geita | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 31. | H/Mji Geita | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 32. | H/W Hai | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 33. | H/W Hanang | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 34. | H/W Handeni | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 35. | H/Mji Handeni | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 36. | H/Mji Ifakara | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 37. | H/W Igunga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 38. | H/W Ikungi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 39. | H/W Ileje | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 40. | H/M Ilemela | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 41. | H/W Iramba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 42. | H/W Iringa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 43. | H/M Iringa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 44. | H/W Itigi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |

| Na. | Jina la Taasisi | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 45. | H/W Itilima | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 46. | H/M Kahama | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 47. | H/W Kakonko | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 48. | H/W Kalambo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 49. | H/W Kaliua | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 50. | H/W Karagwe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 51. | H/W Karatu | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 52. | H/W Kasulu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 53. | H/Mji Kasulu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 54. | H/W Kibaha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 55. | H/Mji Kibaha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 56. | H/W Kibiti | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 57. | H/W Kibondo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 58. | H/M Kigamboni | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 59. | H/W Kigoma | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 60. | H/M Kigoma/Ujiji | Mbaya | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 61. | H/W Kilindi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 62. | H/W Kilolo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 63. | H/W Kilosa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 64. | H/W Kilwa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 65. | H/M Kinondoni | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 66. | H/W Kisarawe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha |
| 67. | H/W Kishapu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 68. | H/W Kiteto | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 69. | H/W Kondoa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Yenye Shaka | Inayoridhisha |
| 70. | H/Mji Kondoa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 71. | H/W Kongwa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 72. | H/W Korogwe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 73. | H/Mji Korogwe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 74. | H/W Kwimba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 75. | H/W Kyela | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 76. | H/W Kyerwa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 77. | H/M Lindi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 78. | H/W Liwale | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 79. | H/W Longido | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha |
| 80. | H/W Ludewa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 81. | H/W Lushoto | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 82. | H/W Madaba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 83. | H/W Mafia | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 84. | H/Mji Mafinga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 85. | H/W Magu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 86. | H/Mji Makambako | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 87. | H/W Makete | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 88. | H/W Malinyi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 89. | H/W Manyoni | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 90. | H/W Masasi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 91. | H/Mji Masasi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |

| Na. | Jina la Taasisi | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 92. | H/W Maswa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 93. | H/W Mbarali | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 94. | H/Jiji Mbeya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 95. | H/W Mbeya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 96. | H/W Mbinga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 97. | H/Mji Mbinga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 98. | H/W Mbogwe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 99. | H/W Mbozi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 100. | H/W Mbulu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 101. | H/Mji Mbulu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 102. | H/W Meatu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 103. | H/W Meru | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 104. | H/W Missenyi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 105. | H/W Misungwi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 106. | H/W Mkalama | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 107. | H/W Mkinga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 108. | H/W Mkuranga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 109. | H/W Mlele | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha |
| 110. | H/W Mlimba | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 111. | H/W Momba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 112. | H/W Monduli | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 113. | H/W Morogoro | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 114. | H/M Morogoro | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 115. | H/W Moshi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 116. | H/M Moshi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 117. | H/W Mpanda | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 118. | H/M Mpanda | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 119. | H/W Mpimbwe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 120. | H/W Mpwapwa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 121. | H/W Msalala | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 122. | H/W Mtama(Awali H/W Lindi) | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 123. | H/W Mtwara | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 124. | H/M Mtwara | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 125. | H/W Mufindi | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 126. | H/W Muheza | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 127. | H/W Muleba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 128. | H/W Musoma | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Yenye Shaka |
| 129. | H/M Musoma | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 130. | H/W Mvomero | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 131. | H/W Mwanga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 132. | H/Jiji Mwanza | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 133. | H/W Nachingwea | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 134. | H/W Namtumbo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 135. | H/Mji Nanyamba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 136. | H/W Nanyumbu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |

| Na. | Jina la Taasisi | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 137. | H/W Newala | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 138. | H/Mji Newala | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 139. | H/W Ngara | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 140. | H/W Ngorongoro | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 141. | H/W Njombe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 142. | H/Mji Njombe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 143. | H/W Nkasi | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 144. | H/W Nsimbo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 145. | H/W Nyanghw'ale | Disclaimer | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 146. | H/W Nyasa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 147. | H/W Nzega | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 148. | H/Mji Nzega | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 149. | H/W Pangani | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 150. | H/W Rombo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 151. | H/W Rorya | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 152. | H/W Ruangwa | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 153. | H/W Rufiji | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 154. | H/W Rungwe | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 155. | H/W Same | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 156. | H/W Sengerema | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Yenye Shaka | Inayoridhisha |
| 157. | H/W Serengeti | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 158. | H/W Shinyanga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 159. | H/M Shinyanga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 160. | H/W Siha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 161. | H/W Sikonge | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 162. | H/W Simanjiro | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 163. | H/W Singida | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 164. | H/M Singida | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 165. | H/W Songea | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 166. | H/M Songea | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 167. | H/W Songwe | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 168. | H/W Sumbawanga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 169. | H/M Sumbawanga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka |
| 170. | H/M Tabora | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 171. | H/W Tandahimba | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 172. | H/Jiji Tanga | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 173. | H/W Tarime | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 174. | H/Mji Tarime | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 175. | H/M Temeke | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 176. | H/Mji Tunduma | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 177. | H/W Tunduru | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 178. | H/M Ubungo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 179. | H/W Ukerewe | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 180. | H/W Ulanga | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Inayoridhisha |

| Na. | Jina la Taasisi | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 181. | H/W Urambo | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Mbaya | Inayoridhisha | Inayoridhisha |
| 182. | H/W Ushetu | Inayoridhisha | Inayoridhisha | Yenye Shaka | Inayoridhisha | Mbaya |
